

20 JUNI, 2013

**BUNGE LA TANZANIA**

-----  
**MAJADILIANO YA BUNGE**

-----  
**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Hamsini na Tatu – Tarehe 20 Juni, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**KIAPO CHA UTII**

Mbunge afuataye alikula Kiapo cha Utii na Kukaa katika nafasi yake Bungeni:-

Mhe. Yussuf Salim Hussein.

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kufuatana na Kanuni yetu, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani hayupo, kwa hiyo, nitaenda moja kwa moja kumwita anayefuatia, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah!

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia leo hii kusimama hapa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, rushwa na ufisadi vinaliangamiza Taifa letu. Hivi karibuni tulimsikia Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, akisikitishwa sana na jinsi rushwa ilivyokithiri katika Chaguzi za Chama chake. Tarehe 16 tumemsikia Spika akikemea na kusikitishwa na rushwa. Siyo hao tu, tumemsikia Jaji Kiongozi wa

20 JUNI, 2013

Mahakama Kuu ya Tanzania, akisikitishwa pia na suala la rushwa. Mihimili yote mitatu inalalamika kuhusu rushwa ilivyokithiri.

Je, Serikali ina mikakati gani madhubuti ya kuweza kudhibiti au kuondoa rushwa hii?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, swali lake zuri sana kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme kwamba, Viongozi hawa wanaposema siyo kwamba wanalalamika, ni namna ya kuwatahadharisha Watanzania, muda wote wakae wanajua kwamba rushwa siyo jambo zuri, ni jambo la hovyoy. Huo ndiyo ujumbe ambao wote wanajaribu kutupa. Hata Bungeni, mnapokuwa mna jambo, juzi nili-*attend* ule Mkutano wa *APNAC*, yale siyo malalamiko ni namna ya kuwaambia Wananchi na Watanzania juu ya uovu wa jambo hili.

Tanzania tuna mikakati gani juu ya mapambano dhidi ya rushwa? Mapambano dhidi ya rushwa yanakabiliwa kwa njia nyingi, lakini moja ni juhudi ambazo tumefanya za kuwa na chombo mahususi ambacho ndiyo kimepewa jukumu la kusimamia eneo hili la rushwa. Upande wa pili ni kuendelea kuziwezesha hasa Mahakama zetu ili ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu katika eneo hili la rushwa.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni letu sote, ndiyo maana mapambano haya ili tufaulu ni lazima kila Mtanzania ajue kwamba, jambo hili siyo jema. Kwa hiyo, mkakati mzuri ni kwa kila Mtanzania kukataa kupokea rushwa au kutoa rushwa. Kama kila mmoja atalifanya hili, Mbunge, Waziri Mkuu, Waziri, Mwananchi wa kawaida, rushwa tunaweza tukaitokomeza. Mtu mmoja mmoja tusipobadilika, tutaendelea kutamani kupokea rushwa, mapambano yatazidi kuendelea kwa muda mrefu. (*Makofi*)

20 JUNI, 2013

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika ahsante sana.

Mkurugenzi wa Kudhibiti na Kuzuia Rushwa, Dkt. Hosea, alisema kwamba, ameshindwa kukabiliana na rushwa kwa sababu amefungwa mikono. Je, Serikali inasema nini kuhusu suala hili? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, niliona kwenye magazeti, nami nilishangaa sana, kwa sababu unaposema umefungwa mikono maana yake nini! Kwa sababu yeye ndiye bado anafanya hiyo kazi, yeye ndiye bado anapeleka watu wote wanaotuhumiwa, ikithibitika kwamba kuna ushahidi wa kutosha, anawezesha watu wale kupelekwa Mahakamani. Kufungwa maana yake nini!

Sasa kama kufungwa maana yake ni ile ridhaa ambayo lazima ipatikane kutoka kwa *DPP*, ni utaratibu ambao tumekubaliana kwamba, iwe hivyo na ni jambo jema tu. Ndiyo maana siku ile kwenye *APNAC* nilisema, ninasikia minong'ono juu ya jambo hili, kama watu wanaona pengine ni utaratibu usiofaa wafanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, hoja ni nini Mheshimiwa Rashid Abdallah? Unapokuwa wewe ni Mpelelezi, unataka wewe mwenyewe uwe ndiyo *Prosecutor*, siyo sahihi; ndiyo maana unawekewa utaratibu wa pili ukusaidie kuweza kuona kama hayo unayotaka kwenda kunifanyia mimi kweli yamejiri au hapana na ndiyo utaratibu wa kawaida hata kwenye kesi za kawaida. Tukisema tukubali kwamba, huyu bwana akishakukamata anavyoona yeye, akishajiridhisha anakwenda Mahakamani, wako wengi mtakaokwenda kule lakini bila kutendewa haki sawasawa. Ndiyo maana ni *checks and balances* katika mfumo na siyo jambo baya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nimesema tu sina hakika, kama hilo ndiyo alikuwa na maana hiyo, maoni yangu yangukuwa ni hayo, lakini kama ana namna nyingine ya

20 JUNI, 2013

kufungwa mikono, nitakuwa radhi kumsikiliza ili tuone tumemfunga kwa namna gani. *(Makofi)*

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Moja ya kichocheo cha kuchochea uzalishaji wa mazao ya kilimo ni upatikanaji wa soko la uhakika wa zao hilo. Hapa nchini Tanzania moja ya zao la biashara ambalo tunaweza tukalipatia soko la uhakika ni zao la pamba, soko lenyewe ni kwa kuimarisha viwanda vinavyotengeneza nguo na kuamuru *uniform* zote za shule za msingi, sekondari na vyuo vinavyovaa *uniform*, kuvaa nguo zinazotokana na pamba ya Tanzania. Majeshi ya Polisi, Jeshi la Kujenga Taifa, Jeshi la Wananchi, pamoja na Taasisi zingine zinazotumia *uniform*, kutumia nguo zinazotokana na pamba.

Niliwahi kushauri suala hili ukasema Serikali inalifanyia kazi. Napenda kujua Serikali imefikia wapi uamuzi wa kufanya zao la pamba ni fahari ya Tanzania na tuweze kutengeneza soko na ajira? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, analolisema Mheshimiwa Nchemba, Waswahili wanasema lina mashiko, ni hoja nzuri tu. Sasa hivi tunachojaribu Serikalini kwanza ni kutoa fursa kubwa sana ya uwekezaji kwenye eneo hili la kilimo hasa kwenye Zao la Pamba. Mimi mwenyewe nimefanya juhudi kujaribu kuzungumza na makampuni mbalimbali na wengi tumeshawaelekeza kwenda Shinyanga na Mwanza. Ninashukuru kwamba, ninaona juhudi zile zinaanza kuzaa matunda mazuri, wapo wameshajitokeza tayari kwa ajili ya kuwekeza kwenye eneo hilo la viwanda vya nguo katika mikoa hiyo miwili, ni jambo zuri.

Mheshimiwa Spika, hiyo itatuwezesha kuwa na uhakika wa matumizi makubwa zaidi ya pamba hapa nchini. Kama Wabunge wote mnavyojua, juhudi hizi tumezianza muda mrefu kidogo, mwaka jana tuliondoa VAT kwa viwanda vyote ambavyo vinazalisha kwa kutumia

20 JUNI, 2013

pamba ya ndani. Mwaka huu tumejaribu kulirejesha tena, kulihimiza kwa lengo hilo hilo, ingawa wapo wanaofikiri kwamba, ingekuwa vizuri kama ingekwenda kutolewa vilevile kwa mlaji. Tatizo inakuwa tu ni namna tutakavyosimamia eneo hilo, kwa sababu watu wengine wanaweza wakanufaika, lakini Mkulima wangu asiweze kupata faida yoyote.

Mheshimiwa Spika, lakini rai yake bado ni nzuri na mimi mwenyewe nilifanya mazungumzo na viwanda hivi, tukazungumza na Jeshi la Wananchi, tukazungumza na Jeshi la Polisi, kuona kama hili jambo linawezekana kufanyika na kwa namna gani. Waliomba sampuli, wameshapelekewa. Kwa hiyo, nafikiri ni suala la muda tu, watakapokuwa wameridhika na zile sampuli, kwa maana kwamba, vitambaa vile vina sifa stahiki, tunadhani wazo hilo la kuweza kuandaa nguo za sare ni jambo zuri, tutaangalia tuone namna ya kulisukuma zaidi.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, viwanda vingi ambavyo tuliwapa wawekezaji, wawekezaji wale wale wamegeuza magodauni na kuanza kuuza bidhaa ghafi nje ya nchi. Kwa nini Serikali kwenye hili ambalo *at least* tuna uhakika na soko lake, isijaribu hata kukopa ama kutenga bajeti ikatengeneza kiwanda kizuri cha mfano kama vilivyo vya China na tukaanzia hapo kuondokana na hii habari ya viwanda kuwa magodauni na Wananchi wengi kupoteza ajira na Tanzania kutokuwa na kiwanda ambacho kina hadhi ya Kimataifa?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ushauri ni mzuri na sidhani kama tuna ubishi katika jambo hilo, lakini tunachosema hapa sasa hivi ni kwamba, tutoe nafasi kwa sekta binafsi, wale wana nafasi kubwa sana, wana uwezo mkubwa sana wa kuweza kusaidia katika eneo hili. Unaweza kuwa na kiwanda hicho kimoja, lakini sisi wote hapa ni mashahidi, viwanda vingi vinapokuwa vinaendeshwa chini ya utaratibu huu vimekuwa na matatizo mengi. Kwa hiyo, wakati nakubaliana na rai yake, lakini mimi bado nasisitiza kwamba ni vyema wote tukajaribu

20 JUNI, 2013

kutoa msukumo, acheni *private sector*, wakijitokeza kwa wingi hawa ndiyo wana uwezo ku-*role* viwanda vingi sana. Tunachohitaji ni matumizi makubwa ya pamba ya ndani. Tukifanikiwa hilo tutaongeza ajira kwa upande mwingine.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukisikiliza nyimbo nyingi za Taifa katika Bara la Afrika zinasema kwamba hekima, umoja na amani ndiyo ngao zetu. Je, hali ambayo imejitokeza katika nchi yetu na matatizo haya ambayo yamejitokeza Arusha na maeneo mengine kama Mtwara; nini tamko la Serikali na Serikali iko tayari kueleza umma ni nini ambacho kimetokea hivi sasa?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, analolisema Mheshimiwa Murtaza Mangungu ni jambo ambalo linatugusa sisi wote. Suala la amani, ulinzi na utulivu ndiyo hasa tunu ambayo kila nchi ingependa kuwa nayo. Anasema hivi karibuni kumejitokeza vurugu, fujo za hapa na pale, kwa hiyo, angependa tuwaeleze Watanzania kama Serikali tunafikiria tufanye nini.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, nataka niseme kwamba, jukumu kubwa hasa ni kwa Viongozi wa Kisiasa. Jambo la kwanza kabisa tuwakabidhi Viongozi wa Kisiasa. Kama Viongozi wa Kisiasa hatutafika mahali na kukubaliana kwamba siyo hoja upo Chama gani, yapo mambo ambayo ni lazima tukubali kwamba ni jukumu letu sisi wote na kila mmoja ni lazima azungumze lugha mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninyi nyote ni mashahidi, CHADEMA waliposhinda hapa wao walikuja waziwazi wakasema tutahakikisha nchi hii haitawaliki. Sasa, Mheshimiwa Mangungu inawezekana pengine ndiyo mwendelezo wa utekelezaji wa kauli hizo. Kubwa hapa la pili ni upande wa Serikali; ni lazima tuhakikishe kwamba, wale wote ambao wanajaribu kuvunja amani kwa namna yoyote ile, kazi kubwa tuliyonayo ni kupambana kwa njia zozote zile zitakazoonekana zinastahili. (*Makofi*)

20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, ninawaomba sana Watanzania, maana kila juhudi zinapoonekana zinaelekea huko, unapata watu wengine tena wanajitokeza aah unajua, unajua! Acheni Serikali itimize wajibu wake, kwa sababu jambo hili ni jambo la msingi na lazima wote tulilinde kwa nguvu zetu zote.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa Watanzania, kila mmoja ajue kwamba siku nchi hii ikiingia katika vurugu hakuna mshindi, wote tutaumia tu na hasa akina mama, watoto na walemavu ndiyo watakaoumia sana. Kwa hiyo, wote ni lazima tuhakikishe hili jambo tunalisimamia vizuri. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, kutokana na hali iliyopo sasa, Wananchi wengi wamekuwa na hofu, lakini pia hata shughuli za uzalishaji mali zinaingia kwenye shaka na kuumiza uchumi wa nchi yetu. Serikali iko tayari kiasi gani kuweza kubainisha na kuchukua hatua stahiki badala ya kusakama makundi fulani ili tujue chanzo halisi cha vurugu hizi na matatizo haya na jinsi gani ambavyo vyombo vya dola vinashughulikia; kwa sababu yapo malalamiko katika baadhi ya maeneo kama Mtwara, Wananchi wanapigwa na Vyombo vya Dola; je, Serikali ipo tayari kutoa kauli ni kiasi gani watafanya uchunguzi na kupata suluhisho la kudumu la matatizo haya?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ndiyo lile lile nililosema; Mheshimiwa Mangungu hapa ameanza vizuri, lakini mwisho anasema Vyombo vya Dola vinapiga watu. Ukifanya fujo, umeambiwa usifanye hiki, wewe ukaamua kukaidi, utapigwa tu maana hakuna namna nyingine. Lazima wote tukubaliane kwamba, nchi hii tunaiendesha kwa misingi ya kisheria. Sasa kama wewe umekaidi, hutaki, unaona ni imara zaidi, wewe ndiyo jeuri zaidi, watakupiga tu na mimi nasema muwapige tu kwa sababu hakuna namna nyingine maana tumechoka sasa. *(Makofi)*

Sasa analolisema ndugu yangu pale, inawezekana kwa sababu anatoka Mikoa ya Kusini. Jana wakati

20 JUNI, 2013

majadiliano yanaendelea, nilimsikiliza Mbunge mmoja kutoka Mtwara, naye alijaribu kugusiagusia kwamba, Vyombo vya Dola vinakamata watu, vinapiga watu. Mara ya mwisho nilisema, tunataka turejeshe hali ya amani katika maeneo haya na Mtwara ni mojawapo. Nikawaambia Watanzania tunawaombeni radhi sana katika jambo hili, tutakapoanza kufuatilia mmoja mmoja, tunajua kuna watu watajitokeza kuanza kusema Vyombo vya Dola vinanyanyasa. Nikawaomba msamaha, tuachieni tufanye hiyo kazi. (*Makofi*)

Mtwara pale tuna orodha ya watu ambao wanasemekana ndiyo vyanzo vya matatizo na vurumai. Sasa mnaacha tusiwakamate? Lazima tuwakamate na kama katika kuwakamata watafanya jeuri jeuri watapigwa tu kabla ya kupelekwa tunakotakiwa kuwapeleka. Hatuwezi kuendelea jamani na hali hii mkadhani kwamba tutafika tunakokwenda. Lazima Serikali ijitahidi na mimi nasema Vyombo vya Dola vijipange imara, wahakikishe wanadhhibiti hali, tuweze kuirejesha na kuwa tulivu. Hakuna namna nyingine. (*Makofi*)

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Ahsante Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mpango wa Taifa unatuonesha kwamba, ifikapo mwaka 2025 Taifa letu linatakiwa liwe na uchumi wa kati na hatuwezi kuwa na uchumi wa kati kama hatujalisha vizuri ubongo wa binadamu. Serikali kwa sasa inaandaa Sera ya Elimu na kutoka kwenye Sera kunakuwa na *National Curriculum Development Framework*, unaenda kwenye Mitaala, Mihitasari, baadaye vitabu.

Kwa sasa vitabu vingi vimetoka na mitaala hii ambayo imetokana na mitaala ya mwaka 1995 ambayo imepitwa na wakati na vitabu hivi vina makosa lukuki. Je, kwa nini Serikali inatumia bilioni 55.2 ambayo ni asilimia 75 ya *change* ya rada kwa ajili ya kusambaza vitabu takribani nakala milioni 18 pamoja na mihitasari ambayo ina makosa, pamoja na zile fedha nyingine za *USAID* bilioni 20,400,000,000



20 JUNI, 2013

kwa ajili ya vitabu vya sekondari nakala milioni mbili na laki tano? Kwa nini tuisubiri tihakikishe tumepata Sera nzuri badala ya kupoteza fedha hizi zaidi ya bilioni 75 wakati mwakani tutaviondoa vyote tuje na vitabu vingine vipya ambavyo vina usahihi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nijaribu kumjibu Mheshimiwa Mbatia swali lake. Kwa upande mmoja kidogo ni la kiutekelezaji zaidi, kwa hiyo, naweza nisiwe na utalam mzuri sana juu ya jambo hili. Rai yake ya msingi ni kwamba, viko vitabu ambavyo yeye kwa maoni yake anaona havistahili kusambazwa kwa sasa na kwamba, tungoje mpaka hapo Sera itakapokuwa imepitishwa, ielekeze upya aina ya vitabu au mfumo wa vitabu ambao unastahili kutumika shuleni.

Mimi nasema kimsingi ni jambo zuri la kufikiria, lakini upande wa pili, napenda niamini vilevile kwamba, walioidhinisha vitabu hivyo vichapishwe, watakuwa waliweka uzito wa kutosha katika eneo hilo la kiasi gani kitabu hiki kasoro zinazosemekana ni za msingi za kufanya kitabu chote kionekane hakifai. Ndiyo imani yangu. Sasa kwa sababu mimi siyo Waziri wa Elimu, pengine nilichukue kama ulivyo-*suggest*, nitajaribu kuzungumza na Waziri wa Elimu, tuone makosa hayo ni makubwa kiasi gani, tuone kama rai yako inawezekana tukaizingatia au pengine haina haja sana ya kutokukubaliana na wale ambao walisema liendelee, basi tutarudisha jibu na kukuarifu, maana siyo mtaalam sana kwenye eneo hili.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

Kwa kuwa imekuwa utamaduni kila Waziri anayeingia kwenye Wizara ya Elimu yeye ndiyo anakuwa Sera, yaani anakuja na mipango yake yeye mwenyewe; na kwa kuwa tarehe 5 mwezi wa sita mwaka huu, Siku ya Jumatano, kwenye Bunge hili Tukufu, Wizara ya Elimu ilikubaliana nami, wakavunja *EMAC*, ambayo ilitoa ithibati kwenye vitabu hivi ambavyo vinasambazwa sasa. Kwa mfano, Watanzania

20 JUNI, 2013

wanafundishwa mbili ni namba tasa wakati siyo namba tasa na vitabu vyote vinaonesha hivyo. Saba mara mbili ni kumi na tano. Vitabu hivi Serikali imeshakiri kwamba vina udhaifu. Sasa kama Serikali yenyewe imekiri ndani ya Bunge hili vina udhaifu; kwa nini tusikubali viondoke kwa sababu vinazidi kuharibu uelewa wa watoto wetu na hii ndiyo inalisha ubongo wa mwanadamu kwa ajili ya kuandaa karne ijavyo ya sayansi na teknolojia?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, najua tutaonekana tunabishana mimi na Mheshimiwa Mbatia. Mimi sipendi kubishana na ndugu yangu pale. Ninachokisema hapa Mheshimiwa Mbatia, inawezekana wewe umepata hata fursa ya kuviona vitabu, umeona uzito wa kasoro hizo, mimi sijaviona. Sina hakika Wizara ya Elimu na Wataalam wao wanasema nini juu ya vitabu hivyo; ndiyo maana nimesema hebu nipe muda na mimi niulize Sekta inayohusika.

Tuulize vyombo vinavyohusika na ikibidi tuangalie ni maeneo gani hasa ambayo yanazungumzwa kwamba yamefanya kitabu chote kisiwe na maana; maana inawezekana kuna hitilafu kweli, lakini kubwa ni za msingi kiasi gani. Mimi nadhani hilo ndiyo litakaloamua juu ya uwezekano wa kukubaliana na wewe au kutokukubaliana.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Ahsante Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, hapo awali umetoa kauli nzito ya kuliambia Taifa hili kwamba, wale raia wote ambao watakuwa wakaidi wapigwe tu na watapigwa tu.

Naomba ninukuu Katiba, Ibara ya 13(6)(b) inayosema hivi: "Ni marufuku kwa mtu yeyote aliyeshitakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo. Pia ibara hiyo hiyo kifungu cha 6(e); ni marufuku kwa mtu yeyote kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza utu, nguvu na kumdhalilisha. (*Makofi*)

20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kauli yako hiyo nzito uliyoitoa; huoni kwamba umevunja Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, namshukuru sana ndugu yangu Khatib Haji, maana kaanza kwa kusoma Katiba yenyewe. Unajua lazima uweke tofauti kati ya mtu ambaye ameshakamatwa, amefikishwa mbele ya Vyombo vya Sheria na ndiyo Katiba hiyo inanielekeza nisiende kufanya jambo lolote katika eneo hilo. *(Makofi)*

Ninayemzungumzia hapa ni mtu ambaye ameamua kufanya vitendo hajakamatwa na ndiyo maana nilikwambia, nikikwambia bwana usiandamane, nikikwambia bwana hapa mahali hutakiwi kwenda, wewe ukaamua kutumia mabavu kwa sababu mko wengi, ndiyo maana nikasema hawa watu tutashughulika nao hivyo hivyo. Mimi sizungumzii mtu ambaye ameshakwenda Mahakamani, amefikishwa huko hata kidogo. Ndiyo maana rai yangu ikawa ni kwamba, jamani kila Mtanzania awe mwepesi wa kutii Sheria bila shuruti ndiyo suluhu ya kweli. *(Makofi)*

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru kidogo kwa kusawazisha hilo neno. Nataka uliambie Taifa hili na uwaambie askari wako kwamba, wale watakaokaidi kutii amri halali za Jeshi la Polisi ndiyo ambao wanahitaji kukutana na mkono wa dola katika hali yoyote na siyo kauli yako ya awali kwamba kuanzia sasa piga tu. Naomba ufute neno piga tu.

**SPIKA:** Hapana, nadhani wewe hukumwelewa hapo. Hukumwelewa na amekuelimisha, kama sisi tumelewa hapa yule atakayekaidi kushikwa; unaona sasa! *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nafikiri wale wote waliosikiliza nadhani watakubaliana nami kwamba, ulichosema wewe na nilichosema mimi ni vitu viwili tofauti kabisa. *(Kicheko/Makofi)*

20 JUNI, 2013

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwanza, nikupe pole Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Swali langu nataka kujielekeza vilevile katika amani, lakini katika nchi za Maziwa Makuu. Hivi karibuni kumetokea sintofahamu ya maneno baina ya Tanzania na Rwanda kutokana na kauli ya ushauri wa Rais Kikwete alioutoa kule AU kuzitaka nchi za Uganda, Rwanda na DRC kukaa pamoja na waasi wa nchi zao ndani ya nchi zao. Nataka kujua ni nini msimamo wa Serikali ya Tanzania katika suala zima la amani ya *DRC?* (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nchi za Maziwa Makuu kwa maana ya DRC, Rwanda, Burundi, Tanzania yenyewe na Uganda, kwetu sisi suala la amani na utulivu ni jambo la msingi sana na kwa upande wa Tanzania ni zaidi, kwa sababu kila kunapotokea vurugu katika nchi hizo, kimbilio la Wananchi wao ni Tanzania. Sisi ndiyo tunaobeba mzigo mkubwa sana wa wakimbizi na ndiyo maana rai ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilikuwa ni jamani hebu tukae chini pamoja tuzungumze, maana namna pekee ya kutatua jambo hili ni kukaa katika meza baina ya pande hizo mbili, wazungumze wafikie mwafaka kwa lengo la kurejesha amani katika eneo hili pamoja na DRC.

Kwa hiyo, sisi msimamo wetu tutaendelea kuziasa nchi hizi. Tutaendelea kuwasihi waone hili ni jambo la msingi na kwa masilahi ya watu wao. Mimi nadhani tukili-*approach* kwa njia hiyo, tutaendelea kuwa sehemu nzuri sana ya kurejesha amani katika eneo hili la Bara la Afrika.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Kwa kuwa kuna baadhi ya nchi huwa haziko tayari kupeleka wanajeshi wao kulinda amani katika baadhi ya maeneo na badala yake hukubali kutoa mchango wao wa kifedha kwa ajili ya kuimarisha amani. Je, ni kwa nini Tanzania inaendelea kupeleka majeshi katika baadhi ya nchi na isitoe tu fedha ili kuhakikisha kwamba hawa vijana wetu wanabaki nchini

kulinda amani ambayo sasa hivi inaonekana kutoweka hapa nchini kwetu?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, tunapeleka askari kwenye nchi mbalimbali kulinda amani, kwa sababu ni moja ya jukumu tu la kimataifa ambalo Tanzania inaona ni jambo la busara kushiriki. Kwa upande mwingine ni namna vilevile ya kusaidia vijana wetu kuwakomaza, kuwapanua upeo katika masuala ya ulinzi na usalama kwa ujumla, kwa sababu unapokuwa kule unakutana na majeshi mengine na kuna kubadilishana uzoefu. Kwa hiyo, ni namna vilevile ya kujifunza kutokana na wengine wanavyoendesha shughuli za ulinzi na amani.

Kwa hiyo, nadhani tusilione upande mmoja tu. Kwa upande wa pili sina hakika kama itakuwa busara sana, kuchukua fedha zetu ambazo tunahangaika hapa kuzipata upeleke nje, wakati kwa kupeleka askari atalipwa posho huko na Umoja wa Mataifa, atapata nini. Mimi nadhani ni busara nzuri, acha tumpeleke tukapate yote, apate fedha, tupate vilevile mafunzo zaidi na tukirudi hapa tunakuwa tumekomaa zaidi kuliko kama tungepeleka fedha peke yake. (*Makofi*)

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwanza kabisa, napenda niishukuru Serikali kwa jinsi ambavyo imeweza kushughulikia masuala ya kazi za sanaa hapa nchini. Pia ningependa kuvipongeza vyombo vyote ambavyo vimekuwa vikisaidia kukuza sanaa, tukianza na *Radio Clouds* na *Steps Entertainment*, Msama, ambao wote hao wamekuwa wakijaribu kuzuia uharamia unaotokana na kazi za wananii. Serikali kwa juhudi kubwa imeamua kuweka *stickers* kwenye kazi za wasanii ili kuzuia uharamia huo. Kwa hiyo, tunashukuru sana.

Je, ni kweli tarehe 1 *stickers* zitaanza kuwekwa kwenye kazi za wasanii; bado kuna utata mkubwa sana kati ya wasanii na vyombo vya usambazaji wa kazi za sanaa; na je, ni nani anayepaswa kulipia zile *stickers*; na ni nani anayepaswa kusambaza zile *stickers*; ni TRA au

20 JUNI, 2013

*COSOTA?* Bado kuna utata mkubwa sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunaomba Serikali itusaidie.

**SPIKA:** Hilo siyo la kisera, lakini basi Mheshimiwa Waziri Mkuu hebu sema sema tu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba nimsaidie dada yangu Mheshimiwa Mlata. Mimi nafikiri ushauri mzuri kwa jambo hili ingekuwa tukae pamoja, *COSOTA*, ninyi wasanii, pamoja na hivi vyombo vya usambazaji na upande mwingine Serikali hasa *TRA*, tulizungumze hilo jambo kwa pamoja, tuone njia mwafaka na wapi kuna kikwazo tuone namna gani kitatatuliwa ili turejee sasa Serikalini na pendekezo ambalo tunafikiri tunaweza tukalipa baraka. Vinginevyo, kutoka kwangu siyo rahisi kuweza kulijibu moja kwa moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kukushukuru sana, kwa kazi uliyoifanya na kujibu maswali uliyoulizwa ya aina mbalimbali. Kwa wale ambao hawakupata nafasi, bahati mbaya muda umepita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mlata, sikuuliza swali la nyongeza kwa sababu hata swali lenyewe lilikuwa siyo la sera. Kwa hiyo, nilitaka tu ajibu. Tunaendelea Katibu, hatua inayofuata.

## **MASWALI YA KAWAIDA**

Na. 432

### **Kuwachimbia Malambo Wananchi wa Vijiji vya Kata ya Vigwaza**

**MHE. ZAINAB M. VULLU** aliuliza:-

Ni Sera ya Serikali kuwapatia Wananchi wake maji safi na salama lakini Wananchi wa Vijiji vya Visezi, Mnhindi na Buyuni, kwa muda mrefu wamekuwa wakihangaika kupata maji kwa ajili ya matumizi yao na mifugo:-

20 JUNI, 2013

Je, ni lini Serikali itawajengea malambo Wananchi wa Vijiji vya Visezi, Buyuni na Kitongoji cha Mnhindi katika Kata ya Vigwaza?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ipo changamoto ya upatikanaji wa huduma za maji kwa matumizi ya binadamu na mifugo katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali kupitia Wizara ya Maji, imeajiri Kampuni ya *Building Water and Earthwork Limited* kwa ajili ya ujenzi wa Mradi wa Maji Chalinze, kwa ajili ya matumizi ya binadamu, ambao utagharimu jumla ya shilingi bilioni 3.7. Kazi ambazo zimekamilika ni ufungaji wa mabomba umbali wa kilomita 13.5 kati ya kilomita 32.3, uchimbaji wa mtaro na ufungaji wa bomba katika umbali wa kilomita 3.5. Aidha, ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji litakalokuwa na ujazo wa lita za ujazo 400 upo katika hatua ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa malambo, Serikali katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, imepanga kufanya ukarabati wa malambo mawili katika Kijiji cha Milo kilichoko katika Kata ya Vigwaza. Aidha, katika mwaka huo, Serikali itatumia shilingi milioni 3.4 kwa ajili ya ukarabati wa lambo katika Kijiji cha Mkenge na shilingi milioni sita kwa ajili ya ukarabati wa lambo katika Kijiji cha Chamakweza. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa malambo katika maeneo mengine kwa kadiri upatikanaji wa fedha utakavyoruhusu.

**MHE. ZAINAB M. VULLU:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Kabla sijauliza maswali yangu ya nyongeza, kwanza,

20 JUNI, 2013

napenda nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa utekelezaji wa ujenzi wa bomba awamu ya pili kutoka Mto Wami, ambao umesaidia Wananchi wa vijiji takriban 41 wa Wilaya ya Bagamoyo kupata maji. Sasa nauliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(i) Swali la msingi limeuliza kuhusu ujenzi wa upatikanaji wa maji kwa ajili ya Wananchi na mifugo, lakini jibu limegusa ujenzi wa bomba ambao mpaka sasa unasuasua pamoja na mkandarasi kupewa kazi hiyo. Sasa naomba nipatiwe majibu; je, ni lini ujenzi huo wa bomba ambao Mheshimiwa Naibu Waziri umeuelezea utakamilika?

(ii) Kwa kuwa mahitaji ya Wananchi wa Kata ya Vigwaza hasa Vijiji vya Viseze, Buyuni na Vigwaza yenyewe kwa jina, wana mahitaji muhimu ya kwao na mifugo, lakini jibu linasema ujenzi utaanza Mwaka huu wa Fedha. Je, Serikali inawahakikishia vipi Wananchi wa Kata hiyo kwamba, sasa watapata maji kutokana na fungu hilo la pesa lililotengwa; ni lini ujenzi utaanza? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Pwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hii awamu tunayoizungumza hapa sasa tunazungumza awamu ya pili, siyo awamu ya kwanza. Awamu ya kwanza kazi kubwa imefanyika pale. Nipende tu kumshukuru sana Mheshimiwa Vullu, kwa ku-*appreciate* kwamba, sehemu kubwa sana ya kazi imefanyika pale. Anasema kwamba, unasuasua ni kweli, lakini nime-*quote* na nimeitaja Kampuni ambayo imepewa kazi hiyo, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, kazi inaanza na inakwenda haraka.

Mheshimiwa Spika, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutafanya kila tunaloweza kulifanya ili



kuhakikisha kwamba, tunaisukuma kazi hii, iende kwa haraka kama Mheshimiwa Zaynab Vullu, anavyoshauri hapa.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu vijiji alivyovitaja vyote na Kata ambazo amezitaja hapa, kwa sababu maswali hapa yameelekezwa katika maeneo mawili makubwa, yameelekezwa katika eneo la maji ya kunywa na katika bajeti hii ukiangalia vizuri, tumetenga bilioni 1.4, ukiacha huu mradi mkubwa ambao tunauzungumza hapa, ambao nina hakika utakwenda ku-*cater* kwa ajili ya hili eneo analolizungumzia Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, hili la pili ambalo analizungumza hapa kuhusu malambo; malambo yalijengwa kwa shilingi milioni 140 yakabomoka na tukaenda kuyatengeneza tena. Vyovyote vile itakavyokuwa, mimi nataka nithibitisha kwamba, malambo haya nayo yatakuwa yanafanya kazi, kwa sababu tumetenga hela kama nilivyokuwa nimeeleza hapa. Namwomba Mheshimiwa Vullu, kama kuna eneo ambalo anafikiri bado haliendi vizuri, tukae nae anieleze vizuri ili niweze kufuatilia na kuhakikisha kwamba, inatekelezwa kama anavyotaka yeye.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Genzabuke. Utapata tatizo utaanza maji ya kwenu na wakati ni Ruvu.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wanawake wamekuwa wakitumia muda mwingi sana kutafuta maji badala ya kufanya shughuli za uzalishaji mali. Je, Serikali ipo tayari sasa mara baada ya kumaliza Bunge hili la Bajeti kuanza shughuli ya kupeleka maji katika vijiji vyote vilivyotajwa, ikiwa ni pamoja na Vijiji vya Heljuu, Mumbigwa na Kasangezi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Genzabuke, kama ifuatavyo:-

20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, kwanza, hili tumeshalifanyia maamuzi na Mheshimiwa Dokta Mahenge, yuko hapa ananisikia tukizungumza. Tumekaa na Wabunge, tumekaa na Mheshimiwa Moses Machali pamoja na wengine wanaotoka Kigoma, tumekubaliana kimsingi kuhusu matatizo yote yanayozungumzwa hapa kwamba, Mheshimiwa Mahenge atakwenda kule, lakini na mimi pia tutaweka katika ratiba zetu kuhakikisha tutakwenda kule.

Na. 433

### **Taratibu za Kulipia *Units* za Umeme**

**MHE. MOZA A. SAIDY** aliuliza:-

Shirika la Umeme Nchini (*TANESCO*), limeweka utaratibu wa kulipia umeme kwa njia ya bili, ambapo wateja hulipa kutokana na *units* wanazotumia:-

- (a) Je, kwa nini kunakuwa na malimbikizo ya bili za wateja?
- (b) Je, kwa nini mteja anayelipia umeme hapewi *units* zinazolingana na fedha alizotoa badala yake kunakuwa na makato?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, malimbikizo ya bili za wateja yanatokana na wateja kutokulipa gharama za kiasi chote cha umeme alichotumia kwa mwezi husika na hivyo kupelekea kiasi alichoshindwa kulipa kuongezwa katika bili ya miezi inayofuata, pamoja na riba ya kutokulipa kwa wakati.

(b) Mheshimiwa Spika, mteja anaponunua umeme anapewa *units* kulingana na fedha alizotoa, ikiwa ni pamoja na kukatwa makato yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria. Makato yaliyopo kwa mujibu wa Sheria kwa mteja wa *TANESCO* ni kama yafutayo: *VAT* asilimia 18 ya kiasi alichotoa; *REA* asilimia tatu ya kiasi alichotoa; *EWURA* asilimia moja ya kiasi alichotoa; na gharama ya huduma kwa mwezi ambayo inatozwa kutegemeana na kundi la matumizi aliloko mteja.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini ningependa kumwuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Wananchi walio wengi wanalalamikia kubambikizwa madeni na kukosa imani na *TANESCO*. Je, ni kwa nini sasa Serikali isipunguze *service charge* kwa Wananchi wa kipato cha chini ili waweze kutumia umeme huo?

(ii) Je, Serikali inatoa tamko gani kwa Mameneja wa *TANESCO* waliokuwa wazembe, nguzo inapoanguka mpaka Waziri atoe maelekezo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu ya msingi, tozo hizi, *charge* hizi zinazochajiwa katika bili za wateja zipo kwa mujibu wa Sheria na Sheria hizi zilipitishwa na Bunge za kuboresha huduma za umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwenye eneo la *Service Charge*, tumelipokea, tutalitazama, tutashauriana wote kwa pamoja, tuone kama tupokee ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ama la.

Mheshimiwa Spika, hili suala la Mameneja wa *TANESCO*, limekuwa likilalamikiwa hapa Bungeni mara kwa mara na Waziri wa Nishati na Madini, ameshatoa tamko hapa mara kadhaa kwamba, sasa hivi Dunia yote inaelekea kwenye *Digital*, Dunia yote sasa hivi inaelekea kwenye *Three Dimension*, Dunia yote sasa hivi ipo kwenye *Fourth Generation*. Sasa kama kuna Mameneja wa analojia, wakati huo umeshapitwa. Sisi Wizara ya Nishati na Madini, tunataka Meneja ambaye atazingatia *performance*, Meneja ambaye atazingatia *good attitude* kwa wateja, lakini Meneja ambaye atazingatia *target* na *results*, mwisho wa siku tuweze kuongeza tija kwa Wateja wetu tunaowahudumia. Sasa kama kuna Mameneja wazembe, ambao bado hawajahama kutoka kwenye analojia kwenda kwenye dijitali kwenye utendaji wao; kwa kweli hatutawavumilia.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mfumo wa kufunga LUKU katika makazi ya Wananchi na sehemu zote ambazo zinatumiya nishati ya madini umeonesha siyo kero kwa watumiaji wa umeme na pia upande wa Serikali, wanakuwa na uhakika wa kupata mapato ambayo wanastahili. Je, Serikali haioni kwamba, kuna umuhimu sasa wa kusambaza LUKU, ikiwezekana nchi nzima ili waondokane na haya matatizo ambayo yanaleta manung'uniko kutoka kwa Wananchi?

**SPIKA:** Lakini ni nishati ya umeme siyo ya madini?

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nishati ya umeme.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* imeendelea na zoezi la ufungaji wa LUKU katika maeneo mbalimbali ya nchi na

20 JUNI, 2013

zoezi hilo ni endelevu, tutaendelea kulifanya ili kuepuka matatizo haya tunayoyapata kwenye bili hizi za kufuata kila baada ya mwisho wa mwezi. Zoezi hilo linaendelea na tuna mradi mkubwa Dar es Salaam, ambao tunafunga LUKU katika viwanda vikubwa na matumizi mengine kama ya makanisa, mashule, ili kuepuka wizi wa umeme unaofanywa katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, LUKU tunazotumia sasa hivi ni zile ambazo mtu bili yake ikiisha tunaweza kukata umeme tukiwa ofisini, hatuhitaji kuingia kwenye geti la nyumba ya mtu ama kuingia kwenye *compound* ya mtu. Kwa hiyo, tume-*advance* zaidi kiteknolojia na sasa hivi tuna *system* ambayo tunaweza tukakata umeme hata tukiwa ofisini na kuangalia matumizi ya kila mteja kutokea ofisini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, zoezi hilo linaendelea na tutaendelea kufanya hivyo.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri kwamba, anahitaji Mameneja wa kidijitali.

Sasa yeye ndiyo yuko kwenye sekta hiyo, tunaomba atusaidie. Hivi sasa kuna Wananchi ambao tayari wameshalipia fedha kwa ajili ya kuwekewa umeme, lakini *TANESCO* wameweka nguzo tu, bado hawajapeleka mita na hawajafanya chochote na ni nchi nzima, watu wako wengi. Toa tamko kama ulivyotoa Geita ili watu wapate umeme. Ahsante.

**SPIKA:** Haya, sijui utoe tamko!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna taarifa za kuwepo Wananchi wengi ambao wamelipia umeme kwenye maeneo mbalimbali ya nchi na hawaendi kuunganishiwa umeme kwa wakati. Zipo sababu wakati mwingine za ki-*logistics* kwamba, vifaa vile vinakuwa vimechelewa kufika kwenye maeneo husika na Mameneja wetu wanakuwa wamepungukiwa; kwa mfano, kama wana nguzo wanakuwa wamepungukiwa nyaya ama mita; hapo tunaelewa na sisi tunatoa msaada mkubwa kwa TANESCO kuhakikisha kwamba, matatizo ya ki-*logistics* yote tunayashughulikia ili Wananchi wasipate shida ya kuunganishiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini yako maeneo mengine Wananchi wanapeleka maombi hawapewi majibu, hawapewi taarifa yoyote kwa nini hawaunganishiwi na anatomia zaidi ya miezi sita bila kuunganishiwa. Hii ni kero kubwa na ambayo haikubaliki.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa anaomba nitoe tamko. Tamko la Serikali ni kwamba: Wananchi wote ambao wamelipia umeme na vifaa vipo, wakaunganishiwe bila vikwazo vyovyote na Meneja ambaye hatafanya hivyo, watuletee taarifa kama wanavyofanya Wananchi wengine wanatutumia meseji na sisi tutashughulika nao moja kwa moja. (*Makofi*)

Na. 434

### **Jeshi la Polisi Kuingia Ubia na Vyombo Vingine**

**MHE. KHATIB SAID HAJI** aliuliza:-

Jeshi la Polisi ndiyo chombo chenye jukumu la kulinda usalama wa raia na mali zao:-

Je, Jeshi hilo kwa upande wa Tanzania Zanzibar limeingia ubia na taasisi au vyombo vingine vyovyote katika kutimiza wajibu wao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khatib Said Khaji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi Tanzania ni Taasisi ya Muungano, ambayo ipo Kikatiba na imeanzishwa na kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Jeshi la Polisi na Polisi Wasaidizi, Sura ya 322. Majukumu ya msingi ya Jeshi la Polisi ni kulinda maisha ya watu na mali zao.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi, halijaingia ubia na mtu au Taasisi yoyote, kufanya shughuli za msingi za Taasisi hii. Hata hivyo, Jeshi la Polisi kwa kutumia Sera yake ya Polisi Jamii, kama moja ya mihimili mitatu ya maboresho yanayoendelea nchini, hushirikiana na wadau mbalimbali wa ulinzi na usalama katika kusogeza huduma zake kwa Wananchi.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Waziri kwamba, Jeshi la Polisi halijaingia ubia wowote katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Kifungu Namba 121, kinatambua kuwepo kwa Vikosi vya SMZ, ambavyo ni pamoja na JKU, KMKM na Chuo Cha Mafunzo:-

(i) Mheshimiwa Spika, kama hivi ndivyo, majukumu ya Vikosi hivi yameainishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na kazi zao zimeelekezwa huko. Je, ni sababu ipi iliyopelekea Askari wa KMKM, kuwapiga watu risasi siku ya uchaguzi wa Bububu, ilhali wakijua kazi ya ulinzi wa usalama na amani ya nchi hii ni ya Jeshi la Polisi na si ya vikosi vingine vyovyote? (*Makofi*)

(ii) Katika uchaguzi mdogo huo wa Jimbo la Bububu, walionekana vijana waliopakizwa kwenye magari ya KMKM wakificha nyuso zao kama vile wanavyotumia vikosi vya waasi wakiwemo Boko Haram, Al-Shabab na Alqaida. Serikali ilikuwepo na Askari wa Polisi walikuwepo na hawakuwaambia lolote wala hawakutoa kauli yoyote kulaani vitendo vile. Je, Serikali ipo tayari kuikemea SMZ na vikosi vyake, wafanye kazi iliyoainishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na si vinginevyo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kuna Vikosi vya SMZ ambavyo vimeundwa Kikatiba, kama lilivyoungwa Jeshi la Polisi la Muungano. Pia ni kweli kwamba, hakuna ubia kati ya Vikosi vya SMZ na Jeshi la Polisi, lakini katika Sheria zote mbili ambazo zimeanzisha Vikosi na ile ambayo imeanzisha Jeshi la Polisi, zinaruhusu matumizi hata ya raia katika kuhakikisha ulinzi unaimarishwa. Kwa hiyo, kupitia hapo inawezekana ndiyo sababu ya kuwa KMKM inashiriki katika baadhi ya mambo ya ulinzi na usalama Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika kufanya hivyo ni kwamba, mara zote *Command* ya Kikosi ambacho kina KMKM, inakuwa chini ya Jeshi la Polisi. Hii inatokea wakati wa maafa au wakati wa *operation* au kama hivyo uchaguzi ambapo pengine Jeshi la Polisi limekuwa *over stretched*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jeshi la KMKM kupiga mtu risasi; taarifa hii hatunayo katika Jeshi la Polisi na kama ipo, basi haijafikishwa Kituo chochote cha Polisi ili tuifanyie kazi na kama imefikishwa, basi tupewe kumbukumbu tuweze kufanya kazi inayotupasa.

Mheshimiwa Spika, la pili, tuikemee SMZ isitumie Vikosi vyake kinyume na sababu za kuundwa kwake. Kama



nilivyosema mwanzoni ni kwamba, Vikosi vya SMZ, Amiri Jeshi wake ni Rais wa Zanzibar, ambaye ikitokea haja ya kuvitumia, yeye ndiye ambaye anatoa maelekezo, kwa hiyo, vinafanya kazi kwa mujibu wa Sheria.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Jeshi la Polisi wajibu wake wa kwanza ni kulinda Wananchi, raia, mali zao na uhai wao; na kwa kuwa kutokana na majukumu yao Jeshi la Polisi, limepewa wajibu wa kuweza hata kuingia kwenye nyumba za raia na kufanya upekuzi muda wowote bila kuambatana hata na Viongozi wa Serikali wa eneo lile; na kwa kuwa pia yametokea matukio mengi ya baadhi ya Polisi kwenda kujifanya wanafanya upekuzi kwenye nyumba za watu, wakati huo huo wanakwenda kuwabambika kesi kubwa, kuweka mafuvu ya watu waliokufa, miili ya maiti, kuweka silaha na bangi na vitu vingine kama hivyo:-

Naomba Serikali iseme sasa kwamba, wako tayari kuhakikisha Polisi hawaruhusiwi kwenda kupekua nyumba za watu bila kuwepo na Serikali ya eneo lile kwa sababu wanakwenda kuchukua hela kwa Wananchi wale na kuwabambika kesi pale ambapo wanashindwa kuwapa hela wanazohitaji? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la moja la Mheshimiwa Sakaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la upekuzi linafanywa Kisheria na inavyotakiwa upekuzi ufanywe mtu akiwa na kibali cha kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli huo, wakati ambapo panatokea tatizo la haraka, mhalifu amekurupuka akaingia kwenye nyumba ya mtu, haitakuwa rahisi kwanza twende tukamtafute Mkuu wa Kijiji aje ndiyo tuweze kumfuata mhalifu. Hayo ndiyo maeneo ambayo Jeshi la Polisi pengine linafanya kazi bila ya kibali hicho. Lazima

20 JUNI, 2013

niseme kwamba, Jeshi la Polisi au Maaskari wake na Maafisa, hawaruhusiwi kuvunja maadili ambayo yameelekezwa na mara zote yanapotokea haya, basi kanuni zinatumika kuhakikisha kwamba, wanaofanya hivyo wanaadhibiwa. Jeshi hili ni la Wananchi na halina sababu ya kuwaadhibu au kuwadhalilisha.

**SPIKA:** Tuendelee na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Mheshimiwa Betty Machangu atauliza swali hilo.

Na. 435

### **Matatizo Yanayolikabili Bwawa la Nyumba ya Mungu**

**MHE. BETTY E. MACHANGU** aliuliza:-

Maji katika Bwawa la Nyumba ya Mungu yamepungua kwa asilimia 25 kwa sababu mbalimbali kama vile utunzaji hafifu, jumla ya watumishi waliopo kutoka Wilaya tatu zinazozunguka Bwawa ni kumi badala ya 36, hakuna mchango au juhudi za Wizara husika za kudhibiti uvuvi haramu, uvamizi wa wavuvi kutoka nchi jirani ni mkubwa na kikosi cha doria cha uvuvi haramu kina makao yake Tanga:-

(a) Je, Serikali itaongeza lini idadi ya wafanyakazi ili kulinda bwana hilo kutokana na vitendo viovu vya uvuvi haramu na kuelekeza maji ya mito inayoingiza maji katika bwawa kwenye kilimo?

(b) Pamoja na kuwepo kwa Kanuni na Taratibu za Uhamiaji za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki; je, kwa nini Serikali inalifumbia macho suala la ujio wa wavuvi kutoka nchi jirani; na kwa nini wavuvi hao hawaondolewi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimwa Betty Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Bwawa la Nyumba ya Mungu lilijengwa mwaka 1965 hadi 1968 na lina eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 140 na urefu kilometa 37. Bwawa hili linamilikiwa na Halmashauri za Mwanga, Moshi Vijijini na Simanjiro. Wananchi wanaozunguka Bwawa wanajishughulisha na uvuvi, kilimo, ufugaji na biashara. Aina ya samaki wanaopatikana katika Bwawa hili ni pegere, kambale, kuyu, gogogo, ningu na dagaa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Bwawa hili muhimu kwa uvuvi linakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo ongezeko la uvuvi haramu, upungufu wa watumishi na ukosefu wa vitendea kazi, ikiwa ni pamoja na boti za doria, usafiri kufika katika maeneo ya uvuvi na kadhalika. Aidha, watumishi wanaohitajika kusimamia shughuli za uvuvi katika Bwawa la Nyumba ya Mungu kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ni 36, ikilinganishwa na watumishi 11 waliopo sasa, ambao bado ni wachache kuweza kufanya kazi yao kikamilifu. Serikali kupitia Halmashauri nilizoitaja, itaendelea kuajiri watumishi kulingana na upatikanaji wa fedha.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri, ikisimamiwa na Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009, Kifungu cha 13(5), kinasisitiza utoaji wa leseni za uvuvi kwa wavuvi wazawa, ambapo mwaka 2013 leseni 22 zilitolewa na mwaka 2012 leseni 103 zilitolewa kwa Wananchi wazawa. Aidha, Serikali imeimarisha usimamizi katika Bwawa la Nyumba ya Mungu kwa kuanzisha vikundi shirikishi vya usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi (*BMUs*) 20 katika Halmashauri za Mwanga 11, Moshi Vijijini vikundi vitatu na Simanjiro vikundi sita, kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu pamoja na wavuvi wageni kutoka maeneo mbalimbali

ndani ya nchi na nchi jirani. Hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali haiwafumbii macho wavuvi kutoka nchi jirani ambao hawafuati sheria na taratibu za nchi.

Naomba kutoa wito kwa *BMUs*, yaani vikundi vya ulinzi shirikishi na Wananchi wote wanaozunguka Bwawa la Nyumba ya Mungu, kufichua wavuvi wote haramu wakiwemo wageni kutoka nchi jirani, kwa kutoa taarifa kwenye vyombo husika ili sheria iweze kuchukua mkondo wake. Serikali itawachukulia hatua kali za kisheria wale wote watakaobainika kushirikiana na wavuvi wageni toka nchi jirani, kuhujumu uvuvi katika Bwawa la Nyumba ya Mungu.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Siku zote fimbo ya mbali haiwi nyoka; ni lini basi Serikali itahamisha Kikosi hicho cha Doria ya Uvuvi Haramu kutoka Tanga kihamie eneo lolote katika Wilaya hizo tatu kwa ajili ya udhibiti zaidi wa Bwawa hilo?

(ii) Ili kuzuia mmomonyoko wa ardhi katika mapito ya Mto Kikuleta na Mto Kifaru unaopeleka maji katika Bwawa la Nyumba ya Mungu; je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu kwa wakulima wanaoishi maeneo hayo ili walinde mazingira na walime kwa matuta kuzuia udongo mwingi kuingia Bwawani?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Betty Machangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kuhamisha kituo, suala hapa ni upatikanaji wa fedha, tungependa kuwa na vituo vya doria kila mahali ambapo kuna uvuvi, lakini kutokana na ufinyu wa bajeti, Kituo cha Tanga ndicho pia kinasimamia uvuvi katika Bwawa la Nyumba ya Mungu.

20 JUNI, 2013

Kitu muhimu hapa siyo kuwa na vituo vingi, kitu muhimu ni kusimamia Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003, vilevile ni kutoa mafunzo kwa wavuvi pamoja na *BMUs* ambazo zinasimamia ulinzi katika maeneo hayo. Vilevile ni kuhakikisha kwamba, mamlaka zinazohusika, yaani Mamlaka za Halmashauri zinatoa vibali na leseni kwa wazawa, pamoja na watu ambao wanastahili kupata leseni hizo.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake lake la kuhakikisha kwamba tunazuia mmomonyoko wa ardhi, ni dhahili wanaelewa Wananchi na bado tunaendelea kuwaelimisha kwamba, wasilime karibu na kingo za mito pamoja na maziwa. Vilevile wasipeleke mifugo katika maeneo hayo ambayo pia husababisha mmomonyoko wa ardhi na kupunguza maji ambayo yanakwenda kwenye maeneo mbalimbali.

**SPIKA:** Ahsante. Muda umekwisha, tunaenda Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Na. 436

### **Mifereji ya Umwagiliaji Kuanza Kufanya Kazi**

**MHE. YUSUPH A. NASSIR (K.n.y. MHE. STEPHEN H. NGONYANI)** aliuliza:-

Katika Kata ya Mswaha Darajani Kijiji cha Mafuleta na Mswaha Darajani kuna banio za umwagiliaji ambazo zimeshajengwa:-

Je, lini mifereji hiyo itaanza kazi ili Wananchi wapate maeneo ya kulima?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Stephen H. Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Skimu ya Umwagiliaji ya Mafuleta ipo katika Kijiji cha Mafuleta, Kata ya Mswaha katika Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe. Skimu hii ina ukubwa wa takribani hekta 700 zinazofaa kutumika kwa kilimo cha umwagiliaji. Eneo linalomwagiliwa kwa sasa ni hekta 300. Katika kuhakikisha kuwa Skimu ya Mafuleta inakamilika, Serikali kupitia Mradi Shirikishi wa *PADEP*, ilitenga na kutumia jumla ya shilingi milioni 35 kwa kujenga sehemu ya mfereji mkuu wenye urefu wa mita 450 katika Mwaka wa Fedha wa 2007/2008.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, kupitia Mpango wa Maendeleo ya Kilimo Wilayani (*DADPs*), imetenga kiasi cha shilingi milioni 203 kukamilisha mnyororo wa thamani. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 180 zitatumika kupima eneo la shamba, kufanya usanifu wa mradi na kujenga banio la kudumu; na shilingi milioni 23 zitatumika kujenga ghala na kununua mashine ya kukoboa mpunga kwa lengo la kukamilisha mnyororo wa thamani wa Zao la Mpunga. Aidha, baadhi ya wakulima wanaendelea na kilimo cha umwagiliaji katika Skimu hii kwa kutumia miundombinu ya asili ambapo kaya takribani 450 za Kijiji cha Mafuleta zinanufaika na Skimu hiyo kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, eneo lote la Skimu ya Mafuleta lenye jumla ya hekta 700, litaweza kumwagilia mara baada ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji unaotarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2013.

Mheshimiwa Spika, wakati nikijibu Swali Na. 288 la Mheshimiwa Ngonyani, mnamo tarehe 28 Mei, 2013, nilitoa maelezo ya kuwa mchakato wa ujenzi wa Skimu ya Mswaha Darajani unaendelea na unatarajiwa kufunguliwa mwezi Agosti, 2013 baada ya kukamilika kwa ujenzi ambao umegharimu shilingi milioni 46 ambazo zimegharimiwa na Mradi wa *PADEP* na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe.

Aidha, Ofisi ya Umwagiliaji Kanda ya Kaskazini imepewa kazi mahususi ya kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Miradi hii ambayo imeshafikia hatua za mwisho kama huo wa Mswaha Darajani na Mafuleta ili kuhakikisha kuwa hakuna ucheleweshaji usio wa lazima.

**MHE. YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Ukiangalia kutoka mwaka 2007/2008 mpaka leo 2013 ni muda mrefu sana; na hii inatokana aidha na kusuasua kwa ufuatiliaji kutoka Ofisi ya Kanda au Wizara kutokupeleka fedha hizi kwa wakati. Nini kauli ya Serikali?

(ii) Kwa kuwa matatizo yaliyopo Skimu ya Mafuleta yanaendana sambamba na Skimu ya Kwamsisi; je, Serikali inawaambia nini Wananchi wa Jimbo la Korogwe Mjini pamoja na Korogwe Vijijini? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhusu kusuasua, nipende tu kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, siyo kwamba tunasuasua, ni kwamba, upatikanaji wa fedha ndiyo hasa chanzo cha kusuasua huko. Kwa kadiri fedha zilivyokuwa zikipatikana, Serikali imeendelea kutekeleza Skimu hii na sasa hivi ipo katika hatua ya kukamilika, kama nilivyosema, kufikia mwezi Oktoba, 2013.

Kuhusu Skimu ya Kwamsisi, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge, kama ambavyo Skimu niliyoitaja mwanzoni ilivyotekelezwa, wakae Halmashauri ya Mji wa Korogwe, watengeneze mpango wa kilimo halafu wawasilishe ombi lao katika Wizara yangu ili tuweze kulifanyia kazi.

20 JUNI, 2013

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha, tena tumepitiliza kidogo.

Sasa naomba niwatambue wageni ambao wapo katika nafasi ya Spika pale; yupo Mheshimiwa Prof. Ibrahim Haruna Lipumba, Mwenyekiti wa *CUF*. Karibu sana Mheshimiwa. Ameambatana na Mheshimiwa Salim Dimani, ambaye ni Kaimu Naibu Katibu Mkuu wa *CUF* na Mkurugenzi wa Haki za Binadamu. Ahsante, karibuni sana, naona mmekuja kuleta matunda ya kazi yenu. (*Makofi*)

Nina wageni wengine; wapo Wazazi wa Ndugu John Joel, walikuja kwenye shughuli ya Ushemasi wa mtoto wao kutoka Bukoba. Wazee naomba msimame hapo mlipo taratibu tu. Ahsante sana. (*Makofi*)

Matangazo mengine ya kazi; Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Khamis Kigwangalla, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 7.15 mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi Na. 219.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 7.15 mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi Na. 219; haiwezekani, mkakubaliane ukumbi, *unless* mna *joint venture* au mpo pamoja, mtajua wenyewe, mtapambana wenyewe huko huko, Kamati zinahusiana.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa Jarome Bwanausi, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 7.15 watakuwa na mkutano wao Chumba Na. 227.

Ofisi inaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba, kesho tarehe 21, kutakuwa na tafrija ya kumpongeza Mheshimiwa Samuel John Sitta (Spika Mstaafu), mara tu baada ya kuahirishwa Bunge jioni kwenye eneo la maegesho ya magari. Kwa hiyo, naomba



20 JUNI, 2013

Waheshimiwa Wabunge wote mjitahidi kuwepo kesho na wenzenu wengine muwaambie. *(Makofi)*

Pia, mimi mwenyewe hapa nina tangazo; napenda kuwafahamisha kuwa, wiki ijayo kutakuwa na uchaguzi wa Wajumbe wawili; Mbunge Mwanamume na Mwanamke wa Baraza la Chuo Kikuu cha Mzumbe. Hivyo, Wabunge wanaopenda kugombea nafasi hizo, watachukua fomu za maombi kwa Katibu wa Bunge na zinaanza kutolewa leo, tarehe 20. Mwisho wa kujereshia hizo fomu ni tarehe 25, saa kumi jioni na uchaguzi utafanyika tarehe 26.

Kwa hiyo, Wajumbe wawili; Mbunge Mwanamke na Mwanamume, wachukue fomu leo kama wanataka, warudishe tarehe 25, saa kumi na uchaguzi tutafanya tarehe 26. Kwa hiyo, mnakaribishwa.

Katibu, hatua inayofuata!

## HOJA ZA SERIKALI

### **Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2012 na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Nitawataja watakaochangia; Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar, Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Moza Abeid Saidy, Mheshimiwa Josephine Genzabuke na Mheshimiwa Mansoor Hiran. Mchangiaji wetu wa kwanza siku ya leo atakuwa Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar na Mheshimiwa Mariam Nassor Kisangi, ajiandae.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza, sina budi kuwapongeza Kamati ya Bajeti, pia nikupongeze na wewe mwenyewe ambaye umebuni mbinu ya kuiunda hii Kamati ya Bunge inayoshughulikia Bajeti,

20 JUNI, 2013

ambayo kazi nzuri iliyofanya hadi leo kila Mbunge ana hamu ya kusimama kuichangia Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, mimi nina machache ya kuzungumza, kwani Wabunge wenzangu wengi tayari wamezungumza mengi na mazito ambayo yanataka kufanyiwa kazi na hata mimi haya yangu machache nitaomba yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ningezungumzia kuhusu suala la *PAYE (Pay As You Earn)*, ugawaji wake ningependa Mheshimiwa Waziri wa Fedha aniambie ukoje, kwa sababu fedha hizi zinachangwa na Wafanyakazi wa Muungano, wa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani. Najua mchakato wake tayari ulikuwa umeanza katika ugawaji, lakini ulikuwa unagawiwa kwamba zigawiwe ziende, lakini zilikuwa hazijafanyiwa uchambuzi, kipi kinatakiwa kiende Zanzibar na kipi kibakie Tanzania Bara. Ninajua Wizara hizi mbili tayari zimekaa, Wizara ya Fedha na Bara walikuwa wamo katika mchakato wa kutazama idadi ya Wafanyakazi wa Muungano waliokuwepo Zanzibar, ambao wanakatwa ili kiwango gani kitaweza kufikiwa waweze kukatwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba tujue huu mchakato umefikia wapi na hizo fedha zinazokatwa ni kiasi gani na zinakatwa kwa kutumia hesabu au mbinu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ninataka kuzungumzia msamaha wa mapato. Msamaha wa mapato wanaofaidika ni wafanyabiashara wakubwa, kwa sababu wao ndiyo wanaopata nafasi ya kuagizia vitu nje na wakaweza kubuni mbinu za kusamehewa. Ninajiuliza; mkulima uliyeko kijijini ananufaika nini katika msamaha wa mapato? Mtanijibu kwamba, anafaidika anapata pembejeo kwa bei ya chini, lakini mimi ninakataa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, anayefaidika bado ni mfanyabiashara, ambaye anaagizia pembejeo ziende kwa mkulima. Hata bei anapanga yeye za kwenda kwa mkulima. Sasa kweli mkulima anafaidika? Hajafaidika.

20 JUNI, 2013

Ushauri ninaoutoa ni kwamba, kuhusu pembejeo za kilimo muwe mnanunua wenyewe Serikali. Serikali ibuni mbinu kama maduka au ibuni njia yoyote, wahakikishe kwamba, wao wenyewe Serikali wanawauzia pembejeo wakulima siyo mfanyabishara aagize halafu akamuuzie mkulima. Bado hujamsaidia mkulima aliyeko kijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia suala la bodaboda. Wanaoendesha bodaboda ni vijana wetu, wengi ni vijana hukuti watu wazima. Hata hao wanaobebwa wengi wao ni vijana, hukuti kapakiwa mtu mzima. Ninaomba kungelikuwa na elimu ya kutosha wakapewa vijana wetu, unajua tunazungumza kwamba ujana ni *ujahir*, lolote unaweza kutenda na ndiyo maana wakawa wanafanya vitu bila kuogopa. Wanajua kifo kipo lakini wanasema kufa kazini. Kama utampa elimu atakuwa mwoga na utamwezesha atii sheria siyo kwa kushurutishwa, atii sheria kwa mujibu wa Katiba ya nchi inavyozungumza. Bado ninaiomba Wizara yako ushirikiane na Vyombo vya Sheria kutoa elimu. Unaweza ukamkuta mwenye bodaboda, akakukata kushoto akaja akakukalia kulia, akarejea tena kushoto, yote ni kwa sababu hana elimu. Kufa anajua, lakini elimu ya kutosha vipi yeye aendelee na vile vyombo vyake wanakuwa hawana. Ninaomba Mheshimiwa tukazanie sheria, ambayo wazee wetu walikuwa wakiizungumza sheria, basi sheria iendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Manaibu wake, pamoja na Watendaji wao, kwa sababu elimu waliyoitoa hapa ya Bajeti walivyotuletea mimi ninawapongeza. Wizara zimekaa zimezungumzia Bajeti zao na Wabunge wakaona matatizo ya Wizara hizo. Kwa ujumla na kwa pamoja, tukaomba ziongezwe hela kwa ajili ya Wizara zao; kwa mfano, Wizara ya Maji, Umeme, Kilimo, Vijana, Wanawake, Afya na vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi hii Mheshimiwa Waziri ameifanya kwa dhati, kwa umakini na kwa uweledi, ndiyo

20 JUNI, 2013

maana hivi leo kila anayeinuka lazima pongezi anakupa jinsi ya kuendelea na utendaji na ufanyaji kazi katika Wizara hiyo ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machche, ninaunga mkono hoja na tutazidi kuendelea katika majukumu yetu ya kila siku. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika Bajeti hii ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda nikupongeze. Ninasema hivi; mnyonge mnyongeni, lakini haki yake mpeni. Lazima tukupe pongezi, umefanya maamuzi magumu na umetengeneza historia katika Bunge letu la Tanzania, katika kuweka mpango mzuri wa Bajeti ya Tanzania. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu kwenye Bajeti hii ya Serikali, nitasimama katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza kabisa, katika vyanzo vya mapato, madhara ya ongezeko la kodi, madeni ya walimu, punguzo la kodi kwa wafanyakazi, changamoto kwa TRA, katika kuleta mapato na kupunguza rushwa.

Mheshimiwa Spika, ninaanza na mada yangu ya kwanza, inayohusu vyanzo vya mapato. Katika Bunge hili ninarudia tena kusema, jamani, tumekuwa tukirudiarudia katika kuongeza bei za vinywaji mbalimbali. Kweli tunahitaji kodi, kuna vinywaji ambavyo siyo lazima katika maisha ya binadamu, hivyo ni lazima ziongezwe na ninakubalina navyo, lakini kuna vinywaji vingine vina umuhimu wa aina yake.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Dar es Salaam kuna wimbi la wanafunzi. Ninarudia tena kusema, wanaishi kwa *Azam Cola* na kipande cha muhogo. Kwa maana hiyo, wanapongezewa bei ya vinywaji hivi ambavyo

havina madhara, kwao wao ni tatizo kulingana na kipato chao. Hawana chakula, chakula chao ni mihogo au *chips* dume na *Azam Cola*, yeye inamsaidia sana. Tunapowapandishia hizi bei, wao wanaathirika.

**SPIKA:** Wenzio hatujui hivyo vyote ulivyovisema. Wakina *naniam-cola* na *chips* dume ni vitu gani hivyo wanavyotakiwa kula?

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mihogo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba niishukuru Serikali kwa kutokuongeza bei ya maji, kwa sababu maji pia ni tatizo kwa vijana wetu waliopo mashuleni. Kwa kuliona hilo, ninaipongeza sana Serikali yangu na ninaomba suala la maji liendelee kuwa hivyo hivyo, kwani maji ni uhai wa binadamu. Watoto hao pia pamoja na kupata hivyo vitafunwa wanaongezea na maji. Kwa hiyo, Serikali kwa kutokupandisha bei ya maji, mimi ninaipongeza na ninaishukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali yangu sasa iangalie vyanzo vipya vya mapato. Tuna vyanzo vingi sana vya mapato. Vingi vimeshazungumzwa na wengine, lakini tuangalie katika viwanda vyetu, kuna utitiri wa viwanda, kuna bidhaa zinazalishwa mle; je, *TRA* wanakagua hizi bidhaa kwa uhakika na kupata kodi?

Viwanda vimekuwa vingi, eneo la Mbagala kuna utitiri wa viwanda vipya na *Bonded Warehousing* mpya. Hivi *TRA* kweli wanasimamia vizuri maeneo haya? Tunaomba waangalie, tunaweza tukapata chochote huko kwa maendeleo ya Taifa. Viwanda vile vinapojengwa kuna kodi nyingi zinachukuliwa; kuna kodi za majengo, kuna kodi za uendelezaji na kuna kodi mbalimbali. Ninataka *TRA* wanieleze; je, tuna mabadiliko kwa sababu sisi Wana-Dar es Salaam na Wakazi wa Mbagala tunaona kuna mabadiliko makubwa? Viwanda vingi na mambo mengi yanafanyika pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa niingie kwenye masuala ya walimu na madeni yao. Haya madeni ya walimu yamekuwa ni tatizo, kila siku wanatengenezewa madeni mapya. Hii Serikali itadaiwa mpaka lini? Naomba Serikali isimame katika madeni ya walimu, kwa sababu mwalimu anakwenda likizo hapewi fedha zake za likizo kwa wakati, anaomba likizo mwaka huu hapewi anakuja analimbikiza na likizo ya mwakani. Matokeo yake, ndiyo pale kila siku Serikali inadaiwa madeni ya walimu na wafanyakazi wengine pia wa Serikali. Naomba Serikali waangalie na hasa Wakurugenzi, waangalie jinsi gani ya kushughulikia malipo ya walimu yafanyike kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, walimu wana matatizo makubwa, kwa hiyo, wanapolipwa fedha zao kwa wakati na wao inawatia moyo ili waende kufanya kazi zao vizuri.

Eneo lingine ambalo Serikali inafanya kazi nzuri ya kuendeleza maendeleo ni afya. Inapeleka fedha kwenye Wizara ya Afya na kwenye Hospitali mbalimbali, lakini dawa zile zinachangiwa na wagonjwa. Je, haya maduhuli ya Serikali yanakusanywa vizuri na kama yanakusanywa vizuri kwa nini hakuna maendeleo?

Mheshimwia Spika, ninasema hivi kwa sababu *ampicilline* inauzwa Sh.1800 kwenye Hospitali ya Serikali na inauzwa Sh.1,800 mpaka Sh. 2,000 kwenye Hospitali ya *Private*; mbona wenzetu wa *Private* wanaendelea na wakati wale wanafanya biashara na sisi huku kwenye Serikali kila siku unakuta changamoto ziko pale pale? Hili suala liangaliwe, tunatoa pesa nyingi Serikalini kupeleka kule; je, kule zinakusanywa vizuri? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama zinakusanywa vizuri zingelikuwa zinarudishwa, mimi nina imani kubwa, *MSD* na mambo mengine, tusingelikuwa na madeni, kwa sababu hizi fedha na hizi dawa zinauzwa kibiashara, hazizwi kwa punguzo. (*Makofi*)

20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nizungumzie masuala ya punguzo la kodi kwa wafanyakazi. Wafanyakazi walio wengi matarajio yao hayakuwa kupunguziwa kodi kwa asilimia moja. Ninatambua umuhimu wa kodi kwa maendeleo, lakini Serikali iangalie angalau tuwapunguzie kwa asilimia tatu mpaka tano. Pia tutafute njia ya kufidia hiyo asilimia tatu mpaka tano katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, natambua kodi ni maendeleo, lakini pia na wao matarajio ya wengi hayakuwa asilimia moja. Ninatambua mwenye mshahara mkubwa atatoa nyingi na mwenye mshahara mdogo atatoa kidogo, lakini hata kidogo kwa mwenye mshahara mdogo, bado kitamfanya yeye ajisikie kwamba angalau Serikali yake imemwona katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe mchango mwingine kuhusiana na *TRA*, katika changamoto za kukusanya mapato kwenye *depot* za mafuta. Nina-*declare interest*, mimi ni mjasiriamali katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, *TRA* inaweka mtu wake kwenye *depot*, hivi mtu yule wamemlisha *yamini* gani; wana uhakika kazi anayoifanya kule ndani ni sahihi? Ninaomba *TRA*, iangalie hivi yule yuko kwa maendeleo ya Taifa au yuko kwa ajili ya maendeleo yake na familia yake. Ninataka kuelewa hilo.

Niseme lingine kwamba; hizi *depot* za mafuta na *Bonded Warehouses*, unapomuweka mtu wa *TRA*, anashika ufunguo kama mali yake; hivi kweli huyu mtu anatenda haki kwa Serikali hii? Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma hivi inawaangalia hawa wanaopewa funguo na wanawasoma huko ndani wakoje? Ninaiomba Serikali ili iangalie suala hili kwa umakini wa kipekee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaomba tozo nyingine kama kuna uwezekano, hii ya Wafanyakazi wapunguziwe. Tozo ya kwenye simu ninaafiki na ikiwezekana angalau kidogo ili watu waache matumizi mabaya ya simu. Simu hizi

zinatumika vibaya hasa kwa vijana wetu, kutwa wana-*chat* tu hata havielewiki wanavyovifanya. Wao michezo yao ni kwenye simu tu, watatufilisi. Mtu akikosa hela ya simu na afadhali akose chakula. Tanzania tumepokea vibaya simu za mikononi.

Mheshimiwa Spika, ile kodi ya simu hizi ikichukuliwa angalau ikafidia pale, wafanyakazi wakapunguziwa kidogo, ingelisaidia sana maana tunapunguziwa na sisi mama zao ule mizigo na wao waweze kuona kwamba sasa simu hazitumiki hovy hovy.

Mheshimiwa Spika, simu ni tatizo na hata wale watu wanaotumia simu kwa kuwatishia wenzao kwa kuwapa lugha mbaya mbaya, sasa watapunguza kwa sababu gharama yake itakuwa kubwa kidogo. Ninaomba nieleweke kwamba, ninatambua kuna wanaotumia vizuri kwenye *computer* zao, lakini kuna wengine wanatumia vibaya na hiyo ninaomba nitoe kama changamoto kwa vijana wetu; hebu someni kwanza, achaneni na hayo mambo, mtayakuta hayaishi, hayo ni ya dunia tu, yanakwenda yanapita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninatambua mengi yamechangiwa na wenzangu na sina sababu ya kuyarudia. Ninarudia tena kusema kuwa, ninaunga mkono hoja, ninakupongeza wewe na ninawapongeza Wananchi wa Kata ya Mianzini, kwa kufanya uamuzi wa busara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nawashukuru wote ambao walishiriki kuandaa Bajeti hii. Bajeti hii kama tukiifuata ilivyokaa, inaweza ikakidhi mahitaji ya Watanzania. Naiomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, ihakikishe kile ambacho Wabunge wameshauri, kiweze kufanyiwa kazi. (*Makofi*)



20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, kama yale yote ambayo Wabunge wameishauri Serikali yataishia hapa Bungeni, hakuna kitu kitakachokuwa kimefanyiwa kazi. Ninawaomba sana, Serikali ielekeze nguvu sana hasa kwenye umeme wa vijijini. Eneo hili ni muhimu sana, litakuza uchumi wa nchi hii kwa karibu uwiano ulio sawa. Taifa hili linategemea kodi kwenye maeneo machache tu ya vileo na vinywaji baridi na sigara. Wakati huo huo Serikali za nchi mbalimbali zinapiga vita sana hasa matumizi ya tumbaku na zinapinga watu wasilewe sana. Sasa endapo watu hawa wataacha kutumia vileo na kuvuta sigara; kodi tutaipata wapi? Nilikuwa ninaishauri Serikalii ihakikishe inaongeza kutafuta vyanzo vya mapato vitakavyoisaidia nchi hii kuweza kukuza uchumi wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, mwaka huu tumepata bahati eneo la Mpanda kutengewa baadhi ya vijiji kupewa umeme vijijini. Sasa isije ikaishia kuonekana kwenye vitabu. Ninaomba sana eneo la Vijiji vya Kabungu, kwenye Kata ya Mpanda Ndogo na Vijiji vya Ifukutwa, vipatiwe umeme kwenye Shule ya Sekondari ya Kabungu, Shule ya Sekondari ya Mpanda Ndogo na Shule ya Sekondari mpya ya Seminari inayojengwa pale eneo la Mpanda Ndogo, zipatiwe umeme mpaka Vijiji vya Majalila.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo litakuza uchumi, kwenye Jimbo langu la Mpanda Vijijini ni kupeleka umeme maeneo ya Ukanda wa Ziwa Tanganyika. Ukanda huu katika Tarafa ya Karema, Vijiji vya Karema, Ikola, Kapalamsenga na Isengule, tukiwawezesha wakapata umeme, Wananchi hawa watakuwa wamepunguza umaskini, watatumia rasilimali ya Ziwa Tanganyika kuweza kuuondoa umaskini, kwa sababu wataweza kusindika samaki na kusafirisha katika maeneo mbalimbali na kuwavutia wawekezaji kwa kuwekeza kwenye viwanda vya kusindika samaki kwenye meneo hayo. Naiomba Serikali yangu ihakikishe Miradi hii inatiliwa mkazo ili iweze kuwasaidia Wananchi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kilimo. Nchi yetu inategemea sana Sekta ya Kilimo. Ili tuweze kuwawezesha Wakulima wa nchi hii ni lazima tuwajengee mazingira ya kuwajengea misingi ya uzalishaji. Hawawezi kuzalisha wakulima kama hawajawezeshwa hasa kwenye pembejeo. Mbolea ni kiungo muhimu sana kwa mkulima ili aweze kuzalisha kwa tija. Naiomba Serikali ihakikishe inapeleka pembejeo kwa wakati mwafaka na ziwe za kutosha. Wakulima walio wengi hawapati pembejeo na ndiyo maana kila siku kunakuwa kuna matatizo ya njaa. Sasa ni wakati mwafaka Serikali kuwapelekea pembejeo wakulima kwa muda unaostahili na tuzipeleke kwa udhibiti wa Serikali, kwani pembejeo nyingi zinazopelekwa zinaishia kwa watu wachache.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali yangu kuhakikisha inawajengea wakulima viwanda ili waweze kusindika mazao yao. Kama tutakuwa tumewawezesha vizuri, tukaandaa viwanda vikawa vinasindika pamba, vikasindika mafuta ya alizeti, vikasindika mazao ya biashara kama vile zao la tumbaku na kuwajengea kiwanda katika maeneo ya Mkoa wa Tabora, ambao utasaidia kukuza uchumi kwa wakulima hawa wa Zao la Tumbaku. *(Makofi)*

Nchi nyingine ambazo zimefanya vizuri katika maeneo haya ya viwanda, zimepiga hatua kubwa sana. Zimewasaidia pia wakulima wao waweze kufanya shughuli zao vizuri na kuwapa tija kwa kupata bei nzuri za mazao wanayozalisha. Sisi hapa viwanda vyetu vya kusindika tumbaku ni vya makampuni ambavyo haviwasaidii wakulima kwa kiwango kinachostahili. Leo hii ukienda nchi nyingine za jirani ambao wameshiriki vizuri na Serikali ikawekeza, imewasaidia sana wakulima wao; mfano ni nchi ya Zambia, Malawi na Zimbabwe, ambapo Zao la Tumbaku lina bei kubwa sana. Kiwango cha ununuzi ni karibu dola sita, wananunua kwa bei iliyo nzuri kuliko hapa Tanzania, ambapo tunauza tumbaku iliyo mbichi kwa dola mbili kwa wastani. Naiomba sana Serikali ihakikishe inaboresha masoko ili iweze kuwasaidia wakulima wetu.

Eneo lingine, naiomba Serikali ihakikishe inaboresha suala la elimu. Jimboni kwangu Mpanda Vijijini tuna matatizo makubwa sana ya elimu hasa katika shule za sekondari ambazo hazina walimu. Huwezi kuendesha Taifa ambalo halina wasomi, kwa sababu Wananchi wengi wanaosoma hasa watoto wetu wanaosoma katika shule ambazo hazina walimu, mategemeo yake makubwa sana ni kuzalisha *zero* nyingi ambazo tunazipigia kelele kila siku. Tunaomba walimu wapelekwe katika Shule ya Sekondari ya Karema, Shule ya Sekondari ya Ikola, Shule ya Sekondari ya Kabungu, Shule ya Sekondari ya Mwese, Katuma na Mishamo. Maeneo haya hayana walimu, kuna shule nyingine zina walimu wawili tu; tunategemea nini watakachokivuna wanafunzi hawa? Zaidi ni kupata sifuri tu! Naomba katika bajeti hii, tuhakikishe tumepeleka upendeleo maalum kwenye maeneo ambayo hakuna walimu wa kutosha basi tuwapeleke waweze kwenda kufundisha watoto wetu. (*Makofi*)

Eneo lingine ni Jeshi la Polisi. Jeshi la Polisi limeachwa nyuma sana. Polisi wengi wanafanya kazi katika mazingira ambayo siyo salama na wanakatishwa tamaa sana. Nina kituo kimoja cha Polisi kipo Mwese, hakina hata ofisi ya kufanyia kazi. Eneo hili hakuna hata jengo la kuhifadhi silaha. Naomba Serikali katika bajeti hii iwapelekee Kituo cha Polisi, kijengwe pale Mwese sambamba na Kituo cha Polisi kilichopo Karema. Tunaomba Serikali iwaangalie Polisi hawa, iwaongezee mishahara na kuangalia mazingira wanayofanyia kazi kwani siyo mazuri.

Mwisho, naiomba Serikali, tuna Kituo cha Jeshi la Ulinzi kilichopo katika Kata ya Ikola, Mwambao wa Ziwa Tanganyika mpakani. Kituo hiki hakina mazingira mazuri, hakina gari la usafiri ulio mzuri na ukiangalia maeneo yale siyo salama. Tunaomba Serikali iwaangalie sana Wanajeshi wanaofanya kazi katika kile kituo. Ukweli ukifika, ukiangalia mazingira yao wanayofanyia kazi, inasikitisha sana. Naiomba Serikali yangu ihakikishe inajenga mazingira ambayo yatawasaidia watumishi hawa wawe na moyo wa kufanya kazi wa kujituma kwa kulinda Taifa letu. Eneo lile ni la mpakani, ambalo hata boti tu za kufanyia doria hawana,

20 JUNI, 2013

ni vyema Serikali ikaangalia mazingira ya kuboresha kituo hicho. Katika bajeti hii watenge fedha ambazo zitasaidia kuwanunulia gari na kupata boti ya kufanya doria katika maeneo ya ukanda mzima wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante na sasa nimwite Mheshimiwa Moza Saidu!

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi na mimi ya kuchangia Bajeti hii.

Kimtazamo, nikiangalia bajeti bado ina mtazamo tofauti wa upande mmoja wa ukuaji wa uchumi, ni upande mmoja tu wa Serikali. Nikitazama upande wa pili, ambao unamgusa Mwananchi na hasa wa kijijini, bado inakuwa ni tegemezi na ni mzigo mkubwa kwa Serikali. Ninapozungumza hivyo nina maana kwamba, katika nchi yetu tunayo makundi na katika makundi hayo, tuna wafanyakazi, wakulima na walemavu ambayo tunayajumlisha na ya wazee.

Sasa ukisema uchumi umekua wakati bado Wananchi wako wanalalamika na wanasema kwamba hali ya maisha ni ngumu, nini tatizo? Tukiangalia bajeti jinsi ilivyokaa ni kweli kwa mtazamo ni nzuri, inastahili na ina uwezekano mkubwa wa kugawana uwiano wa kila sehemu upate kile ambacho kinaweza kuhitajika. Tukilinganisha utofauti unakuja kwamba, Mwananchi wa kawaida anakuwa ana tatizo kubwa sana la kuweza kupata kipato kwa maisha yake ili kuweza kujikimu yeye mwenyewe. Tukiangalia bei ya mafuta ilivyopanda, mafuta yanapopanda ndiyo usafiri unavyokuwa una gharama kubwa. Unapohitaji kubeba mazao yako kuyapeleka sokoni inabidi utumie gharama ya gari, gari linahitaji mafuta kutokana na umbali uliokuwepo, mfumko wa bei unazidi kupanda.

20 JUNI, 2013

Leo hii tunasema tumemwongezea mshahara mfanyakazi, lakini mshahara huu bado tutauongeza mpaka uzidi kuwa makapu na makapu iwapo mfumko wa bei hautarekebisha. Nchi yetu itakuwa bado ina tatizo la kulalamikiwa, bado Serikali itakuwa inalaulamiwa na bado tatizo ni hilo ambalo linaweza kujitokeza.

Nikiangalia upande wa tozo *TRA*, kwa kweli upande wa madini wanavyotoza ushuru ule ni mdogo mno. Ushuru ule unatakiwa uongezwe kwa sababu wale ndiyo wanaobeba mchanga, wanaharibu barabara zetu, wanachimba madini na wanachukua mpaka na udongo, lakini bado ushuru ule unakuwa mdogo. Sasa ninaomba Serikali ielekeze sehemu ambazo zinaharibu uchumi wa nchi hii na ndiyo zinazoharibu hata sura ya nchi, ina maana mtakapoachiwa mashimo, sura ya nchi imekuwa mbaya. Tunaachiwa majanga bila kuwa na faida, kizazi kijacho kitakachokuja kitakuta sura hii imeshazeeke.

Sasa tuangalie ajira zetu kwa vijana, kweli Serikali ajira kwa vijana imeongeza, hiyo milioni mbili ukiiangalia kwa matamshi tu ni nyingi sana, lakini bado haitoi uwiano kwa vijana wetu wa vijijini. Bado tukisema vijana wajari wenyewe, bodaboda zimejaa, kweli ushuru huo umetolewa lakini bodaboda zile ni za watu. Changamoto kubwa inayowakuta vijana wetu na hizi bodaboda, adha kubwa wamezipokea, bodaboda zimezagaa kwa wingi lakini matumizi yake inavyoonekana ni mabaya; wengi wanapoteza maisha, wengi wanatekwa wanakwenda kuuawa na pikipiki zinabebwa. Bado tukisema kwamba kuna ajira, basi ajira hii haina tegemezi zaidi ya kuangalia vijana wengi wanapoteza pia viungo vyao na wengi hawajui, hawana taaluma hizo. Ninaomba kitengo hicho nacho kingezidi kuongezewa fedha ili kiweze kutatua tatizo la ajira kwa vijana waweze kupata ajira nyingi zilizopo.

Nikija kwenye suala la afya, suala la afya tukiliangalia ni kweli tumeipigia kelele sana sekta hii na imeweza kuongezewa fedha, lakini bado haikidhi mahitaji. Wauguzi wengi vijijini hawana nyumba, sehemu nyingi hazina nyumba

za zahanati. Nikitoa mfano mdogo tu, juzi tulikuwa katika Kata ya Dalai kwenye uchaguzi ule, nilichokigundua ni kwamba, akina mama wamekuja kupimwa kliniki, watoto wananing'inizwa chini ya mti. Akina mama wanapimwa chini, kama mama hakwenda na kitanda chake basi anandatika nguo yake anapimwa pale chini. Je, bado tupo kwenye Serikali inayokwenda na mfumo wa kisasa au tunarudi nyuma? Naomba Serikali iangalie vitu kama hivi.

Pia, dawa zinakuwa ni haba mno katika maeneo mengi, inalalamikiwa karibu Tanzania nzima. Dawa zinaonekana kwenye *dispensary* tu, lakini siyo hospitalini kama ilivyo na hela za mgawo zinakwenda, lakini huenda ikawa fedha hizi pengine hazitoshelezi. Lazima tuangalie kwa bajeti ijayo iendelee kuongezwa.

Nikija katika suala la maji, maji imekuwa ni tatizo katika nchi nzima ya Tanzania na wagawaji wa maji wanapotoa michango yao ya maji kwamba wagawe visima hivi viende wapi na hivi viende wapi, wao wanaangalia uwiano wa Wananchi waliokuwa wengi. Ukitaka kutazama kwa mtazamo, Wilaya ya Kondoa Kaskazini ni Wilaya ambayo ina watu wengi na ina sehemu nyingi na ina mahitaji makubwa ya maji, lakini ndiyo kwanza inapewa visima vichache mno, haiangaliwi na inakuwa iko nyuma kwa kila kitu. Juzi tu tumeangalia hata uwiano wa ugawaji wa mawasiliano, umekuwa ni mdogo, Wilaya inaachwa nyuma na ina watu wengi na ina mahitaji mengi. Sasa lini Serikali itakuwa inaangalia sehemu ambazo zina mahitaji ambayo hayajafikiwa kwa wingi iweze kuongezewa au kupunguziwa kutokana na wingi wake wa watu.

Nikija kwenye Sekta za Mahakama, Mahakama zetu ni kweli zinafanya kazi kutegemeana na maeneo, lakini katika maeneo yetu hakuna maeneo mengi yaliyojengwa ya Mahakama. Mahakama nyingi zinakuwa zinategemea Ofisi za Watendaji wa Kata hasa huko vijijini na ukiangalia hii yote ni bajeti ndogo. Sasa kama bajeti ni ndogo haitoshelezi basi angalau tuwe tunaangalia zile bajeti ambazo siyo za muhimu zaidi tukapelekea kwenye sekta

muhimu ambazo zinaweza kutoa haki kwa uwiano uliokuwa sawa kwa wote.

Mheshimiwa Spika, nije katika nyumba za walimu, kwa kweli kama tunahitaji elimu bora, Sekta ya Elimu pia imelalamikiwa sana na nashukuru kiwango mlichokiongeza, lakini bado na kipindi kijacho kiendeleo kuongezwa ili sekta hii ya elimu iweze kujenga nyumba za walimu karibu na maeneo ya shule. Shule ziweze kujengwa karibu na makazi ya Wananchi siyo kujengwa kilomita moja mpaka kumi, mtoto wa kike anatembea mpaka kule, anakutana na matatizo mengi. Hii tumeona katika shule moja ambayo iko Dalai, watoto wanatoka Kitongoji cha Mtitiri wanakwenda kusoma Dalai, ni mbali mno mtoto kutembea hivyo, aweze kupata gari ambalo ni mabasi, wakiomba *lift* wanakataliwa, wanaambiwa labda wachangie nauli na nauli hawana, kama ni watoto wa kike basi wanajiingiza kwenye ambayo siyo sahihi.

Sasa ili Serikali iweze kuangalia vitu kama hivyo na shule nyingi mpaka sasa hivi hazina madawati, watoto wanakaa chini, wanaweka mawe ndiyo wanakalia. Tembeleeni katika Wilaya nzima ya Kondoa, Kondoa Chemba na Kondoa Kaskazini, hebu tuangalie sekta hii ya elimu, ndicho chanzo kikubwa ambacho sasa hivi kinatuongezea sisi katika Wilaya yetu hata kuongezeka kwa kuanguka kwa kiwango hicho. Mwalimu anatoka mbali, anakaa Kondoa Mjini anakwenda kufundisha Tumbelo, Tumbelo ni mbali sana au anakaa Kondoa Mjini anakwenda kufundisha sehemu inaitwa Nkuku, ni mbali sana na maeneo yake. Sasa vitu kama hivi tviangalie ili kuyaongezea bajeti maeneo husika waweze kupata kila mtu uwiano uliokuwa mzuri.

Polisi tukiwaangalia ndiyo wanaolinda mali za raia na wanatulinda Wananchi na sasa hivi tumesikia kwamba, wakikataa kulinda ndiyo hivyo tena au inavyokuwa Serikali inavyoamrisha ndiyo itakavyokuwa. Mimi sipo huko sana, nataka kuzungumzia kwamba, hawa ndiyo walinzi wetu katika nchi yetu wanaolinda mali zetu na mali za raia kwa

20 JUNI, 2013

ujumla. Sasa ni kwa nini hawa Polisi ukitaka kuangalia wanavijenga vijumba vyao wenyewe wanajiunganishia mpaka na umeme, hata hapa Dodoma Mjini ipo hiyo. Vile vijumba siyo sahihi, ni aibu kubwa kuona hasa hapa ndiyo Makao Makuu ya Nchi, unapokwenda unakuta hakuna ujenzi wowote wa nyumba za wafanyakazi karibu na maeneo yao, wanakaa uraiani wanajiunganishia umeme. Umeme ukilipuka ukiwaka halafu utuambie Wabunge tukatoe pole kule. Sasa hii kweli siyo haki, mimi sikubaliani na hilo na siku ikitokea hivyo sitakubaliana na Serikali kwa sababu Serikali ndiyo inayogawa mgawo huu, naomba hili liangaliwe ili askari wale waweze kupatiwa nyumba na wapewe nyumba kwa uwiano.

Mheshimiwa Spika, sasa nitoke huko niingie kwenye kilevi. Bajeti hii nikiangalia kwenye suala la vinywaji, kweli vimepanda bei na ninaomba vipande bei zaidi ya hapo, kwa sababu ndivyo vinavyoathiri hata vijana wetu. Hatutakuwa na Taifa la kesho la vijana wenye nguvu, kwa sababu wanajiingiza kwenye ulevi ambao hata huko mitaani wanapika zile pombe zinazoitwa za moshi, wanakwenda kule wanakunywa, hawana chakula cha kula, wanaisha vijana wetu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Selemani Zedi!

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Hotuba hii muhimu ya Bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, nitaanza na eneo la umeme vijijini. Dira ya Taifa letu ni kwamba, tumepanga ifikapo mwaka 2025 tuwe nchi yenye uchumi wa kati na ili kufikia lengo hilo ni lazima pato la mtu mmoja kwa mwaka liwe angalau dola 2000 mpaka 3000. Sasa hii maana yake ni kwamba, ili uweze kufikia hiyo, uwe na shughuli nyingi za



uzalishaji mali na huwezi kuwa na shughuli nyingi za uzalishaji mali kama huna nishati muhimu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali hasa mwaka huu kwa kuja na mpango mkubwa sana wa kuhakikisha maeneo mengi ya vijijini yatapatiwa nishati muhimu sana ya umeme, ambayo ndiyo itawezesha shughuli za uzalishaji mali za kiuchumi ziweze kufanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *trend* katika miaka miwili iliyopita imeonesha kwamba, zimekuwa zikitengwa fedha kwa ajili ya miradi ya umeme vijijini, lakini mwaka unaisha fedha hizo zinakuwa hazijatolewa au zinatolewa kwa kiwango kidogo sana. Sasa rai yangu kwa Serikali ni kwamba, kama tunataka ku-*make a difference*, sababu mojawapo kubwa inayofanya makusanyo yetu ya ndani kama kodi kuwa machache ni kwamba, tuna shughuli chache sana za uzalishaji mali, kwa hiyo, tunakuwa na *tax base* ndogo, walipa kodi wachache. Sasa ili kuongeza idadi ya walipa kodi ni lazima uongeze shughuli za uzalishaji mali za kiuchumi na ili uongeze shughuli hizo ni lazima nishati muhimu ya umeme ipatikane. Shughuli za uzalishaji mali hazifanyiki bila nishati ya umeme.

Kwa hiyo, *direction* ya kupeleka umeme kwa wingi maeneo mengi ya vijijini ni mwelekeo sahihi lakini ufanyike. Kwa hiyo, napenda huu uwe ni msimamo wa Wabunge wote safari hii kwamba, tuibane Serikali kwa namna yoyote ile fedha ambazo zimepangwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Umeme Vijijini zisipelekwe kwenye shughuli nyingine yoyote. Fedha hizo ni lazima zote asilimia 100 zipelekwe kwenye shughuli za kutekeleza Miradi ya Umeme Vijijini ndipo mahali ambapo tuta-*make a difference* na tutaondoa matatizo mengi na kutengeneza ajira, lakini vilevile wakulima wetu ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakiona kilimo chao hakina tija kwa sababu wamekuwa wakiyauza mazao yao bila kuongeza thamani, ukiwapelekea nishati ya umeme itawawezesha sasa kuongeza thamani ya mazao yao na hivyo kupata bei nzuri na hatimaye kuona kwamba kilimo kina tija.

20 JUNI, 2013

Kwa hiyo, umeme vijijini ni suluhisho la mambo mengi ya kiuchumi na kwa maana hiyo ni eneo ambalo kama nchi lazima tuwe *very serious*, tulizingatie na tusilifanyie mzaha kama tunataka kuleta mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa na mpango wa umeme vijijini wa mwaka huu, hata kule katika Jimbo langu Vijiji vya Mambali, Lububu, Wamala, Mwangoye na Igusule vimo katika mpango. Wananchi wangu kule wameshaka mkao wa kula, wanategemea kabisa kwamba, sasa nishati muhimu ambayo walikuwa wakiisubiri kwa muda mrefu itapatikana ili waweze kubadili maisha yao.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo kama nchi tunapaswa tujipange ili tuweze kupata mapato ya kutosha ambalo ndicho kimekuwa kilio chetu ni rasilimali zetu ambazo tumejaliwa kama nchi kuwa nazo. Kama nchi tumejaliwa kuwa na rasilimali nyingi zikiwemo madini na sasa hivi kuna rasilimali muhimu sana ya gesi. Ili tuweze kupata mapato na kuona faida ya rasilimali hizi ni lazima tujenge uwezo wa kuzisimamia shughuli hizi, kudhibiti matumizi na kuweza kukagua gharama zinazofanywa katika shughuli hizi ili hatimaye tuweze kuona faida inayotokana na rasilimali hizo.

Mheshimiwa Spika, historia na ukweli vimeonesha kwamba, nchi zote ambazo zimefaidika kwa mfano na rasilimali ya gesi, ni zile ambazo zina kampuni zake ambazo ndizo zinafanya kazi ya utafiti na uchimbaji na shughuli zote za gesi. Kwa mfano, Norway wana *Statoil* ambalo ni shirika lao kama nchi linaloendesha shughuli za nchi. Malaysia wana *Petronas*, Trinidad and Tobago wana *National Gas Company (NGC)*. Tanzania tuna *TPDC*, lakini ilivyo sasa hivi inahitaji uwezeshwaji mkubwa ili iweze kudhibiti hizi kampuni ambazo zinafanya utafiti, kuchimba na hatimaye kuuza rasilimali ya gesi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna kampuni moja ya *Panafrican* ambayo ndiyo inachimba gesi kule Songosongo, lakini kama nchi, *TPDC* ina mikataba 26. Sasa huo mkataba

mmoja tu wa *Panafrican* kuna tatizo kubwa sana la uwezo wa *TPDC* kuweza kusimamia kwa maana ya kuhakiki gharama za uwekezaji ili hatimaye kama nchi tupate faida ambayo ni sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakati tunajenga uwezo wa *TPDC*, Shirika letu la Serikali la kuweza kusimamia hii Miradi ya Gesi, sasa hivi miradi yote inafanywa na kampuni za uwekezaji. Ili tuweze kunufaika na tuone faida ya uwekezaji katika maeneo hayo ni lazima *TPDC* iwezeshe. Nitoe angalizo kwamba, pamoja na gesi nyingi ambayo tunategemea kuigundua Mtwara na baada ya miaka mitano, sita au saba, itanza kuzalishwa, kama hatutajipanga na kuwekeza katika Kampuni yetu ya *TPDC* ili iwe na uwezo wa kudhibiti gharama na uendeshaji wa shughuli zote za gesi, tutakuwa na gesi nyingi ambayo inachimbwa na kuuzwa, lakini mwisho wa siku kama nchi tutashangaa manufaa ni madogo mno, kwa sababu ya uwezo wa kudhibiti gharama na uendeshaji wa shughuli zote hizi.

Kwa hiyo, hatuna ujanja, ili tuweze kunufaika na rasilimali hizi na hili ni eneo ambalo linaweza kutupatia mapato makubwa sana, tusiwe wabahiri, tuna miaka mitano mpaka saba ya kujiandaa, ni lazima tuwekeze ipasavyo kwenye Shirika letu la Serikali *TPDC* ili liweze kusimamia kikamilifu hizi kampuni na *eventually* lengo la mwisho ni kwamba, *TPDC* yenyewe iwe kama *Statoil* ya Norway, *Petronas* ya Malaysia na kama *NGC* ya Trinidad and Tobago. Hapo ndipo tutaweza kunufaika na rasilimali yetu hii, kinyume chake tutashangaa kwamba tuna rasilimali nyingi lakini tunaonufaika siyo sisi Watanzania.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nashauri liongezewe nguvu na Serikali ni umwagiliaji. Kama tutaweka nguvu za kutosha katike eneo hili, litaweza kuongeza mapato makubwa sana. Hata hivyo, kumekuwa na *trend* kwamba Serikali au Wizara inajenga miradi ya umwagiliaji lakini haifiki mwisho. Kule kwangu kuna mradi mkubwa sana wa Bwawa la Kamaharanga, ambalo linaweza kumwagilia

20 JUNI, 2013

zaidi ya hekta 5000, lina miaka mitano limekamilika lakini bado halijaweza kutengenezewa miundombinu ya mifereji kupeleka maji mashambani yatumike kumwagilia. Serikali imetumia fedha nyingi karibu milioni 900 au shilingi bilioni moja kujenga bwawa hili, lakini ni miaka mitano sasa haijajenga mifereji, kwa hiyo, bwawa halitumiki. Shilingi bilioni moja imetumika, lakini mifereji haijajengwa hivyo bwawa halitumiki kama ambavyo ilikusudiwa na hivyo zile hekta 5000 hazilimwi na mapato hayapatikani. Kwa hiyo, unaweza kukuta tunatumia fedha lakini zinakuwa hazina *impact* au hazileti manufaa ambayo yalitarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu ni kwamba, Serikali ijipange imalizie miradi ya skimu za umwagiliaji inayoanzishwa, isiwe inajengwa na inaishia katikati, kwa sababu tutakuwa tunatumia fedha halafu hazileti matokeo ambayo tunayataka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ni miaka mitatu imepita tangu Halmashauri ya Nzega tumeingiza kwenye mipango yetu mabwawa kadhaa ya umwagiliaji katika maeneo ya Nindo, Mambali, Budushi, Nkini ziwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Josephine Genzabuke, atafuatia Mheshimiwa Mussa Haji na Mheshimiwa Mansoor, Mheshimiwa Deo Sanga, Mheshimiwa Malocha na Mheshimiwa Agripina wajiandae.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza kabisa, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwenye wingi wa rehema, kwa kunijalia kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu mara nyingine ili nami niweze kuchangia Hotuba hii ya Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, napenda niungane na Wabunge wenzangu, kukupongeza kwa kuweza kuunda Kamati hii ya Bajeti; hongera sana. Pia napenda kumpongeza Waziri wa Fedha kwa kukubaliana na Kamati ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Mtemi Andrew Chenge, kwa kuweza kukaa pamoja na kujadili changamoto hatimaye kufikia kuongeza fedha kwa Wizara ambazo zilihitajika kuongezewa fedha. Hongereni sana kwa kuweza kukaa pamoja na kukubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu ni kwamba, sasa Wizara ya Fedha ihakikishe inapeleka fedha kwenye maeneo yale ambayo fedha hizo zimepangwa kupelekwa, isiwe ni maneno tu yakabakia kwenye karatasi na ndani ya Bunge lako Tukufu. Wafanye kwa vitendo, kule kote ambako fedha hizo zimeelekezwa kwenda zipelekwe ili ziende zikafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Uchukuzi imepangiwa fedha. Nchi zote ambazo zimefanya vizuri zimewekeza kwenye reli na reli ndiyo kichocheo kikuu cha uchumi kwani mizigo yote inapelekwa sokoni kupitia reli. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Uchukuzi fedha zile zipelekwe ili Reli ya Ukanda wa Kati kwa maana ya Kigoma, Tabora na Rukwa na Ukanda wa Ziwa iweze kuimarika hatimaye Wananchi wanaoishi mikoa hiyo na wao waweze kunufaika kutokana na mapato yanayotokana na nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Mikoa hiyo wamekuwa wakipata tabu sana hasa katika kusafiri na kusafirisha mizigo yao. Nina imani fedha hizo zikipelekwa, matatizo hayo yatapungua na wataweza kupata sementi kwa bei ya chini, watapata sukari kwa bei nafuu na hatimaye wataweza kunufaika na Pato la Taifa lao.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maji nao kadhalika wapelekewe fedha na niombe tu kwamba, maji hayo yatakapofika vijijini, Viongozi wa Vijiji wahakikishe shule za sekondari na msingi zinapelekewa maji, kwa sababu mara nyingi zimekuwa zikipata shida; maji hakuna, vyoo hakuna

na hasa watoto wa kike wamekuwa wakiathirika sana kisaikolojia wanapokosa maji shuleni. Mara nyingi kwa sababu za kimaumbile, watoto wa kike wamekuwa wakikosa kwenda shule wakati mwingine kwa mwezi wanapoteza siku saba hawaendi shule. Sasa ukihesabu kwa mwaka mzima kila mwezi watoto wa kike wanapoteza wiki moja kwa mwezi, kwa mwaka wanakuwa wamepoteza siku ngapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishukuru Serikali kuongeza fedha kwenye maji. Naomba maji yapelekwe katika vijiji na vijiji viyapeleke kwenye shule za sekondari na msingi ili watoto wetu waweze kuepukana na shida hiyo.

Mheshimiwa Spika, fedha za *REA* zipelekwe vijijini ili Wananchi waweze kunufaika. Pia naomba yale maeneo ya mijini ambayo Wananchi wamelipia gharama za kusambaziwa umeme na hawajapatiwa umeme, wapewe umeme. Vijiji vile ambavyo viko karibu na mjini ambavyo havijapatiwa umeme navyo vipatiwe umeme. Kwa mfano, nafahamu kabisa kupitia Mpango huu wa *REA*, Vijiji vya Nyakitonto, Makele, Kasangezi, Rusesa na Keru Juu vitanufaika kupitia fedha hizi zitakazopelekwa na *REA* na umeme utaweza kupatikana vijijini. Tunaishukuru sana Serikali kwa kazi nzuri inayofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya vijana na wanawake. Naishukuru sana Serikali kwa kuliona hili, kwa sababu wanawake na vijana wamekuwa wakipata shida sana. Sasa nina imani wataweza kunufaika kupitia fedha hizi ambazo zimetengwa kwa ajili ya vijana na wanawake. Ninaomba sasa mafunzo yatolewe kabla ya fedha hizo kutolewa. Siyo mafunzo tu kwa ajili ya kurejesha mikopo, yawe ni pamoja na mafunzo ya ujasiriamali, ufugaji wa kuku, ng'ombe, mbuzi, kilimo cha mboga mboga pamoja na ufugaji wa nyuki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wakipata mafunzo wataweza kufanya vizuri kwa sababu ukiwapatia mafunzo ya kurejesha

mikopo bila kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali; sasa watarejeshaje mikopo waliyopewa kama hawajawa wajasiriamali? Kwa hiyo, naomba Serikali ijitahidi kutenga fedha na Halmashauri zetu ziweze kupata kazi ya kwenda kutoa elimu kwa Wananchi wetu ili waweze kuwa wajasiriamali wa kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Nimepita sehemu nyingi nikihamasisha wanawake na vijana kujiunga kwenye vikundi, lakini wengi wao hawajapata elimu hiyo. Hata hivyo, niseme wako tayari kabisa kuweza kujiunga kwenye vikundi watakapopatiwa elimu na mafunzo ya ujasiriamali. Tatizo ni kwamba, hawajapata walimu wa kwenda kuwafundisha. Naomba Serikali iliangelie hili ili walimu waweze kupelekwa kwa ajili ya kuwafundisha Wananchi wetu shughuli za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Spika, nimeongea na Viongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kuhusu matatizo ya walimu. Wizara wanasema kwamba, wao pamoja na TAMISEMI wanapeleka taarifa za malipo ya walimu Hazina, lakini tatizo liko Hazina. Niwaombe sasa Hazina wanapopelekewa madai ya walimu wahakikishe wanawalipa walimu wetu ili waepukane na kuishi maisha ya shida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, taarifa zinapopelekwa zinakuwa zimejionyesha; sasa kigugumizi cha kuwalipa walimu stahiki zao kinatoka wapi? Naomba Serikali iliangelie hili ili Hazina iwe inawalipa walimu madai yao mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie kampuni ambazo zinachangia mapato kwenye Taifa letu. Kwa mfano; kuna Bodi ya Taifa ya Michezo ya Kubahatisha. Kwanza, nimpongeze Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Abbasi Tarimba, kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuweza kuchangia Pato la Taifa letu kwa kuingiza fedha nyingi kutokana na michezo hiyo ya kubahatisha. Wakati TRA wanasimamia walikuwa wanaingiza shilingi milioni 900, lakini leo hii kwa mwaka wanaingiza shilingi bilioni tisa. Ninampongeza sana

Mkurugenzi huyo wa Bodi ya Taifa ya Michezo ya Kubahatisha kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuchangia Pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nchi zote ambazo zimefanikiwa kwenye michezo ya kubahatisha ni kwa sababu Wananchi wanajua fedha zile zinapelekwa kwenye shughuli za maendeleo. Naomba sasa fedha zile zitakazopatikana kupitia Bahati Nasibu zipelekwe kwenye kutengeneza madawati. Katika miaka hii miwili iliyobakia, fedha hizo zitakapopatikana zisipelekwe kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina zikakae, zipelekwe kwenye shule ili madawati yaweze kupatikana, watoto wetu waweze kupata sehemu ya kukaa. Katika miaka hii miwili, naomba wahakikishe fedha hizo zinaelekezwa huko kwenye madawati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie mambo ya vileo. Wakati Waziri anawasilisha Hotuba ya Bajeti alisema bia na sigara viongezewe kodi ili viweze kuchangia Pato la Taifa. Nikajjuliza hivi Konyagi nayo si ni kileo? Viroba navyo si ni kileo? Navyo vinachangia Pato la Taifa? Sasa kama Konyagi wanachangia Pato la Taifa, basi mimi naona kuzuiwa kwa viroba siyo suluhisho, isipokuwa Sheria ya Vileo ina upungufu mkubwa unaotoa fursa kwa watoto kuuziwa pombe. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante, kila mtu akifika kwenye vileo kengele inagonga.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya sasa nimwite Mheshimiwa Mussa Haji, Mheshimiwa Mansoor ajiandae na pia Mheshimiwa Deo Sanga kama yupo. Mheshimiwa Mussa Haji.



20 JUNI, 2013

**MBUNGE FULANI:** Hayupo!

**SPIKA:** Hayupo! *Okay*, Mheshimiwa Mansoor yupo? Mheshimiwa Deo Sanga na Mheshimiwa Malocha wajiandae.

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru umenipa nafasi na mimi nichangie hoja hii.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka huu wa 2012/2013 kwa kiasi kikubwa inasuasua, haina *excess revenues*, ina *deficit* na maeneo mengi miradi mingi haijapata fedha za kutosha. Inanishangaza kwamba, mwaka kesho tumepandisha bajeti kwa asilimia 29 na uchumi wetu unakua kwa asilimia 6.7. Je, hii bajeti tunayopitisha itatekelezeka?

Mheshimiwa Spika, suala lingine ningependa ku-*declare interest* kwamba, mimi ni mdau kwenye eneo hili la mafuta. Ningependa kuongelea ongezeko la kodi ya mafuta. Kwenye eneo la kodi ya mafuta Serikali kwa sasa hivi inapata karibu shilingi trilion moja na ushee kwa mwaka huu wa bajeti. Mwaka kesho kwa kuongeza kodi hizo Serikali imepanga kuongeza mapato kwa zaidi ya shilingi bilioni 301. Je, Serikali haioni kupandisha kodi ya asilimia 28 itapandisha bei ya vitu vyote na hususan usafiri, chakula na maisha ya Mwananchi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa kuongelea pia matatizo ya maji katika Mji wa Ngudu. Hiki ni kilio cha siku nyingi, leo katika Mji wa Ngudu upo mgao wa maji, maji ni tatizo. Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipotutembelea pale kwenye ziara yake aliahidi kwamba, hadi kufikia Desemba, 2012, tatizo la maji lingeisha. Leo tuko mwezi wa Sita, tatizo bado liko palepale, hakuna kilichotokea pale. Mwaka huu tumeongeza bilioni 180 kwenye Wizara ya Maji, naomba Ngudu ipewe kipaumbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, gharama ya usafirishaji. Kwenye bajeti ya mwaka ujao *road licence* imepanda kwa asilimia ishirini na tano, kutoka Sh.200,000/= imekuwa Sh.250,000/=. Gharama ya bima kutoka asilimia mbili kwenye trela kwa *comprehensive* imepanda kufikia 6.5%. Mfano kama ulikuwa unalipa shilingi milioni moja sasa kuanzia mwezi Julai, utalipa shilingi milioni sita. Kwenye *comprehensive* ya trela ulikuwa unalipa Sh.1,000,000/= sasa utalipa Sh.3,000,000/= toka mwezi Julai. Kwenye *third part insurance* tulikuwa tunalipa Sh.120,000/= sasa utalipa Sh.300,000/= ongezeko la asilimia mia mbili (200%). Kwenye trela ilikuwa tunalipa Sh.120,000/= sasa utalipa Sh.700,000/=: ongezeko la asilimia mia nne (400%). Gharama ya mafuta imepanda kwa asilimia ishirini na nane (28%). Nyongeza yote hii ya bima, *road licence*, mafuta itapandisha usafiri wa chakula, mabasi na bidhaa zote nchini zitapanda, mwananchi ataumia vibaya mno. Naomba Kamishna wa Bima akae na wadau kujadili kuhusu suala la kuongeza bima ya magari. Hii bima inamgusa kila Mtanzania hata bodaboda inamgusa na sisi Wabunge pia inatugusa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Sheria ya *Deep Sea Fishing*, naomba Serikali ilete sheria ya kutoza *royalty* kwenye *deep sea fishing* katika bahari zetu. Tuna sheria ya *royalty* kwenye maziwa yetu makuu yote, lakini kwenye bahari yetu hatuna sheria ya *royalty*. Nashauri sheria iletwe kwa sababu kuna takwimu tulizifanya, ni-*declare interest*, nilikuwa mjumbe wa Kamati ya Mheshimiwa Spika ya mwaka jana, tunaachia karibu mapato ya shilingi bilioni 300 kwenye *deep sea fishing*. Nashauri Serikali ilete sheria ili tuweze kupata mapato hayo. Biashara ya *deep sea fishing* ni zaidi dola za Marekani bilioni 200 kwa dunia kwa mwaka, sisi Tanzania hapa imekuwa ni shamba la bibi, kila kitu ni bure. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kuhusu bandari ya Dar es Salaam. Bandari yetu hii inaweza kutuingizia zaidi shilingi trilioni moja kwa mwezi kama tukiisimamia vizuri lakini sasa hivi utashangaa bandari ya Dar es Salaam inajenga ghorofa 35 kwa ajili ya ofisi. Suala la kujenga ghorofa ni la *National Housing*, naomba mashirika haya ya

20 JUNI, 2013

umma yaelekeze nguvu zao kwenye masuala ya kazi zao za kutoa mizigo haraka na kwa ufanisi na siyo kujielekeza kwenye kujenga maghorofa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, kuna fedha walizopanga Wizara shilingi trilioni 3.3 kulipa deni la Taifa. Basi niombe pia wazingatie kulipa madeni ya ndani ya wazabuni, ya Walimu, Polisi na kadhalika. Wazabuni wengi ambao wametoa huduma kwa Halmashauri walipwe madeni yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye ukurasa wa 71, Waziri alipendekeza kodi ya Sh.1,450 kwa ajili ya simu kadi kwa kila mwezi ambayo Mheshimiwa Waziri amefuta. Mimi nashauri hiyo kodi ya simu kadi asiifute kwa sababu leo tuna simu kadi ambazo zimesajiliwa zaidi ya milioni 16 mpaka milioni 18. Hizo simu kadi kama tukiendelea kuzitoza kodi hiyo kwa mwezi tutapata kodi shilingi bilioni 23 na kwa mwaka tutapata karibu kodi ya shilingi bilioni 278 mpaka shilingi bilioni 300. Sasa akipata shilingi bilioni 300 kwenye simu kadi hizo, naomba aachane kupandisha kodi kwenye mafuta kwa sababu kwenye mafuta anatafuta shilingi bilioni 300, sasa kama kwenye simu kadi atapata shilingi bilioni 300 na hizi simu kadi zitagusa watu milioni 10, lakini mafuta yatagusa watu milioni 45. Kwa hiyo, namshauri Waziri asifute hii kodi, atoze kodi kwenye simu kadi, tupo tayari kulipa hiyo kodi lakini kwenye mafuta afute kodi yote aliyotaka kuongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Deo Sanga, atafuatiwa Mheshimiwa Malocha, Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mheshimiwa Said Zubeir na Mheshimiwa Tauhida Galos atafikiwa. Mheshimiwa Deo Sanga!

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kushiriki kuchangia.

20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuishukuru Serikali kwa bajeti yake nzuri. Nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete, Mheshimiwa Makamu wake, Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha, Mawaziri wote pamoja na watendaji kwa namna ambavyo bajeti hii ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema bajeti ni nzuri? Bajeti hii imezingatia vilio vikubwa vya Wabunge wote waliochangia katika Wizara mbalimbali ambao walielekeza kwamba kila Wizara fedha hazitoshi, tunaomba ziongezewe. Nikushukuru wewe kwa kuunda Kamati ile ya Bajeti kwa namna ambavyo imeongeza fedha kwa kila Wizara, tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali kwa namna ambavyo sasa bajeti hii ni nzuri badala ya kusubiri makusanyo ya Serikali ili kuzipeleka katika Halmashauri mbalimbali, naiomba Serikali ikope Benki Kuu hela za bajeti hii ili kusudi wakati wanaendelea kukusanya ndiyo wawe wanapeleka kule Benki Kuu ili kutochelewesha utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la bajaji, bodaboda na kadhalika ambapo Serikali imeondoa kodi mbalimbali za bajaji. Niseme tu ni jambo nzuri, lakini niseme tu kwamba jambo hili nilikuwa nadhani lingezingatia sana zile bajaji za vijijini kwa sababu zipo bajaji ambazo zinafanya biashara kubwa kuliko magari mengine yoyote yale hapa nchini. Kwa mfano, unapoondoa kodi mbalimbali katika bajaji, sasa hizi teksi ambazo zipo mjini zinafanya shughuli ya teksi, teksi imepaki hapa na bajaji imepaki hapa, maana yake sasa huyu mtu wa teksi anataona ni vizuri sasa anunue naye bajaji ambayo atakuwa halipi kitu chochote. Mfano hai ninao, wapo wafanyabiashara pale Dar es Salaam, sitaki kuwataja, yupo mtu mmoja ana bajaji zaidi ya 50 na yupo mtu mmoja ana bajaji zaidi ya 30 zipo pale, sasa unapomwondolea huyu maana yake sasa tutalingizia Taifa hasara. Ni jambo njema lakini waangalie zile bajaji ambazo zinafanya biashara kama hizi waone uwezekano wa kulipa kodi. *(Makofi)*

20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie kuhusiana na Jimbo langu. Kwenye bajeti hizi ambazo zimeongezwa kila Wizara, pale Makambako tuna soko la Kimataifa ambalo limezungumzwa kwa miaka mingi, zaidi ya miaka kumi na kitu lakini kupitia bajeti hii sasa kwamba kila Wizara imeongezewa fedha, niombe soko hili la Kimataifa liweze kuingia kwenye mkakati wa kufanyiwa kazi. Ikiwezekana liweze kuanza ili kuondokana na utata ambapo eneo lile limetunzwa zaidi ya miaka 15 na wananchi wanashindwa kupata majibu ni namna gani Serikali imejipanga katika kutatua tatizo hili la Mji wetu wa Makambako.

Mheshimiwa Spika, nizungumze suala la maji katika Mji wetu wa Makambako na vijiji vyake. Kupitia ongezeko la bajeti hili katika Wizara hii ya Maji, nina imani kabisa kwamba angalau katika mgawanyo wa fedha zilizoongezeka sasa angalau kidogo litapunguza tatizo la maji katika Mji wetu wa Makambako hususan tatizo kubwa ambalo tunalipata kuanzia mwezi Oktoba, Novemba na Desemba, hali huwa inakuwa ni mbaya sana. Sasa nina imani kwamba kupitia ongezeko la bajeti hii, hatimaye hata vijiji ambavyo vinakosa maji kama kwa mfano pale Lupembe, Ukalawa, Idamba, Kiumba, Kitandililo vyote hivi sasa vipata angalau kidogokidogo kutokana na ongezeko hili la bajeti ambayo imeongezeka. *(Makoff)*

Mheshimiwa Spika, nizungumze suala la barabara. Niishukuru tena Serikali barabara nyingi katika nchi yetu sasa angalau zinaweza kupitika vizuri kupitia Mfuko huu wa Barabara. Katika Mji wa Makambako mwaka 2012/1013, Mheshimiwa Waziri kupitia TAMISEMI alijibu swali langu hapa kwamba wametenga Sh.700,000,000 kwa ajili ya kutengeneza Mji pale kilomita mbili za lami lakini mpaka sasa walileta fedha za kilomita moja tu na mwaka wa fedha ndiyo kesho kutwa unaisha. Naomba kwa ongezeko hili waweze kumalizia fedha za mwaka 2012/2013 kwa kilomita moja iliyobaki na hatimaye tuweze kuendelea kwa kilomita zingine kwa mwaka mwingine wa fedha.

Mheshimiwa Spika, nije katika kilimo, Mkoa wa Iringa na Njombe, ndiyo Mikoa mikubwa inayojihusisha sana na

suala la kilimo. Sasa kupitia ongezeko la bajeti hii, nina imani sasa Mfuko ule wa Pembejeo kuhusiana na yale masuala ya vocha, sasa watanufaika watu wengi kuliko ilivyokuwa hapo awali. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kuongeza bajeti hii ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimwia Spika, afya. Katika Jimbo langu kiko Kituo cha Afya cha Mji wetu mkubwa kabisa wa Makambako ambapo nimezungumza mara nyingi hapa na Mheshimiwa Rais alipokuja tulimwambia na alituambia kwamba tutapata kibali kuwa hospitali. Tumeendelea kulizungumza, Wizara ya Afya imeendelea kutuma wataalam na hatimaye tumeweza kukamilisha. Niombe sasa kupitia bajeti hii angalau sasa tupate kibali na kuwa hospitali ili kuweza kutoa huduma bora kwa wananchi wangu wa Jimbo langu la Njombe Kaskazini.

Mheshimiwa Sika, hatimaye kule Lupembe kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, tumetenga eneo kwa ajili ya kujenga hospitali ya wananchi wa Lupembe. Kupitia bajeti hii, nina imani sasa tutapata fedha angalau za kuanzia kujenga hospitali yetu ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

Mheshimiwa Spika, umeme. Niipongeze tena Serikali, kupitia bajeti hii miradi yote ya *MCC* na *REA* iliyokuwa imekwama na kama ambavyo Wabunge wenzangu wamekuwa wakichangia hapa, nina imani kabisa itaanza kutekelezwa. Kwa sababu fedha zimetengwa, tuombe sasa miradi hii ianze kwa wakati ili kuweza kupeleka umeme vijijini mfano vijiji vya Kiumba, Ikwete, Lyamkena, Kichiwa, Ikuna, Nyombo na mahali pengine katika Jimbo lile ambapo mradi huu ilionyesha utaanza mwaka huu, mwezi Oktoba. Nina imani sasa kupitia fedha hizi ambazo zinakwenda katika Wizara hii basi vijiji hivi sasa vitanufaika kadri ambavyo Wizara ilikuwa imepanga kwamba mwezi Oktoba vitaanza kupata umeme hususan vijiji vya pale Makambako vinavyozunguka Mji ule kama vile Mashujaa, Kivavi, Majengo, Kipagamo na Uhuru. Vijiji hivi kwenye bajeti vilionekana vitaanza mwezi huu wa sita au saba, basi niamini kwamba fedha hizi zitakuwa zimekwenda huko.

20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kuipongeza Serikali sikivu kwa maana kwamba kadri Wabunge walivyokuwa wameomba kwamba wanaomba kuongezewa fedha katika Wizara ili kusudi Wizara ziweze kufanya kazi katika maeneo yetu kama wawakilishi wa wananchi na Serikali imekubali, naipongeza sana Serikali ya CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na kuipongeza, niungane na Wabunge wenzangu wote waliokwenda katika Majimbo mbalimbali yalikuwa na uchaguzi wa Madiwani, niwapongeze sana kwa ushindi mkubwa tulioupata. Mimi nilikuwa miongoni mwao, nilitumwa kwenda kusimamia katika Mkoa wa Iringa, Wilaya ya Kilolo, kwa Profesa Msola, Mheshimiwa Msolla na Uongozi wako wa Mkoa, nakupongeza sana tumefanya kazi nzuri. Hii ndiyo *indicator* ya mwaka 2014/2015 ya ushindi mkubwa. Yote yanatokana na Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete katika Mkutano Mkuu wa CCM ambapo aliagiza mbinu gani tuweze kutumia ili kushinda katika chaguzi mbalimbali, haya ndio matunda ya mkutano ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi, haya maendeleo yote ya Taifa tunayozungumzia...

*(Hapa kengele ya ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante, muda umekwisha.

**MHE. DEO. K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Malocha, Mheshimiwa Agripina Buyogera na Maida Abdallah.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuungana na wenzangu katika kuchangia hotuba hii ya bajeti.

20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kutoa pole kwa wananchi wakulima na wafanyabiashara ambao wamevamiwa juzi, walikuwa wanatoka Tunduma kuuza Michele yao, walivamiwa wakishuka mlima wa Nyangarua, wameporwa na majambazi yapata karibu shilingi milioni 40 na wengine wamejeruhiwa na walikosa msaada wa haraka kwa sababu eneo hilo halina mtandao na mimi nimekuwa nikisema mara kwa mara hapa kwamba mtandao ni nyenzo muhimu sana katika ulinzi na usalama mali za watu. Nadhani Waziri anayehusika na mitandao ananisikiliza vizuri katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine naomba nichukue fursa hii kumpongeza pacha mwenzangu ambaye amerudi hivi karibuni Bungeni, Mheshimiwa Aeshi, tupo Wilaya moja. Kurudi kwake kunaniimarisha na mimi ili kuunganisha nguvu kwa sababu tunaongozwa na Mkuu wa Wilaya mmoja. Hongera sana Mheshimiwa Aeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kuongezea machache ambayo yanaweza yakanusuru uchumi wa nchi yetu. Ili kuweza kuimarisha uchumi wa nchi yetu, yapo mambo muhimu ambayo wenzangu wameyataja na mimi nirudie kuyasema, kwanza, lazima tuhakikishe reli inafika maeneo yote makuu ya uzalishaji ili kuweza kukuza uchumi wa maeneo hayo. Kujenga miundombinu ya umeme na ninashukuru Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Waziri wa Nishati amelipokea vizuri na Wabunge wamemuimarisha kwa kumwongezea bajeti kuhakikisha umeme unaenea karibu maeneo yote ya vijijini ili kuongeza uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumza hivi kwa sababu yapo maeneo ambayo yangukuwa yamepiga hatua kubwa sana, wamecheleweshwa kwa kukosa nishati ya umeme. Walishajipanga kwenda mbele lakini umeme imekuwa kama *speed governor* kuzuia wasiweze kusoga mbele. Kwa hiyo, katika hilo, kama umeme utasambazwa mpaka vijijini itakuwa ni msaada mkubwa sana wa kukuza uchumi wetu. *(Makofi)*



20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu, elimu ni nyenzo muhimu sana katika kuimarisha uchumi. Mahali popote pale, uchumi hauwezi kukua bila kuwa na elimu. Nyenzo muhimu ya kuimarisha elimu ni kuondoa kero zote zinazohusu Walimu, hiyo ndiyo iwe namba moja na vingine vifuate baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu hata huko nyuma, watu walikuwa wanasomea miembeni lakini walikuwa wanafaulu kwa sababu Walimu walikuwa wazalendo kutokana na kile wanachokipata. Kwa hiyo, kitu cha kwanza ni uzalendo, Mwalimu akiridhishwa uzalendo utamsukuma kufanya jitihada zote kuhakikisha mwanafunzi anaelewa na anafaulu. Kwa hiyo, naomba hilo lianze kufikiwa kuboreshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni afya, ili wananchi wazalishe vizuri lazima wawe na afya njema na ninaishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika sera yake ilishaeleza kwamba lazima kila kijiji kiwe na zahanati, kila Makao Makuu ya Kata yawe na Kituo cha Afya. Utekelezaji huu unakwenda kwa kasi, lakini naona Serikali ndiyo inabaki nyuma. Ukienda katika maeneo mengi, utakuta majengo mengi ya zahanati, vituo vya afya yamesimama, havina mabati. Kwa hiyo, nahimiza Serikali iweze kuanza kufanya tathmini yale majengo yote ya zahanati na vituo vya afya yaezekwe ili huduma ianze kutolewa ili kuwaongezea wananchi afya waweze kutulia na kuzalisha katika maeneo walipo bila ya kwenda mbali na maeneo ya huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuboresha kilimo. Ili uweze kuwavutia wananchi lazima yale mazao yawe na masoko na ili hayo mazao yawe na masoko lazima kuwe na viwanda. Viwanda ni kichocheo muhimu sana cha kufanya mazao yetu yawe na soko. Nashukuru Waziri wa Viwanda kwa jitihada zake anazozifanya anatupa mwelekeo mzuri nadhani huko mbele tuendako mambo yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba wananchi wengi wamehamasika sana katika kilimo, lakini tatizo ni

kwamba ikitokea mwaka huu wamelima vizuri, wakauza vizuri, mwaka unaofuata bei zinashuka. Kwa hiyo, wanakata tamaa, mitaji inakufa, wanabaki wanadaiwa. Mimi sijajua kwa nini Serikali halijaliona hili. Kwa mfano, mwaka huu watu hawajui mchele watauzaje kwa bei gani, mahindi watauzi kwa bei gani, Serikali inaangalia tu umati wa watu wa mjini kwamba chakula kimepanda, wazalishaji usipowaangalia chakula kitatoka wapi. Naomba Serikali iwaangalie kwanza wakulima, hao walioko mjini wengine wamekimbia hata kulima, waende wakalime, wabaki watumishi huko mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nalopenda kulizungumzia, ni suala la kilimo cha umwagiliaji. Naipongeza Serikali yetu imetilia maanani, imeanzisha miradi mingi ya umwagiliaji. Ipo dosari, miradi mingi ya umwagiliaji imeanza mwaka jana mpaka sasa mingine haijapewa fedha, imesimama na kwenye Jimbo langu miradi mingi imesimama na wakati ilishaanza na imetumia fedha nyingi sana. Kwa mfano, mradi ule wa Sakalilo, Ng'ongo, Maleza umepewa fedha lakini toka mwaka juzi, mwaka jana hawajapewa fedha. Serikali ime-*invest* fedha lakini imeshindwa kuendeleza. Sasa sijui ni kitu gani kitatokea, ni hasara kubwa inaweza ikatokea, kwa hiyo, nahimiza Serikali iliangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni misitu. Misitu ni uchumi mkubwa sana, lazima misitu yetu ilindwe na iongezwe na itumike vizuri sio kuvuna misitu bila mpangilio. Misitu ni nyenzo muhimu sana katika suala la uchumi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni madini, madini yetu yasimamiwe na hasa wachimbaji wadogo wawezeshwe ili kuweza kuimarisha uchumi wao. Uchumi ukiimarika kwa mtu mmoja mmoja maana yake uchumi wa Taifa utaimarika.

Mheshimiwa Spika, lingine ni ardhi nzuri ya kilimo tuliyonayo itumike kikamilifu. Tunayo ardhi nzuri sana katika maeneo mbalimbali lakini utashangaa ardhi hiyo imehodhiwa na watu wachache. Wapo wananchi wa kawaida ambao mtaji wao ni nguvu, hawana pa kulima, ili

alime lazima akodi na wale ambao wamehodhi ardhi hawajaiendeleza, hivi Serikali ina kigugumizi gani, mimi napata shida sana. Inawezekana wapo baadhi ya viongozi wapo kwenye madaraka wana hisa na huu mtandao wa kuhodhi ardhi bila ya kuiendeleza. Kwa sababu sioni kinachofanyika, sijaona Serikali inachukua hatua na sijui ni kwa sababu gani? Hii kwa kweli si vizuri, wapo wananchi ambao ni maskini, wana nguvu hawana pa kulima, lakini ardhi imehodhiwa na watu wachache hawaiendelezi maana yake ni nini? Lazima mfike mahali mtatue tatizo hili ili tufike mahali na wakulima wataanza kufanya maandamano sasa sijui mtafanyaje na wakulima wakifanya maandamano ni hatari kubwa katika nchi. Naomba Serikali ilijue hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni ziara za viongozi. Nyenzo muhimu ya kusukuma maendeleo ni ziara za viongozi lakini inashangaza viongozi wanapoenda katika Mkoa, baadhi ya Mikoa Wabunge hawashirikishwi ili waweze kueleza ni sehemu gani ina changamoto ili kiongozi huyo aende. Huenda ikawa ni msaada mkubwa katika kutatua zile changamoto. Wanaelekezwa kule kwenye mambo mazuri, sehemu kubwa ni unafiki tu na kujipendekeza na kulinda madaraka yao. Huo sio utaratibu, lazima kiongozi aende mahali ambapo pana shida na ni kazi yake kutafuta namna gani aweze kutatua matatizo yaliyopo katika maeneo yale. Nashauri Serikali iweke mfumo mzuri wa kushirikisha wawakilishi katika maeneo mbalimbali, Kiongozi anapokwenda washirikiane, waangalie ni sehemu gani ina changamoto huenda kiongozi huyo anaweza akatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni taarifa. Taarifa nyingi zinazotolewa na viongozi katika maeneo mbalimbali wanapofanya ziara si sahihi, zinakuwa za kubumba na anapotoka kiongozi watu wanabaki wanaulizana haya mbona mmeandika sisi hatuyajui, yakoje haya. Kwa hiyo, lazima muwe makini hata ninyi viongozi mnapokwenda kwenye maeneo lazima muwe wadadisi kilichoandikwa ikiwezekana ukione sio kupokea tu bora ni maandishi. Mambo haya yamechukua muda mrefu, kiongozi unapokwenda

mahali ukisomewa taarifa dadisi uione. Mimi nampongeza sana Naibu Waziri wa TAMISEMI, akienda mahali ukimsomea kitu lazima akione kwa kushuhudia na kwa kugusa. Hata kama umeandaa jiwe la msingi kama hajaridhika haweki analiacha kama lilivyo na huo ndio mfumo wa uwajibikaji. Watu wote tukiwa na mfumo wa namna hiyo watu wetu watajirekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine nizungumzie ukubwa wa maeneo ya utawala. Yapo maeneo katika nchi hii yalishasahauliwa unaweza ukadhani hawajapata uhuru lakini yapo maeneo madogo yanagaiwa Wilaya, Majimbo unashangaa hawa wamepataje Jimbo, hawa wamepataje Wilaya, lakini yapo maeneo makubwa ambayo watu wameanza kudai Wilaya toka mwaka 1974 na maeneo ni makubwa. Nazungumzia Ukanda wa Ziwa Rukwa, eneo la Mto Wisa, wameanza kudai Wilaya toka mwaka 1974 na ukienda ni ukanda mkubwa wenye uzalishaji isipokuwa wana changamoto za miundombinu ya barabara kwa sababu wamekingwa na milima, ndiyo maana unakuta hata viongozi wengi hawaendi kule kwa sababu miundombinu ya barabara ni mibaya, lakini hawa watu wakipata utawala karibu, wanaweza wakaleta maendeleo makubwa sana na ni eneo ambalo lina watu wengi, ukanda wa Ziwa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, natoa wito pamoja na mwongozo uliopo lakini vilevile Serikali inapashwa kuangalia mambo hayo ikiwezekana kuunda Tume kuiangalia nchi hii, ni maeneo gani bado ni makubwa? Unajua kunakuwa na upendeleo. Wapo viongozi wengine wanapenda kutawala maeneo makubwa na wanachinjwiwa mbuzi hawaangalii tija ya maendeleo. Kwa hiyo, ni vyema kuunda hata Tume ikaanza kufuatilia maeneo mbalimbali kuona kwa nini watu hawa hawastahili kuwa na Wilaya au Jimbo. Nilitaka nilizungumzie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni bajeti la Halmashauri. Halmashauri zinakokotoa bajeti kuanzia Vijiji, Kata hadi Wilaya. Cha kushangaza...

20 JUNI, 2013

*(Hapa kengele ya ililia kuashiria  
kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

SPIKA: Sasa nimwite Mheshimiwa Agripina Buyogera, Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Said Zubeir na Mheshimiwa Tauhida Galos.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba niungane na Wabunge wenzangu kukupongeza kwa juhudi zako, kwa kutumia taaluma yako, hekima yako na uzoefu ulionao hatimaye kuweza kuleta mfumo mpya wa kujadili bajeti. Pia kuweza kuteua Kamati ya Bajeti inayotokana na Wabunge ili kuweza kuisaidia Serikali katika kukusanya mapato, nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa na Wabunge wenzangu lakini ni vizuri na mimi kama mwakilishi wa Jimbo la Kasulu Vijijini, kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Kasulu Vijijini, nichangie bajeti hii ya Serikali. Kwanza, naomba nianze na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Tumezungumza sana kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na naishukuru Serikali imeongeza fedha lakini kubwa tunaomba sisi tunaishi vijijini tujengewe nyumba za Walimu ndugu zangu. Hatupati Walimu wa masomo ya sayansi. Nimekuwa nikizungumza hapa Bungeni, Mheshimiwa Mgimwa, mimi binafsi nakukubali na Rais kukuteua hakufanya kosa kwa sababu juhudi zako kabla hujawa Waziri za kuchangia kwenye bajeti, ulikuwa unakokotoa mpaka sisi wenyewe tunakubali, sasa umepewa nyundo, umepewa silaha tusaidie Watanzania. *(Makofi)*

20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeongezea fedha Wizara mbalimbali na tumeshazichangia kiasi cha kutosha, tunaomba Wizara ya Fedha, ninaamini kuna wataalamu wazuri sana, wapo wengine mimi nawafahamu hata kwa majina, tuna wataalamu wazuri sana, ni vizuri fedha tulizozipitisha kwenye Bunge lako pamoja na juhudi zote zilizofanywa na Kamati ya Bajeti kusaidiana na Serikali, zipelekwe kwa wakati katika Wizara husika. Imekuwa ni jambo la kusikitisha Bunge lako linapitisha bajeti, fedha hazipelekwi, watu wanakaa wakisubiri fedha ili miradi iweze kutekelezwa vijijini matokeo yake mnasubiri wakati wa kumaliza mwaka ndio mnazipeleka fedha zote kwa mkupuo, kiasi ambacho siku za nyuma mpaka ilikuwa inapelekea kwamba fedha mmeshindwa kuzitumia sasa zinarudi kwa sababu mwaka wa fedha umekwisha.

Mheshimiwa Spika, hili nalo uliangalie kwa makini. Tunahitaji bajeti inayopitishwa, tukienda kuwaambia wananchi wa Jimbo la Kasulu Vijijini kwamba vijiji vyao kadhaa vimepangiwa kupata umeme, fedha hizo zipelekwe na umeme uwake katika vijiji hivyo. Haina maana ya kukaa hapa Bungeni na kupiga kelele na kuishauri Serikali matokeo yake ahadi zote zinazozungumzwa hapa Bungeni hazitekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye barabara. Naipongeza sana Wizara ya Ujenzi inayosimamiwa na Mheshimiwa Magufuli, imekubali kuungana na kauli ya Mheshimiwa Rais ya kuufungua Mkoa wa Kigoma kwa kuhakikisha inatoa fedha ili barabara ya Kidahwe - Nyakanazi ijengwe. Tunaomba fedha hizi zitoke. Ni ahadi ya Kiongozi Mkuu. Nimekuwa nikizungumza humu, muwaheshimu watu wenye mamlaka. Kama Mheshimiwa Rais aliahidi kuufungua Mkoa wa Kigoma, naomba Mawaziri, Serikali mhakikishe hampingani naye muufungue Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiona kiongozi anasema Mkoa fulani ufunguliwe ana maana. Tunapozungumzia vyanzo vya mapato, ukiufungua Mkoa wa Kigoma unainua uchumi wa Taifa, kwa nini nasema hivi? Nyie mnajua Kigoma kuna

bandari, Kigoma tuna Ziwa Tanganyika, Kigoma tuna hifadhi ya Gombe na Mahale lakini pia Kigoma mkitutengenezea barabara, mmefungua mazao mengi ya wakulima ili tuweze kuuza, ili tuweze kusaidia Mikoa ya jirani ambayo ina njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi ukienda kwenye reli, ukiangalia reli ya kati imechoka, choka mbaya lakini ile reli ikiangaliwa vizuri ikarudishwa kwenye hali yake ya kawaida ya miaka ya zamani, umeinua uchumi wa Taifa. Reli ndiyo inabeba mizigo mikubwa. Leo Mheshimiwa Magufuli anahangaika kutengeneza barabara hata kama atatufungulia barabara yetu ya Kidahwe -Nyakanazi, tuna hakika itaharibika kwa muda mfupi kwa sababu mkoa wa Kigoma tunazalisha sana. Mizigo itakayokuwa inapita kwenye ile barabara, itaweza kuharibu barabara ile kwa muda mfupi lakini kama reli itaimarishwa, hatuna mashaka na Mheshimiwa Mwakyembe lakini anafanyaje? Wizara ya Fedha ndiyo imsaidie, fedha tulizopitisha hapa ahakikishe Mwakyembe na watendaji wake wanapata fedha zote waweze kurekebisha reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tumepiga kelele kwamba tunahitaji kupunguza msongamano pale Dar es Salaam, tumeweka treni pale, inabeba abiria kwenda makazini, lakini sina uhakika kama reli zinazotengenezwa katika mji wa Dar es Salaam ni sawasawa na kuimarisha reli ya kati kwa ajili ya kuinua pato la Taifa, hauwezi ukalinganisha. Nina imani kabisa kwamba ukitengeneza reli ya kati pato la Taifa litapanda zaidi kuliko ile reli mliyoimarisha pale ndani ya Jiji la Dar es Salaam. Tuchukue maamuzi ya makusudi kuangalia mahali ambapo tutaelekeza fedha kwa maslahi ya kuinua pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la afya. Tumeleza kwenye sera ya Serikali kwamba kila Kata kuwe na kituo cha afya, kila kijiji kuwe na zahanati na wananchi wachangie. Kule ambako wananchi wamechangia hiyo asilimia 20, wamejitahidi kuanzisha ujenzi wa vituo vya afya mahali ambako hakuna vituo vya afya, je, Serikali haioni kuna

20 JUNI, 2013

haja ya makusudi ya kupanga fedha kwenda kuwasaidia wale wananchi wenye moyo wa kuisaidia Serikali katika kutimiza sera ya Serikali. Kwa mfano, tuna Kata ya Nyamidaho, Makele, Rungwe Mpya ambao tayari wameshajenga vituo vya afya lakini wameshindwa kuendeleza, Halmashauri haina uwezo wa kutoa fedha za kujenga vituo hivyo vya afya, kwa nini Serikali isichukue tu maamuzi ya makusudi ikaangalia wale wananchi wenye moyo, ikawasaidia kwa maslahi ya kuboresha maisha ya wananchi, wapate afya bora waweze kufanya kazi sana walisaidie Taifa letu. Naamini kwamba watakuwa wamenisikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo. Mkoa wa Kigoma ni katika Mikoa bora ya uzalishaji wa mazao ya chakula. Katika ile Mikoa ambayo inategemewa kwa nchi yetu, ni pamoja na Mkoa wa Kigoma. Leo ninazungumzia ni namna gani tumeleta maombi maalum ya kupewa fedha kwa ajili ya kutengeneza barabara ya Makele - Kitanga. Hiyo barabara ukiiitengeneza, umefungua Burundi iingie Tanzania kwa urahisi, ije inunue mahindi ya wananchi wangu wa Kasulu Vijijini wanaolima sana. Utamsaidia kuunganisha Wilaya ya Kasulu na Kibondo. Leo tunategemea barabara moja tu, ikitokea bahati mbaya daraja lile la Malagarasi pale likaleta tatizo lolote, hakuna kwenda Mwanza, hakuna kwenda Kahama, hakuna kuunganisha Mkoa wa Kigoma na maeneo mengine. Ukiipasua tu hii barabara ya Makele - Kitanga tayari umefungua kufika Kibondo na umefungua kufika Burundi. Ukishatengeneza ile barabara, ujambazi utapungua. Mtakuwa mmewasaidia hata Jeshi langu la Polisi, Askari wangu wanaokaa pale Herushingo, wako katikati porini, hawana pa kwenda. Hata wapate taarifa zile barabara ni mbaya! Ni namna gani *OCD* wa Kasulu anaweza kwenda kuwasaidia kule. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ya ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante.



20 JUNI, 2013

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa nimwite Mheshimiwa Maida Abdallah, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Saidi Zubeir.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu kujadili bajeti hii ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze sana kwa kazi unazozifanya na kufikia kuanzishwa mfumo huu au muundo huu wa bajeti kwa mwaka 2013/2014. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliochangia kwa namna moja au nyingine waliosema kuwa ongezeko la bei ya mafuta liondolewe. Naiomba sana Serikali kuweza kuliondoa hili ili wananchi waweze kujipatia mapato yao au kuuondoa mfumuko wa bei kwa sababu wengi wamesema na ni kweli kabisa kwamba kuongezeka kwa bei ya mafuta ni kuongezeka kwa mfumuko wa bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba niungane na wenzangu waliosema misamaha ya kodi ipunguzwe. Ni kweli kuwa misamaha ya kodi inatuathiri katika vyanzo vya mapato au kuongeza mapato ndani ya nchi yetu na mapato haya yatachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza bajeti yetu ya Serikali na kufikia viwango vya juu. Naomba sana Serikali kuangalia kwa kina na kuweka angalau misamaha hii ifikie kiwango cha chini ya 1%. Ni kweli kuwa tunaongeza wigo mpana kwa wawekezaji kuja nchini kwetu lakini angalau kwa mujibu wa sheria tungeweka muda muafaka au wakati maalumu wa kupata huo msamaha siyo waendeleo mpaka mwekezaji anafika mpaka kuondoka bado anaendelea mna msamaha. Kwa hiyo, naomba sana Serikali, hiki ni chanzo kizuri tu cha mapato na kitaweza kutuongezea mapato ndani ya nchi yetu, kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali kulifikiria hili na kuweka kiwango hiki chini ya 1%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168, imeeleza ushuru uliowekwa kwa madereva yaani *motor vehicle*, naomba madereva hawa wapunguziwe ushuru. Kiwango kilichowekwa ni kikubwa na sisi lengo la nchi yetu ni kukuza uchumi na kuondoa umaskini, ndiyo tunakuza uchumi lakini ni kuongeza ajira kwa vijana, kuongeza ajira kwa wananchi wetu kwa hiyo suala hili la ongezeko litasababisha umasikini mkubwa kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuchukulie magari madogo kama *taxi*, gari ile wanalipa ushuru kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kutoka Sh.100,000 mpaka Sh.150,000 na kutoka Sh.150,000 mpaka Sh.200,000, ushuru huu ni mkubwa sana, tuwaonee huruma. Kipindi cha mwaka 2010 lilitokea suala la leseni, madereva hawa kama wa *taxi* walihangaika sana kuhusu suala la kusoma tena wakati wao ni madereva, madereva wote kwa ujumla lakini hawa walikuwa ni wazoefu, wanaaminika kila sehemu, wanaendesha magari kwa uhakika hata Ikulu walikuwa wanaendesha magari wanaaminika kabisa kuajiriwa sehemu yoyote, lakini mwaka huu wakatakiwa kusoma tena upya leseni, kwa hiyo wengi wao kutokana na hali zao za maisha walishindwa kusoma na baadaye waliacha kazi wakawa katika hali za chini. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali kuliangalia hili na kuondoa ongezeko hili ili kuendelea na kodi ileile ili waweze kuongeza mapato yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika suala lile la leseni baadhi yao walikuwa ni watu wazima, hivi kweli utamchukua mtu mzima aende akasomee tena leseni, kwa nini kama ana *Class C* ya leseni asibadilishiwe tu kutoka *Class C* ya zamani na kuja *Class C* ya sasa lakini akatakiwa tena kwenda kusoma tena leseni katika Chuo cha *NIT* na kwenye matawi ya *NIT* yaliyoko *VETA* ili kuweza kujipatia elimu hii ya mafunzo na kuweza kupata leseni nyingine. Kwa kuwa madereva wale ni wazoefu kwa nini wasiendeele kuwabadilishia kutoka kiwango kile walicho nacho na kuja cha sasa? Kwa hiyo, hili pia lilisababisha madereva wengi kuacha kazi na kwenda kuendelea kusoma na kujiona kuwa wakati umepita

hawawezi tena kwenda kuendelea na masomo. Naomba sana Serikali kulifikiria hili na kuweza kuleta imani kwa wananchi wetu wa Tanzania kwa Serikali yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la waendesha bajaji na pikipiki. Ni kweli tunaongeza ajira kwa vijana lakini na hao wenye *taxi*wapo wengi vijana na hata kama siyo vijana lakini tunataka kuondoa umasikini wa Mtanzania. Pamoja na kwamba tunawasamehe wa bajaji na pikipiki lakini pia usimamizi uwepo kwa sababu mtu anajifunza leo pikipiki kesho anachukua abiria anamwangusha barabarani. Kwa hiyo, usimamizi uwepo kwa sababu hawa madereva wa *taxi* wanaachwa kutokana na kuwa bei zao ni kubwa kutokana na kodi walizanzozo dereva wa pikipiki na bajaji, anachukua abiria, anarahisisha foleni ya Dar es Salaam, anamwahisha abiria, dereva wa *taxi* anakaa toka asubuhi mpaka jioni hajavuna chochote. Kwa hiyo, naomba sana Serikali kulifikiria hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu mlundikano wa makontena bandarini. Naiuliza Serikali nini tatizo? Ni uhaba wa eneo ndiko kunakoleta ucheleweshaji na ukaguzi bandarini, ni uhaba wa wafanyakazi wa Idara ya Forodha, umeme kukatika mara kwa mara kusababisha *system* kutokufanya kazi vizuri au kutokuwa na bidii ya kazi na uzalendo kwa watumishi. Utaratibu huu uliokuwepo na unaoendelea kuwepo unasababisha mianya ya rushwa bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara ya Uchukuzi ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe ilivyojitahidi mpaka kufanikisha angalau baadhi ya wafanyakazi wa Bandarini au wa *TRA* kuwasimamisha ili kuweza kuweka utaratibu mzuri utakaowezesha wananchi kwanza kuweza kupata mapato yetu mazuri na kuweza kuwasababishia wananchi kutolewa mizigo yao. Kama hili halitafuatiwa kwa umakini zaidi, litaendelea kuwepo kwa sababu unapokuja na mzigo wako kama mwananchi au mfanyabiashara bandarini, unategemea kuwa siku chache utoe mzigo wako lakini sheria iliyoko bandarini ni kwamba

baada ya wiki moja mzigo ukibaki bandarini kunaongeza *storage*, kwa hiyo *storage* tu ikiongezeka mwananchi wa kawaida anatakiwa kulipa ushuru wa kuongeza *storage*. Hivi utaratibu huu wa kuongezeka kwa *storage* kutoka toka siku ulipokuja na mzigo labda umefika wiki moja iliyosababishwa na watumishi, wiki ya pili iliyosababishwa na watumishi, wiki ya tatu, *storage* hii kweli anatakiwa mfanyabiashara huyu kuilipa wakati aliyesababisha ni mtumishi wa *TRA* au wa Idara ya Forodha, haiwezekani! Tunajenga imani mbaya kwa Serikali yetu. Mapato mengi kupitia *TRA* yanapatikana kama ilivyotueleza bajeti lakini kuna mianya mikubwa ya rushwa pale kusababisha hawa kuongeza *storage* ili kutoa rushwa kuweza kutolewa mizigo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukusanyaji wa mapato, mapato ya kodi na yale yasiyo ya kodi. Kwanza niipongeze sana Serikali kwa kuweza kukusanya mapato kutoka 58% hadi 61%, lakini Serikali imetueleza kwamba mapato yasiyo ya kodi hayaridhishi kutokana na kutokuwa na wataalamu, kutokana na uwezo mdogo wa ukusanyaji, kutokana na vifaa duni na mfumo dhaifu wa ukusanyaji. Hivi Serikali inatueleza nini hapa? Serikali iimarisha hili suala, kwa nini kunakuwa na udhoofishaji hii, kwa nini kunakuwa na kukosa wataalamu kwenye mapato kama haya, kwa sababu tunataka kuongeza mapato ya Serikali, kwa nini kunakuwa na kitu kama hiki? Serikali lazima ifuatilie na isimamie vya kutosha ili kuhakikisha kuwa mapato haya yasiyo ya kodi yanaongezeka. Naipongeze sana Serikali lakini usimamizi uwepo na kuhakikisha vyombo vinawekwa vinavyoweza kukusanya mapato kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, katika Serikali za Mitaa...

**SPIKA:** Ahsante.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Sasa nimwite Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Saidi Zubeir na Mheshimiwa Tauhida Galos Nyimbo.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nianze tu kwa kusema kuwa nawapongeza sana wananchi wa Wilaya ya Muheza kwa kazi nzuri walioifanya. Katika uchaguzi uliopita, Chama cha Mapinduzi kimeshinda katika Kata zote mbili. Wenzetu wa CHADEMA walituletea hata watu wa kuhesabu kura Muheza wakidhani hatujui kusoma wala kuandika lakini naomba niwakumbushe kuwa katika msingi nchi ya Tanganyika, shule ya kwanza kuanzishwa wakati huo Tanganyika ilianzishwa pale Muheza na hata Mwalimu wa Mwalimu wa Baba yetu wa Taifa alitokea Muheza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikupongeze vilevile sasa Bunge limekuwa Bunge kweli katika mfumo wa bajeti. Lilikuwa ni Bunge la kupitisha bajeti kama *rubber stamp* tu kwa sababu mapendekezo yanaletwa na hatuwezi kufanya mabadiliko yoyote, leo mapendekezo ya Wabunge yamepewa thamani na ndiyo maana katika sekta mbalimbali fedha zimeongezeka. Kwa hiyo, tuko katika mfumo kweli wa kusimamia bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini nizungumzie mafanikio hayo katika sekta moja tu, Wizara ya Maji, matatizo ya maji yako kila mahali Tanzania nzima, lakini kutokana na michango mizuri ya Wabunge fedha zinaweza kuongezeka kwa ziadi ya shilingi bilioni 184. Haya ni mafanikio makubwa na naiomba Wizara ya Fedha sasa iangalie na iangalie kipaumbele namna ya kutoa fedha hizi ili kweli miradi ya maji iweze kutekelezwa na tatizo la maji kitaifa liweze kupungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Muheza ni miongoni mwa maeneo yenye matatizo ya maji. Tuna mradi mkubwa ambao ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, nina imani katika fedha hizi zilizoongezeka mradi huo wa Muheza wa maji kutoka Mto Zigi utakamilishwa hasa ukizingatia upembuzi yakinifu umeshakamilishwa na ripoti zote zipo Wizara ya Maji, zipo

20 JUNI, 2013

TAMISEMI na nimeona nakala imeshapelekwa Wizarani ya Fedha. Kwa hiyo, naomba utekelezaji ufanyike.

Mheshimiwa Spika, lakini ni lazima tuangalie nini matataizo yetu katika bajeti zetu. Mimi nitazungumza maeneo machache tu na nitajikita katika Wizara hii ya Nishati na Madini. Katika Wizara hii ya Nishati na Madini kuna matatizo makubwa. Naishukuru Serikali imeunda chombo cha kufanya tathmini na ukaguzi katika sekta ya madini. Katika muda mfupi ambapo chombo hiki kimefanya kazi, wameweza kugundua fedha na kodi nyingi sana ambazo hazikuwa zinalipwa na makampuni makubwa ya madini huko *Geita Mining* wamekiri kwamba ni kweli zipo fedha ambazo walikuwa hawajazilipa. Sasa naomba fedha hizo zikusanywe na chombo hicho kitumiwe vizuri na wale ambao hawakulipa walipe fedha hizo na riba. Ni fedha nyingi sana, taarifa ipo kwa wakaguzi wale, naomba mpate nakala tuweze kufuatilia kwa makini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini niseme vilevile kuwa bandarini bado kuna matatizo, wenzangu pia wamesema tusaidiane na Waziri katika mpango wa kuiwezesha bandari kufanya kazi vizuri. Mapato mengi sana yanachukuliwa na watu binafsi na Serikali haipati kitu, tuangalie huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tungalie pia maeneo mengine ambayo tunatumia fedha nyingi sana za Taifa katika Wizara hiyohiyo ya Nishati na Madini. Katika mfumo huu wa uzalishaji wa umeme wa dharura, *capacity charge* tunazolipa *IPTL*, *SYMBION*, *AGGREKO*, ni fedha nyingi kupita kiasi. Leo mikataba ile inasema kwamba sisi *AGGREKO* mashine zile za kuzalisha umeme siyo za Watanzania ni za kwao lakini mashine zile sisi Watanzania ndiyo tununue mafuta ya kuendesha mashine zile tupate umeme. Ndani ya mikataba hiyohiyo wanasema vilevile mashine zile ambazo siyo za kwetu *TANESCO* ambao ni Tanzania, sisi ndiyo tuzifanyie *service* mashine zao! Hivi kweli mikataba ya namna hiyo itawezesha sisi kupata fedha ya kutekeleza bajeti yetu hii ambayo sasa hivi ni muhimu sana? Tunafanya *service* mashine ambazo siyo za kwetu! Sasa ni lazima tuangalie mfumo wa kuongeza mapato lakini mfumo wa kusimamia matumizi ya

fedha ni muhimu ili fedha tunazozilenga ziweze kwenda kwenye mipango ya maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie jambo lingine ambalo nimeliona. Kuna viwanda vya kuzalisha *cement* hapa, kule Tanga kipo, Dar es salaam na Mbeya, matatizo yameanza kujitokeza, viwanda vina uwezo wa kuzalisha *cement* ya kukidhi mahitaji ya *cement* yaliyoko hapa kwa sasa Tanzania lakini badala ya viwanda hivyo kuzalisha *cement* hiyo kukidhi mahitaji, tunatoa fedha zetu dola kuagiza *cement* kutoka nje! Ni nini matokeo ya mpango huo? Tunatoa fedha zetu tuaangiza *cement* wakati *capacity* ya kuzalisha *cement* hapa ipo. Madhara makubwa ni nini?

Mheshimiwa Spika, viwanda vile wamekuja wawakilishi wao na wanasema kwa sababu tunaagiza *cement* kutoka nje, wao wanapunguza uzalishaji, maana yake ni nini? Maana yake tutaendelea kutumia fedha nyingi kuagiza *cement* na tunasimamisha uzalishaji hapa lakini kibaya kuliko yote ni kwamba wanapunguza wafanyakazi, hawawezi kuzalisha, wanapunguza wafanyakazi. Sasa badala ya kuongeza ajira, sisi tunachangia katika mfumo wa kupunguza ajira. Hili ni jambo ambalo kwa kweli halifai na Waheshimiwa Wabunge ni lazima tulikemee jambo kama hili. Tumemaliza kwa kufunga viwanda vyote vya nguo hapa, kulikuwa na *Killitex*, *Mwatex*, *Sugurates*, viko wapi? Zaidi ya watu 10,000 walikuwa wakiajiriwa na viwanda hivi, vyote tumevisimamisha leo tunahama kutoka viwanda hivi vya nguo tunahamia sasa kwenda kusimamisha ajira katika viwanda vya *cement*. Hili jambo siyo jambo zuri, halifai wala mimi siliungi mkono na nina uhakika Waheshimiwa Wabunge hatutakubaliana nalo. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri kwa kuwa wewe ni Waziri wa Fedha, anayeidhinisha fedha za mauzo ya kuagiza *cement* ni Benki Kuu ya Tanzania kwa kutumia fedha zetu za nje, basi weka mkono wako kule na tuangalie utaratibu kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara pia kuhakikisha hatuagizi *cement* na tunatumia viwanda vyetu na uwezo waliokuwa nao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Said Zuberi ajiandae.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kukupongeza kwa wazo lako zuri la kuanzisha utaratibu huu unaotumika kwa sasa wa kujadili bajeti ya Serikali kuanzia mwezi Aprili mpaka sasa. Nikupongeze pia kwa kuunda Kamati ya Bajeti ambayo imetusaidia sana kuona mambo mengi na kurekebisha mambo mengi na kuishauri Serikali yetu. Nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge ambao wamekwishachangia kwenye sekta mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kwanza suala la amani ya Tanzania. Napata wasiwasi na mshtuko mkubwa ninapooona sasa hivi katika maeneo mbalimbali tunakuwa na wasiwasi na mimi hapa ninaogopa kwenda Arusha kwenye mikusanyiko mbalimbali kule kwa sababu amani ya Mkoa ule imekuwa tete. Nimpongeze Waziri Mkuu na niungane naye kwa majibu yake ya leo kwamba hawa wanaovunja amani ya Tanzania, tuwasake kama tulivyomsaka Nduli Iddi Amini katika kipindi hicho cha miaka ya 1979. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Nawahurumia akina mama na watoto kama alivyosema Waziri Mkuu kwamba vita ikitokea hatuna pa kukimbilia, hatuna mjomba, hatuna shangazi katika nchi za jirani zetu. Kwa hiyo, amani ni wajibu wa kila Mtanzania, tuidumishe amani yetu, tuishi kwa amani ili tuendeleo kuwa kisiwa cha amani kwa majirani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili barabara zetu zidumu lazima reli ifanye kazi. Waheshimiwa Wabunge wameongelea sana suala la reli na niipongeze Serikali kwa kusimamia ujenzi wa barabara za lami kuunganisha Mikoa na Mikoa kwa njia ya lami lakini kama reli haitafanya kazi maana reli inapita katikati ya Tanzania mpaka Mwanza, mpaka Kigoma lakini mpaka Zambia pia na Katavi lakini sasa kama magari ya mizigo kila siku yatapita kwenye barabara zetu za lami, hizi barabara hazitadumu. Nawapongeza sana Wizara ya Uchukuzi kwa juhudi zao wanazozifanya lakini pia uwepo



mkakati maalumu wa kuhakikisha kuwa reli zinafanya kazi siku saba za wiki. Ndiyo tutakapowezesha barabara zetu kudumu la sivyo barabara hazitadumu na kila siku tutakuwa na matengenezo ya mara kwa mara na bado tutakuwa na kazi kubwa ya kutengeneza barabara zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee pia katika sekta ya kilimo. Asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima na Serikali yetu imetangaza mapinduzi ya Kilimo Kwanza lakini asilimia 80 ya wakulima ni wangapi ambao ni wakulima wkaubwa? Wakulima wadogo waliopo hawakopesheki kutokana na riba kubwa ya benki zetu. Uwepo utaratibu, kama kweli Serikali ina nia ya kumwendeleza mkulima ambayo ni asilimia 80 ya Watanzania, basi Benki ya Kilimo ianzishwe haraka sana ili iwasaidie wakulima wadogowadogo. Wakulima wadogowadogo bado wanalima kwa jembe la mkono. Jembe la mkono huwezi kusema kwamba sekta ya kilimo itakua kwa haraka sana, haiwezi kukua kwa haraka! Sekta ya kilimo bado haiwezi kukua kwa haraka kwa sababu ya jembe la mkono, kwa sababu wakulima wadogo hawakopesheki ambao ni karibu asilimia 78 ya wakulima. Uwepo utaratibu wa kuanzisha benki ambayo itatoza riba kidogo sana kwa wakulima wadogowadogo ambao ni asilimia 80 ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee sasa ukusanyaji wa mapato. Huwezi kuamini, Tanzania bado ni nchi ambayo unaweza kununua vitu kwa mamilioni ya pesa na usipate risiti. Kwa njia hii tunaibiwa sana na bado *TRA* wanasema wanajitahidi kukusanya mapato, mimi sikubaliani nao! *TRA* hawakusanyi mapato ipasavyo. Hatupewi risiti kwa manunuzi tunayoyafanya na bado nchi hii manunuzi yanafanyika kwa dola za kimarekani. Nenda Dar es Salaam pale, kuna maduka unauziwa kitu kwa dola za Kimarekani. Tena ukiulizia anakuambia bei imepanda, hasa vifaa vya elektoniki, wanakuambia thamani ya dola imepanda jana mama, kwa hiyo, bei ya jana na bei ya leo tofauti. *TRA* waangalie jambo hili, haiwezekani! *(Makofi)*

20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, wanasema kwamba hawana watalaam, wasomi wamejaa mitaani kibao wanatafuta kazi, si waajiriwe *TRA* wakakusanye mapato? *TRA* wasimamie mauzo na manunuzi, kila anayenunua apewe stakabadhi. Tena wenye maduka wanakupa *option*, unataka risiti ya *TRA* yenye pesa nyingi au unataka risiti isiyo ya *TRA*? Mkulima aliyetoka kijijini atasemaje kuhusu stakabadhi anayotakiwa kupewa? Atachagua ile ambayo haina gharama ambapo *TRA* inapoteza mapato! Hilo *TRA* waliangalie, siyo kila siku kodi inapandishwa kwenye pombe, sigara, siku Watanzania wakiokoka itakuwaje? Tanzania ni nchi tajiri sana, tuna madini, tuna maliasili kiasi kwamba tukisimamia vizuri ukusanyaji wa mapato, tunaweza kufika mbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nisikitike kwamba *TRA* hawa wamezuia silaha ambazo zingetumika kukusanya na kuzuia ujangili katika maeneo ya hifadhi zetu kwamba walipe kodi. Huyo Askari anayezuia ujangili, anauawa na majangili na pesa zinakwenda *TRA* na wao wanakula mezani bila kujua hizo fedha zimetoka wapi lakini silaha wamezuzuia. Naomba Waziri hili ulijibu wakati wa kuhitimisha bajeti yako, kwamba silaha zile ambazo zimekataliwa na *TRA* zisitumike na Maliasili zinaachiwa lini? Kwa sababu Serikali ni moja, kwa nini silaha zile zisiachiwe, zimezuiliwa na *TRA* kwa sababu hawajalipa kodi, kwani hawawezi wakatamia na kesho yake wakalipa kodi? Naomba hili ulijibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la fedha za miradi ya maendeleo. Kwa Mkoa wangu wa Dodoma mpaka mwezi Mei tulikuwa tumepata asilimia 30, Wilaya zingine asilimia 40 na hii husababisha miradi kukwama kwa muda mrefu sana. Tunalo jengo la Mkuu wa Mkoa hapa tangu mwaka 2007/2008 lilikuwa na thamani ya shilingi bilioni tatu lakini mpaka leo lile jengo halijakamilika pamoja na mwaka huu wametengewa fedha lakini fedha ambazo zitatumika kukamilisha lile jengo siyo shilingi bilioni tatu kama tulivyotegemea, hii ni kwa sababu fedha za miradi ya maendeleo zinachelewa sana Hazina.

20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, tuliomba fedha kwa ajili ya maji ya wananchi wa Bahi kwa sababu maji yaliyopo pale hayafai kwa matumizi ya binadamu. Tuliomba shilingi bilioni moja na milioni mia tano, tangu mwaka 2010/2011 mpaka leo hizo fedha hazijaja. Leo mradi ule tena hauna thamani ya shilingi bilioni 1.5 kwa sababu ya kuchelewa kwa mradi fedha zinahitajika zaidi. Halmashauri ya Bahi wameambiwa wahamie Bahi hakuna maji pale, kila bajeti tunaongelea suala hili la maji ya Bahi, hakuna anayeskiliza, hakuna fedha zinazopelekwa pale, wananchi wa pale sijui baada ya miaka kumi inayokuja mtawatibu kwa shilingi ngapi?

Mheshimiwa Spika, kuna mradi wa umwagiliaji kule Bahi, ulitengewa shilingi bilioni na zimetumika, lakini tangu Serikali iingilie suala la kutengeneza miundombinu ya mradi wa umwagiliaji Bahi, ule mradi umesimama. Mchele unaoliwa Dodoma na Singida unatoka Bahi. Mradi ule umesimama, hakuna maji, miundombinu mibovu kwa sababu ya watumishi wa Serikali ambao wametengeneza miundombinu ya pale. Mradi ule ulikuwa unasaidia vijiji vya Mtitaa, Uhelela, Chikopelo, Mtazamo lakini sasa hivi ule mradi umesimama, wakulima wanalia. Pamoja na shilingi bilioni mbili kuteketea pale hakuna kinachoendelea. *(Makoff)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na fedha za miradi ya maendeleo kuchelewa, tuna zahanati ya Dabalo, Makoja, tangu mwaka juzi tumeomba fedha, wanawake wanatembea zaidi ya kilomita 20 kutafuta matibabu, zahanati zile hazijakamilika tena kwa fedha kidogo sana. Niambie leo fedha ambazo zitatakiwa kukamilisha miradi hii ambayo imesimama kwa miaka mitatu minne, ni fedha chungu nzima. Naiomba Wizara ya Fedha sasa, leteni fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, suala la uendelezaji Makao Makuu ya Serikali Dodoma ambalo limepewa jukumu hilo Shirika la CDA. Katika mpango wa maendeleo wa 2015-2025, suala la kuhamia Dodoma halipo kwenye mpango huu wa Serikali. Naomba leo Serikali iwaambie wana Dodoma, hivi wana nia ya dhati kweli kuhamia Dodoma? Kama kwenye mpango

20 JUNI, 2013

wa miaka 2015-2025 hakuna mpango wa kuhamia Dodoma, tuambieni tujue? Mbona mnaendelea kujenga ofisi za Wizara mbalimbali Dar es Salaam? Tuambieni tujue jamani ili tuone namna ya kuendeleza Mji wetu. *CDA* wapo pale, hakuna fedha wanazopewa, mwaka huu wamepewa fedha za maendeleo shilingi milioni mia tano pamoja na kwamba Mradi wa Uendelezaji Miji umetusaidia lakini Serikali inawajibika kuendeleza Mji wa Dodoma kwa nia ya Serikali kuhamia Dodoma. Kuna majengo machache sana ya Serikali ambayo yanajengwa Dodoma lakini mengi yanaendelea kujengwa Dar es Salaam. Wakazi wa Dar es Salaam wanalalamika Mji umebana, watu ni wengi, majengo ni mengi, usafiri ni shida. Ni shida kwa sababu Serikali imekataa kuhamia Dodoma wala haijengi majengo yake Dodoma, wala haisaidii *CDA* kuendelea Mji wa Dodoma. Naomba tamko la Serikali Mpango wa Maendeleo wa 2015-25, mpango wa kuhamia Dodoma haupo, tuambieni mnawaambia nini wananchi wa Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Said Zubeir na Mheshimiwa Tauhida Galos Nyimbo ajiandae.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nami nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na mwenye kurehemu, kwa kunipa uwezo muda huu kuweza kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nimpongeze Waziri wa Fedha pamoja na Mawaziri wenzake, wanafanyakazi kubwa na inayoleta mwelekeo, inaonekana kwamba hawa wana lengo la kutaka kuisaidia nchi hii.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu chake ukurasa wa 53 amezungumzia kuhusu mfumo mpya wa uandaaji na utekelezaji wa vipaumbele vya miradi ya maendeleo. Naendelea kuishauri tu Serikali...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ndani ya Bunge si mahali pa kuongea mtoke mkaongee nje. Endelea.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwamba waendeele kuwa wasikivu na waelewe kwamba hali yetu siyo nzuri, tuwe na vipaumbele vichache kama tuna nia ya kutaka kuongeza mapato kwenye nchi yetu, vinginevyo tutakuwa tuna-*mark time*. Kwa hiyo, walifikirie sana hili na wao ni watalaam watuletee basi vipaumbele badala ya sita angalau viwe vitatu au viwili lakini tujue kwamba hivi tunavishughulikia na vinakamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la umeme. Mimi nafikiri pengine watakapokuja na vipaumbele vyao sijui hicho watakiona ni cha kwanza, cha pili au tatu lakini mimi naona kama ndiyo *generation* ya kuweza kuisaidia nchi hii kutoka hapa ilipo na tukasonga mbele. Hii ni kama jenereta. Tukifanikiwa kwenye suala la umeme basi mambo yetu mengi nahisi yatakaa sawa, kwa sababu bila ya umeme hakuna viwanda na bila ya viwanda hakuna uwekezaji, hakuna mtu atakayekuja hapa wakati pako kiza aseme anakuja kuwekeza. Jambo hili wajaribu kulitazama na kulisaidia naona jitihada ipo kubwa lakini basi tuendeele hasa ku-*dump* pesa kwenye eneo hili ili tuhakikishe kweli tunang' atuka hapa tulipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine kama tunataka tuongeze mapato basi ni lazima tuelekeze nguvu zetu kwenye viwanda vidogovidogo siyo viwanda vikubwa. Sisemi kwamba tuache moja kwa moja kwenye viwanda vikubwa la hasha, ila ni lazima tuwe na *strategic* za kuwasaidia wakulima wadogo pamoja na viwanda vidogo, wapewe nguvu *SIDO* waweze kututengeneza viwanda. Sasa hivi *SIDO* wamekuwa kama wasanii, wanakuja na mashine yao moja, ukiwatazama wenyewe wamenenepa, vitumbo vimetangulia kama vibla vinaongoza, lakini baada ya hiyo mashine yao moja ambayo wanatuonesha kama ni *sample* hawana kitu kingine chochote. Tanzania hii ni nchi kubwa sana huwezi kusema ni moja hata kumi bado ni kidogo, maeneo makubwa ya kulima yapo lakini viwanda

20 JUNI, 2013

vidogovidogo ya kuongeza thamani yale mazao havipo.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna ule mpango wa fedha za Rais tunazoiita fedha za JK, mimi naona fedha kama hizi huu ni wakati muafaka wa kuzichukua na kuzipeleka kwa hawa *middlemen* siyo tupeleke kule chini moja kwa moja kama ilivyofanyika. Fedha utakapozitawanya chini, watu hawana elimu, watapokea zile fedha, watakusanyana kufanya vikao vya harusi pamoja na kwenda *day out* wanamaliza zile pesa lakini kama zingelekewa kwenye *layer* ya katikati ambako ndiyo *source* ya kila kitu, hapo ndipo patapatikana viwanda vidogovidogo na hapa ndipo zitakapopatikana ajira. Maana tunapozungumzia viwanda vidogo tunazungumzia kiwanda ambacho pengine kitaajiri watu wasiopungua 20 ama 15, ajira hapo imeshapatikana, mapato yanaingia, viwanda hivi tutakuwa tunavielewa na vitakuwa vingi kama utitiri kama tunavyoona China wenzetu walivyoweza kuendelea. Kwa hiyo, tutakuwa na uwezo wa kukusanya kodi humu kuliko kuendelea kubana tu humohumo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyobana hizi kodi na tukawaongezea hawa waliojikubalisha kulipa kodi, matokeo yake nao hushawishika kwa kuona sasa ni wakati muafaka wa kukimbia kulipa kodi na kuingia kwenye masuala mengine. Kwa sababu kila siku tunapokaa na kufikiri kwamba wapi tutaongeza kodi au wapi tutapata kodi mpya basi sisi jibu letu ni kwamba wale ambao tayari wapo makini na wameamua kuisaidia nchi wanatoa kodi kama kawaida ndiyo tunawaongezea. Huu mzigo utakuwa ni mkubwa kwao, Watanzania tupo wengi na tuna uwezo wa kuchangishana kidogokidgo kodi ikawa kubwa, sasa tuwawezeshe. Tutawawezesha vipi ili waweze kulipa kodi? Fedha kama hizi zinapopatikana, zipelekwe watu wakahamasishwe watengeneze viwanda vidogovidogo na hivi ndiyo vitatusaidia kwa sababu mtu akishaona huko kijijini kuona kuna kiwanda kidogo atahamasika kwanza yeye mwenyewe kulima ili hicho kiwanda kifanye kazi halafu ndiyo tuwabinafsishe. Tukienda kwa mtindo huu, mimi naona hii nchi kwanza itakuwa haina njaa, tutakuwa tuna uwezo

20 JUNI, 2013

mkubwa wa kuuza chakula nje na mapato yatakuwa makubwa tofauti na tunavyorajia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo naona kila siku ni kizungumkuti, tunazungushana tu, ni malipo yanayotokana na masuala ya madini. Hapo utaambiwa kuna mrahaba, wengine wanakuambia mrabaha ili mradi tunazungushana lakini ukweli ni kwamba kodi hailipwi kama inavyostahili kulipwa. Huko jamani nako twendeni, kama tunahisi wanalipa ndiyo inastahili, tuongezeeni kama tunavyoongeza huku kwenye vinywaji na huko tuongeze tusiwaache! Tunawasahau kwa nini? Kama wakiacha kufanya hizo kazi basi yale madini yaacheni yakae, watakuja kufanya kazi wengine kama ni vizazi vijavyo ama kama ni watu wengine ambao wanahitaji wapate faida na nchi hii iendelee, siyo kuinyonya hii nchi. Halafu sisi tunasahau kabisa kama tuna maeneo mazuri ya kuweza kukusanya kodi lakini matokeo yake tumeelekeza nguvu kwenye bajaji ambao wao ilikuwa waachiwe kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kwenye suala la *deposit TRA*. Suala hili nalizungumza kwa masikitiko sana, haidhuru sasa hivi Rasimu inazungumzia suala la Serikali tatu lakini ile ni Rasimu na tutatizama bado ina mchakato mkubwa lakini bado sisi tuna haki ya kuendelea kutetea lile ambalo kwa wakati huu tunalo. Ni maajabu makubwa kama tunasema sisi ni Watanzania, Tanzania Bara na Tanzania Visiwani lakini mtu anapotoka na gari yake Tanzania Visiwani kuleta huku aambiwe aweke *deposit*. Hili suala halikubaliki! Tukubali kwamba hili suala halikubaliki na tutafute njia za kurekebisha na si kutafuta njia za kurekebisha ni suala la kuondoshwa, tunatafuta njia ya nini na sisi tunasema sote ni Watanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naona sasa umefikia wakati jamani, au kama ndiyo hilo lengo la kuelekea kwenye Serikali tatu mlikuwa nalo mapema, hizi bugudha zingine wala hazina maana, hazina tija. Si suala la kukaa na watu wakatafuta kuchanganua pamoja na utafiti, hili suala lipo ni suala la kuondoshwa tu. Kodi imeshalipa kule, gari mtu

20 JUNI, 2013

atakuja nalo huku kama sisi Wabunge *sometime* tunataka kuchukua gari zetu kule tunaambiwa pale tutoe fedha, hizo fedha huko Majimboni tupeleke fedha, fedha hizo zipo ngapi? Jamani hili naomba liishe mwaka huu, tutakapoanza Serikali tatu tutajua kama na sisi tutatakiwa tulipe ushuru au nini, tutajua baadaye lakini sasa hivi bado tuna Serikali mbili na Tanzania ni moja. Mtu atoke zake Rwanda, atoke huko aje aingize tu gari kiholela, iwe yeye ana nafasi kuliko sisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili halikubaliki nakuomba sana kupitia kwako hili suala limalizike ikiwezekana haraka sana, linatumuuzia. Katika kero kubwa kwa watu wa Zanzibar hili nalo limo, linatusumbua sana. Achilia mbali hayo masuala mengine tunazungumzia ya 4.5, lakini hili liko wazi na sijui nani mhusika maana yake kama kusema tumesema sana hapa lakini bado hakuna marekebisha au watuambie kuna nini, au ndiyo huu mfumo tunakwenda nao sasa hivi wa Serikali tatu, sawa lakini bado hatujafikia huko, bado tuna Serikali mbili mpaka tumalize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba hili suala ikiwezekana Bunge lijalo tuweze kutoa gari zetu kule na sasa hivi Bakharesa ameturahisia kuna meli yake kubwa anachukua tu zile gari zetu anaziingiza mle tunakuja nazo hukoi. Sasa hivi sisi wengine tunapata taabu, anahangaika na teksi ili mradi mashaka kwa sababu anafikiria kwamba pale akalipe pesa, akalipe pesa ya nini na sote ni Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili nimelisema kwa uchungu sana na linatuuma sana watu wa Zanzibar na hili mimi naweza hata nikalia kabisa hapa, katika mambo ambayo yanatusumbua hili ni mojawapo. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Usilie.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Nisilie? *(Kicheko)*



20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, nataka niwakumbushe watu wa Wizara ya Fedha kwamba tuliahidiana kwenye *mini tiger* kupatikana fedha katika bajeti iliyopita lakini...

*(Hapa Kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Eeh!

**SPIKA:** Haya. Sasa namwita Mheshimiwa Tauhida Galos Nyimbo atafuatiwa na Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii kuchangia Wizara hii ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii ya pekee kukipongeza Chama changu cha Mapinduzi kwa ushindi mkubwa walioupata kupitia Katibu Mkuu wetu pamoja na Sekretarieti yake yote. Ningekuwa mtangazaji wa mpira ningesema wamewapa wapinzani wao kipigo cha paka mwizi. Hii ni dalili za kuelekea mwaka 2015. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe mwenyewe binafsi kwa mwenendo mzima wa bajeti tuliouanza mwaka huu. Nisisahau pia kuwapongeza Wabunge wenzetu waliorudi Bungeni hasa kijana mwenzetu Mheshimiwa Aeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Manaibu wake wote wawili. Kazi wanayofanya ni nzuri, inaonekana, inavutia machoni mwa watu lakini machoni mwa jamii inaleta matumaini. Pamoja na kusema haya Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri, bajeti iliyokuja ni nzuri, imewalenga wananchi lakini kuna mambo mawili, matatu, naomba nichukue fursa hii kuyazungumzia. Kuna makato ya wafanyakazi wanaotokana na Wizara za Muungano. Imeibuka kero kubwa na manung'uniko makubwa miongoni mwa Wazanzibar kujua fedha hizi kurudi kwao ndani ya Zanzibar na imekuwa na malalamiko. Hili nililizungumza

wakati nachangia Wizara ya Muungano. Nikasema kwa nini mambo mengi ndani ya Tanzania hayatolewi ufafanuzi kwa wananchi. Narudia kusema tena, mambo mengi mazuri yanayofanywa na Serikali yetu hayatolewi ufafanuzi kwa wananchi. Tumbakiwa nayo sisi viongozi, tunabaki kujua sisi viongozi wachache kuliko kujua wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nifano mdogo wa hili, sisi tutaelewa tulikukuwemo humu ndani, tunawawakilisha wananchi kwamba makato haya yanarudi Zanzibar lakini wananchi wanapotoshwa, wananchi wa Tanzania wanapotoshwa, hawaambiwi ukweli, kama inarudi, inarudi kwa wakati gani? Kipindi gani? Idadi ya wafanyakazi waliokuwemo ndani ya Muungano ni wangapi? Fedha zinarudi kwa kipindi kipi na shilingi ngapi? Kuchelewa kwa mwezi mmoja, miezi miwili, siyo tatizo. Tatizo lililokuweco wananchi waambiwe kwamba fedha hizi zinarudi na zinarudi kwa wakati upi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri kupitia Wizara yako, mchukue mstari wa mbele msaidiane na Wizara ya Muungano kuwapa taaluma wananchi katika hayo mambo mazuri mnayoyafanya. Hili pia tunaomba mlitolee majibu, maana tayari linaanza kuwa motomoto Zanzibar wa kuambiwa kwamba Wizara hairudishi fedha hizi na wakati kitu hicho si kweli.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, nizungumze kwa masikitiko makubwa sana, kuna suala la fedha za Majimbo tutalizungumza hata mara ishirini ndani ya Bunge hili lakini kero zimetukera tutaendelea kuzitungumza. Suala la fedha za Majimbo, leo pesa zinapelekwa ndani ya Halmashauri za Zanzibar, mimi nimekuja hapa natokea ndani ya Halmashauri, nimeuliza wakati nakuja huku mpaka kufikia leo hazijawahi kukaguliwa. Kodi zinatokana na fedha za wananchi iweje zipelekwe halafu zisimamiwe ukaguzi kujulikana fedha zile zinafanya kazi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zile fedha tuone huruma, tuchukue imani pamoja na kwamba tuongeze mapato, Serikali yetu tutafute njia gani, lakini pia tuwe na usimamizi mzuri wa

matumizi ya fedha. Tunataka tujue matumizi ya fedha zile yalivyokwenda na tunataka tujue chombo mhimili kinachosimamia fedha zile. Ukiniambia kwamba sasa hivi ndiyo tunarekebisha fedha zile zitasimamiwa na Bunge, tunataka tujue huko nyuma zilikaguliwa? Kama zilikaguliwa, zimetumika kama Serikali ilivyokusudia? Hayo ndiyo tunayoyataka katika majibu yenu mtakayokujanayo na hilo lije. Mkumbuke zile pesa ni watu wanaodoa kodi ni wanyonge. Kwa hiyo, kama wanyonge ndiyo wanaotoa kodi zile tuhakikishe tunawapa majibu ya fedha zao tunazozikusanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mengi yaliyokuweco, kaka yangu Said kazungumza kuhusu magari lakini suala la bandari Mheshimiwa Waziri na Naibu msaidiane na Wizara zilizokuweco pale, hebu fanyeni ziara muende pale. Bajeti yetu imejikita sana kutatua matatizo ya vijana lakini pale bandarini yako matatizo, vijana na akina mama, nimeshawahi kulizungumza na swali kwa Waziri Mkuu nimeshawahi kuliuliza. Kwa nini kuna kodi ambazo hazina msingi? Kodi zile tunataka kuzijua nani anatoza kodi zile kwamba unatoka na mzigo wako Kariakoo, wanawake, wa mama wajasiriamali, wamenunua bunda za rasta, wamenunua vinguo viwili vitatu wanapita wanaambiwa walipe na risiti wanazo. Zile kodi zinakwenda wapi na nani mkusanyaji wa kodi ile na sababu zipi za kukusanya kodi zile. Bodaboda tumeondosha leseni lakini na pale kero ile iondoke. Mheshimiwa Waziri hizi kero zinawezekana kuondoka, hazina sababu ya kuendelea. Zanzibar haipo kodi ile, wanakuja wanachukua vitu viwili, vitatu wanakuja zao huku kama wajasiriamali wanauza lakini kero ile iko bandari ya Dar es Salaam, tunataka Mheshimiwa Waziri uisikie kero hii na kuiondosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la kuporomoka kwa shilingi yetu ndani ya Tanzania. Fedha ya kigeni imekuwa kila siku inapanda lakini shilingi yetu kila siku inashuka. Hivi Mheshimiwa Waziri nakuuliza ndani ya Wizara hakuna Wachumi na kama wapo hawazioni kazi za kufanya? Muda wao wa kufanya kazi ni muda wa bajeti tu? Maana naamini sana kama Wachumi wamo ndani ya Wizara

yako, wanafanya kazi, kwa nini wasitafute mbinu ya kuipandisha shilingi yetu? Naamini shilingi yetu ikipanda ndani ya Tanzania uchumi unapanda, uchumi utakuwa, bidhaa zitakwenda, kila kitu kitakwenda vizuri lakini kupanda kwa shilingi yetu ndiko kutakakosababisha haya yote kuweko hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala zima la Mfuko wa Pamoja wa Fedha. Mfuko wa Pamoja wa Fedha ulikuwa unatumia kigezo cha 4.5. Mfuko huu umetumika mpaka hapa tulipo wa 4.5 lakini umepitwa na wakati. Tunataka hivyo vikao vimekuweko mpaka leo bado hawajafikiria kubadilisha mfumo huu? Maisha yamebadilika, watu wameongezeka, majukumu yanakua, nchi inakuwa, kwa nini bado tuangalie kigezo hiki hiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii hapa nitapazungumzia kwa sababu hata Rasimu imeonyesha kama kutakuweko na Serikali tatu, Muungano utakuwepo, Serikali mbili, Muungano utakuwepo, Serikali nne Muungano utakuwepo, Serikali moja Muungano utakuweko.

**MBUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALOS NYIMBO:** Hapa paboreshwe, tunataka Mheshimiwa Waziri hapa mpafanyie utatuzi. Tunataka suala la Mfuko wa Pamoja litatuliwe na kero nyingine zote zinazohusu suala la fedha zitatuliwe. Mheshimiwa Waziri tunakuomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nichukue fursa hii ya kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, ndiye msemaji wetu wa mwisho mchana huu.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru wewe kwa kazi kubwa uliyoifanya ndani ya Bunge letu kuanzisha Kamati ya Bajeti. Ni kweli tumeona mabadiliko makubwa kwa sababu miaka ya nyuma katika bajeti tulikuwa tukipitisha tu huku tukisema lakini hakuna mabadiliko yoyote lakini mwaka huu nimeona mabadiliko makubwa kwa sababu kila badiliko lililofanyika kwenye bajeti fulani liliweza kufanyiwa kazi kwenye Kamati ya Bajeti na hatimaye katika bajeti nzima tumeweza kuona mabadiliko makubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, sasa nianze kuchangia bajeti hii. Cha kwanza kabisa, nishukuru Wizara hii ya Fedha kwa mambo makubwa ambayo wameyaonyesha katika bajeti yetu hii lakini napenda tu kusema kwamba nilipokuwa nikiangalia bajeti, nikaangalia sensa ambayo ilifanyika mwaka 2012, niki-*base* katika Wilaya yangu ya Geita, niliona kwamba sensa iliyofanyika inatakiwa *i-reflect* sasa bajeti yetu ya mwaka ujao. Nilipokuwa nikiangalia sensa niliona kwamba karibu Wilaya nyingi za Tanzania nikiangalia katika Kanda ya Ziwa, Wilaya ambayo imeongoza kwa watu wengi ni Wilaya ya Geita yenye *population* ya watu 807,619 ikifuatiwa na Wilaya ya Sengerema yenye *population* ya watu 663,034, ikifuatiwa pia na Wilaya ya Kahama lakini Wilaya zingine katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa, Wilaya moja ina *population* ya watu kati ya laki moja na nusu mpaka laki nne. Kwa jinsi hiyo sasa, nachokiomba katika bajeti hii lazima mgawanyo wa bajeti uangalie idadi ya watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba mgawanyo wa bajeti katika Wilaya ya Geita uangaliwe sana kwa sababu tuna idadi kubwa ya watu, watu laki nane siyo mchezo. Kwa mfano, katika mgawanyo wa huduma za jamii hasa katika sekta ya afya, najua kuna changamoto nyingi lakini tuhakikishe kwamba mgawanyo wa dawa uwe wa kutosha sana. Kwa sababu tukipeleka dawa zile zile kama Wilaya zingine, unakuta baada ya siku mbili tu tayari dawa zimekwisha. Nilikuwa nafanya utafiti huo nikiangalia mbona dawa zinaisha kwa haraka sana. Sasa jibu nimelipata kwamba kumbe tuna idadi kubwa ya watu. Kwa hiyo,

20 JUNI, 2013

niiombe Serikali sasa iweke mkakati wa kitofauti kwa kuangalia kwa kutumia sensa ya watu ambao imepatikana katika mwaka 2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, katika Wilaya yetu ya Geita kwa ujumla pamoja na Mkoa mpya, tuna hospitali moja ambayo ni hospitali ya Wilaya, ningepomba Serikali iwekeze sasa kupandisha hadhi hospitali ya Wilaya Geita iwe hospitali ya Mkoa kihuduma lakini pia kwa wataalam pamoja na vifaa muhimu ambavyo vitaweza kusaidia wananchi walio wengi katika Mkoa mzima wa Geita na Wilaya ya Geita. Nasema hivyo kwa sababu tukiangalia katika Wilaya ile wananchi wengi wanahudumiwa katika Wilaya ya Geita ambayo bado haijapandishwa hadhi. Matokeo yake wananchi hawapati huduma nzuri na iliyo bora. Watu wanalala chini kwa sababu huduma ni chache. Kwa hiyo, niiombe Serikali iangalie uwezekano wa kuweza kufanya maboresho katika hospitali hii ya Wilaya iwe hospitali ya Mkoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali iangalie uwezekano wa kuanzisha hospitali nyingine ya Wilaya ndani ya Wilaya yetu ya Geita. Hata ikiwezekana basi nipendekeze kile Kituo cha Afya cha Katoro kifanyike kuwa ni hospitali ya Wilaya yaani iwe na hadhi ya hospitali ya Wilaya ili wananchi wengi waweze kupata huduma karibu na maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tunavyo vituo vya afya mbalimbali, niombe kwa kweli mgawanyo wa dawa, Serikali iangalie wingi wa watu. Kama tu ambavyo nimekwisha kusema tayari kwamba tuna idadi kubwa ya watu. Kwa hiyo, katika vituo vya afya, katika zahanati, Serikali iangalie namna ya kuweza kuleta huduma hizi vizuri kwa wingi kulingana na idadi ya watu waliopo katika maeneo husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, pia hata huduma za maji. Tunasema kwamba katika Wilaya ya Geita kwa *population* ile lazima tuhakikishe watu hawa wanapata maji safi na salama. Niombe sasa Serikali iangalie uwezekano

wa kuleta maji safi na salama ili watu hawa waweze kunufaika na huduma ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipengele kingine ambacho napenda kuzungumzia pia ni madeni ya watumishi. Katika kitabu cha bajeti, ukurasa wa 49 unaonyesha jinsi ambavyo Serikali imeji-*commit*, imesema kwamba itahakikisha inalipa madeni ya watumishi pamoja na wazabuni. Kutokana na suala hilo ambalo limezungumziwa ndani ya bajeti, naomba sasa kupitia bajeti hii ya mwaka 2013/2014 katika Wilaya ya Geita tu, watumishi wa Serikali hasa Walimu, madeni ni Sh.911,412,448. Kwa kweli deni hili ni kubwa sana, inawafanya watumishi wengi hasa Walimu wafanye kazi zao kwa kinyongo. Kwa hiyo, katika Mkoa wa Geita kwa ujumla, deni la watumishi ambao ni Walimu ni Sh.1,346,705,044. Kwa hiyo, niombe Serikali kabisa kwa bajeti hii ya mwaka tulipe madeni ya watumishi wa Serikali. Hiyo tu nimetoa mfano kwa Walimu lakini kuna watumishi wengine katika Idara mbalimbali za Afya ambao wana madeni makubwa ambayo wanatakiwa Serikali kuwalipa. Kwa hiyo, niombe Serikali kwa kweli madeni ya Walimu ihakikishe inatoa kipaumbele cha kutosha kama jinsi ambavyo imeonyesha ndani ya bajeti ya mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kuzungumza kwa habari ya watumishi wa Serikali, katika bajeti kweli imeonyesha kuna punguzo la kodi kutoka asilimia 14 mpaka asilimia 13. Niseme kwamba naishukuru Serikali kwa punguzo hilo japokuwa ni dogo sana. Naiomba Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza kutoka asilimia 14 kwenda asilimia 10 ili mtumishi huyu aweze kunufaika, afanye kazi zake lakini pia aweze kufanya shughuli za maendeleo kutokana na mshahara anaoupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo pia kuna watumishi ambao wanazungushwa sana kupata haki zao za msingi. Kuna watu mbalimbali ambao pengine wameacha kazi kwa muda mrefu sana ambao wamefuatilia haki zao mpaka wamechoka, mafao yao yamechukua miaka 10. Hapa nina mfano wa mwananchi mmoja kutoka

20 JUNI, 2013

Katoro, anaitwa Koplo Sungwa Malimi ambaye amefuatilia kwa miaka mingi, miaka 10 bado anafuatilia haki zake. Niseme mimi mwenyewe hata baada ya kuingia ndani ya Bunge hili, nimefuatilia haki zake, miaka hii minne ndani ya Bunge hili, kila wakati naenda katika ofisi inayohusika kufuatilia madai ya mwananchi huyu. Kwa hiyo, niombe Serikali kweli iangalie kutoa haki za wananchi, madai wanayodai ihakikishe inawalipa kwa wakati na hii itawezesha nchi kuwa na amani na utulivu bila ya hilo wananchi wanakuwa na manung'uniko kwa sababu ya kutokupewa haki zao kwa wakati. Yako madai mbalimbali mengi sana, kwa hiyo niombe Serikali iangalie uwezekano hasa Wizara ya Fedha na Hazina wahakikishe wanalipa madai hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie kuhusu ongezeko la bajeti. Nashukuru sana Serikali kuongeza bajeti mbalimbali. Kwa mfano, katika Wizara ya Maji, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Vijana, Utamaduni na Michezo. Kweli tumeongezewa fedha kwa mfano katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, tumeongezewa shilingi bilioni mbili kwa ajili ya akina mama. Niombe sasa fedha hizi...

*(Hapa kengele ya ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge muda umekwisha. Tukirudi kipindi cha mchana watakaozungumza watakuwa ni Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, Mheshimiwa Vick Kamata, Mheshimiwa Jitu Vrajlai Soni, Mheshimiwa Mwigulu Mchemba, Mheshimiwa Livingston Lusinde, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Bahati Abeid, Mheshimiwa Aliko Kibona, Mheshimiwa Donald Kelvin Max, Mheshimiwa Ole-Sendeka na Mheshimiwa Chomboh.



20 JUNI, 2013

Waheshimiwa Wabunge, wakati wa chai asubuhi, kuna watu walikwenda kunywa chai na kuna mmoja wenu aliacha mzigo mahali, anione ofisini.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.56 Mchana Bunge lilitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, siwa inapoingia hapa ukumbini na ninapokuwa napita hamtakiwi kuzungumza wala kukaa vikundivikundi, Mheshimiwa Rajab, hatufanyi hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaondoka mchana, niliwataja ambao watapata nafasi ya kuzungumza. Tunaanza na Mheshimiwa Mussa Haji Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Vick Kamata, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni na Mheshimiwa Lusinde. Ngoja tuanze na Mheshimiwa Mussa Haji Kombo.

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu sana ya kuichangia nchi yetu na kutaka maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naiomba Serikali, hii 10% ambayo wamezidisha kutokana na bei ya unga wa ngano iondolewe kwa sababu unga wa ngano ni njia moja ya mapato makubwa kwa wanawake wetu. Wanawake hawa wanaopika chapati, maandazi, wanatumia unga wa ngano. Sasa hali hii ambapo tunawatafutia njia nzuri za maendeleo, tukiwapa mzigo kama huu, tunawaondolea nafasi ya kujiendeleza.

Mheshimiwa Spika, la pili, unapoupandisha unga wa ngano mwezi huu, mwezi unaokuja ni Mfungo wa Ramadhani, Waislamu watanung'unika, watazungumza kwamba Serikali, imetupa mzigo uliokuwa hauna msingi. Sasa

20 JUNI, 2013

mimi masuala haya mawili naomba sana kwa sasa hii 10% ya unga wa ngano ambayo imepandishwa iondolewe. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni kweli ni maamuzi ya Afrika Mashariki. Kenya wao, walikuwa wamepandisha zamani wamefikia 35%, lakini sawa siku nyingine Kenya hali yao ya kiuchumi ilikuwa ni nzuri, wananchi walikuwa hawaoni tofauti hiyo. Kwa hivyo, naiomba sana Serikali, iliangualie suala hili hasa kwa kuwaangalia wanawake wetu na pili waangualie kwa mwezi unaokuja, watu wanaweza wakanung'unika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia suala la udhalilishaji wa Muungano kati ya sehemu moja na sehemu ya pili. Muungano huu ulivyoundwa watu wote waliupenda, wakaukubali na hawakuwa na manung'uniko na muundo wenyewe watu 20 kutoka upande mmoja na 20 upande wa pili, 20 inayotoka Zanzibar, wote walikuwa hawajui kusoma. Wengi wao walimaliza Darasa la IV la Kikoloni lakini walikubali kupitisha Katiba iliyowekwa zamani ambayo sasa hivi tunaibadilisha na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, bahati nzuri alikuwa Sheikh Thabit Kombo, jina lake pia tabu kuliandika, Katibu wake alikuwa Mheshimiwa Pius Msekwa, ambaye ana *degree* ya Sheria lakini umetuchukua kwa muda mrefu, tunakubaliana nao, hauna matatizo mpaka tumefika mahali tukaona kumbe utawala huu wa Muungano sasa hautupendelei. Leo Mzanzibari, siku hizi tuna meli ya Bwana Bakhresa, unapakia gari yako ukifika Dar-es-Salaam unakuja nayo Dodoma; hupati heshima hiyo, unatakiwa kwanza uende ukailipie kodi, sijui nini, ghasia kubwa. Natoka nchi moja ambayo Rais wake ni nchi ileile ninayokwenda. Ni sawasawa kama Wazanzibari hawataniukana kusema natoka Morogoro nakuja Dar-es-Salaam, nabadilisha Mkoa tu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hali hii sasa imetufikisha mahali pabaya sana. Wazanzibari wanaamini kwamba hii ni mbinu maalum inayofanywa na Watanganyika, kuwadhalilisha, kuwaonesha kwamba hawana haki katika Serikali ya

Muungano. Kila siku wanakaa Serikali ya Zanzibar, Serikali ya Muungano, kumaliza matatizo yaliyokuwa maisha hawakai yakaisha. Wazanzibari kule nyumbani wanasema sasa *byebye*, sasa mimi sijui maana yake ni nini *byebye*, lakini siku nyingine tutajua na tutaona. Sasa mimi naiomba sana Serikali, tusiwafikishe hawa wakasema *byebye*, twende mahali ambapo tutaweza kukubaliana kwa uzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tukienda bandarini, *baggage room*, boti inayotoka Zanzibar, mtu mwenye begi, mwanamke ana begi lake linasachiwa mara 10. Udhalilishaji mkubwa sana unaopita mpaka sisi wengine tukipita tunaona aibu, ni nini sababu? Mimi sifikiri kama ni kodi, wale wanawake wanaokuja na mabegi yao sifikirii kama wanatizama kwamba kuna vitu wamezidisha, ni udhalilishaji. Tizameni watu ambao wanaheshima, wanaheshimu Muungano wetu, ukishuka bandarini Zanzibar, shuka na magunia yako 40 ya viazi ambavyo utanunua lringa, watu watakachokifanya ni kumlipa yule atakayekuchukulia begi lako la viazi au sanduku lako la viazi au gunia lako la viazi akakupakilia kwenye gari lako; hakuna udhalilishaji, hakuna tabu yoyote, wanakuja na gari, siku hizi hii meli imewasaidia, watu wengine wanakuja *holidays* pale *weekend*. Wanakuja na magari yao, wanateremka, wanakwenda *Nungwi Beach* na wapi, Jumamosi au Jumapili wanarudi ndani ya boti, tunawaheshimu, tunapenda kuwaona wenzetu, hatuwadhaliishi. Naomba tuliangalie sana suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi tulipewa mkopo wa shilingi milioni 90 wa kununua gari...

**SPIKA:** Sisi nani? Yaani Wabunge au nani?

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Naam?

**SPIKA:** Wabunge au nani unaposema sisi?

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Pamoja na Spika kwa sababu, ni Mbunge.

**SPIKA:** Aaah Wabunge!

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Wabunge sote tulipata mkopo huo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, shilingi milioni 90 zile gari ambalo unaweza kulinunua leo miaka miwili halipo. Sasa wale wanaoambiwa watakonunua magari walipe kodi zaidi ya *25 percent; five percent* inaongezeka. Unakwenda kumwonea halafu nchi nzima ibaki na magari ya matajiri na wale ambao wana uwezo kama sisi Wabunge. Naomba 5% hii iondolewe, itafutwe mahali pengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchini kwetu, uwezo wa kuzalisha saruji ni tani 450,000, *demand* ya nchi ni tani 1,500,000. Naomba wale ambao wanaagizia saruji nje waruhusiwe ili watu wetu wasipate matatizo. Wale ambao wana uwezo wa kupata saruji hizi tani 450,000 wasisababishe hawa watu ambao vyoo vyao wanataka kujenga kidogo isaidie. Kwa hivyo, naiomba Serikali, wasiweke pingamizi lolote la uagizaji wa saruji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana pesa hizi za simu za mikononi ambazo zitapatikana ziwekwe katika fungu lake lijulikane na tujue fungu la Zanzibar ni kiasi gani. Tunataka tujue Zanzibar watapata kiasi gani katika mgawo huu wa pesa. Inawezekana labda tukaingia mlemle kwenye 4.5, sasa ikiwa ni hiyo 4.5, Waziri atatueleza kwamba mgawo wa pesa za simu za mikononi zinaingia kwenye 4.5.

Mheshimiwa Spika, kwa mapenzi makubwa, nakushukuru sana kunipa nafasi hii na *inshallah*, mapenzi yetu hayataondoka, ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Vick Kamata atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwanza napenda niipongeze Serikali, kwa kuweka kipaumbele katika kutatua kero ya maji nchini ambapo jumla ya shilingi bilioni 747.6 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maji nchini. Nina uhakika kabisa katika fungu hilo Geita wanapata na ninaishukuru *ADB*–Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa kuwa imeshaanza kutusaidia watu wa Geita kupata maji na *GGM* pia siwezi kuisahau. Kwa hiyo, ninaamini Geita hivi karibuni itaondokana na tatizo la maji, ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekipitia vizuri hii Hotuba ya Bajeti yetu ya Serikali, nimeona mambo mengi mazuri, lakini sijaona msisitizo wa mbinu na mipango mipya ya kutafuta mapato ya ndani. Sijaona kitu hicho, yaani sijaona kabisa msisitizo wa kutafuta mapato mapya zaidi ya kuonesha matumizi tutakavyotumia, tutatumia hiki na hiki na uleule msisitizo wa miaka yote mfumo wa mwaka 47 wa kupandisha sigara, bia, sioni kitu kingine kipya na sasa wanapandisha na *petrol*, kitu ambacho kitaongeza ugumu wa maisha ya Mtanzania. Kwa sababu, unapopandisha petroli, ina maana umepandisha kila kitu. Kwa hiyo, mimi ninaona bado Serikali inatakiwa ikae, Waziri Mgimwa na Manaibu wake, wana uwezo sana pamoja na wataalam, wakae watuletee mipango mingine mipya ya utafutaji wa mapato ambayo yataleta tija, badala ya kuendelea tu na huu utaniutani wa sigara kila siku na bia.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ninaona linasahaulika, halitiliwi msisitizo ni *real estate*. Mimi nina uhakika kule kuna pesa nyingi sana ambazo hazijafuatiliwa, hazijasimamiwa zikaweza kuongeza pato letu la Taifa. Ninyi wote hapa ni mashahidi, tuangalie miji yote mikubwa kama Dar-es-Salaam, Arusha, Mwanza na maeneo mengine, tunaona majengo makubwamakubwa yanaota kila siku kama uyoga, hivi haya kweli yanalipiwa *corporate tax*, ile 30% kiuhakika? *Real estate* peke yake ingesimamiwa vizuri ingeweza kuongeza pato kubwa sana la Taifa letu, lakini naona hakuna msisitizo katika kutafuta pesa hiyo. Haya maghorofa yanaota kama uyoga kila kukicha, yanalipiwa

30% ya *corporate tax*? Sina uhakika na ninaamini hicho kitu hakipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nitolee mfano tu jengo mojawapo labda niseme *PPF* au *Benjamin Mkapa*; sio mtaalam mzuri sana wa kukadiria, inawezekana lile likawa limejengwa kwa shilingi bilioni nane, 30% ya shilingi bilioni nane ni ngapi kwa wanaojua hesabu? Inawezekana labda ikawa kwenye shilingi bilioni mbili na *point* hivi, kama ninakosea mtanisaidia mnaojua mahesabu. Sasa hizo shilingi bilioni mbili na ushee, hiyo nimesema kwa jengo moja, hebu tuhesabu majengo yote, maghorofa marefu yaliyoota kama uyoga pale Dar-es-Salaam, tuyahesabu yote Mwanza, Arusha na maeneo mengine, kama kweli pesa hiyo ingekusanywa, ingesimamiwa kweli, tungepata pesa kiasi gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo mimi linanisikitisha na ninashangaa sana kuona kwamba Watanzania tunakosa uzalendo, kuna pesa nyingi sana, nyumba za Serikali ziliuzwa kwa baadhi ya viongozi wastaafu, sina maana kwamba ninalaumu au ninafanyaje, lakini nyumba zile ziliuzwa kwa viongozi wa Serikali, wamezinunua hawalipi *property tax*. Inaonekana kama vile kama bado ziko Serikalini, wakati tayari wameshauziwa, kwanza wameuziwa kwa bei chee, jamani, hata kulipa kodi hamtaki, eeh? Lipeni kodi basi *Oysterbay*, Masaki, wananchi wa Geita watengenezewe barabara ili akinamama wanapoenda kujifungua wasifie njiani kwa sababu ya kukosa barabara nzuri. Walipe kodi hawa waliopewa hizi nyumba kwa bei nafuu za *Oysterbay* na Masaki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana kwamba Serikali kupitia Wizara hii ya Fedha pamoja na Taasisi zake zote zinazokusanya mapato kila mahali huko, ziwaangaliwe na hawa, zinawaogopa? Mbona kule Geita, soko letu lile limechoka vibaya, mama anauza dagaa kuanzia asubuhi anapata Sh.5,000/= lakini bado wanamdai kodi, analipa; huyu wa *Oysterbay* ambaye amenunua nyumba ya Serikali kwa bei chee, amejenga ghorofa la bei mbaya, amepangisha Wazungu, anapata hela nyingi, halipi kodi. Hivi

huyo aliyekuwezesha kupata hiyo nyumba kwa bei nafuu, akulipie na kodi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naona hii sio haki hata kidogo. Mimi naomba kwa kweli, tuwe wazalendo. Hii nchi ni yetu wote, tujiangalie, hakuna aliye juu ya Sheria. Inawezekana labda Serikali inaweza ikaogopa kwa sababu ndio nyie wenyewe mliopeana hizo nyumba. Sitaki kwenda upande huo hainihusu sana, lakini inanihusu kama Mtanzania; sitaki kujua ilikuwaje lakini ninachoomba mmeshanunua hizo nyumba, lipeni kodi isaidie wananchi wengine kule, tuboreshe miundombinu ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningependa pia niongelee kuhusu Magereza, ni eneo mojawapo ambalo lingeweza kutusaidia kuongeza pato la Taifa. Tunao wafungwa kama sikosei 36,000 hivi kwenye magereza yetu, inawezekana ikawa zaidi au pungufu, kwa *research* ndogo niliyofanya nimeona iko kama hivyo. Hawa wafungwa wanaamka asubuhi wanaenda kufanya usafi kwa Mkuu wa Gereza, wanarudi. Hivi kweli, tunge-*invest* kwa Magereza peke yake, tukawapa pesa, tukawapa vitendea kazi, hii *irrigation* tunayoisema kila siku hii, tungeanza na Magereza, wana mashamba makubwa, wakalima wakajilisha wao wenyewe, wakatulisha sisi na wakauza na sehemu nyingine. Mimi naamini kabisa kama tungeamua kuwatumia hata hawa Magereza, wangeweza kutusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kabisa kwamba Magereza sio sehemu ya kumpeleka mtu aende kufa huko. Tunaamini kabisa kwamba akifungwa kutokana labda na kosa fulani amefanya, miaka miwili, miaka mitatu, atarudi mwisho wa siku uraiani. Akirudi uraiani, mimi nategemea kwamba Magereza ni Chuo cha Mafunzo, kule ataenda kujifunza *skills* mbalimbali; akirudi atakuwa ameshapata utaalamu wa kuchonga meza, akirudi huyu mfungwa atakuwa ana uwezo wa kufyatua tofali, atarudi anajenga nyumba. Sasa kama tungekuwa tunawawezesha Magereza, tunawapa pesa ya kutosha, wanafanya hizi shughuli, mimi nadhani hata hii shilingi bilioni 8.2 imetengwa kwa ajili ya

20 JUNI, 2013

chakula, kama sikosei, kwa ajili ya Magereza zote, nafikiri tusingekuwa tunahangaika sana, hawa Magereza wangejilisha. Mimi nakumbuka Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere nasikia alikuwa anavaa nguo ambazo zinashonwa na Magereza, walikuwa wanashona suti nzuri, alikuwa anavaa na viatu vizuri. Tungeweka mipango mizuri, ngozi zisiuzwe hovyoye, zikabaki hapa wakapelekewa Magereza, wakapewa vitendea kazi, wakashona viatu. Tungekuwa tunavaa viatu vya hapahapa kwetu, wametengeneza Magereza, Magereza wangekuwa wanashona nguo, Polisi wangeshonewa *uniform* na Magereza, kungekuwa na mzunguko fulani wa pesa kutoka kwa Magereza kuja kwa watu wengine huku na tungeweza kuboresha maisha ya watu wa Magereza na sisi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi juzi nilienda Geita, mimi ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Geita. Nilienda Geita na nikaamua tu kutembelea Gereza la Geita bila taarifa, bahati nzuri nilipokelewa vizuri sana na Mkuu wa Gereza, Bwana Mbilinyi, nikatembezwa pale kwenye yale Magereza. Nimeona vitu vingi sana ambavyo vilinimumiza mimi kama mama, vilinisikitisha sana. Lile Gereza limejengwa tangu mwaka 1947 na Wakoloni, miaka 66 iliyopita na tangu kipindi hicho miundombinu ya majitaka haijawahi kurekebishwa, hawa wafungwa wanavuta hewa chafu na hata hawa Maaskari Magereza wenyewe, wanavuta hewa chafu saa 24, hivi afya zao zitakuwaje? Hiyo haitoshi basi, nikaingia kwenye Gereza lenyewe la akinamama, sio baya sana siwezi kulaumu. Nikaingia kwenye gereza la akinababa, pale ndipo nilipotaka kulia. Gereza lina uwezo wa kuchukua watu 147, lakini nililikuta lina wafungwa zaidi ya 400.

Mheshimiwa Spika, pata picha, uwezo wa Gereza ni 147, mle ndani wako watu zaidi ya 400, niambie ule mbanano ukoje, watu wana-*kiss* bila kupenda, wamebanana, wanaambukizana magonjwa ya ajabu. Sisi tulitegemea kwamba mfungwa anapomaliza kutumikia kifungo chake, arudi uraiani akiwa na afya njema, aende akafanye kazi aisaidie nchi yake, aisaidie familia yake. Ndiyo maana ninasisistiza kusema, Magereza ipewe fedha ya kutosha ili



20 JUNI, 2013

waweze kufanya mambo mazuri. Tupanue Gereza letu hasa la Geita, nimesema limejengwa mwaka 1947, lina uwezo wa kuchukua watu 147, lina wafungwa zaidi ya 400.

Mheshimiwa Spika, Gereza la Geita hakuna hata gari, hivi ninavyoongea, wakitaka kumpeleka mahabusu Mahakamani, wanapanda pikipiki, utakuta Askari Magereza yuko kwenye pikipiki na mtuhumiwa wanakwenda mahakamani, hii ni nini! Mimi ningeomba Serikali iangalie, tuwawezeshe hawa Magereza, kama tunaona vipi, tuwawezeshe hata wanaweza kuwa na miradi yao ambayo watakuwa wanafanya vitu vyao vingine kule tunawasaidia na tunashirikiana nao pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kwanza niwapongeze pia Askari Magereza kwa moyo wao wa uvumilivu na wa kujitolea, wameweza kukarabati nyumba zao maskini, wamepiga plasta angalau zina hali, kwa kujichangisha wao wenyewe tu na sasa wamejenga tena nyumba ambayo imefikia kwenye linta lakini wameishiwa fedha. Labda nitumie fursa hii pia kuiomba Serikali, isiwaogope tu hao, kila mtu alipe kodi. Hao niliowataja hao walipe kodi ili ziende kusaidia maeneo mengine kama hayo ninayoyataja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naomba niunge mkono hoja hii, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Subira na Mheshimiwa Kibona ajandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nikushukuru na nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa hii kusimama ndani ya Bunge lako na mimi kutoa mchango wangu kwenye bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda kwenye hoja ya msingi, naomba niungane na wanachama wa Chama cha Mapinduzi kushangilia ushindi wa Kata 16 na kipekee

20 JUNI, 2013

nishukuru kwa ushindi wa Kata za Genge na Tingeni katika Wilaya ya Muheza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama Wabunge wenzangu walivyokupongeza na mimi naungana nao kwa utaratibu huu ulioanzishwa, kwa maamuzi magumu uliyofanya ya kujaribu, kuthubutu na baadaye inaonekana kama utaratibu huu unaweza kutusaidia wa uwasilishaji wa bajeti mapema kabla ya mwaka wa fedha wa Serikali haujaanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze kazi nzuri iliyofanywa na Kamati ya Bajeti. Ukipitia taarifa yao imeainisha maeneo mbalimbali, mafanikio, changamoto, ushauri na kwenye kupongeza wamepongeza na hasa katika suala zima la uongezaji wa mapato, ushauri wao kwa namna pekee mengine yamezingatiwa, lakini niombe Wizara ya Fedha inayoandaa hii bajeti izingatie mapendekezo yaliyobaki ya vyanzo vya mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja niseme mimi pamoja na kuwapongeza Mawaziri na Watendaji wa Wizara hiyo, naunga mkono hoja hii. Ninayo sababu ya kuunga mkono, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa, maeneo ambayo tumefanikiwa, mipango inayotarajiwa kufanyika na kwa kupitia taarifa hiyo, mimi ninayewakilisha pia Mkoa wa Pwani nimeona mambo ambayo yametetelezeka kwenye suala la maji. Tumeona upanuzi wa mtambo wa Ruvu Chini na Ruvu Juu na kwamba wakazi wa Dar es Salaam, maeneo ya Bagamoyo, ya Kibaha, yatapata maji.

Mheshimiwa Spika, pia naunga mkono kutokana na shughuli mbalimbali zilizofanyika kwenye masuala ya miundombinu ya usafiri na usafirishaji. Tumeona usafiri wa treni Dar es Salaam unavyopunguza foleni, ujenzi wa Bandari mbalimbali, upembuzi yakinifu unaoendelea kwenye Bandari zetu, ya Mtwara, ya Bagamoyo na ya Mwambani Tanga. Ni

matumaini yangu kwenye mwaka huu wa fedha unaokuja, shughuli hizo zitaendelea.

Mheshimiwa Spika, nijielekeze sasa kwenye masuala ya mapato. Tumeona Serikali inatarajia kukusanya shilingi trioni 18, kati ya hizo zaidi ya shilingi trilioni 10 ni kutokana na mapato yetu ya ndani. Naomba niishauri Wizara na *TRA*, mimi nilidhani baada ya Mamlaka ya Utoaji wa Vitambulisho kuanza kutoa Vitambulisho, wangeongeza wigo wa walipa kodi lakini ukipitia hotoba ya Waziri wa Fedha, pamoja na kusheheni data mbalimbali lakini sijaona kati ya mwaka jana na mwaka huu ni idadi ya walipa kodi wangapi wameongezeka, au wamewafikia na vyanzo vipya vya mapato ambavyo vimeainishwa. Pia tuna matokeo ya sensa, Watanzania tuko milioni 44, matumaini yangu ilikuwa katika taarifa mbalimbali ambazo zinakuwa *analyzed* na Ofisi ya Taifa ya Takwimu zingetumika takwimu zile na kuona tunaongeza vipi mapato yetu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia upande wa mapato Serikali za Mitaa, mpaka mwezi Mei, inaonekana ni asilimia 49 tu ambazo zimekusanywa, lakini Kamati yetu ya Bajeti imeweze kuona kwamba tatizo labda ni ubinafisisishaji wa ukusanyaji wa mapato na imekuja na mapendekezo pengine turudie utaratibu wa zamani wa kutumia Watendaji wa Kata. Utaratibu huu ulikuwepo, ni sisi ambao tuliona baadaye una upungufu na kipindi hicho ilionekana mapato mengi yalikuwa yanavuja, ubadhirifu mkubwa na ndiyo maana tuliona tutumie ubinafisisishaji. Mimi tatizo ambalo naliona, ni kwa Halmashauri zetu kutokuwa na mipango ya kutathimini vyanzo vyao, wakapata wana uwezo gani wa kukusanya, halafu wanapotangaza zile tenda, wao wenyewe wanakuwa wameshajua wana uwezo gani wa kukusanya na wale wakandarasi wakisema vile viwango pale inakuwa mazungumzo yanaendelea. Niziombe Halmashauri zetu zifanye kama ilivyokusudiwa ili kuendelea kukusanya mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimesema naunga mkono kwa sababu bajeti hii imekuja na utaratibu mpya wa kupima

20 JUNI, 2013

matokeo (*Big Results Now*) na kwa kutambua vipaumbele sita, pamoja na kwamba ni vingi, lakini kwa kutambua kwamba Mawaziri hao wa Wizara hizo sita wameingia mkataba na Mheshimiwa Rais. Mimi ninaunga mkono kwa sababu nina imani hata wao hawapendi kupoteza nafasi zao, watafanya kila lililokusudiwa ili mambo yote yaliyopangwa kutekelezwa kwenye bajeti zao yatekelezwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiunga mkono vipaumbele hivi, ni imani yangu, kwa mfano, kipaumbele cha maji na kwa kuwa Serikali imekubali kuongeza bajeti, zaidi ya shilingi bilioni 184, Watanzania hasa kina mama ambao ndiyo wazalishaji, wakipata maji ya uhakika, wakitumia muda mfupi kupata maji, wataelekeza muda mwingi unaobaki kwenye shughuli za uzalishaji mali, kwenye sekta ya kilimo. Kama inavyosemekana asilimia 80 wanaoishi vijijini ndiyo wanajishughulisha na kilimo na tumeona mchango wa kilimo katika pato la Taifa ni zaidi ya asilimia 20 pamoja na ukuaji wao siyo wa kuridhisha, ni imani yangu maji yakipatikana vijijini, wengi watajikita kwenye uzalishaji mali. Kilimo kikiboreshwa, wakijikita na mazingira yakiandaliwa vizuri, miundombinu ya usafirishaji ikitulia vizuri, ni imani yangu mapato yataongezeka kutokana na mazao yatakayozalishwa na sekta ya kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, kwenye kipaumbele cha nishati, nakubaliana moja kwa moja na uamuzi au mapendekezo ya Waziri wa Fedha, wa kuongeza tozo ya shilingi 50 kwenye petroli kwa ajili ya kupeleka kwenye Mfuko wa Umeme vijijini *REA*. Ni imani yangu kuwa kazi itakayofanywa na *REA* kupitia chanzo hiki cha mapato, umeme utasambazwa vijijini, viwanda vidogovidogo vya usindikaji vitafunguliwa na viwanda vikubwa, itapunguza gharama za uzalishaji wa vyakula na mwisho wa siku, gharama ndogo kwa maisha ya Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote hayo, lakini katika kupitia taarifa ya Kamati ya Bajeti kwenye suala la matumizi,

pamoja na kwamba Serikali imeanza kujipanga kupunguza matumizi kwenye maeneo mbalimbali, naomba niipongeze, kwenye baadhi ya maeneo ya viburudisho, mwaka huu wamepunguza zaidi ya asilimia 50, gharama za uendeshaji, ununuzi wa magari, matengenezo ya magari na kadhalika. Katika taarifa yao inaonyesha kuna baadhi ya Wizara zinatumia fedha nyingi kuliko ilivyoidhinishwa na Bunge na hapa naomba nijielekeze kwenye Sheria ya Fedha (*Public Finance Act*), Kifungu 19, kinaelezea masuala ya *excess expenditure*, endapo inatokea hali ya matumizi ambayo hayakuidhinishwa na Bunge, lakini yalikuwa na msingi, ni lazima taarifa iwasilishwe ndani ya Bunge na ijadiliwe. Mimi niombe Wizara ya Fedha, kwenye hizi *reallocations*, kwenye matumizi ambayo hayajaidhinishwa, kwa mfano Wizara ya Mambo ya Nje imetumia zaidi ya shilingi bilioni 31, Wizara ya Afya, shilingi bilioni 27, sisi tulitegemea wangeleta *supplementary estimates*, tungejadili kwa sababu nadhani yalikuwa ni matumizi ya msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono pia upunguzaji wa kodi katika mapato ya ajira. Hapa niombe Serikali itazame Watanzania wengi hasa wafanyakazi, wamekuwa ndiyo walipaji wakubwa na kwa kuwa kodi yao wao haina gharama ya kuitafuta au ya kuikusanya kwa sababu moja kwa moja inakatwa, wangeangalia na wangekubali pendekezo la Kamati ya Bajeti, walau ingefika asilimia tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine kuhusu upandishaji wa tozo kwenye mafuta ya petroli, dizeli na ya taa, niombe Wizara ya Fedha, wakubaliane na maoni ya Kamati ya Bajeti, kwa kuwa imependekeza vyanzo vingine, kwa mfano, uvuvi kwenye bahari kuu, sijaona kwenye hotuba na uvuvi pamoja na kwamba bado hatujawekeza zaidi lakini kwa bajeti ya mwaka unaoishia, imechangia shilingi bilioni 10. Utashangaa hata kwenye mipango ya maendeleo ya kwenye uvuvi, imepangwa shilingi milioni 500 tu, sisi tunaowakilisha jamii za wavuvi, kwa kweli suala hili tunaona kama wavuvi

hatutendewi haki. Mimi ningeomba, pendekezo hilo lifanyiwe kazi. Petroli, dizeli ingeachwa kama ilivyo kwa sababu kama lengo ni kupunguza mfumko wa bei, tunapopandisha bidhaa hizi ina maana gharama za uzalishaji wa vyakula zitapanda.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kabla ya kengele haijalia, naomba niunge mkono upandishaji wa *fuel levy* kwa ajili ya ukarabati wa barabara zetu kwa kuwa tumesema miundombinu inachangia kwa kiasi kikubwa kupunguza gharama za vyakula na baadaye maisha bora kwa kila Mtanzania. Pia niungane na wenzangu waliozungumza kuhusu tozo ambayo imependekezwa na Kamati ya Bajeti kwenye *Sim Card*, nadhani Serikali ingelifanyia kazi na kukubali ushauri huo.

Mheshimiwa Spika, nasita kukubali ushauri wa kupunguza kodi inayokwenda kwenye masuala ya elimu ya ufundi (*Development Skills Levy*) kwa asilimia moja. Kwa kweli hatujafanya tathmini, ni mwaka jana tulihangaika, tukakubali asilimia sita, bado tunahitaji Mafundi Mchundo, nchi yetu inajikita kwenye shughuli mbalimbali, gesi sasa hivi imepatikana, mafuta, yote inahitaji Mafundi Mchundo. Naomba hili lisiguswe, iendelee asilimia sita ile ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Kibona atafuatiwa na Mheshimiwa Donald Max, Mheshimiwa Ole-Sendeka na Mheshimiwa Chomboh pia ajiandae.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nami nianze kuwashukuru na kuwapongeza wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kuandaa bajeti hii. Nafahamu mchakato wa kuandaa bajeti unahusisha watu wengi, nampongeza Waziri, wasaidizi wake na yeyote aliyeshiriki kwa namna moja au nyingine. (*Makofi*)

20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono kwa asilimia 100 hoja hii au bajeti hii. Ninazo sababu. Mara nyingi huko nje tumezoea kusikia siku za karibuni watu wakilaumu, mnaunga bajeti, mnaunga bajeti, lakini napenda niseme wazi, wananchi wenzangu, ndugu zangu kule Ileje waelewe kwa nini ninaunga hoja hii, ninazo sababu. Sababu ya kwanza, bajeti hii inakwenda kusanisaidia mimi na wananchi wangu kule Ileje kwenye suala la maji. Nimeona Sh.540,000,000 kwa ajili ya mji wa Isongole na la Itumba, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona bajeti kwa ajili ya vijiji vya Ilanga, Ikumbilo na Chitete. Naunga mkono ili fedha iende ikatengeneze miundombinu ya umeme katika Wilaya yetu ya Ileje na Tanzania kwa ujumla. Maeneo ya Luswisi, Bwenda, Lubanda, Sange, Katengele, Kalembu, Isoko, Ndembo, Chikota, Ikinga, Kapelekesi, Malangali, Ibungu, Bupigu, Chabu, Ilulu na kwa mzee wangu mastaafu, Mheshimiwa Gideon Cheyo kule Mlale, nashukuru sana. Pia maeneo ya Ibaba yanakwenda kupata umeme kupitia bajeti hii, ninazo sababu za kuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono bajeti hii, ninayo machache ya kusema yaliyoelezwa katika bajeti hii. Wilaya yangu ya Ileje tunayo matatizo ya usafiri. Wilaya ile ina milima, mvua za muda mrefu, mwezi huu ni wa sita tunakwenda wa saba, lakini mvua ni nyingi, gari zinateleza, mabasi hayawezi kufika. Naiomba Serikali, katika bajeti zijazo, najua kwa sasa ni ngumu kubadilisha, tuangalie maeneo kama yale ya Ileje. Najua yako maeneo mengine kule Makete na sehemu zingine, maeneo yale yapewe kipaumbele, yatazamwe kwa namna ya pekee, kwa sababu usafiri unakuwa ni shida. Kwa mfano, kule kwangu Ileje, mpaka sasa hivi, miaka 50 ya Uhuru, miundombinu ya barabara ni mibaya, watu wanabeba maiti, wagonjwa kwa kutumia machela kama vile walivyokuwa wakimbaba Mkoloni enzi zile. Hii yote ni kwa sababu ya matatizo ya miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunazo barabara kwa mfano ya kutoka Kibaoni kwenda Ngwililo, Sapanda mpaka Luswisi. Barabara ile, kila tukiweka bajeti kwenye Halmashauri yetu, kuna kauli ambayo Wizara wanasema, ime-*bust*, haiwezi kuhimili, wana kikomo cha bajeti. Kwa hiyo, sisi tunapoomba bajeti kwa ajili ya barabara zetu ambapo mvua ni nyingi, mkandarasi akienda, hawezi kukubali fedha ndogo iliyopangwa, tunapata shida. Tunaomba Mheshimiwa Waziri tutakapokuja na maombi maalum, uweze kutusikiliza.

Mheshimiwa Spika, kabla sijafika kwenye eneo lingine, labda nizungumze kidogo, tunaweza tukawa tunapata laana ambazo pengine hatukustahili. Mimi naomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kujumuisha mjadala huu, hebu naomba aje na maelezo kidogo kuhusiana na wale *pensioners* au wadai wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wale watu, kila inaposogea uchaguzi, mimi sijui nani anakwenda kuwaibua, wengine wanalala barabarani, wengine ni ndugu zetu, inatia huruma sana! Kwa nini katika bajeti hii hatujaweza kuzungumza kuhusu malipo ya watu hawa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie kidogo juu ya jambo hili. Jambo hili kwa kweli limekuwa ni kero ya muda mrefu, hawa wazee ni wazee wetu, ni Watanzania wenzetu, fedha ile walikatwa, ni *provident fund* ya kwao, ni *pension* ya kwao, msuluhishi alikuwa akiitwa Victor Umbritch, tarehe 7 Mei, 1984 aliongea na Marehemu Baba wa Taifa, kujadili juu ya jambo hili. Yule msuluhishi aliyekuwa anazungumzia kugawa mali zilizokuwa za Afrika Mashariki, alizungumzia kipengele cha wastaafu. Tanzania hatujawalipa wastaafu wetu lakini mimi nashindwa kuelewa. Awamu iliyopita Mheshimiwa Mkapa alikuwa akisisitiza mara kwa mara kwamba ukikopa unatakiwa ulipe. Naamini, enzi zile za miaka ya 1984 hali ilikuwa mbaya, sote tunakumbuka, fedha za wazee wetu zilitumika, zilielekezwa kufanya mambo ya muhimu, mambo ya muhimu wakati ule tunakumbuka hali ilikuwa ngumu, baada ya vita vya Kagera na kadhalika, tulikopa fedha za watu. (*Makofi*)



Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri naomba alichukue hili, aweke historia kwamba alipokuwa Waziri Mgimwa, Wazee ambao wameteseka kwa miaka mingi alilipa pesa za Wastaafu hawa. Itakuwa aibu kila mara tukilisemea jambo hili, hawa ni watu wetu, siyo wageni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, nizungumzie kidogo kuhusu mapato. Nakwenda kidogo kinyume na wenzangu, wanaozungumzia kusamehe, kuwapa unafuu watu wa bodaboda.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2012 ukienda kwenye *Hansard*, nilipokuwa nachangia juu ya jambo hili nilisita kama kweli kuna utafiti uliofanyika wa kina. Ukiwauliza wafanyakazi wa *TRA*, sasa hivi wana manung'uniko juu ya jambo hili.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni kama limebebwabebwa kisiasa. Kule kwangu Ileje, kama ni suala la kuwasaidia ajira, vijana wangu walio wengi shughuli zao ni kusuka nyungo. Nyungo unazotiona kule Iringa, kule Dar es Salaam, huku Dodoma na Mwanza na sehemu nyingine zinatoka Ileje.

Mheshimiwa Spika, vijana wale wanapata shida, ni ajira yao pekee, wanapata shida, lakini wakashatengeneza nyungo zao, kodi ni kilio, kila ungo kodi. Akiwa na nyungo 100 ni hela nyingi mno. Kijana anapata shida anakata tamaa, hawezi kuendelea na shughuli hii, haya hao tunawaelezaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna watu wengine pia, nilikuwa napita pale Mbeya, nikamkuta kijana mmoja anasimamia nyumba, nikawa nina maongezi naye. Nikasema nyumba hii unaijenga kwa shilingi ngapi, huyo kijana ni fundi. Akasema, Mkataba wangu ni kulipwa Shilingi Milioni Sita (Sh. 6,000,000/=) mpaka itakapokwisha.

Mheshimiwa Spika, haya huyo kodi yake iko wapi? Maana yule msusi wa ungo kule Ileje, kodi yake ni kubwa

20 JUNI, 2013

hata kama ni Sh. 500/= kwa ungo mmoja au Sh. 200/=, je huyu anayejenga nyumba huko mtaani na mwenye nyumba anamlipa Sh. 6,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, nasema, nchi hii vyanzo vya mapato ni vingi. Inawezekana wale wanaobuni vyanzo vya mapato wanakimbilia kwenye petroli, kwa sababu ni vitu rahisi kuviona. Natoa wazo kwamba, wafanye bidii, waweze kubuni vyanzo vingine. Kuna watu wanakaanga *chips* mahali pengine anakuwa nje ya *Bar*. Kazi anayoifanya, hela anayokusanya ni zaidi ya hela anayokusanya mwenye Hoteli. Kwa hiyo, tujitahidi kubuni vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo juu ya kauli mbiu iliyokuja inasema, *Big Result Now*. Jambo hili...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Ya ngapi.

**SPIKA:** Ya pili.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Na *Big Results Now*. *(Kicheko/Makofi)*

Haya Mheshimiwa Donald Kelvin Max, atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka na Mheshimiwa Bahati Abeid ajiandae.

**MHE. DONALD K. MAX:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nami niungane na Wabunge wenzangu kukupongeza kwa utaratibu huu mpya.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wakazi wa Wilaya ya Geita, *hususan* Jimbo la Geita, naomba nianze na gharama za Bima, sijajua hii *Tabulation* imepigwaje kwa sababu haiwezekani kwenye *Comprehensive*, mimi mwenye

lori la *trailer*, nilikuwa nalipa Sh. 1,000,000/= sasa hivi inakwenda mpaka Sh. 7,000,000/=. Unapokuja kwenye ile zamani ilikuwa ni asilimia 2%, sasa hivi ni asilimia 6% kwenye kichwa peke yake. Ukija kwenye kichwa cha zamani, walikuwa wanalipa asilimia 2% sasa hivi ni asilimia 4.5%.

Mheshimiwa Spika, kibaya zaidi ni kwamba, hawa wadau wa *Transportation* wangeshirikishwa kwenye hili, kwa sababu huku tunalo tatizo la kupandisha *petrol*, huku tunalo tatizo la kwenye Bima. Kwa hiyo, kupeleka mzigo, ina maana nikichanganya hivyo viwili hiyo gharama itakuwa kubwa sana. Inatoka asilimia nne mpaka asilimia 11%.

Mheshimiwa Spika, sasa tukija kwenye *Third Party*, kichwa cha zamani kilikuwa kinalipa Sh.120,000/=. Sasa hivi ni Sh. 300,000/=. Ukija kwenye *trailer* yake badala ya Sh.120,000/= sasa imekuwa Sh. 200,000/=. Kwa hiyo, hapa kwenye Bima na mafuta, hivi vitu viwili ukija kuchanganya ni asilimia karibu 13, itakuwa tabu sana.

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye tatizo la wafanyakazi. Wafanyakazi wa Serikali wanapata shida sana. Mtu mwenye mshahara wa Sh. 750,000/= kwa mwaka analipa karibu shilingi milioni 1.2, ndiyo hayo makato yake ya kodi. Lakini unamkuta mtu anaweza kuwa na *Ka-Guest* kaajabu ajabu hivi, kina vyumba 15, huyu jamaa analipa Sh. 400,000.

Mheshimiwa Spika, sasa huyu mfanyakazi hii rushwa kweli tutaiondoa? Kwa sababu akishakatwa pesa kama hiyo, ina maana kwa mwezi pamoja na Bima za Afya, ana kagari, ana *Insurance*, mfukoni atakuwa anaondoka na Sh. 200,000/= badala ya hiyo Sh.750,000/=.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wakazi wa Geita, namhehimu sana kaka yangu Mgimwa pamoja na Manaibu wake, lakini tuna matatizo hapa. Mwaka 2010 nimeanza kuhangaika na malimbikizo ya pesa za wafanyakazi, Idara ya Afya Wilaya nzima. Mpaka Mheshimiwa Waziri Hawa Ghasia, akaja Geita kufanya *verification*, akakuta kweli ndiyo iko hivyo.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa Afya Wilaya nzima toka mwaka 2008 hadi hii leo, madai yao yako Hazina ni Sh. 448,000,000/= . Kila ukifuatilia hadithi ni ile ile tu. Jamani hawa watu wamefanya kazi miaka mitano, ndiyo sababu unakuta Hospitali zetu dawa zinapotea zile, lazima wachukue wauze, wataishi vipi.

Mheshimiwa Spika, unapokuja kwenye elimu, malimbikizo ya Walimu na yenyewe yanatupa shida. Sasa ningepomba ile Sekta ya Elimu kwa kusema kweli wanaishi kwenye mazingira magumu sana kwa sisi tunaokwenda vijijini. Tunaomba mishahara yao iwe inawahi.

Mheshimiwa Spika, acha Walimu vile vile kuna wastaafu, mpaka leo hii matatizo yako pale pale. Kama mmewaambia kila miezi mitatu, basi wapatiwe stahiki zao. Wastaafu wanatusumbua sana kila siku swali ni lile lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapokuja kwenye Madawati sasa. Naomba haya madawati, naomba uwiano uzingatiwe. Dada yangu asubuhi ya leo, Mheshimiwa Lolensia Bukwimba, ameelezea ukubwa wa Geita. Mahali popote mnapoanzisha machimbo au Biashara kubwa, idadi ya watu inaongezeka na huwezi kuwazuia.

Mheshimiwa Spika, sasa Geita ni Wilaya kubwa, kila wakati *MSD*, ikishusha gari yake pale dawa hazikai zaidi ya siku tatu, zimekwisha. Kwa hiyo, ule uwiano kwa kusema kweli haupendezi pendezi. Kwa hiyo, naomba na kwenye madawati vile vile.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Geita tulijenga mashule mengi sana na tuliwahi Wilaya zote za Mkoa wa Mwanza na sasa hivi tumeongeza shule zingine. Sasa ukisema kwamba hii hela ya madawati uwiano uwe sawa kwa Wilaya zote, hamtatutendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije kwenye suala ambalo kwa kusema kweli linatusikitisha sana. Nafikiri Mheshimiwa Naibu

Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Masele, alituita pamoja na Mgodini wa dhahabu wa Geita hapa Dodoma mwaka 2012. Mpaka leo hii Halmashauri ya Wilaya ya Geita bado inadai Dola Milioni 1.2 *Service Levy*, kwa sababu mle ndani kuna zaidi ya Makampuni 40 yanafanya kazi na kuondoka na hela za watu.

Mheshimiwa Spika, sasa Halmashauri yetu inashindwa kupiga hatua, tunataka kujenga machinjio, kwa sababu ukiangalia machinjio ya sasa hivi hapakanyagiki pale. Sasa tungellomba Wizara husika, siyo kwamba Madini wahangaika peke yao ni pamoja na Wizara ya Fedha, tunaomba hizi Dola Milioni 1.2, Halmashauri ya Wilaya ya Geita ipokee hela yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naomba kuipongeza Wizara ya Maji, Ujenzi na Umeme. Wizara ya Maji na mimi ni mjumbe kwenye Kamati hiyo, namshukuru Mheshimiwa Waziri ametupatia Geita Shilingi Bilioni 6.5 ili tuweze kusambaza maji nyumba kwa nyumba. Nampa pongezi zangu.

Mheshimiwa Spika, pale Geita Mjini kwa sababu ya ule udongo mwekundu na vumbi, tumepewa kilomita nne, halafu umeme Vijijini, Igate, Sungusira, Nzela kwenda Katoma mpaka Nkome mpaka Kakubilo, *REA* wameshapita, wameshafanya usanifu, kwa hiyo, nimeongea na Naibu Waziri wa Nishati, nafikiri *by* mwisho wa mwaka huu, Kata hizi zitapata umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba nikushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Ole-Sendeka halafu Mheshimiwa Chomboh na Mheshimiwa Bahati Abeid ajiandae.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Nianze kwa kukushukuru kwa mambo makubwa mawili.

La kwanza, kwa jinsi ambavyo unaendelea kuliongoza Bunge hili na kuturejeshwa kwenye barabara inayostahili, ya Maadili ya Kibunge, pale ambapo tunapotoka. Lakini kwa ukweli kwa ubunifu wako uliopheleka kuwa na mfumo mpya wa kujadili na kuanza kuibua hoja za Bajeti ambazo ni shirikishi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila, kama sitaungana na wenzangu kwa matukio yaliyofanyika au kwa uamuzi uliofanywa na Watanzania siku ya Jumapili iliyopita, kumgawia kila mtu, au kila chama kile alichokistahili. Kwa hiyo, nawapongeza wale waliopata walichokipata, lakini nawapongeza sana Watanzania kwa kuendelea kukiamini sana Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako mambo ya msingi ambayo ni lazima tukumbushane kama Taifa. Nimefuatilia sana hali ya kisiasa hapa nchini. Lakini zaidi katika mwenendo huu wakati huu wa uchaguzi mdogo wa Madiwani. Nikalazimika kutatufa hotuba moja ya Mwalimu aliyoitoa tarehe 18 Februari, 1992, kwenye Mkutano Mkuu wa CCM uliofanyika Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Mwalimu katika kuzungumzia kile kinachoitwa Kanuni za lazima za utaratibu wa Vyama Vingi Tanzania, alisema hivi, naomba kunukuu:

“Chama cha Siasa kisiruhusiwe, ikiwa hakikubali msingi wa usawa, wa haki na heshima kwa raia wote. Kusiwepo utetezi wala uchochezi wa kuleta fujo, dhidi ya watu binafsi, au vikundi vya jamii, vya siasa au vya uchumi, au dhidi ya dola yenyewe, ninarudia, dhidi ya dola yenyewe, utakaoruhusiwa kwa Vyama vya Siasa, kama ambavyo watu binafsi na vikundi vya jamii haviruhusiwi kufanya hivyo.

Vyama vya Siasa tunavyovitaka ni vyama vya kushawishi wananchi kwa nguvu ya hoja na siyo kwa hoja ya nguvu”. Mwalimu anaendelea kusema: “Chama cha Siasa kisiruhusiwe, ikiwa msingi wake ni kabila au Wilaya au Mkoa au sehemu moja ya Jamhuri ya Muungano. CCM ni Chama

cha Tanzania nzima. Mwalimu anasema mwenyewe. Washindani wake watahitilafiana katika mambo mengine lakini siyo katika jambo hili. Vyama vyetu lazima vyote viwe ni vyama vya Kitaifa, Vyama vya Tanzania nzima, vitashindania kura za Watanzania, katika kuiongoza Tanzania na siyo katika kuigawa Tanzania, au kuliongoza kabila, kugawa nchi ni uhaini. *(Makofi)*

Katiba ya nchi yetu kwa utaratibu wowote utakaokuwepo lazima wakati ihakikishe kuwa uhaini unashughulikiwa kwa ukali na kwa haraka sana.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, hii ni hotuba ya Mwalimu ya tarehe 18 Februari, 1992, Dar es Salaam, akizungumza kwenye Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema hivyo kwa sababu amani ya Tanzania haina mbadala na leo umoja wa Kitaifa unatishiwa na baadhi ya kauli zetu wanasiasa. Jambo hili likiendelea kuachiwa, umoja wa Kitaifa na mshikamano wa Watanzania utakuwa hatarini.

Mheshimiwa Spika, jana nimetoka Arusha, kwa macho yangu nimeshuhudia, sitaki kuzungumzia lile la mabomu maana linaendelea kwenye utaratibu wake. Lakini juzi siku ambayo Waziri Mkuu alikwenda kuwapa pole wale ambao walipata matatizo. Wakati tukitoka pale kwenye Hosptali ya Arusha *Lutheran Medical Centre*, bila haya Watanzania wasiokuwa na utu kabisa baada ya kuleweshwa, wengine wanapita barabarani wakipiga *Peoples* wakati maiti za watu zimelala *Mortuary*, hii ni aibu kwa Taifa hili linalojulikana kwa amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kana kwamba hiyo haitoshi mchana, watu waliwasha matairi barabarani na kuziba na kuweka mawe barabarani na kuimba wimbo wa chama fulani cha siasa. Ni aibu, ni hatari, Serikali isikubali kucheza na watu wa aina hii, nchi hii itamwaga damu kwa kiasi kinachohatarisha umoja wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ifanye uamuzi wa dhati, isicheze na watu wanaohatarisha umoja wa nchi yetu. Umoja wa nchi yetu hauna mbadala. Nataka niwaambieni, Mji wa Arusha na Kaskazini mwa nchi yetu, ni maeneo ya utalii. Katika matukio yanayotishia tasnia nzima ya utalii nchini na hasa katika Kanda ya Kaskazini, ni matukio yanayotokea katika Mji wa Arusha.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi ichukue hatua madhubuti za kuwahakikishia wananchi wa Arusha, usalama wa mali zao na usalama wa maisha yao wenyewe. Kuendelea kuwaruhusu wanasiasa wanaochochea uchochezi wa kuwafanya wananchi waichukie Serikali, kwa sababu za utashi na matakwa binafsi ya wanasiasa uchwara, ni kuhatarisha umoja wa Taifa hili na kuhatarisha mali za Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeona niliseme hili, kwa sababu hiyo ndiyo sababu ambayo jana wananchi wa Arusha wameniomba na wale hasa niliozunguka nao wakati nikishuhudia matairi yakichomwa pale barabarani, namshukuru sana Binti mmoja anayelitwa Jamila wa *Channel Ten*, ni mama lakini kwa ujasiri wake alizunguka pamoja na mawe yale, lakini aliweza kuchukua *Video* ya vituko na vioja vilivyokuwa vinafanywa na wale, ili kuifanya nchi ijue vituko vinavyofanywa na watu wasiokuwa na imani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tasnia ya Utalii, ukiacha sasa hilo nililolizungumza, ambalo linaweza likawafanya sasa watalii wakaenda nchi za jirani, nalo limekwazwa kwa baadhi ya mapendekezo na hasa ya kufuta msamaha wa *VAT* unatolewa kwenye huduma ya Utalii.

Mheshimiwa Spika, ningependa kumwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwanza nampongeza sana, yeye na Manaibu wake na Wizara nzima, Mzee Mgimwa anafanya kazi kubwa sana ya heshima. Naomba sana sana katika hili wenzetu wamelalamika, wadau wa sekta hii wameshafunga mikataba na Watalii ambao wanaingia katika msimu huu.



Mheshimiwa Spika, wakati wameshafunga mikataba na kumaliza, katikati ya Mikataba ile tunapoanzisha kodi mpya, ni vizuri tukaweka utaratibu kwanza shirikishi, lakini ni vizuri kama tunapanga hivyo, tuandae katika muda ambao watu hawajafunga mikataba, vinginevyo Makampuni ya Kitanzania yanayofanya biashara hiyo tutawafilisi na pengine kuwafanya Watalii wengine kwenda katika nchi nyingine za jirani badala ya kuja huku kwetu.

Mheshimiwa Spika, hilo ni pendekezo langu katika maeneo yale yote ambayo yameongezwa kodi, ambayo imetolewa katika muda ambao watu wameshafunga mikataba ili isiathiri utalii na tujipe muda wa kuangalia nchi za jirani zetu na washindani katika sekta hii, ambao tunashinda nao wamefanya nini.

Mheshimiwa Spika, nasimama nikitamka bayana kuunga mkono Bajeti hii na nina kila sababu za kuunga mkono Bajeti hii, kwa sababu Sekta ya Maji imepewa kipaumbele na ziko fedha zilizotengwa kwa ajili ya maji na pengine wananchi wa Simanjiro wanaweza wakapata maji katika Makao Makuu ya Wilaya yetu ya Olkesmet, kufuatia mapendekezo na nyongeza ya Bajeti iliyotolewa. Lakini tuna imani pia pengine fedha zilizokuwa zimetengwa zitawasaidia wananchi waweze kupata maji katika maeneo ambayo hakuna maji.

Mheshimiwa Spika, hofu yangu katika hili na hili niliseme bayana na nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, tumegawana majukumu kati ya Mihimili ya Dola, Bunge lina jukumu la kupitisha Bajeti. Lakini kwa mujibu wa Sheria pia kwenye *Public Finance Act*, Waziri anaweza kuhamisha fedha kutoka katika eneo hili kwenda eneo lingine. Naomba katika mwaka huu haya yasifanyike. Tumefanya hivyo kwa mujibu wa sheria, lakini nadhani ni udhaifu pia tulioutumia. Lazima tuweke ukomo wa kiasi cha fedha kinachohamishwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye sekta ya Umeme, tulitenga karibu Shilingi bilioni 47, lakini matumizi halisi kwenye mitambo ya kukodi ya umeme, tulitumia zaidi ya Shilingi Trilioni

1.2, asilimia 17% ya Bajeti ya nchi ya fedha za ndani zinazokusanywa, fedha hizi hazijapata idhini ya Bunge, ila Waziri kwa kutumia Mamlaka aliyopewa, ambayo hayo ndiyo Mamlaka ninayosema, Bunge lazima lisikubali kunyonyoa madaraka yake, Serikali iliamua kuhamisha fedha hizo, bila ridhaa ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu hauna manufaa na unamomonyoa Mamlaka ya Mhimili mwingine wa Dola ambao ni Bunge, ni vizuri Wabunge na sisi tukawa tunashirikishwa katika hilo. Vinginevyo hakuna maana ya kuja kukaa hapa miezi mitatu, tukapanga fedha katika sekta mbalimbali, lakini baadaye Waziri akaweza kuzihamisha fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, tumekosa fedha za kupeleka Umeme Vijijini, kwa sababu zimepelekwa katika mitambo ya kukodi. Mitambo ya kukodi ya nani, zaidi ni ya watu binafsi. Lakini mle mle nilieleza ufisadi uliokuwemo katika hotuba yangu iliyopita kwenye Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kuwa muda ni mfupi, nakusudia kutafuta muda wa kutoa hoja, hata kama iliwaudhi wengine wakafanya waliyoyafanya dhidi yangu baada ya kutoka hapa. Nitapata muda wa kukueleza wewe mwenyewe nikitoka maana hapa siji kuomba kinga ya Bunge katika hili, najiamini kujilinda hata kama vitisho vingine vinafanywa na baadhi ya Watendaji Wakuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zinapotengwa kama zile za maji zive *ring phased*, lakini tukisema hata hivyo zifanyiwe hivyo, ni ngumu kwa sababu Waziri bado ana mamlaka ya kwetu yanaweza kuwa ni ushauri tu, lakini Waziri bado anapewa mamlaka. Kuna haja ya kutazama sheria hii ili ipunguze mamlaka wanayopewa Mawaziri na hasa Waziri wa Fedha, si lazima awe Mzee Mgimwa hata akija mwingine yeyote, ili tu kuona kwamba mgawanyo wa madaraka nao unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo nakubaliana na

Kamati ya Bunge ambayo inaongozwa na Mzee wetu Chenge kwa mapendekezo waliyoyatoa na ushauri waliouona katika ukurasa wa 36, juu ya kutahadharisha fedha hizi ambazo zilikuwa zimepelekwa katika mitambo ya umeme ya kukodi na ile ya *TANESCO*. Katika ukurasa huo Kamati iliweka bayana kwamba kwa bajeti ya mwaka huu zilitengwa shilingi bilioni 273 lakini hitaji kamili ni shilingi trilioni 1.2 kwenye kikao cha pamoja.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Chomboh na Mheshimiwa Bahati Abeid na Mheshimiwa Ngeleja wajiandae.

**MHE. MUHAMMAD AMOUR CHOMBOH:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu ya kusimama jioni hii, lakini pia nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuiunga mkono hoja hii, lakini nitakuwa tofauti kidogo na wenzangu, sitawapongeza Mawaziri sasa hivi bali nitawapongeza baada ya kuona haya yote ambayo tumeyapanga yametimizwa.

Mheshimiwa Spika, haya ambayo katika kipindi chote cha miezi mitatu tuliyokuwa hapa, tukichambua Wizara moja baada ya nyingine, mapato na matumizi na hatimaye kila Wizara tukaibariki na kuipa fungu la fedha kwa ajili ya maendeleo na matumizi kwa madhumuni ya kuweza kupatikana mustakabali wa maendeleo wa nchi yetu na watu wake, baada ya kuja hapa mwakani tukijaaliwa *Inshallah*, nikiona kwamba yale yote ambayo tumeyapanga kwa kipindi chote hiki yamefanikiwa, hapo nitatoa pongezi zangu.

Mheshimiwa Spika, nasema hayo kwa sababu Watanzania mategemeo yao mengi sana yapo katika bajeti hii, lakini tuna uzoefu ambao hata Watanzania wengine wana uzoefu kwamba, sisi ni mahodari sana wa kupanga mipango mizuri yenye kuleta matumaini na kila mmoja akawa na mategemeo kwamba, sasa hapa tumetoka. Lakini matokeo yake, usimamizi na utekelezaji wa yale yote ambayo tumeyapanga inakuwa hakuna kabisa.

Mheshimiwa Spika, tatizo letu ni kwamba sheria na taratibu na kanuni tulizojiwekea ambazo nyingi sana huwa zinapitishwa katika Bunge hili hatuzifuati na hatuzisimamii ipasavyo. Tunatakiwa Watanzania sasa hivi tubadilike na kila mmoja atimize wajibu wake na asimamie na afuate sheria na taratibu ambazo zinamwongoza katika sehemu yake aliyopo.

Mheshimiwa Spika, Watanzania walio wengi na hasa vijana ambao ndiyo wengi sana katika *generation* tuliyokuwa nayo sasa hivi, wanapenda sana starehe, hawapendi raha, nafikiri mnanielewa. Wanapenda starehe hawapendi raha, starehe ni kitu ambacho unaweza ukakipata bila taabu yoyote ile hata kwa kukirimiwa, lakini inachukua muda mdogo sana na wala haina taabu, mtu yeyote na wakati wowote anaweza akakupa starehe, lakini raha huwezi kuipata kama hujajihangaikia na wala hujaitafuta kwa njia yoyote.

Mheshimiwa Spika, raha ni kitu cha kuendelea, lakini starehe ni kitu cha muda mdogo sana. Lakini raha hutaweza kuipata kama hujajipinda kwelikweli, upate shida sana, uhangaike sana na ndiyo unaweza ukapata raha ya kuendelea. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania nawaomba tubadilike, tusipende starehe na tupende raha na raha haiji hivi hivi bali raha inabidi tujipinde, tuhangaike, tufanye kazi. Mwenyezi Mungu ametuumba sisi binadamu tufanye kazi, lakini sisi Watanzania hatufanyi kazi, tunajipangia muda wa starehe zaidi kuliko muda wa kufanya kazi. Katika saa 24,

Mtanzania anaweza kufanya kazi saa sita au tano, lakini muda mwingi kabisa uko kwenye kustarehe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunatakiwa tubadilike na Serikali ina wajibu wa kusimamia haya hasa kwa wale watendaji ambao wamepewa dhamana ya kututoa hapa tulipo, ni lazima watimize wajibu wao na Serikali iweze kusimamia. Kwa mfano, kama kauli ya leo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndiyo tunataka Waziri Mkuu wa Tanzania wa sasa hivi awe. Yale yasiwe kwa wale tu bali yawe mpaka kwa wafanyakazi. Wafanyakazi waliokuwa hawawajibiki kamata, fukuza, ajiri mwingine na wale wezi wakamatwe na kunyang'anywa mali zao twende mbele, tusioneane aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila siku ya Mungu tunakuwa tunabembelezana, hatufiki! Kila siku tunajaribu kusema kwamba nchi za jirani wameendelea kwani tusiendeleo sisi ni nani na wale ni nani? Tatizo letu tumeendelea starehe zaidi, Watanzania sasa hivi hakuna siku ya *weekend*, watu wote kuanzia Jumatatu mpaka Jumapili ni starehe tu kwenye majumba ya starehe. Leo taarabu kule, leo dansi huku yaani ni starehe kila asubuhi na jioni, tutapata wapi raha ndugu zangu? Tutafute njia ya kujikwamua.

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia pia suala la taratibu hizo hizo za kufuata sheria, ujenzi wa majumba ambayo yanajengwa katika miji yote ya Tanzania kwa kukosa kusimamia Sheria ya Mipango Miji, tunajijengea nyumba ambazo hazina utaratibu kabisa, kuna Idara ya Mipango Miji ambayo inapanga, lakini watekelezaji wa ujenzi ule wanajifanyia wanavyotaka bila kufuata sheria na taratibu za mipango Miji. Matokeo yake tunaona uchafu unaotokea Kariakoo, ule siyo mji bali ni uchafu!

Mheshimiwa Spika, sasa hivi umeanza katika Vitongoji vya Magomeni, Ilala. Manispaa zote za Jiji la Dar es Salaam zinaanza kujenga na hakuna utaratibu wa kusimamia mipangomiji kwa sababu hatusimamii taratibu na sheria tulizojiwekea.

Mheshimiwa Spika, nyumba ambazo zimejengwa Kariakoo kama mnavyoziona, nyumba zile kiutaratibu zinatakiwa ziwe na *packing* chini ya kila nyumba, lakini matokeo yake nyumba zile hazina *packing* na zinajengwa hovyo hovyo tu. Kwa hiyo, ni wajibu wa Serikali kusimamia taratibu na sheria ndiyo tutakavyotoka.

Mheshimiwa Spika, rushwa, wenzetu wa nchi jirani ya Rwanda wameweza kunufaika kwa sababu ya kuizuia rushwa kwa njia moja. Wamezoea mtindo mmoja, Rwanda kuna taratibu za kwamba, Askari wa Barabarani ili kuwazuia wasipokee rushwa wanamtumia dereva kwenda kufanya makosa, wanampa pesa ili Askari apokee ile rushwa, wakati wazuia rushwa wanakaa wanamwangualia. Askari akipokea rushwa, basi wanakwenda kumkamata kwamba Askari kapokea rushwa,

Mheshimiwa Spika, matokeo yake sasa hivi Askari anamwogopa raia na raia anamwogopa Askari, kila mmoja anamwogopa mwenzake, hakuna rushwa. Pia wenzetu wanasimamia maamuzi ambayo wanaamua. Tatizo letu Tanzania ni pale pale hatuwezi kuendelea kama hatujasimamia maamuzi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa bajeti hii tunayoipitisha leo, ikiwa hatukwenda kuitekeleza kama vile tulivyokubaliana na tulivyokaa miezi mitatu hapa, basi mwakani tukija tukirudi na stori zile zile ina maana haina faida hata kitu kimoja. Tusimamie na tuweze kuona utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, barabara zetu zinazotoka Dar es Salaam kwenda mikoani tunaziona zinavyoharibika na matatizo haya nashauri Serikali tuchukue ule mpango wa *PPP* yaani *Public Private Partnership* ili barabara hizi ziweze kupewa Wakandarasi wasimamie na watoze *road toll* na wazisimamie. Zikiharibika wawe wanatengeneza ili kusudi hayo magari mazito yanayopita kuchukua mizigo, basi yawe yanaweza kutozwa tozo ili kuweza kutengeneza barabara zile.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali ijenge barabara za mikoani ndani ndani ambazo siyo *main road* ili ziweze kutoa bidhaa kutoka ndani ya Vijiji na ndani ya Wilaya zipeleke barabara kuu kwa ajili ya kuweza kuzifikisha sokoni. Kwa kufanya mpango huo, tutaweza kuzisimamia barabara zetu na kila siku zitakuwa zinaonekana ziko katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kodi au tozo za *sim card*, napendekeza kwamba ni vizuri kodi zile zipatikane au ziwepo, lakini siyo katika kiwango kile cha sh. 1,450/= kwa mwezi. Serikali ikae na itazame ni kiasi gani inaweza kuwapunguzia, lakini kuna haja ya kuweza kupatikana kodi kupitia kadi za simu.

Mheshimiwa Spika, halafu pia ningeshauri makampuni ya simu yashauriwe, kuwe na usimamizi wa kuweza kusimamia hizo *sim card*, zisiwe zinauzwa kama karanga tu barabarani, hakuna hata nchi moja duniani kadi za simu zinauzwa kama Tanzania.

Mheshimiwa Spika, watu wanatumia kadi za simu kwa maslahi yao na kwa kutukana watu na huu usajili uliofanyika hapa ni kama kiinimacho tu, mtu ananunua kadi asubuhi anamtukana mtu, anaichana jioni. Hakuna uwezekano wa ku-*control* kadi za simu, makampuni ya simu yashauriwe kwamba, kadi za simu yaani *sim card* zidhibitiwe, siyo mtu anakwenda kununua kadi ya simu tu kama vile anavyonunua karanga, haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, hakuna kwingine kokote zaidi ya Tanzania hapa, unaweza kwenda nchi za nje, ukitaka kutafuta kadi ya simu ni lazima utoe na *passport* yako au uwe na mwenyeji wa kuweza kukudhamini kupata *sim card*, lakini hapa unakwenda kununua hata kumi kwa wakati mmoja kwa kampuni yoyote ukazitumia na ukazivuruga kama unavyotaka bila mtu yeyote kuweza kujua. Hii nafikiri siyo sawa, makampuni ya simu yasimamie utoaji wa *sim card*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Hotuba yako ilikuwa nzuri sana kwa sababu bila kufanya kazim umaskini hautoki. Mheshimiwa Bahati Ally Abeid, atafuatiwa na Mheshimiwa Ngeleja!

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niwe mchangiaji kwenye hotuba hizi zilizo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kabla sijasahau, napenda niunge mkono hotuba hizi kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia niungane na wenzangu kukupongeza wewe binafsi kwa kulifanya Bunge letu sasa kujadili bajeti ambayo imetufanya tuonekane Bunge hili sasa linakwenda na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia bajeti hii kwa kuanza kusema, naiomba Serikali yangu ongezeko hili la kodi ya mafuta ya dizeli na petroli kwa mwaka huu, hii kodi uifute. Kupanda kwa kodi hii au ongezeko la kodi ya mafuta huwa linasababisha mfumuko mkubwa wa bei za chakula, lakini nauli kwa abiria wetu au wafanyakazi wetu lakini kwa mambo yote ambayo yanahitajika na jamii kwa wakati huu. Jamii yetu ya Watanzania inalalamika sana bei za vyakula...

**SPIKA:** Jamani nitawataja wote wanaopiga kelele sasa hivi, nawaomba mtulie. Mheshimiwa Bahati endelea!

**MHE. BAHATI ALI ABEID:** Mheshimiwa Spika, dakika zangu mbili hizo zilindwe basi!

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ongezeko hili la bei ya vyakula, mafuta yanapopandishwa kodi inakuwa ni kubwa sana, tuwahurumie Watanzania, Watanzania wanatupenda na sisi tuwapende. Naomba kwa mwaka huu Mheshimiwa Waziri afute kabisa ongezeko hili la mafuta ya petroli na dizeli, naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sasa niende kwenye



mabenki, Watanzania wajasiriamali na wafanyabiashara ndogo ndogo wakati mwingi tunasema hawakopesheki na wale wanaothubutu basi huwa wanakabiliwa na riba kubwa ya mabenki yetu haya ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashindwa kuelewa, hivi Serikali inashindwa nini, Waziri wa Fedha na Gavana wanashindwa nini kukaa na haya mabenki kuangalia hali halisi na mazingira yetu ya Watanzania wakaweza kuwapunguzia riba wafanyabiashara na hasa wafanyabiashara wadogo wadogo ili waweze kukopesheka na kufanya biashara na kupata faida. Sasa hivi wanafanya biashara kwa kuyanufaisha mabenki tu, lakini hawana faida yoyote wanayoipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii siyo sahihi, watu wanasema kula nikule, kama benki inapata basi na mfanyabiashara huyu anatakiwa apate. Naiomba sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi ambayo ni sikivu, namwomba Waziri na Gavana wetu na watalaam wengine tuweze kukaa na haya mabenki, kuyashauri vizuri ili tuweze kuwanufaisha Watanzania walio wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine nasema kwa nini Benki ya Wanawake kwenye kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri imeeleza vizuri jinsi Benki ya Wanawake inavyofanya kazi, inahudumia wanawake na wanaume, inatoa mikopo kwa masharti nafuu na riba ndogo.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako Watanzania tuiunge mkono benki hii kwa wingi ili iweze kufungua matawi katika maeneo mengi ya Tanzania hata kule Zanzibar ili Watanzania waweze kunufaika na mikopo yenye masharti nafuu lakini pia yenye riba ndogo.

Mheshimiwa Spika, nadhani tunaweza lakini hatujajipanga vizuri kwenye mabenki, lakini tukijipanga vizuri tunaweza.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo

nataka niligusie ingawa sina maneno mengi sana ya kusema kwenye bajeti hii, nataka nigusie wafanyakazi ambao wanafanya kazi kwenye Wizara za Muungano ambao wako Zanzibar na wenzangu wamegusiagusia na mimi napenda nigusie.

Mheshimiwa Spika, zile pesa ambazo zinatakiwa zipelekwe na kwa kweli zimepelekwa, lakini kuna baadhi ya miezi hazikupelekwa, haya ni mambo madogo sana. Lakini kuna watu wengine wameshikia bango jambo hili, wameshikia bango mambo madogo madogo ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha anaweza akaambiwa na akarekebisha tu, ni mambo ya kurekebisha, lakini watu wameshikia bango.

Mheshimiwa Spika, naona hawa ni wale wale watu ambao wameuchokonya Muungano wetu mzuri, wamechokonya chokonya mpaka tukaanza kuingia dosari na sasa unatufikisha tunakokwenda. Naomba mambo kama haya yasipewe nafasi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri arekebishe haya mambo na katika Wizara yake kama kuna mtu na yeye anapelekapeleka hizi taarifa ambazo hazina msingi wowote, basi achukuliwe hatua.

Mheshimiwa Spika, siku zote nikisimama hapa nasema hatuna shida na wafanyakazi, vijana wetu wamesoma wako kila eneo la nchi yetu waajiriwe. Yeyote ambaye anaonekana hafuati masharti na misingi ya kazi yake, basi anaweza akafuata wakati wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwa kweli hii ni kero ambayo haiwapati Wazanzibari tu, bali inawapata Watanzania walio wengi, kero ya kutoa gari Zanzibar kuleta Tanzania Bara. Kwa kweli Wabunge wako pia tunapata tabu, maana ingekuwa hakuna ushuru wowote mbona ni rahisi tu unakuja na gari lako mpaka Dodoma, Bunge likiisha unatoka mwenyewe unakwenda nalo mpaka Zanzibar, unalisafirisha

kwani kusafirisha gari siyo ghali. Kwa hiyo ungekuwa unasafiri nalo kwenda Zanzibar na kurudi, isingekuwa inaleta matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wenzenu tuko katika hali ngumu, ukiwa Tanzania Bara ununue gari, hakuna tena ule msamaha wala nini unalinunulia huku huku tena unatafuta gari ndogo tu. Ni Wabunge wangapi Wazanzibari hapa wamepata ajali kwa gari ndogo ndogo? Tunanunua gari ndogo, tunapata ajali nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana hili suala tulione ni muhimu sana kwa wakati huu tulionao. Kama kawaida yangu husema yangu moja kwa moja, sina maneno mengi, naunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana, sitaki kukupotezea muda. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, hata dakika zako mbili wala hatukukurudishia. Sasa nimwite Mheshimiwa Ngeleja, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina yumo na atafuatiwa na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii na moja kwa moja naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu kukupongeza wewe awali kabisa kwa kuanzisha utaratibu huu wa kujadili bajeti yetu ambapo tunahitimisha baada ya kujadili Wizara ambazo zimewasilisha maombi yao ya fedha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kukushukuru wewe kwa kuunda Kamati ya Bajeti ambayo imetusaidia sana kama Taifa. Pia tumpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa Andrew Chenge na Wajumbe wake kwa kazi kubwa ambayo wameifanya.

Mheshimiwa Spika, vile vile tunaipongeza sana Serikali

kupitia Waziri wa Fedha, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Wasira anayehusika na mambo ya Uratibu na Mahusiano.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo sasa niseme sababu za kuunga mkono bajeti hii kama ambavyo wenzangu wamesema.

Mheshimiwa Spika, sababu ya kwanza, kama ilivyojitokeza, bajeti hii ni kati ya bajeti bora tulizowahi kuwa nazo tangu tupate uhuru wa Taifa hili. Nasema hivyo kwa sababu kama Taifa tukiongozwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tumeendelea kubaini na kuibua fursa ambazo zinaweza kututoa hapa tulipo na kutusogeza mbele zaidi.

Mheshimiwa Spika, utaratibu tuliona hivi sasa wa vipaumbele hivi sita ambavyo vimeanishwa katika utaratibu wa *Big Results Now* ni kielelezo sahihi cha kuona jinsi gani ambavyo Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa tayari muda wote kufanya mapinduzi na mabadiliko ya kweli ili kama alivyosema Mheshimiwa Chomboh, kuleta raha ya muda mrefu kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ambayo tumeyabainisha kama vipaumbele tukianza na eneo la maji, sisi wananchi wa Wilaya ya Sengerema ni kati ya wanufaika wakubwa katika eneo hili. Pamoja na fedha kuongezwa baada ya mjadala mkubwa uliozuka wakati tunaendelea na bajeti ya Wizara ya Maji, bado Sengerema tunanufaika na mpango huu kupitia bajeti hii kwa kuzingatia mradi mkubwa wa Maji safi na Mazingira unaotekelezwa katika Mji wa Sengerema.

Mheshimiwa Spika, katika Mradi huu Sengerema imepata dola za kimarekani milioni 14, ambazo ni sawa na shilingi bilioni 23. Pia kuna miradi mbalimbali ya maji ukiwemo ule ambao unatoa maji Ziwa Viktoria kupeleka kwenye vijiji vya Bitoto kupitia Biyagu na Kalangalala.

Mheshimiwa Spika, tunaona katika bajeti hii pia kupitia

utaratibu ambao tumeuanzisha na kupitia vipaumbele hivi ambavyo Serikali imevileta, tumeainisha na hatimaye tumeongeza fedha kwenye maeneo ambayo tunaamini ndiyo yatatuongezea kasi ya kufikia malengo ya dira yetu ya mwaka 2025. Hili eneo la Nishati nimeona fedha zimeongezwa zaidi ya shilingi bilioni mia moja hamsini na kitu, kwenye maji tumeongeza zaidi ya shilingi bilioni 184.

Mheshimiwa Spika, tumeona pia maeneo mengine kama kilimo, elimu, uchukuzi na kuongeza mapato. Kwa hatua kama hizi kwa kweli ni vyema kuiunga mkono Serikali katika shughuli ambazo inazifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu ambao Mheshimiwa Rais ameuanzisha kupitia kile kitengo ambacho kitakuwa kinafuatilia usimamizi wa miradi, *Presidential Delivery Bureau* ni hatua ya kujivunia na kujisifu kwa sababu ni eneo ambalo litatusaidia sana katika utekelezaji wa miradi ambayo vinginevyo ingeweza kuwa inachukua muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii imetuonesha kwamba, usimamizi wa uchumi ni mzuri na ndiyo maana leo tunaona mfumuko wa bei umeshuka mpaka asilimia 8.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo linanifanya niunge mkono hoja hii ni lile ambalo limekuwa kero kwa Watanzania kwa muda mrefu na hasa kwa sababu ni kero katika kundi kubwa...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hatuko nje, tuko ndani ya Bunge.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, eneo hili ninalozungumzia ni kuhusu kazi na ajira. Ukisoma hotuba hii unaona program ambayo Serikali inakuja nayo ya ajira kwa vijana nchini, itakayotekelezwa kwa miaka mitatu kuanzia mwaka huu hadi 2016. Hili ni jambo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mikakati mbalimbali imeelezwa hapa na kuhusu hili naomba kuwaasa Watanzania wenzangu

popote walipo na hasa vijana kwamba, ni Chama cha Mapinduzi na Serikali yake pekee ndiyo kinaweza kuja na program ambayo inaainisha na kuonesha dhamira ya kweli kulisaidia kundi hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunafahamu katika siku za mwisho hizi na kama ambavyo maandiko matakatifu yanasema, yapo makundi yatakuja kupotosha watu kwa kusema habari za uongo. Hata hivyo, Chama cha Mapinduzi, lazima kisimamie ukweli kwa sababu tuna deni kwa Watanzania. Wenzetu ambao hawana mamlaka au dhamana yoyote ya kuongoza Watanzania, wanaweza kusema lolote, lakini kama tunavyofahamu maendeleo ni hatua hayawezi kuja kwa siku moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi muda wote imekuwa ikieleza Watanzania kwamba maendeleo ya wananchi hayawezi kufikiwa kwa siku moja, ni mpaka kwenda hatua kwa hatua. Ndiyo maana tunakumbushwa hapa wanaofuatilia historia za nchi iliyoendelea kama Marekani, mpaka wakati wanafikisha miaka 160 tangu wapate uhuru, hali yao ya umeme ilikuwa kama Tanzania tulivyo leo.

Mheshimiwa Spika, Marekani walipata uhuru tarehe 4 Julai, 1776 lakini wameanzisha kitengo kinachofanana na cha kwetu cha umeme vijijini, *REA* mwaka 1935 na hasa baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia. Miaka 159 mpaka 160 hali ya umeme kwa Wamarekani ilikuwa chini ya asilimia 30 ukiondoa Jimbo la California ambao walikuwa zaidi kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ni ajabu gani kwa Watanzania leo tukiwasimulia habari ya miaka 50 ya uhuru kuwaeleza kwamba mikakati ipo na hatua zinazidi kuchukuliwa? Watu wanataka kuwaaminisha Watanzania kwamba mambo haya yangeweza kufanyika kwa muda mfupi, haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii habari ya kutulinganisha

Tanzania na nchi jirani katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, nataka niseme kwamba ni vyema tukawaambia Watanzania jambo la kweli, wafahamu kwamba shilingi ya Tanzania ambayo tunaipata katika mradi wowote ukilinganisha na nchi zote hizi nne zingine katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, ujue kwamba sisi kama Taifa shilingi hiyo tunaitumia kwa eneo dogo sana ukilinganisha na wenzetu kwa sababu nchi tano za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mfano; Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi kwa pamoja ni eneo dogo kwa kiwango cha kilomita za mraba kuliko eneo la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia habari ya kueneza maji katika nchi hii, kusambaza umeme, kujenga barabara, ni tofauti na kuzungumzia habari ya Kenya, Uganda, Rwanda ama Burundi. Haya ni mambo ya kweli, ni lazima tuyaseme, tusipowaambia Watanzania watazidi kupotoshwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia tuipongeze sana Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), wanafanya kazi kubwa na kwa kiasi kikubwa, wanatembea kwenye maeneo yao. Pamoja na kuwapongeza niseme kwamba, ufanisi unaojitokeza katika Mamlaka ya Mapato Tanzania ni pamoja na vyombo vya maamuzi hasa vinavyoshughulikia migogoro ya kodi likiwepo Baraza la Kodi pamoja na Bodi ya Kodi.

Mheshimiwa Spika, ninachoomba ni kwamba, maeneo haya pia tuyaimarishe kwa kuyapa bajeti ya kutosha, yajengewe majengo yao ikiwezekana na pia vitendea kazi viboreshwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo la utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA) awamu ya pili, tumeona wamefanya kazi kubwa. Wameshafanya tathmini ya kiwango cha umaskini kwa Watanzania kwa kaya sasa na tunaaminishwa na Mheshimiwa Waziri kwamba bajeti hii imepangwa kwa kuzingatia matokeo ya sensa iliyofanyika mwaka jana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maana yake ni nini? Serikali

inafanya kazi ya kweli kuwahudumia Watanzania kwa sababu kuanzia sasa tutakuwa na takwimu sahihi ambazo zinatuwezesha Watanzania kupanga mpango wetu kwa uzuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la bodaboda, naunga mkono ziendelee kupata hiyo nafuu kwa sababu pamoja na kwamba, tumekuwa na hofu wakati mwingine katika baadhi ya maeneo kwamba bodaboda siyo za hao wanaoziendesha, lakini yapo maeneo ambayo wenye bodaboda ni wale wanaoziendesha. Kwa hiyo, ni vyema tukaendelea kuwapa unafuu.

Mheshimiwa Spika, deni la Taifa lisiwatie hofu Watanzania. Hili ni eneo la kitaalam na tumeambiwa kwamba sasa hivi tuko kwenye asilimia kidogo, kwenye *ceiling* hatujafikia asilimia 50, tulichotumia sasa hivi ni asilimia 18.9, hofu ya nini? Kuna watu wanapotosha Watanzania kwa kuwaambia kila mtu anadaiwa sh. 500,000/= watoto, walemavu na nini. Haya ni masuala ya kitaalam na haiwezekani yakaongelewa na kila mmoja. Kama dunia nzima inasema kwamba, bado deni linahimilika, hofu ya nini? Ushauri wangu ni kwamba tuendelee kukopa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, Kanda ya Ziwa zao kubwa ni pamba, tuliangalie kwa kujenga viwanda, lakini pia ikiwezekana ile *beam* iliyokuwa inasemwa ya mazao. Mwaka jana tulikuwa tunaiongelea, lakini sasa hivi hatujajua. Hata hivyo, haya hayatawezekana kama Watanzania hatutakuwa pamoja kutetea amani yetu. Tusipoitetea amani ya nchi hii haya tunayosema hayatawezekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naendelea kutoa wito kwa Watanzania wote wa kada zote na makundi yote, tukae pamoja tushirikiane kulinda amani hii, lakini pia uwajibikaji uwe ndiyo nguzo. Mafanikio yatakutana na uwajibikaji wa kila mmoja alipo, ndipo ambapo tunaweza kufaidi matunda ya mipango mema inayofanywa sasa hivi na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)



Mheshimiwa Spika, naungana na Watanzania wenzangu kukipongeza Chama cha Mapinduzi, kwa ushindi kilioukata katika uchaguzi wa Kata unaoendelea na *Inshallah* tunaamini hata Arusha mambo yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nashukuru sana na naendelea kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana kwa mchango wako wenye elimu ya kutosha. Sasa nimwite Mheshimiwa Kikwembe atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, halafu atafuatia Mheshimiwa Mwigulu Nchemba.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyoko hapa mbele yetu. Nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitaungana na Wabunge wenzangu kukushukuru kwa namna ya pekee ambavyo umeweza kuwa mbunifu kwa kuanzisha Kamati hii ya Bajeti ambayo kwa kushirikiana na Serikali imeweza kutufikisha hapa tulipo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia niungane na Watanzania wenzangu hasa wa Chama cha Mapinduzi, kujipongeza na kuwaambia ushindi upo kwa mwaka 2015 na wala wasiwe na wasiwasi. Suala la msingi niwaombe Watanzania kwamba tushirikiane katika kusimamia miradi ya maendeleo ili kuhakikisha ushindi unapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda nichangie kwa kuanzia na uhamishwaji wa fungu moja la fedha kati ya zilizoidhinishwa na Bunge na zile zilizotumika. Napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge walioongelea hili.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli si utaratibu mzuri, Bunge linapokuwa limeidhinisha fedha halafu Waziri kwa kutumia mamlaka yake anaamua kuidhinisha fedha nyingine nje na utaratibu wa Bunge. Huu unakuwa utaratibu ambao unatia hofu na shaka kwa hizo fedha nyingine ambazo zinakuwa zimeongezwa nje ya utaratibu uliopangwa na Serikali. Kwa

hiyo, ni vema kabisa niungane na Mheshimiwa Ole Sendeka kwamba, kama kuna uwezekano wa kupunguza haya matumizi, maana yake inawezekana wengine wakawa na haya mamlaka na wakaweza kuyatumia visivyo ambayo ni kinyume na utaratibu.

Mheshimiwa Spika, pia inatia hofu kwa sababu tunakuwa hatuelewi hizo fedha zilizoongezwa zinakwenda kufanya kazi gani? Kama Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii walivyofanya, kama tungeambiwa humu ndani kwamba vitanda vimeongezeka pale *MOI* ningeweza kuelewa, lakini sasa tunakuta fedha zinaongezwa lakini matatizo yako pale pale. Kwa kweli huo siyo utaratibu mzuri na napenda Serikali iweze kuliangalia hilo na kulifanyia utaratibu unaohusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine naiunga mkono hoja kwa maana moja; Serikali katika kipindi hiki cha bajeti imeweza kukusanya na kupokea michango ya Wabunge na kuweza kuifanyia kazi. Hilo ni jambo jema na napenda kwa kweli katika bajeti zinazokuja, Serikali iendelee kuwa na utaratibu huo wa kuwa na bajeti shirikishi.

Mheshimiwa Spika, hii ndiyo bajeti shirikishi ambayo unamsikiliza Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya wananchi, na wananchi hapa kwa namna moja ama nyingine wanakuwa wameshirikishwa katika kufanya maamuzi kwenye hiyo bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, narudia tena kusema naunga mkono hoja kwa sababu kwanza, katika Wizara ya Maji kama Wabunge wenzangu wote waliotangulia walivyosema, fedha zimeongezeka. Kwa hiyo, naamini kabisa ndugu zangu wa Kasansa, Mamba, Mpimbwe, Katuma na Mwese, hawatapata matatizo ya maji.

Mheshimiwa Spika, hizi fedha naamini na wao zitakuwa kwenye mgao kwa ajili ya kupata maji, hasa ndugu zangu wa Majimoto ambao ndugu zangu wa upande wa

pili wamekuwa mara kwa mara wakiwapotosha wananchi wa Majimoto pale kwamba yale maji ya moto yana sumu wakati si kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine, napenda niongelee suala la ukusanyaji wa mapato kwa njia zingine tofauti na kuongeza kodi/ushuru kwenye mafuta. Sisi watu wa vijijini unapotuongezea kodi kwenye mafuta kwa kweli ni tatizo. Kauli mbiu ya Chama cha Mapinduzi na Serikali ni maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kama ni maisha bora kwa kila Mtanzania mafuta yanapopanda bei, vifaa vya ujenzi vinavyotoka Dar es Salaam mpaka vifike Katavi - Mpanda vitauzwa shilingi ngapi? Wakati tunataka mwananchi wa kawaida naye aondoke kwenye nyumba ya tope na nyasi. Ndugu zangu wa Singida wanaosema aondokane na nyumba za tembe sasa kama vifaa hivi vitapanda bei mwananchi wa kijijini, je, ataweza kumudu hizi gharama? Naomba Serikali iangalie hilo suala.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane kabisa na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia kusema, hakuna sababu kwa kipindi hiki kuongeza huo ushuru wakati tuna vyanzo vingine vya mapato kama kwenye ardhi na majengo. Waheshimiwa Wabunge wengine wameshachangia kuhusu hilo, kwa hiyo, naomba nalo Serikali ilifanyie utaratibu na iangalie namna gani ambavyo inaweza ikatumia vyanzo vingine kupata mapato.

Mheshimiwa Spika, kuongeza ushuru kwenye petroli ni sawa na kumwonea mwananchi wa kule kwetu Katavi, Kasansa, Milekwa na Kalema. Mwananchi huyu atapelekaje simenti kule ili akajenge nyumba?

Mheshimiwa Spika, kutoka Mpanda mpaka Tabora, nauli sasa hivi ni sh. 30,000/=, kutoka Tabora mpaka hapa Dodoma ni sh. 40,000/=, kwa hiyo inakuwa sh. 70,000/= hiyo ni nauli ya kawaida sasa hivi. Tutakapoongeza kodi hapa sina shaka inaweza ikafika 150,000/=.

Mheshimiwa Spika, sasa tutakuwa tunafanya nini kwa mwananchi wa kawaida anayesubiri kipindi hiki avune mazao yake ambayo si ajabu hana uhakika sana kwa sababu mvua hazikuwa nzuri sana, akapata kidogo, hiyo hiyo fedha apeleke watoto shule, asafiri aende Bugando kwani ndiyo hospitali tunayoitegemea ama Dar es Salaam!

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mtu wa Katavi tutakuwa hatumtendei haki hata kidogo, kwa sababu nimezaliwa na kukulia huko na shida za huko nazifahamu ndani na nje na wananchi wa kwetu kule tunawafahamu. Naomba hata baadhi ya viongozi mfike Katavi ili maamuzi haya tunayoyafanya muweze kujionea.

Mheshimiwa Spika, si Katavi tu bali hata kule Ruvuma kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama, huwezi kutoa sementi hapa ukaipeleka Ruvuma kwa bei ile ya Dar es Salaam. Tutakuwa hatumtendei haki mkulima, kwa hiyo, naomba kabisa hilo nalo liangaliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna hili suala la ukusanyaji wa mapato kwa hawa watu wa *TRA*. Tumekuwa tukiwalalamikia sana mara kwa mara kwamba kuna mianya ya rushwa, kupandisha au kushusha thamani ya vifaa, suala ambalo linapelekea zaidi rushwa. Sasa ifike mahali hawa *TRA* wawe wabunifu na waangalie ni taratibu zipi watakazozitumia kupata haya mapato na si kumuonea mlaji wa mwisho ambaye ndiye msafirishaji.

Mheshimiwa Spika, naliongea hili kwa sababu gani? Kama kumekuwa na malalamiko ya mara kwa mara kuhusu rushwa, TAKUKURU ipo, iende pale ikafanye uchunguzi ituletee hayo matokeo na sisi tuweze kufanya maamuzi, kwa sababu tunafanya hivyo kwa ajili ya wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine napenda tu niongelee kuhusu watendaji. Najua bajeti hii itapita, fedha zitatoka zitapelekwa kwenye Halmashauri na wapi. Nakuomba sana kupitia Serikali, Serikali iwachukulie hatua watendaji wabadhirifu kwa kuwapeleka Mahakamani, hii nchi

inaongozwa na Sheria na si kuwahamisha kutoka Halmashauri moja kwenda kufanya ubadhirifu Halmashauri nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia wale wote waliokwamisha miradi kwa mfano, kama mradi wa barabara kutoka Sumbawanga – Kizi - Kibaoni wale Wakandarasi wamekaa pale, hawana shughuli ya kufanya, ni kama vile wapo *picnic* Lyambalyamfipa pale. Ukiuliza wanakwambia hawana watu wenye utalam, waliwezaje kupata ile *tender*, hao watu wanatakiwa kuchukuliwa hatua. Kuanzia Meneja wa *TANROAD* na kwa nini hawawaelezi wananchi kuhusu maendeleo ya hizo shughuli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, watumishi wazembe kama hao wanapaswa kuchukuliwa hatua za kisheria ili iwe fundisho kwa watu wengine wanaokwamisha miradi kwa makusudi ambayo inashindwa kumalizika, kwa sababu tunapanga hapa fedha za maendeleo, kwa hiyo, fedha hizo zitoke kwa wakati zikafanye kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia Kamati za Bunge kupitia Wizara zake ziweze kusimamia kikamilifu. Juzi juzi hapa, wiki iliyopita, Mheshimiwa Mbunge aliomba namna ambavyo Kamati zinaweza kushirikishwa kusimamia miradi. Mheshimiwa Waziri alitoa majibu hapa akasema; wale wanaokagua wengi ni *experienced*, wana elimu hiyo, ma-*engineer*, lakini kama barabara mbovu hata kwa macho unaweza kuona hata kama hujakwenda shule. Kwa hiyo, Kamati za Bunge zisimamie kikamilifu matumizi ya fedha ambazo tunazipitisha.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niombe katika fedha zilizoongezwa kwa ajili ya vijana na akinamama. Uzoefu unaonesha kwamba hizi fedha nyingi zinaishia mijini, vijana wa vijijini na akinamama vijijini kuzipata ni tatizo. Niombe Wizara husika hizi fedha ziende kwenye Wilaya, kila Wilaya kuna Benki za Posta, wakaweka pale madirisha ili wanawake hasa wa Katavi, Sumbawanga, Simiyu, Songea, Mbeya kule kwa ndugu yangu wa lleje na Njombe kwako Mheshimiwa Spika, waweze kupata huduma hizi kwa urahisi. Kwa sababu

20 JUNI, 2013

mtu hawezi kutoka Njombe, Katavi au Sumbawanga aende Dar es Salaam kwa ajili ya kufuatilia mkopo wa 500,000/= au wa 2,000,000/=.

Mheshimiwa Spika, nimeambiwa na Kilolo ...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante, nimeanza kukutilia mashaka. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na Mheshimiwa Hawa Ghasia na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya.

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nianze kuungana na wenzangu kwa kukupongeza kwa *innovation* yako ya kubadilisha muundo wa uwasilishaji wa bajeti pamoja na kuunda Kamati ya Bajeti ambayo imeanza kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikiwasikiliza Waheshimiwa Wabunge wenzangu wakiogelea katika kuchangia hotuba hii kwa kuzungumza maji, umeme na kadhalika. Lakini tukumbuke kwamba Waziri wa Fedha akisaidiana na *Pay Master General* wake, Katibu Mkuu na Manaibu Mawaziri, wao kazi yao ni *collect* mapato, halafu wanagawa hizo fedha kwenye Wizara mbalimbali. Sasa kila Waziri ana *portfolio* yake na *mandate* yake ya kugawa fedha anavyotaka.

Mheshimiwa Spika, sasa Wabunge wamekuwa wakilalamika kuhusu *inequitable distribution of resource*. Nadhani kazi hii tumpe Waziri Mkuu, Waziri Mkuu ndiye anatakiwa kusimamia *equitable distribution of resource*.

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye Wizara ya Fedha, nianze kumpongeza Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya, lakini namwomba

Mheshimiwa Waziri aanze kwa ku-*put his house in order*, nina maana gani? Wizara ya Fedha inasimamia vyombo kama *TRA*, inasimamia Benki Kuu, lakini mimi nimekuwa Serikalini kwa muda mrefu, sijui kama mambo yamebadilika, wataalam wa *TRA* na wataalam wa Benki Kuu wamebobeza zaidi kuliko wataalam waliopo Hazina.

Mheshimiwa Spika, sasa inabidi Hazina kwa kweli wazidi kuwaongezea uwezo. Watu wa *TRA* wamebobeza katika *taxation*, watu wa Benki Kuu wamebobeza katika *monetary policies*. Kwa hiyo, inabidi m-*put your house in order* kwa kuwa na wataalam ambao wanaweza kusimamia haya mashirika ambayo yana wataalam waliobobeza.

Mheshimiwa Spika, urasimu katika *TIC*, mwaka jana tulitembelea Uingereza na tukapata nafasi ya kuzungumza na Balozi pamoja na Maafisa wake. Balozi wa Uingereza alizungumza kwa masikitiko sana kwamba katika *TIC* kuna urasimu kwamba, wawekezaji kutoka Uingereza wanapata shida na wameanza kukata tamaa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie jambo hilo. Inawezekana kabisa kuna urasimu pia *TRA*, kuna rasimu kule *BRELA*, Wizara ya Viwanda na Biashara, nao lazima waangalie jambo hilo. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri alingalie jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi. Sekta binafsi bado ni ndogo, lakini inakua kwa haraka sana kutokana na wawekezaji kutoka nje kuja kuwekeza. Wawekezaji wanaokuja *they are very sophisticated in terms of management skills* pamoja na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, inabidi Maafisa wetu tuwajengee uwezo waweze kuzungumza lugha moja na hawa wawekezaji. Kwa hiyo, ushauri wangu ni kuzidi kuwajengea uwezo, kwa mfano, kuwapa *negotiation skills*, hata Wanasheria wanaoshughulikia mikataba nao wapewe *negotiation skills*.

Mheshimiwa Spika, sasa hii sekta binafsi inakua haraka sana, lakini katika nchi ambayo ni maskini na nchi inayoendelea hatuwezi kuiachia *private sector* ifanye kila kitu, hatuwezi kuiachia *market forces* i-determine mambo yote. Ie nadharia ya Adam Smith ya *invisible hand* hatuwezi kuitumia hapa.

Mheshimiwa Spika, lazima Serikali katika hiyo *partnership* ingawa *private sector* itakuwa mhimili wa uchumi, lakini Serikali iwe kiongozi, iweze ku-*regulate private sector* without *stayfolding it* yaani iweze ku-*regulate, regulate* Kiswahili siyo udhibiti, lakini kuna neno ku-*regulate without stayfolding* maana yake bila kuikaba roho hiyo *private sector*, lakini kui-*regulate*.

Mheshimiwa Spika, kupanua wigo wa kutoza kodi. Hii iko chini pia ya Tume ya Mipango au Mheshimiwa Stephen Wasira ana huu mpango mzuri wa MKURABITA, tuutumie mpango huu wa MKURABITA, tuwape fedha za kutosha kwa sababu hawa ndiyo tegemeo la wananchi wa kawaida. Kama tunavyopeleka fedha kwenye maji kwa ajili ya wananchi wa huko vijijini pamoja na umeme basi tuiwezeshe hii MKURABITA ambayo itawasaidia kuwawezesha kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, juzi walikuwa Ngara, lakini waliweza kupima mashamba ya vijijini viwili tu kati ya vijiji 73, k kwa sababu hawana fedha za kutosha. Naomba sana MKURABITA tuiangalie kama mkombozi wa watu wa kawaida, kwa hiyo, tuipatie fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni *the big results now*, hii naiweka kwenye Tume ya Mipango. Niliizungumzia wakati nachangia Wizara ya Viwanda na Biashara, lakini naona Waziri hakuigusia.

Mheshimiwa Spika, *Big results now* ni Mpango ambao tumeukopi kutoka Malaysia, lakini Malaysia haijawa nchi ya maendeleo makubwa kwa sababu ya *big results now, big results now* ni mbinu ambayo imegunduliwa juzi juzi tu.



Mheshimiwa Spika, wamekuwa nchi ya maendeleo ya uchumi sana kwa sababu ya sera zao nzuri za uchumi. Sera mojawapo, ni sera ya wazawa. Katika miaka ya 80 aliyekuwa Waziri Mkuu Mahadhiri Mohammed aliwaambia Wachina walioko wanamiliki uchumi wa Malaysia, akawaambia tusipowashirikisha hawa wazawa *indigenous Malays*, watawachinja, ndiyo wakaanzisha sera za upendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa huu Mpango chini ya Mheshimiwa Mary Nagu ni mzuri, lakini ni mdogo sana kwamba, Baraza la Uwezeshaji linasaidia VICOBA, lakini tunachotaka ni kuwa na akina Mengi wengi, Watanzania wazawa wengi tuiwaingize wawe ndiyo wamiliki ili tumiliki uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya rasilimali watu. Nimeona pia maendeleo rasilimali watu katika kitabu cha maendeleo ukurasa wa 22. Nilichangia kwa maandishi wakati wa Wizara ya Viwanda na Biashara, lakini naona Waziri hakuigusia.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itekeleze ndoto nzuri ya marehemu Mwalimu Nyerere, marehemu Mwalimu Nyerere alitaka kujenga Kijiji cha Sayansi, *a Science Village* kwa kuwaweka watoto wadogo kwenye vipaji vya sayansi pamoja ili *wa-develop into greatest scientific* tuwe na akina Newton, tuwe na Albert Einstein.

Mheshimiwa Spika, sasa nikizungumza na watu wa Ikulu wanasema kwamba, Chuo cha Nelson Mandela, ndiyo kutengeneza ndoto ya marehemu Mwalimu Nyerere, hapana. Chuo cha Nelson Mandela kinatoa shahada za Uzamili na Uzamivu kama vyuo vingine vyote, hatuwezi *ku-develop great scientists* kutokana na Chuo cha Nelson Mandela.

Mheshimiwa Spika, *disbursement* ni mbaya sana pale kwa Mheshimiwa Waziri, ni kwamba fedha zinazoidhinishwa siyo tunazozipata, anahitajika aliangalie suala hili. Sasa sijui

ni kutokana na wigo mdogo wa ukusanyaji mapato, lazima tupanue wigo wa kutoza kodi. Katika kupanua wigo wa kutoza kodi, ndiyo nimezungumzia MKURABITA kwamba itasaidia.

Mheshimiwa Spika, mgodi wa Kabanga *nickel* ni mgodi wa pili duniani baada ya ule wa Canada, lakini wawekezaji wamesita kuwekeza au kuanza kuchimba kwa sababu ya matatizo mawili. Umeme ambapo wanahitaji megawati 40 pamoja na reli, hii reli ya Isaka – Kenza – Msongati - Burundi ndiyo wanaitegemea, lakini bado ipo kwenye upembuzi yakinifu. Kule Burundi ambao wana robo sisi tuna robo tatu kwa sababu ni milima hiyo hiyo, wao wameanza kuchimba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Serikali au Waziri aifikirie sana hiyo, wanahitaji megawati 40 za umeme. Ule mradi wetu wa Rusumo utatoa megawati 20 tu kwa kila nchi Burundi na Rwanda na Tanzania. Kwa hiyo hautoshi, tunahitaji msaada huo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Mwigulu Nchemba na Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu ajiandae.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza, nitoe pole kwa wale waliopatwa na tatizo Arusha na pili niwapongeze wanasiasa na wananchi wa maeneo mengine, waliokipa ushindi wa kishindo Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, awali ya yote niweke wazi kwamba, naunga mkono hoja na nimwombe tu Waziri wa Fedha aniwahishie fedha walizoniahidi kwa ajili ya kukamilisha kipande cha barabara kutoka Old Kiomboi kwenda hospitali ya Wilaya kwa kiwango cha lami kwa sababu wagonjwa na akinamama wajawazito wamekuwa wakipata shida sana.

Mheshimiwa Spika, vile vile waniwahishie fedha

walizoniahidi kwa ajili ya maji, lakini pia na kukamilisha miradi ambayo imefikia hatua za mwisho kwa ajili ya maji pale Ndango na Mingela. Pia na miji inayoendelea ambako waliniahidi Kinampanda na pamoja na Uremo pamoja na vijiji ambavyo vina shida kubwa sana ya maji.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya kazi kubwa sana. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kupitisha bajeti ili huduma za wananchi ziweze kutekelezwa na wananchi waweze kujipatia maendeleo, hilo halina mashaka.

Mheshimiwa Spika, nisemee mambo mawili ya haraka haraka ambayo ni ushauri wangu kwa Serikali. Jambo la kwanza, mabadiliko tuliyoyaleta ya kupitisha bajeti kwa wakati huu, tumelenga kusaidia maeneo ambako fedha zilikuwa zinachelewa kufika.

Mheshimiwa Spika, moja ya eneo ambalo naomba Serikali wawe wakali ni eneo la pembejeo ambazo zilikuwa zinachelewa, maeneo mengine zinafika wakati msimu ambao zilikuwa zikihitajika umeshapita. Watalaam wetu wanajua kila eneo msimu wa kilimo ni wakati gani. Kwa hiyo, sitarajii tena kuona pembejeo zinakuja Singida mwezi Februari, wakati watu wapo kwenye palizi, wakati walitegemea wapewe kwa ajili ya kupandia.

Mheshimiwa Spika, hivyo hivyo maeneo mengine sitarajii kuona pembejeo zinakwenda wakati watu walishavuka kipindi hicho ambacho walikuwa wanatarajia pembejeo. Kufanya hivyo ni hujuma na ni kuwasababishia wananchi umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine wawe makini, isitokee tena kwamba, pembejeo zinapelekwa za zao lingine katika eneo ambalo wananchi hawalimi zao hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili, tumeongeza bajeti na tumejitahidi sana kubana maeneo tofauti tofauti kwa ajili ya kuendana na vipaumbele. Niiombe sana Serikali

na hasa hasa Waziri Fedha atakapokuja aliniambie rasmi, ni lini ataleta marekebicho ya sheria ya manunuzi ya umma.

Mheshimiwa Spika, nimelisema sana hili na narudia tena na leo. Nia ya Serikali ilikuwa nzuri, lakini kuweka Sheria ya Manunuzi ya Umma kimegeuka kuwa kichaka cha watu kuiba kwa utaratibu, wanarahisisha namna ya kuiba kwa namna ambayo hawatakatwa.

Mheshimiwa Spika, najiuliza sana kwamba tunatambua kabisa kabisa bei za bidhaa, tunazitambua lakini punde inapofanyika kwa manunuzi ya Serikali bidhaa ile inakuwa na bei zaidi ya mara tatu ya bidhaa ya kawaida, hili ni kosa na ni wizi na ni unyonyaji.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri alete haraka sheria hii, lakini wakati anaandaa hiyo sheria, hili naongea kama Mbunge na naongea kama Kiongozi wa Chama, awaambie wataalam wanaosoma kwa kodi za Watanzania, hivi ni kweli kabisa kabisa wao hawajui kabisa bei wanasubiri bei zinazoletwa na wazabuni.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa yake Mheshimiwa Waziri, hawa wanaofanya hizo zabuni wamekuwa wakiifuatilia fedha kuanzia inatoka Wilayani inakwenda kwenye *RCC* Mkoani na siku inapotamkwa kwamba imepitishwa hapa, wakati nyie mnapongezana kwamba bajeti imepita na wao kule wanasema tayari wametajirika. Kwa hiyo, ili kuweza kuepuka hili namwomba Waziri alete ile sheria tuirekebishe ili tuwe tunapima ubora.

Mheshimiwa Spika, naweza nikakupa mfano tu, jengo lililojengwa la darasa kwa zabuni ni ghali kuliko jengo la Kanisa au la Msikiti na linakuwa imara lile lilojengwa na wananchi tu ambao hata hawajafuatilia hivyo viwango. Lakini hili jengo ambalo utaambiwa limejengwa kwa kufuata viwango na zabuni linakuwa ni la ovyo na la bei ya juu. Kwa hiyo, lazima sheria hii tuirekebishe ili fedha hizi tunazopitisha wananchi waweze kufaidika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tuliwahi kusema siasa ni kilimo, lakini sasa hivi siasa imebadilika ni ajira. Ukiona watu hawana adabu ni kwa sababu ya njaa, njaa haina adabu, kwa hiyo na mtu mwenye njaa hana adabu. Ukiona watu hawana utii ni njaa, njaa haina utii, kwa hiyo na mtu mwenye njaa hana utii. Sasa sehemu nyingi sana na nchi ambazo zimepata *economy social unrest* ni kwa sababu kiwango cha watu wanaokosa ajira kimekuwa kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili lazima tuliandalie mpango ambao ni mahsusi ambao utawezesha vijana wengi kupata ajira waliokwenda shule na ambao hawajakwenda shule. Eneo pekee kama nilivyopendekeza asubuhi ni kwenye viwanda. Eneo la viwanda linachanganya watu, linachukua waliosoma na wale ambao wanafanya kazi za watu wengi na hii itatusaidia sana kuweza kuweka mazingira sawa.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ambalo napenda nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ni eneo la kubana matumizi. Hili bado ni tatizo, matumizi yanapokuwa makubwa kuliko kasi ya ukuaji wa ukusanyaji wa mapato ni tatizo katika Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni lazima Serikali ibane matumizi, lakini pia inapobana matumizi ipeleke fedha ilizozitunza katika maeneo ambayo yanastahili na kwenye maeneo ambayo yanagusa maisha ya wananchi walio wengi. Maendeleo lazima yawe maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, hii napendekeza kwamba, tuna eneo lingine ambalo tunaweza tukabana fedha, lakini pia tukawasaidia vijana. Kwa mfano, niseme uwepo wa Mfuko wa Elimu ya Juu, Mfuko huu ungeweza kusaidia sana vijana, lakini sasa hivi kuna vijana wanaopoteza miaka miwili mpaka mitatu, hawana ajira na hawana fedha za kuweza kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ibane fedha vijana ambao wamekosa ajira wapelekwe shuleni. Kwa mfano, mtu ana *diploma* anapoteza miaka minne anasubiri kazi. Kijana huyo

angekuwa na fedha kwenda shule angeshaongeza elimu na angeshaongeza ujuzi wa kuweza kulitumikia zaidi Taifa katika kipindi kingine kinachofuata.

Mheshimiwa Spika, kule kwenye ofisi zetu tuweke ukomo wa watu kwenda kujifunza, mtu ameshabakiza mwaka mmoja astaaifu, anakwenda kusoma Geneva kwa fedha kubwa ambayo ingeweza kusomesha vijana watano, anakwenda kusoma ili atumike wapi? Kwa hiyo, hii nayo tuweke ukomo tufanye *saving*, tufanye vitu kwa mpango na kwa malengo.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine niliongezee, jambo la usalama wa nchi. Tena mara nyingi huwa nikiongea kwa haraka haraka, naona watu huwa hawanielewi. Niliseme kwa utaratibu; jambo la usalama, nimekuwa nikilisema na mpaka nimekuwa nikiomba kama yule Eliya alivyomwambia mtumishi wake kwamba, anamwomba Mungu amfungue macho ya Kimungu ili ajione jinsi yeye anavyoona.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikiliongelea sana suala hili. Jambo kama hili lililotokea Arusha, nimeyaongea sana mambo haya. Sasa hivi ilivyotokea, nitasema tena na wenzetu nimekuwa nikiwasema mara wanasema watakwenda Jimboni, nawashauri kwamba, wala siende tu Jimboni, wakajenge kabisa Makao Makuu ya Chama chao, lakini ukweli nitasema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni lazima tuwaze, tuvuke mipaka, kuna mambo ambayo yanawezekana kabisa yakawa yamejificha pale. Watu wanaojitoa ufahamu wanafikiria kwamba CCM inaweza ikashiriki.

Mheshimiwa Spika, niwaambieni, CCM hata bila kushiriki ni moja kwa moja inaingia tu kwenye lawama, jambo la aina hiyo likitokea. Kwa hiyo, haina *incentive* ya aina yoyote ya kushiriki kwenye jambo la aina, kwa sababu ndiyo watu wake na ndiyo ambayo inatakiwa kupitia Serikali yake

kuwahakikishia usalama. Ni lazima tuangalie maana yake wengine waliojaa ushabiki, linatokea jambo wanakwenda moja kwa moja kufikiri inawezekana CCM imeshiriki.

Mheshimiwa Spika, lakini pia lazima tuangalie mazingira ya nchi tuliyonayo sasa hivi, hivi hata tunapopata tu ugeni mkubwa mkubwa ametoka Rais wa China Taifa kubwa, anakuja na mwingine, hivi Mataifa mengine ambayo yanajua ujio wa wageni ni biashara. Maana yake Watanzania ujio wa wageni tunadhani ni siasa, kwa wenzetu ugeni mkubwa kama huo ni biashara, hivi wanapenda hiyo? Namna ya kuweza kupunguza wageni kuja hapa ni kuondoa heshima ya Tanzania, ionekane sio Taifa salama. Hivi hilo tumeliangalia, sisi tunakimbilia tu CCM. Hilo ni eneo mojawapo.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo lingine Tanzania imekuwa kisiwa cha amani, hivi wale ambao hawatutakii mema, hivi mnajua eneo ambalo wanaweza wakagusa. Moja ya eneo ni eneo la dini, wanaweza wakaangalia wapi pana mwanya. Eneo lingine ni mihemko ya siasa, watu wameshaona kwamba, wanaabudu siasa Watanzania wanaweza wakapitishia pale.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine nimefuatilia na nilisema hata mahali pengine, nimeangalia ripoti ya Jukwaa la Wahariri wakati wanafanya uchunguzi wa kutekwa kwa Bwana Kibanda, wakasema watu waliohojiwa, watu wenye heshima zao, wasio na vyama, wamedai kuwa CHADEMA kimepewa mafunzo toka nje ya nchi na kikitumia baadhi ya watumishi wa vyombo vya dola wasio waaminifu kwa kuteka watu, kuumiza na hata kuu baadhi ya watu maarufu nchini wakiwepo Waandishi wa Habari, Wanasiasa na kadhalika, watu basi wataamini kwamba CCM na Serikali yake imeshindwa kuongoza na sasa imeanza kuu watu.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kulisema hili kwamba kuna mambo mengine yanafanyika kwa hujuma na tumeziona hizo hujuma, lakini watu wengine wanawahi kuamini haraka haraka. Hii ni taarifa ya Jukwaa la Wahariri wakati wanafanya

uchunguzi, iko ukurasa wa nane namba 6.7, nitakupa hiyo taarifa. Wameandika na wale hawana chama.

Mheshimiwa Spika, lakini kitu kingine hawa wenzetu kama waliwahi kumvalisha raia jezi ya Jeshi na yule mtu alihukumiwa, hivi kila wakati, wao wanaposema Polisi, Polisi tunashindwaje kuamini kama hawakumvalisha mtu nguo za Polisi halafu akafanya yale.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu taarifa zilizopo yule kijana aliyeuawa Morogoro, hakuuawa na Polisi, ni wao wenyewe, walitoka pale wakatengeneza ile vurugu, wakamfyatulia risasi ili kutengeneza kwamba Serikali ya CCM inakandamiza Upinzani, tutashindwaje kwenye hilo na wameweka mkanda kwenye video angalieni kwenye *You Tubes* wale mnaoweza kuziona.

Mheshimiwa Spika, ukiuangalia ule mkanda utaona moja kwa moja kama una ushabiki na kama Taifa liko moyoni mwako, utaona moja kwa moja kile kitu kimepangwa, kwa nini nasema hivyo? Kwanza hata yule aliyekuwa anachukua video, eti hakushtushwa kabisa na lile bomu aliendelea tu kufuatilia kama vile ni mkanda wa harusi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, iliwahi kutokea wapi mtu anachukua *video* kwenye mkutano wa hadhara, kwenye kitu ambacho hakikupangwa, kitu kinalipuka, kinaua watu, yeye anaendelea kama vile anachukua picha za *sendoff*, ilitokea wapi hiyo, kimepangwa na kimepangwa kwa kiwango cha chini.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikiwaambia watu hawa hawana kitu wanachoshindwa kupanga cha kinyama punde unapoongelea jambo la madaraka. Hata ukiangalia wale viongozi walivyofika, eti watu wamekufa pale damu zimetapakaa Mbunge wa palepale ameshikilia boksi lenye hela kwa raha zake. Kiongozi wake yule pale yuko pale pale, alishamaliza kuhutubia amekaa kama mita 50 alikuwa anasuburi nini? Eti lilivyofyatuka ndio wakarudi, ni jambo la kupanga.



20 JUNI, 2013

Mheshimiwa Spika, lakini Watanzania wakishaambiwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Bibilia yangu inasema: "Watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa".

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kuongeza kiwango cha ushuru wa magari yenye umri wa miaka kumi na zaidi kutoka 20% mpaka 25% sababu zilizotolewa na Serikali kwamba ni kupunguza uingizwaji wa magari chakavu kulinda mazingira na kupunguza ajali.

Mheshimiwa Spika, tunayo magari yaliyochaka hapa nchini hadi yanakufa. Yanatoa moshi barabara nzima, yanaharibu mazingira, yanasababisha ajali kila leo, haya yameruhusiwa kutumika na kila siku yapo barabarani. Ni Watanzania wangapi wenye uwezo wa kununua magari mapya ya miaka miwili mpaka mitano? Gari siyo *luxury* ni kitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepunguza kodi ya mapato kwa watumishi kwa asilimia moja. Hili punguzo ni dogo sana, halijamsaidia Mwananchi kupunguza makali ya maisha aliyo nayo.

Mheshimiwa Spika, watumishi waliandamana Siku ya Wafanyakazi kumwomba Rais awasaidie kupunguza kodi hali ni ngumu, wengine wanakimbia familia zao, kila kitu

kimepanda na huduma zote zimepanda. Serikali ipunguze angalau kwa asilimia tatu - tano ili ilete nafuu kwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeondoa kodi (*road licence*) kwa vyombo vya moto vya pikipiki na bajaji. Sababu zinazotolewa kwamba ni kuongeza ajira kwa vijana, zinaonesha ni kwa jinsi gani Serikali imeshindwa kubuni mipango makini na mikakati ya kuwapatia vijana walio wengi ajira.

Mheshimiwa Spika, kodi iliyoondolewa kwenye vyombo hivi inakwenda kuwanufaisha watu binafsi, matajiri, wenye uwezo na ni wafanyabiashara na siyo hao vijana ambao ni vibarua tu wanalipwa ujira wao ule ule.

Mheshimiwa Spika, pikipiki na bajaji zinamaliza maisha ya watu kila siku. Hospitalini majeruhi wamejaa, walemavu wameongezeka na wategemezi wameongezeka.

Mheshimiwa Spika, Serikali imenyamaza kimya kuhusu maisha ya Watanzania yanayokatizwa kwa vyombo hivi vya moto. Hakuna hatua zozote zinazochukuliwa kukabiliana na hali hiyo kama vile wale vijana wanaoteketea kwa pikipiki ni wanyama. Kitendo cha Serikali kueleza inatafutia ajira vijana ambazo zinawamaliza ni kupunguza idadi ya vijana kwa njia hii.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali irudishe kodi kwenye vyombo hivi, kodi hiyo iwekwe kwenye mifuko maalum ya kuwezesha vijana kufungua miradi mikubwa; kwa mfano, kilimo kule Igunga ambapo vijana wengi watajajiri lakini pia hawatateketea kwa ajali barabarani.

Mheshimiwa Spika, hivi ni vyanzo vya mapato makubwa sana, tusitumie siasa kuikosesha Serikali mapato. Hili limefanyika kisiasa baada ya kuona vijana wengi wako mitaani na wameichukia Serikali yao kwa kushindwa kubaini mikakati ya kuwapatia ajira. Tuache siasa kwenye masuala ya msingi.

Mheshimiwa Spika, vipaumbele ni vipi hatuwezi kuvitekeleza kwa ufanisi na kwa viwango vinavyopimika. Tuamue tuchague vipaumbele vitatu tu tuwekeze kwa nguvu zote ndani ya mwaka mmoja. Tujipime, tutathmini, tuendeleo, mwaka mwingine tuhame. Fedha zetu ndani ambazo ndizo za uhakika hatuwezi kugawa kidogo kidogo *then* tukapata matunda mazuri.

Mheshimiwa Spika, bei ya vyakula hapa nchini zimekuwa zinapanda sana muda mfupi tu baada ya mavuno na kusababisha bei kwenye masoko yote kuwa juu. Tatizo kubwa ni wafanyabiashara wa vyakula kununua vyakula vyote kutoka kwa wakulima kwa bei chee na kutunza *store* tani kwa tani wanasubiri kupandisha bei wanayoitaka wao kwa muda wao huku Wananchi wanateseka kwa kukosa vyakula.

Mheshimiwa Spika, hili ndilo lililosababisha Serikali kutoa vibali vya kuagiza mchele nje ya nchi. Ulipoingia tu, wafanyabiashara wakaanza kulalamika kwa kuwa walikuwa na *stock* kubwa ya mchele kwenye *store* zao.

Mheshimiwa Spika, ni lazima Serikali iweke utaratibu wa kudhibiti bei za vyakula kwa wafanyabiashara na siyo kuacha wajipangie; wanataka *super profit* na wanaumiza Wananchi.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, ili kuinua uchumi wa nchi ni lazima tuhakikishe tunaimarisha muindombinu ya reli, umeme, elimu, afya na maji na kuboresha kilimo katika kukuza masoko ya mazao.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Serikali inapaswa kuliangalia ili kuweka usimamizi wa karibu ni kusogeza utawala karibu na Wananchi.

Mheshimiwa Spika, vigezo vya kusogza utawala kwa Wananchi vinajulikana; idadi ya watu, ukubwa wa eneo, sifa za shughuli za kiuchumi, eneo lilivyo kijiografia na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, inashangaza sana maeneo yenye

sifa kama hizo hayajafikiriwa kugawiwa aidha Wilaya, Tarafa, Kata au Vijiji. Cha kushangaza, baadhi ya maeneo yanapata Wilaya au Majimbo kwa upendeleo na maeneo mengine kuachwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ifikirie kuigawa Wilaya ya Sumbawanga kuwa Wilaya mbili; Wilaya ya Ukanda wa Ziwa Rukwa (Mtowisa).

Mheshimiwa Spika, kuhusu ziara za Viongozi kuwachagulia sehemu nzuri ya kwenda na kuacha kuwapeleka sehemu ambayo Wananchi wana shida, hawana barabara nzuri, ndiko Viongozi wapelekwe.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia Bajeti za Halmashauri kutohaminiwa.

Mheshimiwa Spika, Madiwani wanakaa na kukokotoa bajeti toka ngazi ya Kijiji, Kata hadi Wilaya. Cha kushangaza, bajeti hizo baada ya kupitishwa na Baraza la Madiwani, Serikali inakuja kuipangua kwa kuishusha chini. Je, hiyo ni haki; ni vigezo vipi Serikali inatumia?

Mheshimiwa Spika, njia mojawapo ya kukuza kilimo ni bei nzuri ya mazao.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali imesimama kutoa fedha kwa Miradi ya Umwagiliaji ambayo tayari ilikwisha kuanza utekelezaji? Naomba Mradi wa Sakalilo, Mradi wa Ng'ongo na Mradi wa Maleza ipewe fedha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja na naipongeza Serikali kwa kuwa sikivu kwa maoni ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naupongeza Uongozi wa Bunge, kwa kuanzisha Kamati ya Bajeti na napendekeza ifanye kazi muda wote ili iendeleo kuishauri Serikali kwa mwaka mzima,

kuhakikisha malengo yanafikiwa na kurekebisha pale ambapo wanaona panatetereka.

Mheshimiwa Spika, napongeza kuongeza shilingi bilioni mbili za maendeleo ya akina mama; ni hatua nzuri lakini fedha hizo ni kidogo sana kulingana na idadi ya wanawake. Serikali kupitia Halmashauri inatenga fedha asilimia tano, lakini hakuna Halmashauri inayotenga asilimia hiyo. Iwapo watapatiwa fedha hizo, akina mama wangeweza kuinua vipato vyao na kupitia uwezo wao kuchangia Pato la Taifa moja kwa moja au kupitia ununuzi wa bidhaa.

Mheshimiwa Spika, mimi bado nasema kuna mapato mengi ambayo hayakusanywi. Hili nilianza kulisema toka mwaka jana, kwenye Bajeti ya Wizara ya Fedha, nimelisema mwaka huu lakini bado. Kodi ya Majengo (*Property Tax*), Serikali bado haijaweza kukusanya kodi hii na kwa kweli kama hatukubadili mfumo wa sasa, hatuwezi kukusanya.

Mheshimiwa Spika, eneo hili inaonekana Serikali kulidharau, lakini ni eneo ambalo Serikali ingeweza kuongeza mapato makubwa sana. Naendelea kushauri eneo hili lifanyiwe kazi sawasawa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeondoa leseni za barabara kwa bodaboda na bajaji. Nadhani Mheshimiwa Waziri hakushauriwa vizuri. Hizi Bodaboda na bajaji nyingi vijana ni madereva, wapo wachache ni zao, lakini idadi kubwa siyo zao.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa Serikali kuongeza bei ya mafuta, *petrol* na *diesel* ni kuzidi kumkandamiza huyu dereva wa bodaboda na bajaji. Ili kumsaidia kijana awe mmiliki au dereva wa bajaji ni kumtolea gharama za leseni. Leseni ya barabara inalipwa na mmiliki wa bodaboda na siyo dereva. Hesabu ya mwajiri anapotakiwa dereva apeleke haipungui bali inaongezeka kwa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kutenga kiasi cha bilioni 28 kwa Barabara za Dar es Salaam. Hii ni hatua

nzuri, lakini ukichukua uharibifu wa Barabara za Dar es Salaam kutokana na ongezeko la barabara za ndani kwa sababu ya matengenezo ya Barabara Kuu zinazotoka mikoani, barabara hizi hazikutengenezwa kubeba uzito mkubwa; matokeo yake Halmashauri inaingia gharama kubwa sana kuliko ongezeko la hizo za fedha.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya nishati na usafirishaji ni muhimu sana kwa maendeleo na uzalishaji wa nchi. Kwa nini Serikali isitafute fedha mahususi kwa ajili ya eneo hili? Serikali ina gesi nyingi; kwa nini isikope ili kuimarisha miundombinu kikamilifu? Ninafahamu kwa mtindo huu wa kukopa mauzo ya gesi tunaweza kupata bei ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwanza, bei inajulikana, ni heri kuuza kiasi kidogo cha gesi yetu na kutumia mapato hayo kufungua mapato mengine. Ile tofauti ya bei itafidiwa na mapato ya ziada ambayo vinginevyo yangebidi kusubiri muda mrefu kupatikana. Hii itasaidia siyo tu kuongeza mapato ya nchi bali na ya watu binafsi. Ninaomba Serikali ilichukue hili na kulifanyia kazi.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, je ni lini Wilaya ya Ludewa itapata umeme wa *REA* kwani hivi sasa Wilaya ya Ludewa ina umeme vijijini katika vijiji vichache sana kama vile Ludewa, Luana na Mawengi, lakini maeneo mengi sana yakiwemo kata za Madope, Madilu, Lupingu, Manda, Lwela na Luilo hakuna kabisa umeme? Kati ya Kata 25 za Ludewa ni Kata tano tu zenye umeme wa uhakika, Kata zingine zote hazina umeme.

Mheshimiwa Spika, suala la maji katika Wilaya ya Ludewa bado ni changamoto kubwa sana. Mashule hayana maji ya uhakika, vijiji havina maji ya uhakika kama Kijiji cha Ilininda, eneo la Mwambao, Nkoningombe, Milo, Amani na Mundindi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua Serikali ina

mpango gani juu ya upungufu wa maji? Kwa kuwa kuna nchi zingine ambazo wametaka Makampuni ya Simu ya *float shares* kwenye *Stock Exchange Market*; je, ni lini Tanzania Makampuni ya *Voda*, *Tigo*, *Zantel* na *Celtel* yanauza *shares* zao kwa wananchi?

Mheshimiwa Spika, eneo la Kusini mwa Tanzania barabara bado sana. Hatujaweza kuunganisha Wilaya na Wilaya kwa kiwango cha lami. Eneo la Njombe – Ludewa, Njombe – Makete, Ludewa – Lupingu, Tunduma – Rukwa, Ludewa – Makete, maeneo haya yote ni barabara za vumbi, tunaomba sana suala la barabara liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, barabara itaongeza uchumi na kupunguza gharama za usafiri hasa uuzaji wa mazao eneo la Ludewa (mahindi). Kutokana na barabara, wafanyabiashara wanaishia Njombe hawaendi Makete na Ludewa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme vijijini; nashauri utaratibu uwe *transparent*. Maeneo ya Ludewa kati ya Kata 25, zenye umeme ni takribani Kata tano tu. Ludewa ina Kata 22, zenye umeme ni Kata nne tu, yaani umeme vijijini ni chini ya asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi sana zina Muungano; mfano, India, USA States zote Rais mmoja, United Kingdom *Queen* na kadhalika. Matatizo ya Muungano hayaondoshwi na kuongeza Serikali. Naomba suala la kero za Muungano, *formula* ya mgao iangaliwe vyema sana maana hata tukisema Serikali nne bado kutakuwa na kero. Hivyo, *solution* ni kuondoa kero za Muungano na siyo kuongeza wingi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mikoa mipya; tumeongeza Bajeti ya Mikoa mipya ikiwemo Njombe na Wilaya ya Wanging'ombe, naomba fedha ziende tufanye kazi. Nafasi nyingi za Makatibu Wakuu na Wakurugenzi zinakaimiwa, naomba wateuliwe waapishwe wafanye kazi.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa kuondoa kodi ya bajaji, naomba vijana sasa wapewe elimu wasipate ajali za pikipiki. Vijana wa Mlangali, Madope, Iwawa, Lugarawa na Njombe wafanye kazi za ujasiriamali vyema.

Mheshimiwa Spika, wanawake wapewe mikopo ya riba ndogo, wawezeshwe hata *TIB* fedha za kilimo.

Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Kibena Njombe kwa sasa itumike kama Hospitali ya Mkoa; hivyo, naomba ipelekewe madawa.

Mheshimiwa Spika, Bajeti naomba iweke malengo, *three feet programme*. Tujue baada ya Bajeti hii Idara ya Elimu tunahitaji ku-*achieve* nini. *Quality Education*.

Mheshimiwa Spika, huduma za Afya lazima ziwe bora sana, madawa, vitendea kazi, *x-ray* na kadhalika. Sasa Bajeti hii lazima iwe na *Enforcement Mechanism*. Suala siyo tu kutoa fedha; je, zimefika zinakwenda kwa wakati, zimefanya tunachokusudia? *We need to trace every cent provided for the projects* na mambo mengine pia.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupeleka hela kwenye Miradi, ushauri wangu ni kuwa hela itoke Hazina iende moja kwa moja kwenye Miradi. Mfano, fedha za maendeleo za Mikoa mipya zitoke Hazina ziende Njombe na siyo Tawala za Mikoa kisha *RAS* Njombe. Ushauri huu unapendekeza kupunguza mlolongo wa maeneo ya kupitisha fedha; na kupunguza *bank charges* na *interest*.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, nashauri Kamati ya Bajeti ipewe fursa ya kuwasiliana na Mabunge ya Nchi Washiriki wa Maendeleo (Wahisani) ili kubaini sababu zinazopelekea nchi hizo kuchelewa ama kutotimiza ahadi ya misaada na mikopo wanayoitoa baada ya kusaini mikataba na nchi yetu. Kwa hatua hii, Kamati ya Bajeti itasaidia Serikali kwa kusukuma upatikanaji wa fedha za nje shilingi 3,855.2 bilioni.



Mheshimiwa Spika, aidha, watendaji wabanwe kutayarisha taarifa za Miradi inayofadhiliwa na Washiriki wa Maendeleo, taarifa za hatua kwa hatua za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kila kipindi cha robo mwaka. Tumesikia kwamba, mara kadhaa wahisani wamekuwa wakisuasua kutoa fedha kutokana na kutopelekewa taarifa ya utekelezaji wa miradi wanayofadhili kwa wakati. Tabia hii ya kuchelewesha taarifa imekithiri mpaka kwa fedha za ndani na haishangazi kuona hata Serikali za vijiji hazisomi taarifa za mapato na matumizi!

Mheshimiwa Spika, nashauri vipaumbele sita vya Kitaifa vifanyiwe marekebisho na ikiwezekana tujikite kwenye vipaumbele vitatu tu vya miundombinu, kilimo na viwanda. Miaka ya 1950 Serikali ya Sweden ilijiwekea vipaumbele vitatu tu vya elimu, kudhibiti idadi ya watu wake (*Population Control*) na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, walijipanga vizuri katika mazingira yao na miaka 20 baada (miaka ya 70), Sweden walipaa kiuchumi na kuwa kati ya nchi za Scandinavia zilikopesha nchi za dunia ya tatu Tanzania ikiwemo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Watumishi wa Serikali walipwe mishahara inayolingana na gharama halisi za maisha sokoni ili kupunguza wizi na ubadhirifu wa fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ifungue fursa za uchumi *Corridor* ya Singida – Chunya – Mbeya. Eneo hili lina utajiri mkubwa kwa Taifa. Miundombinu ya umeme na barabara ya lami ijengwe ili ku-*harness resources* za eneo hilo pana lenye utajiri wa rasilimali za misitu, wanyamapori na madini.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ielekeze mwekezaji wa kiwanda cha saruji eneo la Itigi (Manyoni) ambako kuna madini mengi ya *gypsum* na miundombinu ya reli, barabara na umeme.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, kodi zitozwe kwenye ng'ombe (wafugaji kwa ng'ombe), TV na majumba ya kupangisha yatozwe kodi kulingana na sehemu yalipo. Vilevile wauza mitumba wote watozwe kodi na wafugaji wa kuku, nguruwe, ng'ombe wa maziwa na samaki na kwa machangudoa nao watozwe kodi.

Kama Serikali Kuu haiwezi kukusanya kodi ya ng'ombe, tuzipe uwezo Halmashauri zetu zikusanye ili ziongeze mapato kama zamani, maana Halmashauri inachukua ushuru wa mazao asilimia tatu - tano kwa vipi ng'ombe wanaachwa? Hii inatokana na baadhi ya Wabunge kuwa na mifugo ya ng'ombe, tunapoteza pesa bila sababu, rudisha ushuru wa ng'ombe mara moja kuokoa Halmashauri zetu.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, tozo za kodi za chumvi kuwa nyingi na pia kukosa soko la chumvi; Tanzania kuna maendeleo ya wakulima, chumvi (Pwani, Tanga, Zanzibar, Bagamoyo, Shinyanga, Singida, Mbeya, Dar es Salaam, Dodoma, Mtwara na Lindi). Wakulima hawa wana matatizo makubwa sana yafuatayo:-

(i) Mheshimiwa Spika, chumvi hutozwa kodi nyingi kwa Wizara tano.

(ii) Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya (*UNICEF*) huwaamuru wakulima wa chumvi kununua madini ya *iodine* (madini joto) kutia ndani ya chumvi ili binadamu aweze kuipata mwillini mwake baada ya kubaini kuwa miili mingi ya Watanzania haina madini joto.

Kilo moja ya madini joto ni shilingi laki moja; ambayo hutiwa ndani ya pakiti 320. Kwa nini madini joto yasitolewe bure kuwapa wakulima wa chumvi maana Serikali ndiyo ilitaka watu wale madini joto kupitia chumvi; sasa mzigo wote wa kulisha madini joto katika miili ya watu humkuta mkulima wa chumvi?

(iii) Wizara ya Ardhi wanadai pesa za usajili wa shamba kila mwaka shilingi laki mbili ambapo Sheria haisemi hivyo.

(iv) Wizara ya TAMISEMI humdai mkulima wa chumvi ushuru wa Halmashauri kila kilo 50 alipe shilingi 50 (asilimia tatu ya mauzo ya chumvi) mrabaha ni ghali sana.

(v) Wizara ya Maliasili inamtoza mkulima wa chumvi shilingi 80,000 kila hekta mbili na nusu kwa mwaka kwa ajili ya msitu wa mikoko iliyokatwa; *why?*

(vi) Wizara ya Madini; mkulima wa chumvi anatakiwa kulipa shilingi 50,000 kila mwaka kwa Wizara kwa ajili ya ardhi za upana wa 100 kwa 500.

Hizo ni Wizara zipatazo tano ambazo mkulima wa chumvi anatakiwa apitie na kulipia ushuru (tozo mbalimbali).

Mheshimiwa Spika, chumvi yenyewe haina bei, tangu wakati wa uhuru hadi leo bei ni hiyo hiyo ya shilingi 1,500 kwa kiloba cha kilo 50. Huu ni uonevu mkubwa sana. Hawana, vitu vimepanda bei sana, lakini pia chumvi hizi hazina soko. Kiwanda cha Mgololo ambaye alikuwa ananunua chumvi, siku hizi hanunui Tanzania, ananunua nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, wazalishaji wa chumvi wanaomba mambo haya yafanywe:-

(i) Watafutiwe soko ili chumvi inunuliwe.

(ii) Serikali itoe ruzuku ya madini joto kwa wakulima wa chumvi kwani chumvi sasa ni dawa na siyo biashara, kwani Serikali hupitishia madini joto ili wale binadamu wa Tanzania.

(iii) Ushuru wa mikoko wa shilingi 80,000 wa kila mwaka kwa hekta mbili na nusu tunaomba walipe mara moja kwa mwaka na siyo kila mwaka maana mikoko hiyo imekatwa mara moja tu na haioti tena.

(iv) Serikali ituambie chumvi ipo katika Wizara ngapi? Wananchi wanasumbuka katika Wizara tano kulipia ushuru, kwa nini wasiweke katika eneo moja la madini kwa kulipia hizo kodi kadhaa?

(v) Chumvi isitafsiriwe kama madini kwa thamani kama dhahabu au almasi. Wakulima hawa ni maskini. Chumvi ni chakula sio dhahabu. Tunaomba Mheshimiwa Waziri uje Lindi uone wakulima wa chumvi wanavyopata tabu.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika kodi nyingi katika nyumba za kulala wageni (*Guest House*), tunaomba tusaidiwe, wamiliki wanalalamika kutozwa kodi nyingi. Kuna kodi ya mapato asilimia mia moja ya mwaka; kuna kodi ya *TRA* asilimia kumi kwa mwaka na kuna kodi ya *Hostel Levy* asilimia ishirini kwa mwezi bila kujali shughuli za msingi anazofanya mwenye *guest* kama malipo ya wahudumu, ununuzi wa shuka, sabuni, umeme na maji ya *guest*.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali ichunguze upya Sheria ya *BARA (Business Activities Registration Act)*, kuona maboresho ya Sheria hiyo na upanuzi wa wigo wa biashara katika ngazi za Wilaya, Halmashauri za Wilaya, Majiji na Mkoa. Tunaomba *Hostel Levy* ipunguzwe, kodi nyingi.

Mheshimiwa Spika, kodi zinazotowza kwa ajili ya nyumba za makazi zifutwe, hazina tija yoyote. Nyumba za makazi siyo sahihi kutozwa kodi, watoze nyumba za biashara tena katika Mji kama Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na kadhalika. Miji maskini iachwe watu hawana pesa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nashukuru sana.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwa vile "*PAYE*" ni suala la Muungano na kodi hiyo inachangiwa na Wafanyakazi wote na Muungano waliopo Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, hayo ni makato ya kodi ya mapato ya mishahara yao. Suala hilo lipo katika Ofisi yako katika mchakato wa kuamua fedha zipi ziende Tanzania Visiwani (Zanzibar) na zipi zibakie Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, je, mchakato wa uchambuzi huo utamalizika lini ili watoe idadi sahihi ya fedha hizo baina ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani? Je, tutegemee katika mwaka huu wa fedha wa 2013/2014 suala hilo litakuwa limemalizika kabisa na mgao huo kuwa sahihi?

Mheshimiwa Spika, ingawa kwa taarifa zilizopo, fedha hizo sasa kwa makisio yasiyo sahihi zinapelekwa Zanzibar. Je, ukweli sahihi ukoje?

Mheshimiwa Spika, ninaomba Wizara yako itoe jibu sahihi ili kuondosha kelele na mvutano uliopo hivi sasa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi huko Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. ATHUMAN R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kodi ya majengo (*Property Tax*) ni chanzo muhimu cha mapato. Taarifa za Kamati ya TAMISEMI; mimi ni Mjumbe, ni kwamba, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya kukusanya kodi za majengo zinaandaliwa. Kuchelewa kwake ni kucheleweshwa mapato ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Hivyo, kucheleweshwa miradi ya maendeleo kutekelezwa. Uthamini wa majengo bado; hivyo, Serikali hajaanza kutoza kodi.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ianze kutumia wathamini waliopo na kuajiri wengine ili wakisie kodi za majengo mara moja na kukusanya kodi hiyo na kutoa risiti kwa malipo hayo. Baada ya utaratibu wa makisio halisi kujulikana na kodi kufanyiwa ukokotoaji, nyongeza ya kodi ilipwe na kama kodi imelipwa zaidi mmiliki arejeshewe ziada (*refund*). Hii inafanyika Marekani, nasi Tanzania tunaweza. Tujipange na tuongeze mapato ya Serikali kwa kutoa kodi za majengo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara zetu kwa kutumia fedha za ndani unaleta riba kubwa kila

tunapochelewa kulipa wakandarasi baada ya siku 56. Tunaweza kuepuka riba kubwa kwa kutumia ukwasi wa fedha za ndani zilizoko Benki Kuu ili kuhimili na kudhibiti mfumko wa bei (*Mopping Excess Liquidity*) na kumpata mkandarasi au wakandarasi wa nje na kuwalipa fedha kwa sharti kuwa watazitemia nje ya nchi bila kuathiri akiba ya Taifa (*reserves*) kama itaruhusu.

Mheshimiwa Spika, kipaumbele kwenye uchumi cha sayansi na teknolojia hakina mjadala wala mbadala. TEHAMA na Mkongo wa Taifa ni lazima viendane na maandalizi ya kuwa na wataalam wengi nchini, wenye weledi wa sayansi, teknolojia na hisabati.

Mheshimiwa Spika, maandalizi yako katika uwekezaji tangu shule za msingi, sekondari na vyo vikiu. Tujipange na tuwekeze ili tuwe na uchumi utakaokua haraka; tujifunze kutoka Malaysia na Singapore ambao sasa wana *Knowledge Economies*.

*E-Medicine, E-Commerce, E-Government, E-Business Processing*, yote yanawezekana, tunao Mkongo wa Taifa. Jamaica wana *E-Business Processing* wakitumia Mkongo kutoka Florida na New York; hivyo, vijana wanapata ajira za *ICT* kutoka Marekani.

Mheshimiwa Spika, tujifunze pia kutoka Silicon Valley, California na Wizara za Fedha na Uchumi, Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na Ardhi, Nyumba na Makazi zipate eneo haraka Kigamboni kwa kuanzisha *ICT – Industrial Park* na *E-Business Processing* kwa kuingia mikataba na Makampuni mbalimbali ya USA, Canada, Europe, China, Malaysia na Singapore.

**MHE. ABDULSALAAM S. AMER:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa pongezi kwako wewe kwa kuunda Kamati ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya mwaka huu wa 2013/2014 imegusa maeneo mengi sana ya kijamii. Pamoja na kauli ya muda mrefu ya Serikali kasungura kadogo, imesababisha kuongeza juhudi na mikakati maalum ya kuongeza kipato.

Mheshimiwa Spika, napenda niongelee maeneo mawili ambayo nahisi yanaweza kuongeza kipato kwa nchi yetu. Kwanza, kwenye madini. Eneo hili litazamwe kwa macho mawili; kuna makampuni mengi ya mfukoni au yaliyosajiliwa lakini hawana rekodi yoyote ya uzalishaji wanayofanya katika kutoa hesabu halisi ya uzalishaji katika madini. Naomba liangaliwe kwa upande wa uzalishaji wa shaba.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni uvuvi. Eneo hili Serikali naona bado hawajatilia mkazo katika kukusanya kodi yake. Baadhi ya nchi duniani wanategemea sana uvuvi ili kuongeza kipato cha kuendesha nchi. Kuna Bahari ya Hindi, Ziwa Nyasa, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika; Mwenyezi Mungu katubariki katika neema ya Dunia lakini hatuitumii. Naomba Serikali iangalie kwa macho mawili.

Mheshimiwa Spika, naomba suala la riba katika Benki zetu; Benki zetu zinatoza riba kubwa sana, kwa mfano, Benki ya *TIB* inatoza riba ya asilimia 17 katika mkopo wa biashara. Sasa Benki ya Serikali inatoza asilimia 17; je, hizo za binafsi zitaweza kupunguza? Leo Taasisi za Fedha zinazojifanya kuwasaidia wajasiriamali wetu wadogo wanatoza riba mpaka asilimia 27; kuna msaada hapo au kuzidi kuwakandamiza?

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ni kuziba mianya ya rushwa kwa jumla katika sehemu zote ambazo kuna dalili hiyo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza kwa mfumo mpya wa kujadili bajeti, ni utaratibu wenye tija.

Naipongeza Serikali kwa kukubali michango ya Wabunge iliyopelekea kuongezeka kwa mafungu katika maeneo yenye shida kama maji. Sekta ya Maji ina matatizo nchi nzima hasa jimboni kwangu.

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Maji la Kawa limejengwa kwa fedha ya Serikali kwenye shamba la mtu binafsi na Wabunge tumelisemea sana suala hili kuwa zaidi ya shilingi bilioni 1.2 zimetumika, hakuna Mwananchi hata mmoja anayepata huduma hiyo ya maji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati akifunga bajeti ya mwaka jana alieleza kuwa, vijiji vinavyozunguka Bwawa hilo vya Fyengelezya, Nkundi na Kalundi, watapata maji mpaka leo hakuna kinachoendelea; kuna nini?

Kama hakuna hatua zozote katika bajeti hii, naahidi kuchukua hatua ya kuja na hoja binafsi kuona uhalali wa Serikali kutopeleka maji kwenye vijiji nilivyovitaja hapo juu, ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu alivitaja wakati akiahirisha Bunge la Bajeti la mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Nkasi Kusini kuna Mabonde ya Umwagiliaji ya Namanji na Kate; hakuna kinachoendelea licha ya fedha kuonekana kutengwa karibu kila mwaka; kulikoni?

Nkasi Kusini kuna shida ya barabara zinazoenda Mwambao mwa Ziwa Tanganyika. Mara kadhaa tumeomba zipandishwe hadhi ili zihudumiwe na *TANROAD*, tukijua Halmashauri haiwezi kuzimudu kabisa.

Mheshimiwa Spika, vikao vyote vimependekeza hilo ikiwemo Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Rukwa (*RCC*) na kutembelewa na Kamati ya Kitaifa ambayo iliafiki lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea.



Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Wampembe iliyoko kandokando mwa Ziwa Tanganyika, Kata za Ninde, Kala na Wampembe haitembelewi na Viongozi wa Kitaifa kabisa na Wananchi wanahoji na wanasema ni kwa vile barabara zao hazifai. Naomba liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *PPP* ishawishi wawekezaji wanaoweza kuwekeza katika maeneo ya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo ili tufanikiwe. Umeme mkubwa unahitajika Mkoani Rukwa ili kushamiri kwa viwanda vikubwa. Tunaomba tuunganishwe na Gridi ya Taifa inayotokea Nyakanazi – Kigoma – Mpanda – Rukwa – Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa hakuna matrekta licha ya sera na utaratibu mzuri uliowekwa na Serikali. Mwaka jana tulifanikiwa kupata matrekta sita tu wakati majirani zetu Mpanda walipata matrekta 37, Ruvuma zaidi ya matrekta 100.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Rukwa hatukupata? Ni uzito wa Viongozi Waandamizi wa Rukwa. Rukwa ni Mkoa wa kimkakati katika kilimo. Kama Taifa, lazima kuona ni Viongozi gani unawapeleka Rukwa. Tusiwe wanasiasa kupita kiasi, tutaangusha nchi.

Mheshimiwa Spika, mifugo katika nchi hii ni mingi sana na uharibifu wa mazingira ambao kwa sasa ni tishio kwa nchi yetu na mchango wa mifugo kwenye uharibifu wa mazingira ni zaidi ya asilimia 40.

Mheshimiwa Spika, naomba ushuru wa mifugo urudishwe. Ng'ombe, mbuzi, kondoo na punda vyote vitolewe ushuru; vinginevyo, ninyi wasuasujaji mmewekeza katika eneo hili maana tunaweza tukasema jambo kumbe wakubwa ndiyo wenye miradi.

Mheshimiwa Spika, rudisha ushuru wa mifugo tafadhali tupate fedha ya kusaidia Wananchi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali yangu ya CCM, kwa kuwa sikivu na kuongeza au kufanya marekebisho ya bajeti ya maendeleo kwenye fungu 62 na Mafungu mengine ya Wizara ya Maji, Mfuko wa Mahakama, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Nianze na Mradi wa Reli wa Mtwara – Mbamba Bay – Mchuchuma. Mradi huu umetengewa jumla ya shilingi bilioni 5.58 kwa ajili ya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu ni muhimu sana kwa ustawi wa *Mtwara Corridor* na kumekuwa na lugha za mazoea humu ndani ya Bunge ya upembuzi yakinifu unaendelea, mchakato uko mbioni, taratibu zinaendelea; katika majumuisho ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ningeomba kupata jibu, upembuzi yakinifu huu utaanza lini, utaisha lini na ujenzi wa reli hii utaanza lini?

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa inayofanya ya kuimarisha mtandao wa barabara. Ninafahamu utengenezaji wa barabara ni gharama sana na unachukua pesa nyingi, lakini nilitaka kuishauri Serikali kwamba, katika maeneo ambayo barabara zake ni za udongo, ingebadilisha mfumo wa matengenezo ya barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, ni vyema kutengeneza barabara hizo sasa kwa kiwango cha changarawe zaidi badala ya kuchonga tu. Kwa mfano, kama kuna eneo ambalo linahitaji kuchongwa likawekewa changarawe kabisa, nina uhakika sehemu hiyo itaimarika vizuri zaidi. Nimeona maeneo mengi ambayo yametengenezwa kwa kiwango cha changarawe, uharibifu wakati wa masika umekuwa siyo mkubwa sana ukilinganisha na maeneo yanayochongwa tu.

Mheshimiwa Spika, ni bora kutengeneza kilometa 80 badala ya kilometa 100 kwa kiwango cha changarawe kuliko kutengeneza kilometa 100 nyingi zake zikiwa zimekwanguuliwa. Kwa utaratibu huu, naona barabara zitaweza kuimarika zaidi na kupunguza matumizi makubwa yanayofanywa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, katikati ya mpaka wa Wilaya ya Liwale na Nachingwea kuna Mto Mbwemkuru. Mto huu ni mkubwa na daraja lake ni refu sana; daraja hili limejengwa miaka ya zamani sana hata kabla sijazaliwa.

Mheshimiwa Spika, daraja hili kuna kipande kimeanza kubomoka na kwa ujumla linahitaji ama ukarabati mkubwa au kujengwa upya. Ninaiomba Serikali ilichukulie suala hili kwa uzito mkubwa na kulifanyia kazi, daraja hili limekaa vibaya na wakati wowote, siku yoyote, linaweza kuleta shida.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa naomba kuishukuru Serikali na hasa Mheshimiwa Rais, kwa jitihada alizozifanya za kuhakikisha kwamba, Liwale wanapata umeme wa uhakika. Pamoja na mafanikio haya, bado kuna umuhimu wa Wilaya ya Liwale kuunganishwa kwenye umeme unaotokana na *gas*.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa *REA* wa kusambaza umeme, kwa mwaka huu 2013/2014, nimeona kwamba, Liwale tutaanza kujengewa *transmission line* kutoka Ruangwa hadi Liwale na kwa utaratibu huu, vijiji vingi vilivyoko kandokando ya Barabara ya Nachingwea hadi Liwale vitafaidika na Mradi huu.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni jema sana, licha ya kwamba, Wananchi wengi watafaidika na Mradi huu, hata Serikali yenyewe kwa kiwango kikubwa itapunguza gharama kubwa zinazotumika hivi sasa kwa ajili ya kuendesha *generators* zilizoko sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekta ya Viwanda, ninaomba niongelee viwanda vya kubangua korosho

vilivyoko Mkoa wa Mtwara, Lindi na Mkoa wa Pwani. Viwanda vya kubangua korosho vilivyoko katika mikoa hiyo niliyoitaja, hata vikifufuliwa leo havitaweza kuendana na mahitaji ya sasa ya kubangua korosho.

Mheshimiwa Spika, Viwanda hivi ni chakavu mno na vilitengenezwa kwa teknolojia ya zamani ambayo kwa sasa haviwezi kukidhi mahitaji ya ubanguaji wa korosho hizo ndani ya mikoa hiyo. Tunasikia katika vyombo vya habari kwamba, Mtwara kuna viwanda takribani sita vya kubangua korosho, vitakwenda kuwekeza Mtwara katika sekta hii ya kubangua Korosho.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, katika mgawanyo tu wa rasilimali na sisi Mkoa wa Lindi tunahitaji pia wawekezaji hao wa viwanda vya kubangua korosho angalau na sisi Mkoa wa Lindi tupatiwe hata wawekezaji. Liwale sasa hivi kuna umeme wa uhakika, tunawakaribisha na sisi kwetu waje kuwekeza katika sekta hii ya viwanda vya kubangua korosho.

Mheshimiwa Spika, Television ya Taifa *TBC* na *Radio Tanzania* ni vyombo ambavyo Watanzania wengi huko vijijini wanavitegemea sana. *TBC*, *Television* na *Radio Tanzania* kwa sasa imekuwa ni kero kubwa huko vijijini, matangazo hayafiki sawasawa.

Mheshimiwa Spika, malalamiko kuhusu *TBC* na *Radio Tanzania* huko mikoani ni mengi sana. Wilaya ya Liwale, *TBC* na *Radio Tanzania* havipatikani tena. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, *TCRA* na vyombo vingine vilivyoko chini yake, viimarisha vitengo hivi, sisi huko mkoani *TBC* na *Radio Tanzania* ndiyo mkombozi wetu. Wizara imetengewa pesa za kutosha na misaada mbalimbali pamoja na mikakati mbalimbali tumeisikia, tafadhali imarisheni vitengo hivi kwa manufaa ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika,

nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pamoja na kuwa nimeshachangia, lakini kuna masuala mawili ninataka kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kupanda kwa ushuru wa ngano kutoka asilimia sifuri mpaka asilimia kumi. Pamoja na kupanda huku, umetumika katika ushuru wa bidhaa za E.A. lakini kama sisi Tanzania ni zito tunaweza kupunguza.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunalalamika kuwa unga wa ngano ni bei kubwa, lakini Serikali imeamua kuwa ngano ilipe asilimia kumi badala ya asilimia sifuri ili bei ya unga wa ngano izidi kupanda.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maisha ni magumu, naomba suala la chakula lisamehewe mambo yote, mwananchi anaweza kukosa na akaishi lakini chakula hawezi kukosa. Naomba uzingatie hivi sasa tunaelekea mwezi Mtukufu wa Ramadhani na chakula kingi tunachokula tunatumia unga, naomba bora eneo hili uliache.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu utalii. Naipongeza Serikali kutoza ushuru maeneo ya utalii na ninaomba hapa pasiguswe ibaki hivyo hivyo na kama pana uwezekano basi hii VAT izidi. Kwa mfano, hapo Kenya kwa nini wanachangia kwenye utalii pesa nyingi na wanakusanya mapato mengi kuliko sisi na sisi tuna vituo vingi vya utalii na vinavutia kuliko vya Kenya. Mfano mdogo, huu Mlima wa Kilimanjaro uko Tanzania; kwa nini Kenya wanakusanya mapato mengi kuliko Tanzania?

Hii misamaha wanayopewa kwenye hoteli, hoteli mbili huwa wanaagizia vifaa vya kujenga hoteli kumi na vingine tunaviona vinauzwa Kariakoo kama vile mabati, vitu vya *electronic* na vinginevyo. Sababu ya kusema kwamba tayari wameshafanya mkataba na nchi kwa ajili ya utalii, kwa mabadiliko haya yatawaumiza, lakini huu ni mwaka mpya lazima wategeme mabadiliko.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu kuchangia Hotuba hii ya Bajeti. Bajeti hii ina mtazamo tofauti kubadili changamoto kubwa kukuza uchumi upande mmoja wa Serikali. Ukitazama upande wa pili wa Wananchi wake hasa wa vijijini, haina tija kabisa ukizingatia Mwananchi anategemea kilimo.

Mheshimiwa Spika, mfumko wa bei unakua kwa kasi huku Serikali inasema mfumko huu umeshuka. Hali hii itawaumiza Wananchi hasa wa kipato cha chini. Serikali ingewajibika kujali Wananchi wake, haya yote yanayotokea mbele yetu yasingekuwepo.

Mheshimiwa Spika, niongelee Makundi ya Wananchi kwa uwiano. Afya: Nyumba zijengwe kwenye vituo vyote vya zahanati na nyumba za wauguzi, kwani maeneo mengi hayajakamilika, hasa Wilaya ya Kondoa, Chemba akina mama wengi hupoteza maisha na watoto. Hii yote bajeti haielekei maeneo yote kulingana na wingi wa watu.

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji Wilaya ya Kondoa bado ni kubwa. Naomba bajeti hii itakapotoa mgao wake iangalie Kondoa Kaskazini, wanawake wanapata tabu na wengine kujeruhiwa na Fisi wanapokwenda kungojea maji.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ni kubwa, naiomba Serikali iliangalie. Wilaya haina mawasiliano au nishati mbadala kwani uharibifu wa mazingira unakithiri mno, hii ni kutofikisha umeme mapema Kondoa na kutotoa elimu kwa Wananchi juu ya athari za tabia ya mabadiliko ya nchi kwa kukosa matumizi mbadala.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iongeze bei iwe kubwa kwenye kileo kwani pombe zinaharibu afya za wengi baadaye tutakuwa na Taifa lenye vijana wasio na nguvukazi. Sigara ni hatari kwa maisha yetu ya nini tukuze zao hili? Wakati Serikali ilitupa semina leo tunaongeza kodi basi izidi mara tatu ili kupunguza zaidi watumiaji kwa vilevi hivi hatari kwa afya za watu.

Mheshimiwa Spika, suala la walimu liboreshwe, bila elimu hatutafika popote. Serikali inangoja nini kuwajengea nyumba, kuwalipa pensheni zao kwa wakati na kuwaboresha maisha yao na waweze kuthamini kazi zao, kwani bila kufanya hivyo bado itakuwa tatizo la kutuzalishia watoto wasiojua kusoma na kuandika. Serikali iangalie yote haya.

Mheshimiwa Spika, madini ni chanzo cha uchumi wetu, sasa tuangalie hawa wachimbaji wanachimba madini, tozo ndogo wakati wanaharibu hata barabara zetu. Waongezewe tozo na mashimo wayafukie.

Mheshimiwa Spika, kilimo kipewe kipaumbele kwani wanajitahidi, lakini Serikali haiwajali kabisa wakulima, kila kitu wao halafu unawatoza ushuru. Naomba ufutwe na Serikali iwaangalie mawakala wa pembejeo, wapeleke mbegu kwa wakulima, mbegu nzima na pembejeo zilizo imara.

Mheshimiwa Spika, ukubwa wa Wilaya ya Kondoa kieneo na jiografia yake hasa Kondoa Kaskazini; ni lini Serikali itaangalia eneo hilo na ni lini sasa itapanda hadhi kuwa Mji wa Kondoa? Maendeleo hayatakuja kwa ukubwa wa eneo kwani hata ukitoa bado haitatosha. Mahitaji hata nyumba za Polisi au Askari Magereza bado, kulisha mahabusu ni tatizo kwa Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie vyanzo vingine vya mapato, kupandisha mafuta siyo haki kwani litawagharimu wengi hata wasio na uwezo kama vile walemavu na wazee kwa ongezeko la nauli. Hili liangaliwe upya.

Mheshimiwa Spika, kufanya hivi ni kuvunja moyo wa wakulima kwa kukuza Zao la Alizeti ili liwe zao kubwa nchini na tusiruhusu mafuta yatoke nje kama Korie yauzwe hapa, alizeti yetu inakosa pato la ndani.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kutamka wakati nachangia kwa kuzungumza jana, naiunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Kamati ya Chenge (Bajeti), kwa uchambuzi, ukokotoaji na ushauri mzuri sana kwa Serikali. Bajeti hii ni tofauti na ya mwaka jana.

Nashauri Bajeti hii itekeleze mambo muhimu iliyojipangia hasa upelekaji wa fedha za maendeleo. Fedha za maendeleo muda mwingi hupelekwa kwa kuchelewa. Uwiano wa fedha za maendeleo zinazopelekwa katika miji yetu zinapishana sana, zipo Halmashauri zinapata fedha nyingi tofauti na Halmashauri zingine.

Mheshimiwa Spika, sipendi kutoa mifano lakini hali halisi inajulikana, upendeleo wa aina hiyo unaweza kuleta uhasama kati ya Serikali na Wananchi kwa sababu sisi Wabunge tunaona kwenye vitabu.

Mheshimiwa Spika, jana wakati nachangia niliomba Serikali kuhusu kuibadilisha Bandari ya Dar es Salaam iwe bandari ya kiuchumi, tofauti na sasa ambapo bandari hiyo inanufaisha watu binafsi. Wapo wafanyakazi wasio waaminifu wanaitumia bandari kama mali yao, hali inayopelekea kupoteza mapato makubwa ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wa *TPA*, *TRA* na yale makampuni ya *Clearing & forwarding*, yanashirikiana kuiibia Serikali na hili siyo kama Serikali haiwajui inawajua, Serikali ichukue hatua. Bandari ya Dar es Salaam ni Mgodu ukisimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba niishauri Serikali kuhusu upandishwaji wa mafuta, bima na kadhalika, lakini sana sana nizungumzie upandishwaji wa Bima katika magari hasa yale yanayosafirisha bidhaa. Gharama imepanda maradufu mfano:-

(a) Gari moja hapo awali lilikuwa linakatiwa bima ya asilimia mbili ya thamani, hivi sasa ni 6.5% kwa *trailer*, kichwa (*tractor*) pia ilikuwa ni asilimia mbili kwa sasa ni 4.5% (*comprehensive*).



(b) Endapo utaamua kulipa kwa aina ya *T/Party* gari hilo hilo kichwa kutoka shilingi 120,000 - 300,000, *trailer* kutoka shilingi 120,000 - 700,000; gharama hizi hatazibeba mwenye gari bali mlaji wa mwisho.

Mheshimiwa Spika, ongezeko hili ni kubwa sana. Naomba Kamishna wa Bima akutane na wadau wa usafirishaji ili kuondoa manung'uniko yaliyopo. Waziri atakapohitimisha anijulishe hivi katika kupandisha gharama hiyo alishirikisha wadau?

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, mapato ya ndani hayatoshi kugharamia Miradi yetu ya Maendeleo: Makusanyo ya ndani = *11.5 trillion*; Mikopo na misaada ya ndani/nje = *6.7 trillion*; Bajeti ya matumizi ya kawaida = *12.5 trillion*; Bajeti ya Maendeleo = Jumla: *5.6 trillion*; na Fedha za ndani = *2.9 trillion*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mfumko wa Bei: kushuka kwa asilimia 50 katika kipindi cha miezi 12 kutoka asilimia 18.7 Juni, 2012 hadi asilimia 9.4 Juni, 2013 siyo kitu cha kawaida, kupungua huku ni sawa na kushuka kwa wastani wa asilimia 4.2 kila mwezi. Hili linawezekana lakini kwa gharama zipi? Suala hili linahitaji maelezo na ufafanuzi wa ziada.

Mheshimiwa Spika, nyongeza ya thamani kwenye mazao ya kilimo kama pamba, korosho, (ngano, shairi); *offer* ya *NSSF*?

Vipaumbele vingi mno: (Sura ya 3 ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2013/2014, ukurasa wa 46 - 72):-

(a) Miradi ya Kitaifa ya Kimkakati: Miundombinu (miradi 42): Reli (miradi 9), Barabara (miradi 8), Bandari (miradi 7), Nishati (miradi 10), Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (miradi 4), Maji (miradi 4); Kilimo (miradi 8); Viwanda (miradi 7). (Jumla 57). Maendeleo ya Rasilimali Watu; Utalii na Huduma za Fedha.

(b) Miradi mingine muhimu (maeneo 17 @ ina orodha ya miradi). Katika ugawaji fedha, vipaumbele havionekani kama vilivyotajwa hapo juu; ni bajeti ya kijamaa (kila Sekta au Wizara ipate walau kidogo kidogo. Ni Bajeti ya "Sogea Nikae."

Sekta zinaongezewa fedha kidogo kidogo kutoka kwenye viwango vya mwaka uliopita. Kwa hiyo, hakuna vipaumbele, *big results* hazitakuja sasa. Tuwe na Bajeti ya Mchezo wa Mpira. Unachagua *First Eleven* ndiyo zinainga uwanjani japo timu ina wachezaji 30.

Mwisho, mabadiliko ya *Budget Cycle* yatasaidia kurekebisha baadhi ya upungufu na changamoto zilizopo. Utaratibu huu mpya uungwe mkono na wadau wote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, Serikali katika kujikita kwenye ukusanyaji wa mapato, ichunguze pia utendaji wa SUMATRA! Wananchi wenye magari tunapewa *sticker* feki ambazo si halali kisheria.

Mheshimiwa Spika, upande wa maziwa, pia kuna mapato yanayopotea yanayosababishwa na watumishi wa Serikali kwa samaki kusafirishwa kuelekea nchi jirani bila kulipiwa ushuru.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya benki za Mikoani zina utendaji usioridhisha katika utoaji wa mikopo pale watendaji wanapojipanga na watu wa nje wasiohusika na utendaji wa Benki, basi dhuruma hutawala na wafanyakazi hujenga majumba, hununua magari ya kifahari kwa muda mfupi na wafanyakazi hao wanapoungana na watu wao wa nje huwanyanyasa sana hasa Walimu na kuwapangia riba kubwa kwa sababu kuna mkondo mrefu zinapopitia hata benki ya *NMB* Sumbawanga imelalamikiwa sana na wananchi wa Rukwa juu ya utendaji unaojihusisha na

matapeli. Tunaomba mfanye uchunguzi wa kina na kuona ni jinsi gani watu walivyotoa namba zao za siri na kuwapa kadi zao na kila mwisho wa mwezi hu-*draw* pesa wenyewe.

Mheshimiwa Spika, tunaomba tukopeshwe matrekta kwa Mkoa inayolima sana. Mkoa wa Rukwa tuna matrekta sita tu wakati wengine walikopeshwa matrekta mengi zaidi. Tuangalieni kwa jicho la huruma na uelewa wetu jinsi ulivyo.

Mheshimiwa Spika, lazima Serikali iwe macho kwa fedha zinazopelekwa katika vyuo mbalimbali kwani pesa nyingi huonyesha zimetumika lakini wakuu wengi huambiwa wazirudishe baada ya kukatiwa risiti. Si hivyo tu, naiomba Serikali iunganishe simu za wakuu katika mfumo wa kisasa ili muwanase vizuri na kubaini watendaji wazuri na wabovu.

Mheshimiwa Spika, watendaji wabovu kuwahamisha wanapokuwa na tuhuma huo ni udhaifu wa Serikali ambayo haiwataki Watanzania mema. Kwani Mwalimu Nyerere alifanya kazi iliyowavutia wengi katika kupanga watendaji wake, kuwashusha, kufukuza na wengine kupanda vyeo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana Mkoa wa Rukwa, mipango ya maendeleo safari ijayo tupewe na sisi kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na mchango wa kusema, niwasilishe tena mchango wa maandishi. Hii ndiyo bajeti ya jumla ikiunganisha mapendekezo na matakwa ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TRA* imeanzisha *operation* ya kukagua mizigo bandarini kwa kukagua kila kitu kimoja kimoja. Utaratibu huu ulioondoa mfumo wa *direct release* ambao uliwanufaisha watu wachache na kuikoshesha Serikali kiasi cha mapato lakini una upungufu mkubwa. Hali

hii iliwahi kutokea miaka ya 1980 na ikashindikana pamoja na kuwa wakati huo mizigo ilikuwa michache.

Mheshimiwa Spika, suluhisho la kisayansi ni matumizi ya *scanners*, zifungwe *scanners* njia zote, zifungwe *scanners* nyingi, mizigo inayoingia na ile inayotoka yote ipitie kwenye *scanners*. Kenya wameweka *scanners*, Namibia wamefunga *scanners* na Msumbiji, udhibiti ni mkubwa. Hali hiyo ya udhibiti wa nchi za jirani ndiyo maana nyara na madini toka nchi jirani yote zinapitia katika bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, upo utaratibu wa kutumia *scanners* za kuhamisha (*mobile scanners*), hii pamoja na kuwatia hofu wahalifu lakini huwapa amani ya moyo wananchi wenye mashaka na baadhi ya mizigo. Mashaka kuwa makontena yatokayo migodini yana matofali ya dhahabu, kirahisi yatathibitishwa na kuwaondolea watu mashaka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono uamuzi wa Serikali kuongeza tozo kwenye mafuta, *fuel levy*, ili tupate fedha ya kujenga barabara. Nimeunga mkono ili barabara yangu ya Muhutwe – Kamachumu, kilometa nane tu zilizoahidiwa na Mheshimiwa Rais iweze kujengwa.

Mheshimiwa Spika, lipo daraja la Kishala, mradi sugu kwa miaka zaidi ya 20 litajengwa tukiongeza tozo kwenye mafuta. Barabara za Wabunge zinazoombewa kupandishwa *TANROAD* zitapandishwa tu iwapo tutakuwa tayari kama Taifa kulipa Sh.263 kwa kila lita ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, *REA* imeshindwa kwa miaka zaidi ya mitatu kwenda na mipango yake. Utaratibu wa tozo ya Sh.50 kwa kila lita ya mafuta na fedha hiyo kuwa *ring fenced*, ndiyo njia muafaka ya kueneza umeme vijijini kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono ongezeko la tozo katika mafuta, upo upungufu katika

mwonekano wa bei kwenye *pump* za mauzo. Bei ya petroli imetwishwa Sh.713 ilihali dizeli ikitwishwa Sh.530.

Mheshimiwa Spika, Kanuni ya bei inaonyesha tofauti ya Sh.231 kati ya dizeli na petroli na mafuta ya taa. Hii si kawaida, tofauti ya dizeli na petroli kwa kawaida hutofautiana kwa shilingi kati ya 40 – 80. Nashauri bei ya petroli ipunguzwe ili kuleta uwiano bila kuathiri mapato ya Serikali na hii inawezekana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, lipo tatizo la tofauti ya mafuta ya ndege, ya migodi na *transit* kuwa na tofauti kubwa. Hii itachochea uchakachujaji wa kodi iliyokusudiwa. Mamlaka za *TMAA*, *TRA* na *EWURA* kwa pamoja washirikiane kudhibiti uchakachujaji huo utakaoletwa na ongezeko la tozo/ kodi.

Mheshimiwa Spika, hoja hapa ni kuwa tunahitaji mpango kazi ambao utaonyesha utekelezaji hatua kwa hatua. Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya Nishati inapaswa kubeba jukumu kiongozi kusimamia tishio hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeongeza karibu billioni ishirini kwenye bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Ushauri wangu ni kuwa shilingi bilioni tano zitengwe kulenga uendelezaji wa ufugaji wa samaki. Eneo linalohitaji msaada wa Serikali, ni mashine za kutengeneza chakula. Hizi ni mashine maalum na si rahisi kuziunda hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, rai hapa ni kuwa, kwa wananchi kufuga samaki kwa wingi kutaongeza kipato kwa wananchi na kutaokoa fedha za kigeni zinazotumika sasa kuagiza samaki toka Yemen na Afrika Kusini. Muhimu kwa Serikali kuelewa ni kuwa, kuna uagizaji mkubwa wa samaki toka nje na samaki katika Ziwa Victoria wamepungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuhitimisha Bunge la bajeti, nirejee siri ya maendeleo ya Taifa la China. China wameweza kuvuka kwa kuwekeza katika elimu, elimu ya maadili na

uzalendo, elimu ya kawaida kama hapa kwetu na zaidi wamewekeza katika elimu ya ufundi. Tanzania kama Taifa tumekosea kwa kuacha mkondo wa ufundi, tunapashwa kurudi huko kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kusisitiza utamaduni wa kulipa kodi, tunatafuta mapato kwa kutoza ushuru na tozo kwenye mafuta, utaratibu huu si mzuri. Tunavunja kanuni za uchumi kwa kutoza kodi malighafi tena mafuta hali ambayo huchochea *inflation* na hali ngumu ya maisha.

Mheshimiwa Spika, hii inaweza kuepokika iwapo wananchi watajenga utamaduni wa kulipa kodi/tozo stahili, Serikali na Idara zake watakuwa makini katika matumizi ya fedha za bajeti na mamlaka za Serikali zenye wajibu wa kukusanya kodi/ushuru wataendesha shughuli hizi kwa uadilifu na weledi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza nami nakupa pongezi kwa utaratibu mpya ambao umeubuni katika kujadili bajeti ya nchi yetu. Ni utaratibu mzuri ambao unaipa nafasi Serikali ya kujipanga na kujibu hoja za Wabunge na hatimaye kuja na majibu sahihi yenye kutoa tija kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kupongeza Serikali kwa bajeti ambayo naomba niseme naunga mkono ili pesa ipatikane na naamini yale ambayo yapo Majimboni kwetu yataenda kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mazuri hayo, niombe Wizara katika kuandaa bajeti ya mwakani waangalie jinsi gani Serikali inaungana na Kamati ya bajeti ya Bunge kukabiliana na ugumu wa maisha kwa kupunguza kodi ya mapato toka 19% hadi 13%. Nadhani ni wakati muafaka kwa Serikali kufikia hadi 10% ya mshahara wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, sanjari na hili, nafikiri ili kumpunguzia mzigo mfanyakazi katika ukali wa maisha, ni wakati muafaka vilevile wa Serikali kumwondolea mfanyakazi kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika manunuzi anayofanya katika mahitaji yake ya msingi mfano vifaa vya ujenzi, nguo, viatu, chakula na mengineyo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika, kuendelea kumtoa VAT mfanyakazi ni kumkandamiza bila ya sababu ya msingi, mfanyakazi ni mutumiaji wa mwisho na hana pakwenda kudai ongezeko hilo kama mfanyabiashara ambaye anatoa na kuidai Serikali baadaye. Kwa kufanya hivyo, tutasaidia wafanyakazi wa nchi hii kujenga nyumba bora, kula chakula chenye afya na kupata mahitaji ya msingi ya maisha yao.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kulizungumzia, ni suala la uwajibikaji kwa wananchi wetu. Maendeleo yote ambayo tutayapata, yatatokana na wananchi kufanya kazi. Niiombe Serikali itafute utaratibu wa kila mwananchi wa Taifa hili afanye kazi ili kuongeza kipato kwa Serikali na hatimaye Serikali iweze kuwa na pesa za kumudu kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na la watu kufanya kazi, niiombe Serikali kupunguza matumizi yasiyo na lazima katika utendaji wa kazi zake. Vilevile Serikali ihakikishe mafungu ya Wizara ambayo tunayapitisha na yaliyopitishwa na Bunge hili yanaenda kunakohusika na kufanya kazi ambazo tumeziainishia.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu wa Bunge la bajeti hili ambalo litaisha Juni hii na kuruhusu Serikali kuanza kutumia pesa mapema Julai, ni dhahiri Serikali itakuwa na muda wa mwaka mzima hadi kufikia Bunge la bajeti mwakani kuweza kuwahudumia ipasavyo Wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, niombe ikiwezekana Kamati yetu

ya Bunge yaBbajeti na Kamati za Kudumu za Kisekta za Bunge kusimamia kwa dhati mafungu yaendayo Wizarani na hasa Wizara ya Fedha ikifuata vipaumbele ambavyo tumejiwekea.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niombe Serikali katika mwaka wa fedha ujao, itenge pesa kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu mapya ya Wilaya ya Morogoro ili kuweza kurahisha maendeleo ya watu wa Morogoro Vijijini sanjari na kuwa karibu na wananchi ambao Serikali inataka kuwahudumia.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitenga kwa mara ya mwisho mwaka 2009, Sh.50,000,000/=, niombe Serikali itusaidie.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DKT. TEREZYA P.L. HUVISA:** Mheshimiwa Spika, natoa pongezi nyingi kwa kazi nzuri ya kudhibiti makusanyo ya fedha katika Wizara. Suala la kutunza na kuhifadhi mazingira, ni suala muhimu sana lakini kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri halijapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, hii ni hatari kubwa kwa sababu mazingira yakiendelea kuharibiwa, mapato yatazidi kuteremka, uharibifu wa mazingira una athari ya ukosefu wa mvua, hivyo kusababisha ukame wa muda mrefu. Aidha, mvua zisizotabirika zinasababisha mafuriko.

Mheshimiwa Spika, matatizo yote hayo niliyoyataja hapo juu husababisha maradhi, njaa na tatizo la kutozalisha mazao ya biashara. Sasa hivi kuna tatizo kubwa la mabadiliko ya tabianchi. Tukiliacha bila kuwa na mpango maalumu wa kuelimisha wananchi, tatizo hilo hatutaweza kulirekebisha.

Mheshimiwa Spika, naomba sana suala la bajeti ya mazingira litiliwe maanani ili programu za mazingira ziweze kutekelezwa, ikiwemo programu kabambe ya kuelimisha wananchi.



**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunipa afya njema na kuniwezesha nami nichangie bajeti hii muhimu ya Wizara ya Fedha ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa bajeti yake nzuri na makini iliyoandaliwa kwa utaalum wa hali ya juu na yenye kutekelezeka. Napenda kuipongeza Wizara hii kwa kusimamia vizuri masuala yote ambayo yako chini ya Wizara hii kwa umakini mkubwa kwa manufaa ya Taifa letu ili kuzidisha ukuaji wa uchumi wetu na watu wake.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni muhimu sana kwani ndio inatoa mustakabali wa bajeti nzima ya Serikali kwa mwaka mzima wa fedha. Uandaaji wa bajeti hiyo, unahitaji umakini na utaalumu wa hali ya juu sana ukizingatia Taifa letu bado ni changa na hatujafikia hatua ya kujitosheleza katika bajeti yetu wenyewe bila kupata msaada kwa wahisani kutoka nchi marafiki wa nje.

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu inajitahidi sana kuandaa bajeti ambayo itakidhi mahitaji ya Watanzania wote katika kila idara na sekta mbalimbali lakini kumekuwa na changamoto nyingi sana katika mgawanyiko na vipaumbele mbalimbali vya bajeti katika Mawizara.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikija na sera mbalimbali za kuweza kuwasaidia wananchi lakini kumekuwa hakuna maendeleo mazuri katika sera hizo huku fedha zilizowekwa kupotea bila kuwafikia walengwa na malengo husika.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuzingatia mambo muhimu yanayowakabili wananchi na kuyachukulia kama dharura ili kuyapa vipaumbele katika bajeti hii. Serikali imekuwa ikitoa kipaumbele kikubwa kwa sekta ya kilimo, hapa tunazungumzia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi kutumia mbinu

mbalimbali kuwakwamua wakulima kwani kilimo ndio uti wa mgongo wa Taifa letu, lakini kuna changamoto mbalimbali katika kukabiliana nazo kwani Serikali imekuwa haitoi fedha za kutosha katika sekta hiyo na kufanya jitihada zote ambazo Serikali inazifanya pamoja na ile Sera ya Kilimo Kwanza kuonekana kutofanya vizuri na kushindwa kufikia malengo ya kuwasaidia wakulima ambao wanafanya kilimo katika mazingira magumu na hata wakivuna mazao yao bado thamani yake katika soko imekuwa sio ya kuridhisha kwa bei ya mazao hayo kuwa chini na kupelekea wakulima kupata hasara kubwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kama ingekuwa inatenga fedha za kutosha kwa Wizara husika basi tungefikia malengo yetu katika Kilimo Kwanza lakini kwa kuwapa pia wakulima elimu kwanza ili waweze kufanya kilimo cha kisasa na chenye tija kwa kuwanufaisha.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika sekta hii ya kilimo, Serikali ilikuja na mkakati wa Kilimo Kwanza lakini imeonekana mkakati huo kutokufanya vizuri kwani wakulima hawana elimu ya kutosha kuhusu kilimo. Ingependeza Serikali ianzishe mkakati wa elimu kwanza kwa kutoa elimu ya kutosha kwa wakulima kwa kuwa wakulima hawa wanaokusudiwa katika Kilimo Kwanza hawana elimu ya kutosha kuhusu kilimo.

Mheshimiwa Spika, tukija na mkakati wa elimu kwanza itasaidia wakulima kupata elimu, kuelimishwa kuhusu kilimo bora na kilimo safi. Kufanya hivyo, itasaidia pia kuwapeleka wataalam wetu vijijini na kutoa mafunzo kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, napenda niikumbushe Serikali, tuna wataalam wengi wa fani za kilimo hapa nchini, lakini tuna tatizo moja la hawa wataalam wakipangiwa kazi vijiji huenda kuripoti na baada ya muda wa mwaka mmoja au miwili huomba ruhusa ya kwenda kusoma na kuacha kituo hakina mtu.

Mheshimiwa Spika, kufanya hivyo, husababisha wananchi kukosa wataalam wa kuwapa elimu bora. Serikali

inapowapeleka hawa wataalam basi naiomba isisahau kupeleka wataalam wengine ili kuziba nafasi iliyoachwa wazi kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali itenge fedha za kutosha kuvinyanyua vyama vya ushirika viweze kuwasaidia wakulima wetu, kwani vyama hivi baadhi vimeshakufa na kutokufanya kazi tena na vingine kushindwa kufanya kazi kwa kukosa fedha za kujiendesha. Haya yote yatawezekana pale tu Serikali itakapokuwa inatenga bajeti ya kutosha kwa Wizara hii ili iweze kukidhi mahitaji ya wadau wote.

Mheshimiwa Spika, katika mpango mzima wa Serikali kutimiza majukumu yake kikamilifu, fedha za kutosha zinahitajika kutengwa kwa ajili ya hizi Wizara zetu ili ziweze kufanya kazi zake vizuri na kutimiza malengo yake kwa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia katika suala zima la umuhimu wa Wizara, Wizara zote zina umuhimu sawa kwani zinawahudumia wananchi katika Taifa letu na hakuna sababu ya kuona baadhi ya Wizara zina umuhimu kuliko nyingine na hivyo kutengewa bajeti za juu zaidi kuliko Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, mfano, napenda kuongelea baadhi ya bajeti zilizowakilishwa na Serikali hapa Bungeni kupitia Wizara mbalimbali hazikidhi mahitaji halisi ya upatikanaji wa huduma kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia bajeti ya Wizara ya Maji, tatizo la maji limekuwa ni tatizo sugu hasa katika maeneo ya vijijini na mijini kufanya mpaka karne hii akina mama huku wakiwa wamebeba watoto migongoni, kukesha kwenye mabomba ya maji usiku kucha ama kwenye visima wakingoja foleni, ilihali upande wa pili wa Serikali unaitengea bajeti ndogo Wizara ya Maji ambayo haiwezi kukidhi mahitaji na kutatua tatizo la kutokupatikana maji kwa asilimia 100%.

Mheshimiwa Spika, Serikali ingeweka mkakati

madhubuti kwa sekta hii ili kutokomeza kabisa tatizo la upatikanaji wa maji kwa kutenga fedha za kutosha ili kutokomeza kabisa tatizo la upatikanaji wa maji kwa kutenga fedha za kutosha ili kushughulikia miradi mikubwa ya maji ili ikamilike na kuanza kusambaza maji maeneo mbalimbali nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikigharamia miradi ya maji na miundombinu yake kwa fedha nyingi za walipa kodi lakini miradi hiyo ikimalizika imekuwa haitoi huduma ya maji kwa wananchi kama ilivyokusudiwa na tatizo ni uhaba wa fedha za kukarabati miundombinu ya maji ili kuweza kusafirisha maji kwa usalama mpaka kwa mtumiaji wa mwisho. Serikali isisite kabisa kuipa Wizara hii ya Maji bajeti nzuri na ya kutosha kama tunataka kuwaondolea adha wananchi wetu wa mjini lakini hasa vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuiangalia pia bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii, nayo haijitoshelezi kulingana na umuhimu wa sekta hiyo ambayo inalingizia Taifa fedha za kigeni. Wizara hii inatakiwa kuwa na bajeti nzuri kwani matatizo mengi hujitokeza katika sekta ya utalii. Mfano ujangili wa wanyama wetu ambao wengi wako katika kundi la kutoweka duniani na majangili hayo yanafanikiwa kufanya ujangili huo na kutokomea kwa sababu ya Wizara kutokuwa na fedha za kutosha za kuwawezesha kufanya doria muda wote.

Mheshimiwa Spika, hali hii imekuwa ikililetea Taifa letu shida na kuwa katika hatari ya kupoteza wanyama hao ambao ni adimu duniani. Bajeti ya Wizara hii ikiwa nzuri na yenye kujitosheleza, itarahisisha mambo mengi katika sekta nzima ya utalii kwa kupata fursa ya kuweka matangazo mbalimbali ya kuvitangaza vivutio vyetu katika viwanja vya ndege, luninga na mabango nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo, itasaidia sana kupata watalii wengi kuja nchini kwani watakuwa wanapata taarifa za vivutio vyetu kutoka katika matangazo hayo. Tumejionea wenyewe kutokuwa na matangazo ya kutosha athari zake

kwani baadhi ya nchi tulizopakana nazo wanadiriki kutangaza baadhi ya vivutio vyetu na kusema viko kwao na hivyo kupata wageni na kulikosesha Taifa pato la fedha za kigeni. Naiomba Serikali kuliangalia hili kwa mapana yake na umuhimu kwa manufaa ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia pia katika sekta nzima ya maliasili nayo imekuwa na changamoto nyingi zitokanazo na ufinyu wa bajeti kwa Wizara husika na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira kwani watu wamekuwa wakikata miti, kuwasha moto hovyo katika misitu yetu na kusababisha majangwa ambayo madhara yake ni kwa nchi kupatwa na ukame.

Mheshimiwa Spika, hali hii yote inatokana na Wizara kutengewa bajeti ndogo na hivyo kusababisha kukosekana kwa doria ya kutosha, vitendea kazi duni na kutokuwa na posho za kuwapa watumishi ili kufanikisha zoezi zima la usimamizi wa sekta hiyo. leleweke kwamba pale Serikali inapoweka bajeti nzuri, hakika matatizo kama haya husaidia kuyamaliza kwa urahisi na hivyo wananchi kufaidika zaidi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuweka mkakati madhubuti katika sekta ya misitu ili iweze kushirikiana na sekta ya elimu katika suala zima la upatikanaji wa mbaao ambazo zitasaidia utengenezaji wa madawati kwa wanafunzi wetu ambao mpaka leo hii wanakaa chini na kusomea chini.

Mheshimiwa Spika, hali hii inashangaza kwa kuwa tumejaliwa misitu mingi na kwa nini Wizara hizi mbili zisikubaliane kwa pamoja katika mpango huo na Serikali itenge fedha kwa ajili ya gharama zote zitakazohitajika katika mradi huo.

Mheshimiwa Spika, inafahamika kabisa viwanda ndio nguzo kubwa ya kiuchumi katika Taifa lolote lile. Nchi ambazo ziko juu kiuchumi, zote ni kutokana na kuwa na viwanda vikubwa na sera nzuri zenye kutekelezeka juu ya kuimarisha na kuboresha viwanda. Hapa nazungumzia Wizara ya Viwanda na Biashara kwani pia bajeti ya Wizara hii

haijajitosheleza ili kukidhi mahitaji husika ya nchi yetu kupitia sekta ya viwanda na kuamua kuwekeza huko katika viwanda vidogovidogo maeneo mbalimbali nchini ili kuweza kusaidia vijana wetu kujajiri wenyewe kwa kuanzisha vikundi vidogovidogo na kupunguza tatizo la ajira kwa vijana ambalo limekuwa sugu kwa siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, pia Wizara ingepatiwa fedha za kutosha katika kukabiliana na changamoto zake ingesaidia sana katika sekta ya biashara kwa kujenga masoko ya kisasa kila pembezoni mwa miji yetu na kusaidia kupunguza misongamano ambayo ipo kwa hivi sasa katika masoko yetu yaliyopo ambayo yamezidiwa na watu wengi na sehemu za kuhifadhia mazao zimekuwa chache kutokana na uwingi wa wachuuzi na ukuaji wa rasilimali watu mjini.

Mheshimiwa Spika, kufanya hivyo kungesaidia pia kupunguza wafanyabiashara ambao hukosa mahali pa kufanyia biashara na kuamua kuweka biashara zao kandokando mwa barabara kitu ambacho ni hatari kwa maisha yao. Naiomba Serikali kuzingatia sekta hizi katika bajeti zake kwani kufanya hivyo kutasaidia sana kutatua changamoto zilizokuwepo na zinazozidi kuwepo na kuwa adha kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, suala zima la maendeleo ya jamii na jinsia na watoto, ni jambo ambalo linaigusa jamii moja kwa moja lakini Wizara hii pia imekuwa na bajeti finyu ambayo haikidhi mahitaji. Kwenye jamii, kuna matatizo makubwa katika mpango mzima wa kuwatunza wazee wetu wasiojiweza na hali hii imetokana na kukosekana na maeneo ya kutosha ya kuweza kuwaweka wazee hawa wenye mahitaji maalum na kuwasaidia kwa huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwa na mkanganyiko kuhusu masuala ya watoto wa mitaani kutokujaliwa kabisa na kuzagaa kila kona ya miji yetu na kuombaomba hovyoo. Watoto hao imefika mahali hupata mimba, maambukizi ya maradhi mbalimbali ikiwamo ya Ukimwi. Hali hiyo husababisha tatizo kuwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, vilevile tatizo la mimba zisizotarajiwa kwa akina mama na kutelekezwa na waume zao na kuishia kuishi maisha magumu ambayo huwafanya kuwatupa watoto wao na baadhi yao huwatumia watoto hao kama kitega uchumi cha familia kwa kuwatumia mitaani na barabarani kupita na kuombaomba.

Mheshimiwa Spika, kitendo hiki kinatokana na hawa akina mama kukosa shughuli ya kufanya ama biashara ndogondogo. Wakiwezesha, wataweza kutunza familia zao ilhali wamekimbiwa na waume zao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na haya yote lakini Serikali inatakiwa kuitengea bajeti ya kutosha kwani Wizara hii itasaidia kutatua mambo yote hayo na kuwa na Taifa ambalo halina watoto wa mitaani na wazee kupata sehemu ya kujisitiri na kupatiwa huduma muhimu na akina mama kupata unafuu wa makali ya maisha waliyokuwa nayo hivi sasa na pengine kuweza kupunguza matatizo haya kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi kwa umuhimu wake, napenda kuipongeza Serikali kwa kujitahidi kuitengea bajeti nzuri ambayo kwa kiasi fulani imejaribu kukidhi mahitaji ya sekta nzima ya ujenzi lakini kuna changamoto mbalimbali katika suala zima la miundombinu yetu kwani baadhi ya barabara bado hazijatengewa fedha na kuzifanya kuendelea kuwa tatizo kwa maeneo husika kwa kupitika kwa kipindi maalum tu lakini pindi mvua zinaponyesha hali huwa ni mbaya na kushindikana kabisa kupitika kwa urahisi. Naishauri Serikali kuiongezea fedha Wizara hii ili iweze kukidhi mahitaji ya barabara zetu ili ziweze kuwa katika hali ya kupitika muda wote wa mwaka.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuishauri Serikali, baadhi ya barabara ambazo zipo chini ya Halmashauri sasa ikibidi ziwe chini ya Wizara hii ili ziwekwe kwenye mipango ya Wizara kwani imeonekana baadhi ya barabara ambazo ziko chini ya Halmashauri kutokuwa na kiwango kizuri na mara nyingi hukarabatiwa na si kujengwa upya katika kiwango

kinachotakiwa. Nyingi kusema ukweli zimechoka sana ukilinganisha na barabara zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi. Bajeti nzuri ikitengwa kwa Wizara hii, tutakuwa tumetatia matatizo mengi yanayoikabili sekta nzima ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara zetu ili ziweze kufanya kazi vizuri na kukabiliana na changamoto zilizopo, ni lazima zitengewe bajeti ya kutosha ili kukidhi mahitaji yake. Katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na bajeti yake iliyotengewa lakini bado ni ndogo kutokukidhi baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunakabiliwa na tatizo la ongezeko la vipodozi visivyofaa kwa matumizi ya binadamu. Tatizo hili limekuwa sugu na kuwaathiri watumiaji wa vipodozi hivi ingawa Serikali imechukua juhudi za makusudi kuelimisha wananchi na kupitia mamlaka husika kuviangamiza vipodozi hivi lakini uingiaji wake nchini umekuwa mkubwa kiasi ambacho hurudisha nyuma juhudi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuongeza udhibiti na ukaguzi wa mara kwa mara katika maduka na mipakani, bandarini kuweza kuzuia uingizaji na kuwafikia wananchi na ikiwezekana kutunga sheria ndogo kwa ajili ya kuwashughulikia wale wote watakaokiuka na kubainika kuingiza nchini vipodozi hivi.

Mheshimiwa Spika, mpango mzima huo unahitaji fedha za kutosha ili kwenda sambamba na hali halisi vinginevyo bila kuwa na fedha za kutosha hatutaweza kudhibiti ipasavyo matatizo haya ya kuendelea kuwa jalala la vipodozi hivi na watu wetu kuendelea kuathirika.

Mheshimiwa Spika, tengeo la bajeti ya sekta ya afya nchini halikidhi Azimio la Abuja la mwaka 2001 linazoitaka kila nchi mwanachama wa Umoja wa Afrika kutenga 15% ya bajeti yake kwa ajili ya sekta ya afya. Vilevile kuna kasi ndogo ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM 2007 – 2017).



Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuzungumzia huduma zetu katika hospitali, vituo vya afya, kiujumla haziridhishi hata kidogo kwani wagonjwa wamekuwa wakijazana mawodini mpaka wengine wanalala chini kwa kukosa mahali pa kulala yaani vitanda, hali hiyo inatokana na uchache wa vitanda na wodi, bajeti inayotengwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa kutokidhi mahitaji halisi, mazingira duni ya utoaji wa huduma za afya katika zahanati na vituo vya afya nchini hasa katika maeneo ya vijijini ikiwemo upungufu wa watumishi, vifaa tiba na vitendanishi.

Mheshimiwa Spika, pia utolewaji duni wa huduma ya afya ya mama na mtoto hasa katika maeneo ya vijijini imekuwa ni tatizo la muda mrefu, uwepo wa idadi kubwa ya dawa zilizo chini ya viwango, maeneo hayo yamekuwa yakikabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo pia za ukosefu wa usafiri, ukosefu wa umeme, upungufu wa watumishi na mazingira duni ya utolewaji wa huduma za afya, hali inayosababisha kuendelea kuwepo kwa vifo vinavyotokana na uzazi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kufanya juhudi za makusudi kupunguza vifo vya mama na mtoto. Naiomba Serikali kutenga fedha za kutosha kwa Wizara hii ili kuweza kukidhi mahitaji husika ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali imekuwa ikiingia gharama kubwa kwa kuwapeleka viongozi mbalimbali nje ya nchi kwa matibabu, hali hiyo imekuwa ikigharimu Serikali fedha nyingi na kuacha sekta nyingine muhimu ambazo hutoa huduma kwa wananchi walio wengi kuwa na upungufu mwingi kwa huduma muhimu kukosekana.

Mheshimiwa Spika, kwa Serikali kuwekeza hapahapa nchini katika tiba muhimu ambazo tumekuwa tukizifuata nje ya nchi, itasaidia kwanza kwa wengi kupata huduma hizo na pia kuipunguzia gharama kubwa ambayo inaipata hivi sasa na hivyo fedha ambazo zingetumika kwa kuwapeleka viongozi wetu nje ya nchi kutumika katika kukuza huduma mbalimbali za kiafya katika jamii.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali, kwa kuwa utekelezaji wa utoaji wa huduma za afya unahusu uwezo wa Serikali, katika kutenga bajeti inayokidhi mahitaji ya sekta ya afya nchini, naiomba Serikali ijizatiti kupanua wigo wa walipa kodi na pia kuangalia vyanzo mbalimbali vya mapato ambavyo viko chini ya Wizara, vikisimamiwa vizuri vitaongeze mapato ya ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, vyanzo hivyo ni pamoja na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (*TFDA*), Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali (*Chief Government Chemist*), Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa MOI na Taasisi ya Chakula na Lishe. Serikali ikiweka mikakati mizuri ya kukusanya mapato, itasaidia kwa kiwango kikubwa uendeshaji wa sekta ya afya nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, hospitali za Rufaa za Mikoa zitumie mapato yake ya ndani kugharamia baadhi ya shughuli za utoaji wa huduma za afya katika taasisi zao. Kufanya hivyo kutaongeza vyanzo zaidi vya mapato ya ndani na kupunguza mianya ya ukwepaji kodi.

Mheshimiwa Spika, hatua hii itawezesha Serikali kutenga 15% ya bajeti yake na kufikia malengo ya Abuja. Sekta ya afya ipewe kipaumbele cha kudumu kibajeti ili iweze kutoa huduma bora za afya kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie Bohari Kuu ya Dawa, kwani ina jukumu la kununua, kuhifadhi na kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika hospitali na vituo vya afya vya Serikali nchini. Uzoefu unaonyesha kuwa, kuna tatizo kubwa la huduma za (*MSD*) kutofika katika vituo vya afya kwa wakati na kuwa na ufinyu wa bajeti, baadhi ya watumishi wasiokuwa waaminifu wamekuwa wakihamishia dawa kwenye maduka ya dawa ya watu binafsi hali inayosababisha ukosefu wa huduma ya dawa katika vituo vya afya nchini.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na hili, nashauri Serikali kufanya uchambuzi yakinifu ili kutathmini mfumo

mzima wa mnyororo wa ugavi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi utakaokidhi mahitaji ya nchi. Serikali ifanye maboresho ya kimfumo na kiutendaji katika taasisi ya (*MSD*). Kamati za Afya za Wilaya na Kamati za Mapokezi za hospitali ziimarishwe na zihushishwe katika kupokea na kuhifadhi dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali ifanye tathmini ya mahitaji halisi (*Forecasting and Quantification*) ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi vinavyohitajika nchini. Aidha, elimu ya kukadiria mahitaji ya dawa itolewe kwa wahusika, kiundwe chombo maalum kinachojitegemea cha kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi kutoka *MSD* mpaka kwenye vituo vya afya nchini, *MSD* ibaki na jukumu la ununuzi na uhifadhi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

Mheshimiwa Spika, vile vile Halmashauri zihimizwe kupeleka mahitaji ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi *MSD* mapema iwezekanavyo ili kutoa muda wa kutosha kwa ununuzi wake.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia majeshi yake imekuwa ikifanya kazi zake katika wakati mgumu sana kwani wamekuwa wakikumbana na changamoto nyingi sana na changamoto hizo ni za kifedha, kutokuwa na bajeti ya kutosha ili kuwawezesha kupambana nazo lakini nichukue fursa hii kuipongeza Wizara hii kwa kuwa na moyo wa ufanyaji kazi mzuri na wa kujitoa ingawa matatizo yamekuwa ni mengi. Kutokana na umuhimu wa Wizara hii kubeba majukumu mazito ya usalama wa raia na mali zao, Idara ya Uhamiaji na Magereza lakini bado wananchi wamekuwa wakilalamika kutoridhishwa na baadhi ya utendaji wa Idara hizo kutokukidhi na kutenda haki kwa maana ya usawa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuangalia suala zima la uboreshaji wa mahabusu zetu kwani baadhi ya mahabusu haziridhishi kimazingira. Mahabusu hizo kumekuwa hakuna sehemu salama za kujisaidia na zikiwepo basi si salama kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, vile vile utaratibu wa kuwapelekea chakula mahabusu huwalazimu kulia humohumo ndani ilhali eneo lenyewe si salama na safi na kupelekea kuwa hatarishi kwa afya za walaji. Serikali ingetenga fedha za kutosha kwa kuwajengea mahabusu sehemu nzuri ya kulia chakula pale wanapoletewa na ndugu zao.

Mheshimiwa Spika, pia tatizo la mbu kwenye mahabusu limekuwa ni sugu, mahabusu kutokuwa na taa, halikadhalika kutokufanyiwa usafi, kiujumla baadhi ya mahabusu zetu zimekuwa si salama kwani haziko katika mazingira mazuri. Kwa kuweka mkakati wa kifedha wa upulizaji dawa za kuua wadudu ambukizi kama mbu kungesaidia kuepusha maradhi.

Mheshimiwa Spika, ingawa Serikali imekuwa ikijitahidi kwa kuendelea kujenga nyumba za Maafisa wa Polisi ili na wao waweze kukaa sehemu nzuri lakini bado kumekuwa na changamoto nyingi kwani bado Askari wetu wamekuwa wakiishi mitaani na raia, hali hiyo ni hatari kwao kwani uhalisia wa kazi wafanyayo huwajengea maadui katika maisha yao.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie kama janga kwa Wizara hii suala la nyumba za Askari ili waweze kuepukana na adha waipatayo hivi sasa. Ujenzi wa nyumba hizi uende sambamba na kuwaboresha mishahara na marupurupu na pia kujengwa zaidi kwa Vituo vya Polisi nchini kote, kwani kuna baadhi ya maeneo yamekuwa na upungufu wa vituo hivyo na hata baadhi ya wananchi wamekuwa wakijitolea kujenga vituo hivyo na kushindwa kupatiwa Polisi ili waende kuanza kutoa huduma kwa jamii husika na sababu kubwa imekuwa ni Wizara kutokuwa na fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Wizara hii kutokutengewa bajeti ya kutosha, kunapelekea baadhi ya maeneo kutokuwa na Askari Polisi wa kutosha na pia kupelekea kutokuwa na vitendea kazi muhimu kama magari, pikipiki kwa ajili ya kufanyia doria katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, jambo hili liangaliwe kama ni

janga kwani matatizo haya yakiendelea bila kutatuliwa basi usalama wa raia utakuwa matatani, mambo haya pia yaangaliwe na kwa upande wa Jeshi la Magereza na Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria imekuwa ikikumbana na changamoto nyingi kwani nayo haijatengewa bajeti ya kutosha ili kupambana na changamoto zilizopo. Wizara hii imekuwa ikikabiliwa na uchakavu wa majengo ya Mahakama kutokukidhi uhalisia wa kazi husika.

Mheshimiwa Spika, majengo hayo hayajakarabatiwa kwa muda mrefu na kupelekea hata ufanisi wa kazi kwa Mahakimu kupungua kwani mazingira ya ufanyaji wa kazi yanakuwa magumu sana na si mazuri. Uhifadhi wa majalada umekuwa wa kienyeji kiasi ambacho inapeleka urahisi wa hata kupotea kwa baadhi ya majalada na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo wananchi wamekuwa wakitembea umbali mrefu kufuata mashauri ya Kimahakama katika Wilaya nyingine na hali hiyo hutokea kwa wao kukosa Mahakama za Wilaya zao.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuiwezesha zaidi kibajeti Divisheni ya Mashtaki ili iweze kutekeleza mpango wake wa kutenganisha mashtaka na upelelezi (*Civilianization of Prosecution Service*) kwa nchi nzima kwani bado kuna maeneo mengine ya nchi yetu kwenye Mikoa na Wilaya ambapo mpango huo haujafika na hivyo kuendeleza wasiwasi katika mfumo wa utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nadhani hivi sasa umefika wakati wa Mahakama zetu kufanya kazi kwa teknolojia ya juu zaidi kuliko inavyofanyika hivi sasa. Kwa mfano, uandishi wa mashauri Mahakamani ambapo Hakimu au Jaji hulazimika kuandika kwa mkono maneno ya shahidi au mtuhumiwa wakati shauri likiendelea.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu sio wa uhakika sana kwa sababu Hakimu au Jaji ni binadamu na hivyo kuna uwezekano mkubwa wa kukosea kwa kuongeza au kupunguza maneno yanayotolewa na shahidi au mtuhumiwa. Hali hiyo imekuwa sababu ya malalamiko ya kesi nyingi dhidi ya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, ni vema hivi sasa mfumo wa (*Hansard*) kuanza kutumika ili kudhihirisha kwamba si tu haki inatendeka bali pia inaonekana kutendeka (*justice must not only be done, but must be seen done*) kwa Serikali kutoa fedha za kutosha kwa Wizara ya Katiba na Sheria ili kuweza kuandaa mifumo hiyo ya kisasa kwa ajili ya utoaji wa haki na kwenda sambamba na wenzetu katika nchi nyingine wanaotumia mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, vile vile kutenga fedha kwa ajili ya kuwapeleka Wanasheria wetu nje ya nchi kusoma zaidi sheria za mikataba ili kutuepusha na mikataba mingi ambayo tumekuwa tunaingia na haina tija kwa Taifa letu na kutuletea hasara.

Mheshimiwa Spika, kupitia Wizara ya Uchukuzi, tumejionea mengi yamefanyika na utendaji mzuri wa uhakika ukiendelea kufanyika lakini pia kumekuwa na changamoto zake katika Wizara hii. Tatizo la fedha za kutosha limekuwa likiwakwamisha watendaji wa Wizara hii kukabiliana na changamoto hizo na kuleta mabadiliko katika sekta nzima ya uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na bandari yetu ya Dar es Salaam kuwa na umuhimu mkubwa Kitaifa na kutumika na Mataifa mengine, hali hiyo huifanya bandari hii kuwa ni sehemu muhimu ya kulingizia Taifa pato na fedha za kigeni na kufanya uchumi wa Taifa hili kukua kwa haraka lakini bandari yetu imekuwa na upungufu mwingi ambao unahitaji fedha za kutosha ili kukabiliana nao na kupelekea Taifa letu kuendelea kuingiza fedha za kutosha kupitia bandari hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ikitengewa fedha za

kutosha pia itawezesha bandari za Mtwara, Tanga pamoja na nyinginezo ndogondogo kuweza kuboreshwa katika hali ambayo itaweza kukuza pato la Taifa letu kwa kiasi kikubwa. Umuhimu wa bandari hii haupaswi kubezwa hata kidogo. Kwa kutumia bandari hii pekee, tutafaidika kwa kiasi kikubwa kiuchumi kwani idadi ya meli na mizigo toka nje ya nchi itazidi na hivyo pato kukua.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali iangalie suala zima la uboreshwaji wa reli zetu kwa kutengea fedha za kutosha kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, fedha kwa ajili ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo bado ni ndogo ukilinganisha na majukumu ya Wizara hii. Wizara hii imekuwa ikishughulikia masuala ya habari, vijana, utamaduni na michezo ambayo yote yana umuhimu mkubwa lakini suala zima la vijana kwa umuhimu wake linahitaji fedha za kutosha ili kuweza kukidhi mahitaji na changamoto zinazowakabili.

Mheshimiwa Spika, Serikali itenge fedha za kutosha kwa Wizara ili waweze kukabiliana na matatizo makubwa yanayowakabili vijana kwani tatizo kubwa limekuwa ni ajira, mitaji na baadhi kutumia madawa ya kulevya na kufanya vitendo vya kihalifu. Kwa kuwatengea fedha za kutosha Wizara hii wataweza kuwa na mikakati mizuri ya kuweza kuwasaidia vijana wetu kwani tatizo hili linapozidi litakuwa hatari hapo siku za mbeleni.

Mheshimiwa Spika, pia suala zima la utamaduni limekuwa likisuasua kwa kukosekana fedha za kutosha. Utamaduni ni jambo muhimu sana kwa Taifa lolote. Naiomba Serikali kuliangalia suala hilo na kulitengea fedha ili utamaduni zetu ziweze kudumishwa kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya michezo ni eneo ambalo kama likiwekezwa vyema inaweza kuwa ni mojawapo ya vyanzo vikuu vya mapato na kuchangia katika pato la Taifa.

Tanzania ni mojawapo ya nchi ambazo wananchi wake wengi ni wapenzi wa michezo (mpira wa miguu, pete, kikapu, masumbwi, riadha, bao na kadhalika).

Mheshimiwa Spika, hili linajidhihirisha kutokana na uchangiaji wa hiari katika sekta nzima ya michezo hususani ujenzi wa viwanja vya michezo, uchangiaji wa timu mbalimbali za michezo zinapokuwa zikijiandaa katika mashindano mbalimbali katika ngazi ya Taifa hadi Kimataifa. Hivi sasa michezo imekuwa ni ajira kwani watu kupitia michezo wanalipwa fedha nyingi na kuendesha maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, hapo awali michezo haikudhaniwa kama ingeweza kuwa ajira lakini hivi sasa vijana wamekuwa wakifaidika na michezo na kumekuwa na matukio mengi ya michezo yanayohusu kuuza na kununua wachezaji kwa timu za ndani na nje lakini kwa masikitiko makubwa, Serikali imekuwa haina takwimu za kutosha za kujua ni kiasi gani cha fedha Serikali inafaidika kutokana na biashara hiyo kama stahiki yake ya kodi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuweka mkazo katika hilo ili stahiki hizo ziweze kuingia katika Mfuko wa Serikali kama kodi na si kupotea kama ifanyikavyo hivi sasa. Taifa letu bado changa sana ila kwa kupitia sekta hii ya michezo tungeweza kulitangaza zaidi, likajulikana duniani kama wafanyavyo wenzetu.

Mheshimiwa Spika, tungekuwa na utaratibu mzuri wa kukuza vipaji na kuviendeleza. Hapo awali tulikuwa tuna utaratibu mzuri sana tokea ngazi za chini kielimu, kuanzia shule zetu za msingi na sekondari, tuliweka utaratibu wa michezo na mashindano mashuleni lakini miaka ya karibuni utaratibu huo ulifutwa bila kuangalia athari zake.

Mheshimiwa Spika, leo hii tunakosa na kupoteza vipaji vingi sana ambavyo tungeweza kuvipata toka mashuleni na kuvikuza ili vije kusaidia Taifa letu. Kurudisha mashindano mashuleni kutasaidia sana kukuza vipaji mbalimbali vya vijana



wetu tangia wakiwa wadogo na kupata wanamichezo wazuri ambao baadaye watakuwa mashuhuri na kulitangaza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kurudisha michezo mashuleni na kuboresha zaidi utaratibu huo na kutenga maeneo zaidi ya wazi kwa ajili ya michezo mbalimbali. Hali hiyo itasaidia kupata vijana wenye vipaji mbalimbali vitakavyokuja kusaidia Taifa letu hapo baadaye na kutoa mwanya wa vijana kupata ajira kupitia michezo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali pia kutenga fedha za kutosha kwa Wizara hii ili kukidhi mahitaji katika sekta nzima ya michezo hapa nchini na kuweza kuliingizia Taifa pato.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto nyingi sana kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu. Wizara hii kwa miaka mingi sasa imekuwa na matatizo mengi na kulalamikiwa na wadau mbalimbali. Malalamiko hayo mengi yanatokana na Wizara kutokufikia malengo yake kwa kupatiwa bajeti ndogo ambayo haitoshelezi kukabiliana na matatizo yanayoikabili Wizara hii katika sekta ya elimu. Kwa umuhimu wa elimu ulivyo, niliona ni jambo jema zaidi kama Wizara hii ingepatiwa fedha za kutosha ili kukabiliana na matatizo ya majengo chakavu katika mashule yetu, upungufu wa maabara, matundu ya choo, Walimu wa masomo ya sayansi na madawati.

Mheshimiwa Spika, ukizungumzia suala la upungufu wa madawati na kupelekea wanafunzi kukaa chini, ni aibu kwa Taifa letu ambapo tuna misitu mingi mikubwa ambayo ingetusaidia kwa kupata mbao za kutengenezea madawati kwa watoto wetu na kumaliza tatizo la ukaaji chini wawapo kwenye masomo yao.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa upatikanaji wa elimu bora unahitaji fedha za kutosha ili kukidhi mahitaji ya vitabu mashuleni na vitendea kazi kwa Walimu pamoja na motisha

nzuri kwa Walimu. Walimu wamekuwa wakiidai Serikali fedha nyingi za marupurupu yao ambayo ni ya siku nyingi lakini mpaka hivi leo hawajalipwa.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo hupunguza ufanisi wa ufanyaji wa kazi kwa Walimu hawa kwani wamekuwa wakiishi maisha duni sana na kufanya kazi katika mazingira magumu. Wizara itenge bajeti ya kutosha ili kuweza kuwajengea Walimu nyumba za kuishi na kuwapa motisha wale wanaokwenda kufundisha shule za vijijini ambazo nyingi zimesahaulika.

Mheshimiwa Spika, nadhani ni jambo jema sasa kwa Wizara hii kupewa bajeti nzuri ili ijitosheleze pia katika mafunzo ya ufundi kwa vijana wetu. Kwani tumejionea wenyewe faida za mafunzo haya ambayo yamesaidia vijana wengi kujajiri wenyewe kutokana na kupata elimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, ifike wakati sasa Serikali kuipa fedha Wizara ili iweze kuongeza vyo vya ufundi katika maeneo yote nchini ili kutoa mwanya kwa vijana wengi kupata elimu hiyo na kujajiri wenyewe na kuondokana na tatizo la ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, Sekta hizi za elimu na mafunzo ya ufundi ni muhimu sana, bajeti iangaliwe kwa upana wake na kuangalia masuala muhimu ya kuweza kutatua matatizo sugu ya sekta hii ambayo ni ya siku nyingi na yamekuwa yakisababisha kushuka kwa kiwango cha elimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, tumejionea migogoro mingi ya ardhi hapa nchini ikitokea na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kushindwa kuitatua, haijulikani tatizo liko wapi lakini Wizara inahitaji fedha za kutosha ili kukabiliana na changamoto hizo na kuondokana na migogoro hiyo ambayo wananchi hawajui hatma yake ni lini.

Mheshimiwa Spika, tuna matatizo pia ya upimaji wa maeneo ambayo mpaka leo hii bado kuna maeneo hayajapimwa kutokana na ufinyu wa bajeti ya Wizara hii.

Kupimwa kwa maeneo kutawasaidia wananchi wetu kutumia hati zao kama dhamana kupata mikopo kwenye mabanki yetu na kufanya shughuli zao na kuinua pato la nchi.

Mheshimiwa Spika, tunakabiliwa na changamoto kubwa ya mipango miji ambayo imekuwa ni tatizo la muda sasa, tukiiwezesha Wizara hii fedha za kutosha, hakika matatizo mengi yatafungua kama si kumalizika kabisa kwani imeonekana ufinyu wa fedha ndio husababisha mipango mingi kutokukamilika na kufanya Wizara kutofikia malengo yake.

Mheshimiwa Spika, tatizo la kazi na ajira limezidi kusumbua Taifa letu ingawa Serikali ina mipango mingi ya kullitua lakini imeonekana bado kuna ugumu wake kwani fedha zinazotengwa kwa Wizara hii bado zimekuwa ni ndogo na hazikidhi mahitaji halisi ya changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuiomba Serikali kuangalia upya suala la ajira kwa vijana kwani mpaka sasa idadi ya vijana wasiokuwa na ajira inazidi kukua siku hadi siku. Vijana hawa imefikia kukata tamaa na kutokujua nini hatma yao. Serikali yetu imekuwa ikitangaza nafasi za kazi nyingi lakini upatikanaji wake umekuwa mdogo na mgumu sana na hata zikitangazwa baadhi ya nafasi zinakuwa chache mno kiasi ambacho hata upatikanaji wake unakuwa mgumu sana.

Mheshimiwa Spika, vijana wanaomaliza vyo vikiu kila mwaka ni wengi lakini wanaobahatika kupata ajira ni wachache hata wale wanaomaliza darasa la saba, *form four* na *form six* pia ni tatizo kupata ajira. Ukiangalia kwa wastani huo utagundua kuwa tatizo ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ningepomba Serikali kuweka utaratibu wa kuwapa elimu ya ujasiriamali vijana hawa tokea wakiwa vyaoni, hali hiyo itawasaidia pale wamalizapo elimu zao kujajiri wenyewe na si kusubiri Serikali kuwajiri.

Mheshimiwa Spika, kuna njia nyingi za kuweza

kuwawezesha hawa vijana waliomaliza vyuo na kufaulu vizuri. Nashauri ungewekwa utaratibu mzuri wa kuwapatia mikopo midogomidogo kutoka kwenye mabengi yetu au kupitia bajeti ya Wizara, Serikali iweke utaratibu huo ili waanzishe miradi midogomidogo, kwa njia nyingine watakuwa wamejajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, tunaweza kuweka utaratibu wa kuchukua vyeti vyao vya vyuo walivyomaliza yaani (*original certificate*) vikawa kama dhamana kwenye hayo mabengi ambayo watapatiwa hiyo mikopo ama kwa Serikali kupitia Wizara husika kufanya hivyo itawasaidia.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu utasaidia sana pale tu Serikali itakapokaa na haya mabengi na kuzungumza nayo na kuangalia mahali pa kuboresha utaratibu huu ambao Serikali kupitia Wizara watakuwa wameshatenga fedha za kutosha kutatua tatizo hili kwani tatizo hili la kukosa ajira likizidi ni hatarishi kwa siku za usoni.

Mheshimiwa Spika, pia kutokana na tatizo la vijana kukosa ajira tuna mifano mbalimbali toka nchi nyingine kwa matatizo kama haya ya kuwa na vijana wengi waliosoma na kukosa ajira, kumesababisha kutokea vurugu na uvunjifu wa amani na nchi kuingia katika majanga makubwa. Hatma ya hawa vijana na tatizo hili lazima lipewe kipaumbele kwani nguvu kazi kubwa ya Taifa ambayo ingekuwa na ajira, ingefanya uzalishaji mkubwa na kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili kupatiwa ufumbuzi linawezekana sana tukiamua kuweka mkakati wa kitaifa wa kutokomeza tatizo hili kama tufanyavyo kwenye matatizo mengine na kuweka mikakati ya kitaifa kuyamaliza matatizo kwa kutenga fedha kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya uvuvi ina changamoto nyingi sana kutokana na umuhimu wake, ikiboreshwa na kutengewa fedha za kutosha itasaidia kuchangia pato la nchi kwa kiasi kikubwa sana. Hapa nazungumzia kama tukiweza kuboresha usimamizi wa meli za kigeni za uvuvi zinazolingia

hapa nchini na kufanya uvuvi haramu. Kwa kuipatia Wizara fedha za kutosha, itasaidia kuchangia pato la nchi kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, hapa nazungumzia kama tukiweza kuboresha usimamizi wa meli za kigeni za uvuvi zinazolingia hapa nchini na kufanya uvuvi haramu. Kwa kuipatia Wizara fedha za kutosha, tutakuwa tumewawezesha kufanya doria za mara kwa mara na hivyo itasaidia sana kuwazuia wavuvi haramu wanaokuja na kuweka kambi katikati ya bahari na kuanza kuvua samaki kiholela huku kama Taifa hatufaidiki na chochote kutokana na uvuvi huo.

Mheshimiwa Spika, uvuvi haramu hauishii kwa wageni tu kuja kuvua bali pia kuna uvuvi unaoendelea hapa katika bahari na maziwa, uvuvi huo ni wa baruti. leleweke kwamba wananchi wanaofanya uvuvi huo wanahitaji kuelimishwa ili kujua athari za uvuvi huo na si kuwakamata na kuwachukulia hatua za kisheria tu kwani kufanya hivyo haitoshi bila kuwapa elimu ya kuachana na uvuvi huo haramu wa baruti.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kupitia Wizara iwezeshe kifedha na iweke mikakati ya kuwekeza katika sekta ya uvuvi kwa kujenga viwanda vya kusindika minofu ya samaki ambayo itakuwa inasafirishwa kwenda nje ya nchi. Kufanya hivyo, itasaidia Taifa letu kukua kiuchumi na kuzalisha ajira kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naiomba Serikali kutoa elimu kwa wananchi kuepuka kukata miti kandokando ya vijito na maziwa kwani kufanya hivyo ni kuharibu mazingira na kuleta mmomonyoko wa ardhi. Vilevile Serikali iwekeze fedha za kutosha katika suala zima la kuwainua wavuvi wadogo wadogo ili na wao waweze kufanya uvuvi wa kisasa na kuwaletea tija na manufaa.

Mheshimiwa Spika, pia itenge fedha kwa Wizara hii kufanya uvuvi wa kisasa na kuwaletea tija na manufaa. Aidha, itenge fedha kwa Wizara hii ili iweze kufanya tathmini katika mito mbalimbali na kugundua samaki wa aina gani

tuliokuwa nao kwani katika mito yetu kumekuwa na samaki wa aina mbalimbali ambao wangeweza kusaidia kunyanyua pato la mwananchi wa kawaida na Taifa kiujumla kwa kuweka mkakati wa kuboreshwa kwa uvuvi huo.

Mheshimiwa Spika, sekta nzima ya mifugo imekuwa na matatizo yake pia kwani ni kama imesahaulika kwa kutozingatia na kuhamasisha ufugaji wa kisasa ambao ungeleta tija kwa wananchi wetu pamoja na Taifa kiujumla. Serikali inahitaji kutenga fedha za kutosha kwa Wizara hii ili kuweza kufikia malengo katika sekta nzima ya mifugo ili tuweze kuzalisha nyama bora na kuuzwa nje ya nchi ili kuliingizia Taifa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, inafanya kazi zake vizuri lakini Wizara hii imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo hazina budi kuchukuliwa hatua za haraka kuzitatua kwa Serikali kuiongezea nguvu na fedha Wizara hii ili.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa vyuo vya Serikali vilivyojikita katika kutoa shahada za sayansi na uhandisi hapa nchini ni Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson cha Arusha, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Mbeya. Vyuo hivi vina wataalam wengi wenye sifa za kihandisi na wanaweza kubuni vitu mbalimbali na kufanya tafiti zinazoweza kuwa na manufaa kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, ili kuepuka kutegemea wataalam kutoka nje ya nchi, hapa nashauri Serikali kuweka utaratibu wa kuwaunganisha wataalam na wabunifu kutoka vyuo na taasisi hizi na watumiaji wa utaalum huo katika jamii. Aidha, kwa kuwa taasisi hizi zinafanya kazi zinazofanana, ziunganishwe kwenye mtandao ili kubadilishana uzoefu na kukabiliana na changamoto mbalimbali kwa pamoja na Serikali kutenga fedha zaidi ili kuweza kujengwa vyuo hivi zaidi ili kuwezesha kupata wataalam wengi katika fani hiyo.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa sekta ya umeme ni

mkubwa sana lakini katika Taifa letu bado hali ya upatikanaji wa umeme siyo wa kuridhisha na hii inatokana na sababu mbalimbali ambazo zimekuwa zikisababisha hali hiyo kutokea ikiwemo ya mabadiliko ya tabia nchi yanayopelekea ukosefu wa mvua za kutosha na hivyo kuathiri mitambo ambayo inatumia maji.

Mheshimiwa Spika, haishangazi kusikia *TANESCO* ina hali mbaya kifedha kwa sababu tangu Shirika hilo lianzishwe mwaka 1964 limeshindwa kutoa huduma ya umeme kwa walau nusu ya Watanzania. Hata hao waliounganishiwa, hawapati umeme wa uhakika. Wizara inayoismamia *TANESCO* imeshaongozwa na Mawaziri 21 na Makatibu wakuu 18. Hoja za baadhi yao ni Shirika hilo kuzidiwa kimajukumu, ikiwamo mzigo wa madeni unaolikabili Shirika hilo tangu awali na mpaka sasa.

Mheshimiwa Spika, hofu iliyopo hapa ni pale ifikapo miezi ya kiangazi ya Agosti mpaka Oktoba, hatutaweza kuzalisha sehemu kubwa ya umeme utokanao na maji na hivyo kutegemea umeme unaozalishwa kwa gesi na mafuta tu. Hofu nyingine inatokana na ukwei kwamba wazabuni wanaoiuzia *TANESCO* mafuta na gesi wanaidai kiasi kikubwa cha fedha na endapo watasimamisha kutoa huduma ya gesi na mafuta katika kipindi ambacho hakuna maji ya kuzalisha umeme wa kutosha basi ifahamike kwamba nchi nzima itaingia gizani.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukosefu wa maji na hofu ya madeni, kuna suala moja limesahaulika kwa muda mrefu na kujikuta umeme mwingi unaozalishwa hupotea njiani na mwingine kushindikana kusafirishwa kwenda kwa watumiaji. Ni ukweli usiopingika kuwa Serikali imefanya juhudi na gharama kubwa sana katika sekta ndogo ya uzalishaji umeme lakini naishauri kuweka mkakati kabambe ili umma uweze kufaidika kwa kuboresha mfumo wa usafirishaji mpaka kwa mtumiaji wa mwisho.

Mheshimiwa Spika, matatizo yatokanayo na sekta hii yamekuwa kero kubwa kwa wananchi. Tatizo la

kukatikakatika kwa umeme kusikokuwa na taarifa yoyote, limekuwa la kudumu na bado halijapatiwa ufumbuzi. Si jambo zuri kwa Taifa letu kuwa na migao ya umeme isiyokuwa rasmi.

Mheshimiwa Spika, hali hii inaonyesha kama hatutaki kubadilika kwa kujifunza mbinu walizotumia nchi nyingine kuepukana na adha hii. Ikumbukwe umeme una umuhimu mkubwa sana katika nchi yoyote ile. Katika nyanja za kukuza uchumi, bila umeme maofisini kazi zinazorota, mahospitalini wagonjwa huhatarisha maisha yao, viwanda havitazalisha ama uzalishaji utapungua na kushusha uchumi wa nchi na mashuleni na vyuoni wanafunzi hawatajismea nyakati za usiku.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itilie mkazo katika hilo ili tuondokane na matatizo haya na hata ikionekana njia hii ya uzalishaji umeme wetu ndio tatizo basi zifanyike juhudi za makusudi kupata njia mbadala.

Mheshimiwa Spika, leo hii tumesikia *TANESCO* imeshindwa rufani ya kesi iliyokuwa inapinga kullipia Kampuni ya *Dowans* kwa maana hiyo *Dowans* inatakiwa ilipwe. Naishauri Serikali kuliangalia hili kwani *TANESCO* haina uwezo wa kulipa fedha hizo vinginevyo mzigo huu wanaweza kutupiwa wananchi katika njia ya kupandishwa bei ya umeme na kugeuka kuwa mzigo kwa wananchi. Serikali haina budi kuchukua hatua thabiti kwa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imebarikiwa kuwa na vyanzo vingi vya kuzalisha umeme ikiwemo gesi asilia, makaa ya mawe na upepo. Vyanzo hivi vikitumiwa vizuri, hakika suala la upungufu wa umeme litapungua kama si kwisha kabisa kwani umeme utakaozalishwa utaweza kuwafikia wananchi wengi zaidi ikilinganishwa na idadi iliyopo kwani kwa sasa ni asilimia 17 tu ya Watanzania ndiyo wanapata umeme na kati ya hao asilimia 14 ni wale wanaoishi vijijini na kati yao asilimia tatu tu ndiyo wanapata umeme. Hiyo inadhihirisha kuwa usambazaji umeme hauna uwiano mzuri hali inayopaswa kurekebishwa.



Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa kiwango cha asilimia 17 kwa nchi ni kidogo lakini asilimia tatu kwa Watanzania wanaotumia nishati hii vijijini pia bado hairidhishi. Hali hii inapingana na mpango wa Taifa wa Maendeleo Wa Muda Mfupi ambao unataka ifikapo mwaka 2016 wananchi wa vijijini wafikiwe na umeme kwa asilimia 16.

Mheshimiwa Spika, haimaanishi vijijini hakuna umuhimu wa kuwapo na umeme kwa kuwa shughuli nyingi hufanyika mijini ila kupeleka umeme vijijini kutaweza kuinua uchumi wa vijijini na kupata manufaa ya kiuchumi na kijamii vijijini na mijini. Napenda kuishauri Serikali kuongeza bajeti ya Wakala wa Umeme Vijijini ili wananchi wengi zaidi waweze kunufaika na huduma hii muhimu kwani uwepo wa umeme kutasaidia kuongeza thamani ya mazao yapatikanayo vijijini kwa kuwa na viwanda vya usindikaji kuliko ilivyo hivi sasa mazao yapatikanayo vijijini yamekuwa yakiharibika kabla ya sokoni. Vilevile Serikali ingeweka nguvu za ziada kwa kuwasambazia umeme unaotokana na nguvu ya jua (*solar*) wakati tukisubiri gridi ya Taifa kufika katika maeneo vya vijijini.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali sasa kuweka mkakati mzuri wa kutatua matatizo haya yanayoikabili *TANESCO* kwa kuipa Wizara fedha za kutosha ili Shirika hili nalo liweze kufanya kazi zake vizuri na kuwafikia wananchi wote kwa kuwapatia umeme wa uhakika na kufanya malengo yao kukamilika kwani mzigo wa madeni unaolikumbwa Shirika hili ni mkubwa na hakuna budi Serikali kuingilia kati na kuliokoa Shirika hili. Pia Serikali iweze kuilipa *TANESCO* madeni yake kwani katika wadeni sugu wanaodaiwa na *TANESCO* pia Serikali ipo.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wamekuwa wakisahaulika, wamekuwa hawapati elimu ya kutosha katika masoko, masuala ya utafutaji, uchimbaji, uongezaji thamani na kufanya utendaji wao wa kazi kuwa mgumu. Naiomba Serikali iweke utaratibu utakaowawezesha wachimbaji wadogo kupata mafunzo hayo muhimu.

Mheshimiwa Spika, pia wamekuwa na uhaba wa

maeneo ya uchimbaji kwani maeneo mengi yamechukuliwa na wachimbaji wakubwa na baadhi yao wanayamiliki maeneo hayo bila kuyafanyia kazi hali inayowanyima fursa wawekezaji wadogo. Wachimbaji hawa wadogo wamekuwa hawana vitendea kazi vya kutosha kutokana na kodi kuwa kubwa na kushindwa kumudu ilhali wawekezaji wakubwa wanapewa misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kuwafikiria wachimbaji hawa ili nao wapewe misamaha ya kodi katika vifaa kazi na ikibidi Serikali kupitia bajeti ya Wizara kuwawezesha wachimbaji hawa ili na wao wanyanyuke kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, bila kusahau, naiomba Serikali iweke mkakati wa kuainisha maeneo ya wachimbaji wakubwa na wadogo kulingana na wingi wa madini ili kuepusha mwingiliano. Vilevile Serikali iweke mfumo utakaosaidia kujua mchango wa uchimbaji mdogo kwenye pato la Taifa. Hii itasaidia kuweka mikakati ya kuongeza juhudi.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (*TMAA*) wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana na kusaidia kupungua kwa utorohaji wa madini hapa nchini na kuongeza pato la uchumi wetu. Pamoja na kazi nzuri wanayoifanya lakini bado kuna changamoto mbalimbali kama elimu ndogo kwa wachimbaji wadogo hasa katika masuala ya usimamizi wa mazingira na kushamiri kwa biashara haramu ya madini na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuifanya Wakala iwe mamlaka na kuitengea fedha za kutosha ili kuipa nguvu na wigo mkubwa zaidi wa ufanyaji kazi wake katika kulisaidia Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa moyo wa dhati na furaha kubwa nakupongeza wewe Spika kwa kubuni mfumo huu mpya wa kuboresha uwakilishaji wa bajeti ya Serikali ambao umetuhusisha na sisi Wabunge katika kutayarisha bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri wa Fedha na Naibu Waziri wake na wataalamu wote wa Wizara ya Fedha kwa jinsi walivyotuletea bajeti inayolisogeza Taifa kutoka hapa tulipo na kusonga mbele kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, bajeti ni mapato na matumizi, ili tuwe na mapato ya kutosha ni lazima tuhakikishe tunalinda mianya yote inayowezesha mapato yetu ya nchi kupotea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madini, Tanzania tumejaliwa kuwa na madini ya aina nyingi sana, nina uhakika kabisa iwapo tungeziba mianya yote ya kupoteza mapato kutokana na madini yanayoibiwa na kusafirishwa nje ya nchi kinyume, Taifa letu lingepata mapato makubwa sana na kufanya uchumi wa nchi hii kukua kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini iliipa kazi *TMAA* ya kukagua, kusimamia na kudhibiti mianya yote ya kupoteza mapato kutokana na madini kuibiwa na kodi stahili kutokulipwa. Kwa muda mfupi ambao *TMAA* imekuwa ikifanya kazi hii, tumeona mafanikio makubwa sana. Mfano, *TMAA* ilianzisha Madawati ya Ukaguzi wa Madini kwenye viwanja vya ndege vya Kimataifa vya Kilimanjaro, Dar es Salaam na Mwanza.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kifupi tu cha kati ya kipindi cha kuanzia Oktoba, 2012 na Aprili, 2013, madini yenye thamani ya takribani shilingi bilioni 13.12 yalikamatwa yakisafirishwa nje ya nchi na wafanyabiashara 11 kinyume cha sheria. Kazi inayofanywa na *TMAA* ni kubwa na inaokoa mapato ya Taifa kwa kiwango kikubwa sana. Hizo shilingi bilioni 13.12 nilizozitaja hapo juu ni mfano mmoja tu lakini wameokoa mapato yaliyokuwa yanapotea kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naisihi Serikali kwa unyenyekevu *TMAA* ijengewe uwezo wa kibajeti na rasilimali watu ili iweze kuwepo kila mahala ambapo panaweza pakawa na mwanya wa kuvujisha mapato mfano, bandarini, mipakani ili kudhibiti madini yetu yasisafirishwe nje isivyo halali na kutupunguzia mapato.

Mheshimiwa Spika, *TMAA* itengewe uwezo wa kibajeti ili iende sambamba na ukuaji wa sekta ya madini nchini na *Specialized Auditing Agency*. Niisihi Serikali kupitia Wizara ya Fedha iitengee fungu maalum *TMAA* ili ikapanue wigo kwani ili upate mapato ya uhakika mahala popote ni lazima utumie fedha.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naiomba Wizara ya Fedha itafakari hili, ahsante sana.

**MHE. NASSIB S. OMAR:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja ya Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Benki ya Kilimo; uchumi wetu unategemea sana kilimo, lakini bado kilimo chetu kimebakia kile kile cha kutegemea jembe la mkono. Bado wakulima wengi wadogo wadogo hawapati pembejeo za kutosha. Pia kuna upungufu wa maghala na mashine za kuvunia mazao kama mpunga.

Mheshimiwa Spika, ili kuondokana na matatizo haya, kuna umuhimu wa kuanzisha Benki ya Kilimo ambayo itaweza kutoa mikopo yenye riba ndogo na mkopo wa muda mrefu. Nchi nyingi duniani zimeanzisha Benki ya Kilimo. Mfano mzuri ni nchi ya Italy ambayo imeanzisha Benki ya Kilimo iitwayo *Bank Agrecole*.

Mheshimiwa Spika, benki hii hutoa mikopo ya muda mrefu na yenye riba ndogo. Mikopo hii, imesaidia sana kukua kwa kilimo Italy. Hawana upungufu wa chakula na vile vile wanauza chakula nje ya nchi yao na kuongeza pato la fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia rushwa katika Taasisi ya *TRA* wanashirikiana na wafanyabiashara ili kuikomeshwa Serikali kodi halisi. Wengi wa Maafisa wa *TRA* ni mamilionea kutokana na kuibia Serikali kodi. Serikali lazima ichukue hatua za dharura ili kudhibiti suala hili. Maofisa wabadilishwe nafasi zao za kazi ili kuepusha Maafisa hawa kukaa katika maeneo ya kazi kwa muda mrefu.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kwa njia ya maandishi kumpongeza Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dkt. William Mgemwa na Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Janeth Mbene na Mheshimiwa Saada Salum Mkuya, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii ambayo imewajali sana wananchi wenye kukabiliwa na umaskini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupanda kwa petroli na dizeli; napenda kuikumbusha Serikali yetu ya CCM kuwa mafuta ya petroli na dizeli ni nishati inayotumiwa na wananchi wa aina zote wenye uwezo mdogo na mkubwa hata maskini katika kujitafutia riziki zao.

Hivyo kupanda kwa bei ya nishati hizi ni kuwafanya Watanzania walio wengi washindwe kutumia miundombinu hii, mfano magari kwenda shambani kubeba mazao, matrekta kulima na kadhalika. Nashauri Serikali itafute vyanzo vingine vya kuongeza pato la Serikali ili mafuta ya petroli na dizeli bei ipunguzwe, nategemea kupata maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuondoa Kodi ya Mapato kwenye mishahara ya wafanyakazi; napenda niipongeze Serikali kwa kupandisha mishahara ya wafanyakazi wote nchini kila mara. Kupitia sherehe za Mei Mosi, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Serikali ya Muungano wa Tanzania alitangaza kupanda kwa mishahara kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri; tatizo la mishahara kutotosheleza mahitaji muhimu ya wafanyakazi ni kutokana

na makato makubwa ya kodi ya mapato kwenye mishahara yao. Pamoja na kupunguza asilimia moja bado tatizo liko pale pale.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kuondoa kodi ya mapato kwenye mishahara kwani kodi wanayolipa kupitia bidhaa mbalimbali wananunua inatosha sana. Napenda kujua Serikali itaondoa kodi hii kwenye mishahara lini ama ipungue kubaki angalau asilimia tano?

Mheshimiwa Spika, kuhusu posho ya mazingira magumu kwa wafanyakazi wote nchini; napenda kuifahamisha Serikali kuwa wafanyakazi wote wanafanya kazi kwa mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, hivyo ni vema wote wapewe posho ya mazingira magumu ili kuwapa moja ya kazi wakiwemo Walimu, Wauguzi na kadhalika tena mpango huu uanze bajeti hii 2013/2014, nina imani kubwa watapata moyo wa kujituma na tutaondoa rushwa na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wafanyakazi kupatiwa nyumba za kuishi; napenda kuiomba Serikali kutenga bajeti kubwa kwa ajili ya kujenga nyumba za kutosha kwa wafanyakazi wote hususani walimu na wauguzi ambao wengi wao hufanya kazi vijijini.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua mkakati wa Serikali kuhusu kutoa tenda ya ujenzi kwa Mashirika ya Serikali mfano, *NSSF*, *PPF*, *LAPF* na kadhalika ili kuondoa kabisa kero kubwa ya nyumba za kuishi wafanyakazi. Nangojea majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Hospitali ya Rufaa, Mkoa wa Singida; napiga magoti kwa niaba ya wana Singida wote kwa Serikali yangu ya CCM ili itufikirie kututafutia fedha milioni mia nane tu ili kumalizia jengo ambalo likikamilika Hospitali hii itaanza kufanya kazi ili vifaa tulivyopewa na wahisani kupitia Mkuu wa Mkoa Dkt. Parseko Kone visiharibike. Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nimalizie mchango wangu kwa kuunga mkono hoja nikitegemea kuwa hoja zangu zitafanyiwa kazi na nitapewa majibu.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukuaji wa uchumi; Sekta ya mawasiliano imekuwa kwa 20.6% (2012), imechangia 2.3% tu katika pato la Taifa; Sekta ya Kilimo imekuwa kwa asilimia ndogo, lakini imechangia 24.7% katika pato la Taifa (2012).

Mheshimiwa Spika, hii ni dalili mbaya sana katika ukuaji wa uchumi kwani haiwezekani maskini ndiyo wanalipa kodi sana ikilinganishwa na wawekezaji wa Makampuni makubwa kama ya simu (*Tele com Industry*).

Mheshimiwa Spika, pamoja na wakulima kuchangia 24.7% ya pato la Taifa, lakini bado wanazalisha na kuuza mazao yao kwa hasara, Sheria haziko rafiki kwa wakulima, Sheria zinalenga kuwalinda wawekezaji hasa wa viwanda na kuwaacha wakulima wakapata hasara na kuendelea kuwa maskini.

Mheshimiwa Spika, mfano, wakulima wa miwa Wilaya ya Mvomero wamekuwa wanaiomba Serikali iruhusu kujengwe Kiwanda cha Sukari kingine kwani kilichopo sasa cha Mtibwa *Sugar*, kimeleemewa, hakina uwezo wa kununua miwa yote inayozalishwa na wakulima, lakini Serikali inang'ang'ania Sheria kandamizi kwa wakulima ambayo inaeleza hairuhusiwi kujenga kiwanda kingine karibu na kiwanda cha awali.

Mheshimiwa Spika, wakulima wamekuwa wakipata hasara kwani pamoja na kwamba fedha za kilimo wamekopa kwenye Taasisi mbalimbali za fedha, wanashindwa kurejesha mikopo hiyo na kuendelea kuwa maskini.

Mheshimiwa Spika, pato la Taifa; limekuwa

likiongezeka kwa asilimia ndogo sana ikilinganishwa na rasilimali za nchi tulizonazo.

- Mwaka 2011 pato la Taifa lilikuwa 6.4%;
- Mwaka 2012 pato la Taifa lilikuwa 6.9%;
- Mwaka 2013 pato la Taifa linatarjiwa kuwa 7.0%; na
- Mwaka 2014 pato la Taifa linatarajiwa kuwa 7.2%.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tunatekeleza mpango wa maendeleo wa miaka mitano ambao tunatekeleza kila mwaka pia tuna program mpya *President's Delivery Bureau (PDB)* unaojulikana kama *Big Results now*, lakini mbona tumejiwekea malengo kidogo kwenye ongezeko la pato la Taifa kwani inaonesha bado inajiwekea malengo sawa na kabla hatujapitisha hii mipango kabambe ya kukuza uchumi wa nchi na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, kutoza ushuru wa bidhaa wa 14.5 kwenye huduma zote za simu (*call mobile phone services*) za simu ya mkononi badala ya muda wa maongezi tu (*air time alone*).

Mheshimiwa Spika, ongezeko hili ni kubwa sana, huku ni kuwanyima wananchi haki ya kupata mawasiliano hasa ya *Internet* na huduma za fedha za *M-pesa*, *Tigo-pesa*, *Airtel money* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuanzisha huduma za *M-pesa* zililenga kuwasaidia wananchi wa kipato cha chini ambao hawana *access* na huduma za mabanki makubwa. Sasa leo nashangaa kwa nini huduma za *M-pesa* ziwekewe kodi kubwa, hivyo ambazo zinakwenda kumwathiri mlaji ambaye ni maskini wa Tanzania. Wakati matajiri wanatumia



Mabenki kuweka na kutumia fedha bila kukatwa hizo *excise duty*. Haiwezekani huyu maskini ndiye achangie gharama za elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, gharama za simu zimepanda maradufu ikilinganishwa na Nchi za East Afrika ambao ni asilimia 10 tu, Tanzania tumetoka kwenye 12% mwaka jana sasa tunapandisha iwe 14.5%.

Mheshimiwa Spika, sekta ya Madini, madini yanayotoroshwa bila kulipiwa kodi watuhumiwa wakikamatwa wanatoroshwa, bandarini makontena hayalipiwi kodi inayostahili. Nashauri Serikali iweke mkazo kwenye ukusanyaji wa kodi wenye tija iache kuwabana watazania kutumia huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Kupunguza kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato ya ajira kutoka 14%.naomba tupunguze kwa asilimia nne iwe 10% kupunguza 1% haipunguzi makali ya maisha kwa mfanyakazi.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, naipongeze Serikali pamoja na Bunge kwa kuja na wazo na mpango mpya wa mzunguko wa Bajeti ya Serikali kuanzia mwezi Aprili mpaka Juni, ili fedha ziweze kupelekwa katika uwekezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali nchini mapema mwanzoni mwa mwezi Julai kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, naipongeze sana Serikali kwa kuja na mpango mzuri wa kuwa na vipaumbele vichache vyenye kuweza kuleta matokeo sasa *Big results now (BRN)*:-

(i) Miundombinu; nishati, usafirishaji na barabara, reli, viwanja vya ndege, usafiri wa majini, TEHAMA, maji safi na maji taka na umwagiliaji.

(ii) Viwanda vinavyotumia malighafi za ndani na kuongeza thamani, viwanda vikubwa vya mbolea na saruji,

viwanda vya kanda maalum za kiuchumi, kielektroniki na TEHAMA.

(iii) Kilimo cha mazao ya chakula na biashara, malighafi ya viwandani, ufugaji uvuvi na misitu.

(iv) Maendeleo ya rasilimali watu.

(v) Uendeshaji wa huduma za utalii biashara na fedha.

(vi) Huduma za jamii kuboresha upatikanaji na ubora wa huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali wa *Big Results Now (BRN)* ni ubunifu muafaka, ambapo sekta chache za vipaumbele ndiyo zimepewa kipaumbele. Sekta hizi kimsingi kwa hakika zikiimarishwa zitaleta mapinduzi ya hali ya juu katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kwa kiwango kikubwa imejaaliwa kuwa na rasilimali ambazo zilikuwa chachu ya mapinduzi ya viwanda katika nchi za wenzetu za Ulaya mojawapo ya rasilimali zilizochangia kuleta mabadiliko haya ni uwepo wa makaa ya mawe na chuma. Nchi yetu imejaliwa kuwa na makaa ya mawe na madini ya chuma huko Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, imani yangu kabisa ni kwamba, tukihakikisha uzalishaji wa umeme ukiimarishwa na kuwa wa uhakika, wawekezaji katika sekta ya viwanda wataongezeka na kuongeza ajira kwa vijana wetu ambao kila kukicha wanatafuta ajira.

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo ambayo inaajiri Watanzania walio wengi, ni busara kabisa kutenga kiasi kikubwa cha fedha ili kuwaboresha tija katika kuinua uzalishaji na kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kheri kwa Serikali yetu

kuweka kipaumbele katika nchi yetu kwa siku za karibuni na dunia kwa ujumla inakabiliwa na mabadiliko ya tabianchi yamesababisha mvua zisizokuwa za kuaminika na hivyo kuathiri mazao ya chakula na biashara na hivyo mazao haya kunyauka na kuathirika kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nchi za Ulaya katika hatua za mwanzo za kuanzishwa kwa iliyokuwa Jumuiya ya Uchumi ya Nchi za Ulaya zilizoanza katika kile kilichoitwa *Coal and Steel Cooperation of Europe*.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri kabisa sisi Mwenyezi Mungu ametujalia kuwa na Makaa ya Mawe na Chuma, lakini hatua madhubuti hazijachukuliwa kuhakikisha kwamba Taifa la Tanzania linakuwa miongoni mwa Mataifa yanatoa chuma kwa wingi ulimwenguni.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji madhubuti wa chuma utasaidia kwa kiasi kikubwa katika kuleta mapinduzi ya viwanda nchini. Uzalishaji wa uhakika wa chuma unakwenda sambamba na uzalishaji wa umeme utokanao na makaa ya mawe yanayotumika katika kuzalisha chuma cha pua (*steel*).

Mheshimiwa Spika, ni jambo jema sana kwa Wizara ya Fedha kuona uwezekano wa kuongeza fedha zaidi katika sekta ya maji. Maji ni uhai na maji yanahitajika katika maisha ya kila siku ya mwanadamu na viumbe vyote vilivyo hai. Naishukuru Serikali kuongeza fedha.

Sensa ya watu na makazi imefanyika mwaka 2012 na kuonesha kwamba, Tanzania ina idadi ya watu wapatao milioni 44.9. Jambo hili ni vema likaangaliwa kwani ulipukaji wa ongezeko la watu kiholela litakuwa na athari kubwa katika ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kuwa na mpango wa kuhakikisha kuwa kunakuwepo na upunguzaji wa vifo vya akinamama na mtoto, lakini niishauri Serikali ije na mpango kabambe wa kuboresha elimu juu ya uzazi wa

mpango ili kudhibiti ongezeko la watu. Niombe Serikali itoe fedha za kusaidia ujenzi wa ofisi na nyumba za kuishi katika maeneo mapya ya kiutawala katika Mikoa na Wilaya mpya.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kupeleka umeme maeneo ya vijijini. Naamini hatua hizi za Serikali zitasaidia kwa kiwango kikubwa kupunguza uhamiaji wa watu kutoka vijijini kukimbillia mijini.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya huduma ya mawasiliano ya simu za mkononi kwa kuanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa wote. Wilaya ya Mbogwe imeahidiwa kujengewa minara ya mawasiliano katika Kata za Mbogwe, Iponya na Bukandwe. Kwa kifupi naipongeze Serikali kwa kuja na Bajeti nzuri inayojali wananchi wetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya fedha kuhakikisha kwamba inaweka mkazo katika kuliwezesha Shirika la Maendeleo (*NDC*) katika harakati za kuhakikisha kwamban uzalishaji wa chuma ili kuiokoa nchi hii na kansa inayoweza kulemaza uchumi wa nchi katika biashara ya vyuma chakavu.

Mheshimiwa Spika, vyuma chakavu ni biashara ambayo imekuwa ikishamirisha uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara, madaraja, reli na hata kwenye majengo na Bandari.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Wizara ya fedha katika kupanga vipaumbele kujumuisha uzalishaji mkubwa wa chuma kule Liganga na Mchuchuma kwani upatikanaji wa chuma hapa nchini kutasimamisha kwa kiasi kikubwa biashara ya vyuma chakavu.

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa chuma utasaidia kuleta mapinduzi ya viwanda pamoja na kukomesha biashara ya uharibifu unaotokana na biashara ya vyuma chakavu.

Mheshimiwa Spika, reli zetu na ujenzi wa Bandari, Majengo, Madaraja, Viwanda vikubwa vitashamiri nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, chuma kwa Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, uwiano wa fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Halmashauri na kuwepo kwa wataalam husika kwa utoshelezi wa idadi na umahiri.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa *disbursement* licha ya kufuata utaratibu wa *cash budget* hazizingatii uwepo huo wa wataalam, hasa katika Halmashauri za Wilaya. Utaratibu huu unaitia hasara Serikali na Taifa kwa kuwa utekelezaji wa miradi hiyo bila rasilimali watu sahihi hauwezi kutuhakikishia *value for money*. Mpango wa maendeleo wa miaka mitano kuzingatia hitaji hili. Pale ambapo wataalam wenye sifa wameshiriki na wakasababisha hasara vifungu vya *Professional Ethics* vitumike.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, upelekaji wa fedha uzingatie uwepo wa wataalam. Mikoza inaweza kutumia utaratibu wa *resource sharing* miongoni mwa Wilaya zake kwa ku-*mobilize* wataalam kutoka Wilaya zisizokuwa na *active projects* ili watumike kule wanakohitajika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa Programu ya Mtwara *corridor* Programu ya Mtwara *corridor* inahusisha miradi kadhaa ikiwemo:-

- Bandari ya Mtwara;
- Reli – Mtwara – Mbamba Bay;
- Bandari – Mbamba Bay;
- Barabara ya Mtwara, Tunduma, Songea, Mbamba bay;
- Miradi ya Makaa ya Mawe;
- Miradi ya Chuma;

- Miradi ya Urani; na
- Miradi ya Gesi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji uwiano na mahusiano barabara katika kutekeleza Programu hii. Kwa sasa kila Wizara (*Sector Ministry*) inatekeleza miradi yake, hivyo kukosa *Coordination* – mradi upi unaanza lini unakwisha lini unahusianaje na kuanza na kukamilika kwa mwingine na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ushauri; kiundwe chombo mahsusi kwa ajili ya kuratibu utekelezaji wa program ya Mtwara *corridor*, jambo ambalo litaihakikishia pia Serikali kuwa na *one stop centre* kwa ajili ya uratibu, lakini pia kujibu hoja zote zinazohusu kila mradi katika Programu na kuimarisha utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa mfano, kukamilisha uzalishaji wa shehena zilizotajwa hapo juu bila kukamilisha, reli na barabara ni tatizo la wazi.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ukusanyaji wa kodi; eneo hili ni muhimu sana kwa Taifa letu, lakini limebainika kwamba, watendaji wanaohusika na ukusanyaji wa kodi hususan *TRA* si waaminifu na hawana uchungu na nchi yao.

Mheshimiwa Spika, hivyo, naiomba Serikali kuweka mfumo sahihi wa mtandao wa kompyuta utakaoweza kuwabana watendaji wote ili pesa zetu zibaki salama, suala la kupenya mapato bado lipo maeneo ya Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vyanzo vya ukusanyaji wa mapato naipongeza Serikali kwa kuongeza vyanzo vipya vya mapato. Hata hivyo, bado naishauri Serikali kutafuta vyanzo vingine vya mapato pamoja na kodi mbalimbali, mfano, kuna watu wengi wanakodisha nyumba zao binafsi lakini hawalipi kodi.

Mheshimiwa Spika, kuna watu wanauza maji mengi tu, lakini hawalipi kodi, kuna viwanda vidogo vidogo vingi viko kinyemela nyemela vinafanya kazi kila siku tena viko mitaani, navyo vinasemekana havilipi kodi. Hivyo, naiomba Serikali kuweka mpango mkakati wa kuona kodi hizo zinakusanywa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la upelekaji wa fedha katika Wizara kwa wakati. Ni mpango mzuri wa Bunge na Serikali uliowekwa katika kipindi hicho cha mpangilio wa ugawaji wa fedha. Lakini zoezi la kuboresha utendaji litakuwa halina maana iwapo fedha hazitapelekwa kwa wakati katika Wizara zetu. Naiomba sana Wizara ya Fedha kupeleka fedha kwa wakati na kama itatokea suala lolote ambalo litakwamisha utoaji wa fedha, ni vyema taarifa itolewe.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu nzima kwa kuandaa bajeti nzuri na yenye mwelekeo wa kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ushuru wa magari madogo, nashauri ile nia ya kuongeza ushuru wa magari madogo yenye umri wa zaidi ya miaka kumi isitekelezwe. Haya ndiyo magari ya watu wetu wa kawaida na hayaharibu mazingira. Misingi mizuri ya kodi hutozwa walio nacho kama ni kutozwa yatozwe magari mapya.

Mheshimiwa Spika, ushuru kwenye magari makubwa; ile nia ya kuongeza ushuru kwenye magari makubwa yenye umri wa zaidi ya miaka kumi, lisitekelezwe. Magari haya mazee ndiyo yananunuliwa na Watanzania wazawa na kutumika vijijini. Misingi ya kodi ni kukusanya kwa matajiri, ongeza kwa wenye kununua magari mapya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu VAT kwenye shughuli za utalii; nashauri mabadiliko yawe *effective* tarehe 1 Januari, 2014 badala ya 1 Julai, 2013. Hii ni kwa kuwa katika shughuli hii mikataba na malipo hufanywa mapema na wateja wa mwaka/msimu huu wamekwisha *contract* na kulipa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VITA R.M. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza Waziri na Manaibu Waziri, Katibu Mkuu, Kamishna wa Bajeti wa Wizara hii ya Fedha na Uchumi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya ku- *manage* mapato, matumizi na uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanyika, lakini ushauri wangu Serikali iongeze utengaji wa fedha katika kusomesha wataalam wa madini na mafuta na *gas* katika eneo la sheria katika sekta hii na wale wa uchimbaji na uendelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna uvumbuzi wa madini mengi na wawekezaji ni wengi, lakini inaonekana hakuna rasilimali watu wa kutosha kukabiliana na kazi za sekta hii muhimu katika kununua mapato na uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Serikali itufafanulie kwa kina ni namna gani Serikali imejipanga kulinda rasilimali ya madini yetu kwa kuwa na wataalam wa kutosha kuangalia madini, mafuta na gesi hayatoroshiwa bila ya kulipiwa ushuru na kusimamia uwazi wa Taarifa zake. Hasa tukizingatia makampuni ya kigeni yana wataalam wa kiwango cha juu na itasimamia wao wapate zaidi.

Mheshimiwa Spika, mkutano wa *G8* uliofanyika mwezi Juni, 2013 nchini Uingereza ulitoa kauli ya kuhakikisha kuwa na uwazi wa uzalishaji na ulipaji kodi kwa makampuni na Serikali za nchi yenye madini, gesi na mafuta.

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tuna Sheria mbili za Madini, Mafuta na Gesi zinazo katazo la kutoa Taarifa. Katika sehemu ya tatu (iii) kifungu cha (25), Sheria ya Uchimbaji Madini ina katazo la kutotoa taarifa wazi za Makampuni ya Madini. Lakini pia sehemu ya pili (ii) kifungu cha (10) uchimbaji wa gesi na mafuta kuna katazo la kutotoa taarifa za wazi za uchimbaji na uendelezaji wake wazi.



Mheshimiwa Spika, sasa Serikali inajipangaje kukabiliana na azma nzuri waliyoiona viongozi wa Mataifa makubwa kiuchumi duniani 98 na sisi tuvifute vifungu hivi ili kuondokana na kifungo hiki cha kutopata taarifa zilizo wazi ambazo zinaweza kusaidia makadirio yaliyo sahihi ya kodi zetu kisheria na kuongeza pato la Serikali.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu mwingine, Serikali ihakikishe mnakwenda kupeleka hitaji la nchi ya Tanzania la kisheria kwa nchi zote zilizokuwa zime-*list* katika *stock market and stock exchange*, kampuni ambazo zina miradi mikubwa ya uchimbaji madini, gesi, mafuta na mawasiliano katika nchi yetu, kuwa kama watauza *shares* au kuuza kabisa kampuni zao zilizopo Tanzania watambue kuwa watahitajika kulipa *Capital Gain Tax Tanzania* pia.

Mheshimiwa Spika, hili linawezekana nchi za wenzetu kama Nigeria wamefanya hivyo na wanafanikiwa. Lifanyieni kazi kuliko kusubiri na kwenda Mahakamani kabla ya kuweka angalizo hilo katika *stock market* hizo. Matokeo yake tutashindwa kesi na kupoteza mapato na gharama za kuendeshea kesi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwanza nipongeze utaratibu wa bajeti mwaka huu 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kuhusu misamaha ya kodi katika ukurasa wa 38 Serikali imeainisha changamoto zinazoendeleza upatikanaji wa fedha kutoka vyanzo vya mapato na kuchelewesha kupeleka fedha katika sekta husika.

Mheshimiwa Spika, pia Serikali imesema zitaendelea kutafutiwa ufumbuzi, lakini suala la misamaha ya kodi halijaainishwa ambapo linaendelea kwa kiasi kikubwa kuikoshesha Serikali mapato kama chanzo cha mapato, vile vile miongoni mwa changamoto hizo ni mfumuko wa bei na mabadiliko ya tabia nchi.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuondoa mfumuko wa bei wakati katika bajeti hiyo hiyo imeongeza bei ya mafuta na tunatambua kwamba, bei za mafuta ndizo zinazochangia kwa kiasi kikubwa mfumuko wa bei nchini.

Mheshimiwa Spika, pia mfumuko wa bei unachangiwa pia na kushuka kwa sekta ya kilimo, pia kunaongeza mfumuko wa bei na bila ya kuboresha miundombinu ya umwagiliaji sekta ya kilimo inaendelea kuporomoka siku hadi siku hasa tukiangalia kwamba, tunategemea sana mvua katika maeneo mengi ya kilimo nchini ambapo huwa kuna unafuu kunapokuwa na hali nzuri ya hewa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kupunguza kiwango cha bei ya mafuta iliyopo ili wananchi wa kipato cha chini waweze kumudu gharama za maisha. Pia Serikali kujielekeza zaidi kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji nchini ili kukuza zaidi sekta ya kilimo nchini. Pia kupunguza misamaha ya kodi angalau chini ya asilimia 1% ili kuongeza mapato ya nchi ikiwa ni moja kati ya vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho atueleze, tutaweza kupunguza misamaha ya kodi kwa kiwango gani baada ya michango ya Waheshimiwa Wabunge kulalamikia suala hili kwa muda mrefu ambalo ni moja kati ya vyanzo vinavyotusababishia kutokupata mapato ya kutosha nchini?

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba Serikali inaongeza wigo mpana kwa wawekezaji, lakini basi iwekwe kwa muda na sio mpaka mwekezaji anafika kuondoka na kuja mwingine katika sehemu hiyo hiyo moja, je hili Serikali hailioni?

Mheshimiwa Spika, kuhusu makontena Bandarini; mrundikanao wa makontena bandarini tatizo ni nini? Kauli za *TPA* na *TRA* zinatofautiana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti zilizopita tulijulishwa

kwamba, suala la urasimu bandarini linatafutiwa ufumbuzi kwa kuweka mtandao wa *Computer* Bandarini, ambao utawezesha watumishi kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi na haraka ili kuondoa usumbufu uliopo na kuwavutia wafanyabiashara wanaoendelea kuleta mizigo yao katika Bandari ya Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, mambo sio hayo urasimu bado unaendelea kuongezeka na wafanyabiashara wanaendelea kukerwa na huduma finyu zilizopo Bandarini, Dar es salaam na wengi kuamua kuacha kushusha mizigo yao kupitia bandarini hapo. Kwa maana hiyo basi kutokana na kuendelea na urasimu huo lazima tujiulize maswali yafuatayo:-

Je, ni uhaba wa eneo ndio kunaleta ucheleweshaji wa ukaguzi na upekuzi wa mizigo kwa wakati? Je, ni uhaba wa wafanyakazi wa Idara ya forodha? Je, ni miundombinu bado hajakamilika na kuridhisha? Je, ni kutokana na kukosa bidii ya kazi kwa watumishi husika? Je, ni kwa nini tunawanyonya wananchi wakiwemo wafanyabiashara wa kipato cha chini na kuwasababisha kutokuendelea na biashara zao kwa kuwalipisha (kiwango cha kusababisha *storage*) kodi wasizozitarajia kwa sababu za watumishi wa *TRA* au *system* bandarini au Kuzimika kwa umeme?

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kuyajibu maswali haya wakati wa majumuisho kwa Tanzania, tunaendelea kukosa kodi zaidi kwa wafanyabiashara walio wengi, wakubwa na wadogo kwa kuacha kuleta mizigo yao Bandari ya Dar es salaam kutokana na matatizo ya Idara ya forodha au *TRA* au Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu uliopo ndio unaoendelea kusababisha rushwa bandarini katika utaratibu wa kutoa mizigo. Kuendelea kukaa mizigo bandarini kunawasababisha ulaji watumishi wa Idara ya Forodha na kuendeleza malalamiko kwa wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Pato la Taifa; katika kukusanya mapato ya Serikali kuna mapato ya kodi na yale yasiyo ya kodi pia kukua kwa sekta ya kilimo nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetueleza kwamba itakusudia kuchukua hatua mbalimbali za kuimarisha mapato ya ndani yale ya kodi na yasiyo ya kodi nchini. Pia Serikali imetayarisha mwongozo wa ukaguzi wa ndani kwa kuzingatia viwango vya Kimataifa ambao utaleta ufanisi katika makusanyo ya mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Serikali kupitia bajeti hii imetujulisha kwamba, makusanyo ya mapato yasiyo ya kodi yamekuwa hayaridhishi kutokana na uwezo mdogo wa ukusanyaji na kukosa wataalam, vifaa duni na mifumo dhaifu ya ukusanyaji wa mapato ambayo huchangia upotevu wa mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo basi, tunajenga imani kwamba, kutakuwepo wataalam waliobobea, vifaa bora vinavyoendana na wakati ili makusanyo ya kodi yaweze kukusanywa kwa utaratibu unaofaa. Katika bajeti ijayo au kabla kama hotuba hii ilivyotamka kwamba ifikapo mwezi Julai, 2013 angalau mwezi Oktoba 2013 tuelezwe utaratibu uliofikiwa wa mwenendo wa maendeleo ya makusanyo ya kodi unavyoendelea na namna wataalam wanavyosimamiwa ipasavyo kuhusiana na ukusanyaji wa mapato hayo. Utekelezaji wa bajeti hii uendelee kujielekeza katika makusanyo hayo ili mapato ya nchi yaweze kuongezeka na kuondoa utegemezi uliotukabili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu pato la kila (mtu) Mtanzania la sh. 1,025,038/= sawa na asilimia 17.9, hali hiyo haifanani kutokana na hali ya maisha ya watu wenyewe hasa ukiangalia wale wa kipato cha chini kwani matumizi hayo kwao ni ndoto. Zipo kaya katika Tanzania hii wanakosa hata sh. 500/= kwa siku.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke mikakati madhubuti kwa mantiki ya kuimarisha hali za Watanzania, jitihada za

Serikali zinaonekana, lakini wapo wachache wanajinyakulia maslahi kutokana na kukosa usimamizi wa kutosha kutokana na ufisadi na rushwa hivi havitatufikisha mahali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uuzwaji wa kiwanja Na. 10 kilichouzwa na Bodi (*CHC*) haukufuata taratibu na sheria za manunuzi (*PPRA*).

Mheshimiwa Spika, kama hilo ni kweli na kwa vile hadi leo hii malalamiko yamekuwa ni mengi sana. Je, Serikali inachukua hatua gani kuhusu Bodi ya Menejimenti ya *CHC*? Kama uuzaji huo ni batili je mnunuzi amechukuliwa hatua gani? Je, kwa nini Serikali isifute manunuzi batili yaliyofanywa na Bodi ya *CHC*. Naiomba Serikali kuchukua hatua za kinidhamu kwa kukiuka taratibu na sheria za manunuzi kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo machache, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri ambao ameshirikiana nao katika kufanikisha kukamilisha kwa taarifa hii ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168. Marekebisho yaliyofanywa na Serikali kuhusu leseni za madereva hasa kwa madereva wenye magari madogo, bado haijawatendea haki. Kwa mfano, madereva wa *tax*. Miaka ya hivi karibuni madereva hawa pamoja na leseni walizonazo tokea nyuma walitakiwa kwenda kusoma tena *VETA* ili kupata leseni zenye viwango vya sasa *class C*, madereva hawa walisumbuka sana kwani baadhi yao walishaanza kazi hiyo toka miaka ya nyuma na walikuwa ni madereva wazuri wanaoaminika na kuwa na leseni aina ya *class C* za kipindi hicho, lakini pamoja na hayo walitakiwa tena kwenda kusoma *VETA* na kupata leseni aina ya *class C* ya sasa.

Mheshimiwa Spika, kusomea leseni ni gharama na wao walikuwa na uwezo mdogo na tukiangalia kwamba tayari wanazo leseni, lakini Serikali walifanya kutozitambua tena leseni hizo.

Mheshimiwa Spika, udereva sio kuwa na gari yako mwenyewe, wapo matajiri wanaowapa madereva magari kujitafutia riziki zao. Baadhi ya madereva ambao ni wazoefu wameshakuwa watu wazima, hivi ni haki kweli kumpeleka mtu wa namna hii kwenda tena shuleni kusomea leseni? Huku ni kuwakomoa madereva hawa na wengi wao wameshapoteza kazi zao za udereva kutokana na kushindwa kumudu gharama za masomo kutokana na halli zao kimaisha.

Mheshimiwa Spika, isitoshe walipokuja madereva wa pikipiki na bajaji, madereva hawa wakawa hawana tena kazi kutokana na wimbi la abiria kukimbilia boda boda na bajaji.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tena sheria inatamka kuwapandisha kodi ya leseni zao na kuendelea kuwasamehe kodi wanaoendesha pikipiki na bajaji. Ndiyo tunaongeza wigo wa ajira kwa vijana, lakini tuangalie na maisha yao kuwa hatarini.

Mheshimiwa Spika, hili ni vurugu kwani baadhi ya waendesha pikipiki hawana fani za kuendesha chombo husika, anajifundisha siku chache, baadaye anachukua abiria. Ndiyo maana wengi wao wamesababisha ajali za barabarani na wengine kufa kabisa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itengeneze utaratibu utakaotumika ili vurugu ambazo zinatarajiwa zisiwe za kutokea. Pia madereva wa *tax* kuendelea na viwango vile vile na kutengenezwa mazingira mazuri ili na wao waweze kujikimu kimaisha katika kazi zao za kujitafutia riziki.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo, naunga mkono hoja.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mazingira haya yote ya maendeleo tunayozungumzia ni lazima tutenge fedha za kutosha katika maeneo ya:-

(1) *Adaptation to climate change*; suala hili ni *real* na lazima tuhakikishe kwamba tuna- *mitigate against issues* za tabianchi. Kilimo, viwanda bila mazingira haina maana. Tutaendelea na ukosefu wa mvua na maji kwa ajili ya viwanda na kadhalika.

(2) Upandaji miti; lazima tuwe na *big national drive* ya upandaji miti. Hii itasaidia *sustainability* ya miti na mvua.

(3) Kutenga fedha katika bajeti ya Serikali; Serikali kutenga 0.5% *of the overall budget* ya Serikali au *GDP* katika suala la mazingira, msilachie Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira peke yake lazima kuwe na *National Approach*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, nipongeze kazi kubwa iliyofanywa na Serikali na Bunge letu Tukufu katika kupanga na kuichambua bajeti na hatimaye kuipitisha.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa sasa muda umefika wa nchi yetu kujitegemea kwa mapato yetu ya ndani.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ya kutotoza kodi kwa biashara ya bodaboda kwa maana ya *threshold* ya sh. 3,000,000 ni nzuri, lakini ni lazima Serikali itambue pia kwamba kuna afanyabiashara na wajasiriamali wadogo wadogo wenye biashara ndogo ndogo, maduka na vioski vidogo vidogo, nao wapewe fursa sawa na wafikiriwe kusamehewa kodi kama wenzao wa bodaboda hii italeta usawa kwa wafanyabiashara hawa wadogo wadogo, mfano mzuri ni wale wafanyabiashara wadogo wadogo walioko sokoni na stendi ya mabasi ya pale maili moja Kibaha.

Mheshimiwa Spika, mjenga nchi ni mwananchi. Kama kweli tunataka kupata maendeleo ya haraka tena kwa kujitegemea ni lazima tuhakikishe kuwa kundi la vijana ambao ndio wengi linatambuliwa ipasavyo na linaelekezwa katika kujenga uchumi kwa kutumia sera muafaka.

Mheshimiwa Spika, hata kama *TRA* watakusanya fedha nyingi kiasi gani kama hakutakuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha hizi, ni kazi bure, angalia kijana anayemaliza Chuo na hususan Chuo Kikuu anakabiliwa na changamoto ya nyumba ya kukaa, gari la kutembelea na kufanyia kazi chakula, mavazi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa mfumo wa sasa yote haya kijana huyu anatakiwa kulipa kwa fedha taslim yaani *cash life* tena kama ni nyuma kwa miezi sita hadi miezi kumi na mbili. Kijana huyu ndiye tunayempa dhamana ya kutoza kulinda kulipa na kupanga matumizi ya fedha za Serikali na tunamtegemea awe mwadilifu. Ni jambo ambalo ni lazima sasa Serikali ilifanyie kazi maana linachochea rushwa na hii ndio adui wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali ichukue hatua ya kuhakikisha kuwa kizazi tulichonacho na kijacho sasa kinajenga misingi imara ya kuleta mapinduzi ya kiuchumi kwa kuwashirikisha vyema Watanzania, lakini pia kwa kuwahakikishia maisha bora. Serikali iangalie sasa uwezekano wa kusimamia utekelezaji wa haraka wa kuwapatia vijana makazi, mikopo ya usafiri na kadhalika ili kuondoa dhana ya *cash life throughout*.

Mheshimiwa Spika, hii ndio inatufanya sasa kila mtu ananunua na kulipa kwa *cash* hata *ATM* za mabenki sasa hazitoshi. Niiombe Wizara husika itoe na kuongeza sera itakayotupeleka kwenye *credit life* na hii itatengeneza nidhamu ya fedha maana hata fedha chafu hazitakuwa na nafasi.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa bajeti ni kuchochea (*stimulate*) uchumi Tanzania. Tunafahamu vyema kuwa asilimia zaidi ya 70% wanaishi vijijini na kazi yao kubwa ni kilimo na mifugo. Nashauri kwa dhati kabisa sasa mipango ya Serikali kwa makusudi ilenge katika miundombinu ya umwagiliaji na barabara za mabonde maalum ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyokaa hapa



tunatenga fedha za barabara, basi tukae tutenge fedha za miundombinu ya kilimo. Miundombinu hii ni pamoja na kujenga vyanzo vya umwagiliaji maji kwa kujenga mifereji na *pump* za maji ya kilimo na kukuza kilimo. Tuache kabisa kutegemea kilimo cha kubahatisha kwa kutegemea mvua, maana hata kama tutaleta trekta ngapi kama hamna umwagiliaji na mvua ni haba ni bure na ni hasara zaidi kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu asilimia kubwa ya mfumuko wa bei hapa nchini ni bei za vyakula. Ukitazama takwimu za 2010/2011 wakati mfumuko wa bei ulikuwa 19 zaidi ya asilimia 40, mfumuko huo ulikuwa ni wa mazao ya chakula.

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivyo kwanza Taifa litajitoshesheza kwa chakula, vijana hawatahama kutoka vijijini kwenda mijini, hakutakuwa na migogoro ya wakulima na wafugaji na kubwa zaidi kila mwananchi ataweza kuona unafuu wa ukuaji wa uchumi maana hata mkulima atanufaika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mawaziri wa sekta zote wakiongozwa na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, kwa mipango ya mwaka 2013/2014 iliyoandaliwa kwa makini na kuwasilishwa mbele ya Bunge hili ambayo imekuwa msingi wa Bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nawapongeza Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa, Waziri wa Fedha pamoja na Naibu Mawaziri; Mheshimiwa Stephen Wassira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu kwa kuandaa na kuwasilisha Bajeti ya mwaka 2013/2014 na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, Mpango na bajeti vimezingatia maoni ya wananchi yaliyowasilishwa na Waheshimiwa

Wabunge. Tuna matumaini makubwa kuwa ikitekelezwa kama ilivyopangwa itaimarisha imani ya wananchi kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo amebuni na kusimamia maandalizi wa mpango wa *Big Results Now* ambao hakika tukiutekeleza kama ulivyopangwa tutapata mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, namshukuru kwa namna ya pekee kwa kukubali kuongeza maji kuwa moja ya vipaumbele vya Kitaifa. Maji sio siasa bali ni uhai wetu, hivyo namwomba sana Waziri wa Fedha na watendaji wa Wizara wahakikishe kuwa fedha zilizoidhinishwa zinatolewa ili miradi ilivyopangwa itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa maendeleo vipaumbele vilivyoainishwa na kutengewa fedha vinastahili kupata fursa hiyo kwa sababu ya umuhimu wake katika maendeleo ya Taifa. Hata hivyo, ni vizuri tukumbuke kuwa tunapojenga nyumba hatuwezi kujenga kuta kabla ya msingi.

Mheshimiwa Spika, Chama cha Mapinduzi kinatambua hili na ndiyo sababu katika Ilani yake ya uchaguzi ya 2010, Ibara ya 57 inatamka kuwa ardhi ndiyo rasilimali namba moja. Mpango wa Maendeleo wa 2013/2014 unaelekeza kuwa ili kukidhi mahitaji ya wawekezaji kwenye sekta za kilimo na nyinginezo itengwe ardhi ili kuwapatia watakaoonsesha nia ya kuwekeza. Hata hivyo fedha iliyotengwa kwa ajili ya kupanga matumizi ya ardhi haitoshi kupanga hata vijiji mia moja.

Mheshimiwa Spika, naamini kuwa hii imetokana na upungufu kwa upande wa wataalam ambao walipoambiwa kuwa tunataka kuzalisha chakula cha kutosha na kujenga viwanda hawakujua kuwa vyote hivyo vitafanyika juu ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, ili kuepuka upungufu kama huo,

nashauri kuwa kwa miaka ijayo ni vizuri wataalam wanaoshauri wafanye ulinganisho wa shughuli za sekta mbalimbali kwa namna zinavyotegemeana na hivyo kupunga mipango itakayotekelezeka bila kikwazo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwiano wa maendeleo nchini ni ukweli kuwa maendeleo katika Mikoa na Wilaya mbalimbali nchini imepishana sana. Kwa bahati mbaya wanaoandaa mipango hawazingatii hali hiyo bali huzidi kupeleka miradi mingine kwenye maeneo ambayo tayari yamepiga hatua badala ya kupunga maeneo ambayo yameachwa nyuma kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa Tume ya Mipango ifanye ziara kwenye Mikoa na Wilaya nchini ili ijue hali halisi ya upungufu ulio kwenye Wilaya zetu, badala ya kuandaa kwa kutegemea taarifa zinazoandaliwa mezani na Maafisa wa Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa ahadi za Rais, hii ni bajeti ya tatu tokea Uchaguzi Mkuu wa 2010 umalizike. Katika Wilaya yangu Rais aliahidi mambo yafuatayo:-

(i) Ujenzi wa barabara ya lami toka njia panda ya Ngaramtoni hadi Sambasha. Vile vile aliahidi kuwa barabara zote za Wilaya zitatengenezwa ili zipitike mwaka mzima.

(ii) Kuandaa na kutekeleza mpango kabambe wa Mji ili Wilaya nzima ipate maji kabla ya 2015.

(iii) Tarehe 1 Novemba, 2012 wakati akizindua hospitali ya Wilaya aliahidi kujenga barabara ya lami toka redio habari maalum hadi hospitali ya Wilaya Olturumet.

Halmashauri ya Wilaya ya Arusha imejitahidi kuandaa maandiko ya miradi kwa ajili ya utekelezaji wa ahadi hizo, lakini hadi sasa hakuna hata mmoja ulioingizwa kwenye mpango wa Taifa na kutengewa fedha kwa ajili ya

kutekelezwa. Je tunataka ifike 2015 wananchi wapoteze imani kwa Rais wao mpendwa? Naomba tutengewe fedha tuanze kutekeleza ahadi hizo za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha; mwaka jana Serikali iliagiza Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kuwa itoe ardhi iliyokuwa imenunua toka kampuni ya *Valhala* ili itumike kwa ajili ya ofisi za Mashirika ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kulipa gharama zote za Halmashauri ikiwemo mkopo wa Benki na nyinginezo. Uongozi wa Halmashauri umekuwa ukifuatilia malipo ya gharama zake lakini hadi leo hakuna hata shilingi iliyolipwa.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ilisimamisha utekelezaji wa miradi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa jengo la ofisi ili kulipa riba ya mkopo wa Benki. Tumeomba turejeshewe fedha hizo tulipe madeni ya Mkandarasi, lakini hadi leo bado. Naomba ahadi ya Serikali itimizwe kwani ucheleweshaji huo unaathiri utekelezaji wa miradi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *PAYE*; naishukuru Serikali kwa kupunguza kodi ya mapato kwa wafanyakazi kwa asilimia moja. Kwa maoni yangu kiwango hicho ni kidogo sana ikilinganishwa na gharama halisi ya maisha. Nashauri kuwa punguzo la kodi liongezwe angalau liwe asilimia nne (4%).

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, hoja ya *Stimulus Package*; naomba itolewe ufafanuzi kwa Bunge kuletewa majina yote ya watu waliofaidika na fedha hizo za 1.7 trilioni ambapo zipo taarifa za kutosha kuwa zimeliwa vibaya/kifisadi na *CAG* amepata kuonesha wasiwasi huo katika ripoti ya 2011. Spika ameshaagiza tangu 2012, majina yaletwe lakini Serikali /Wizara ya Fedha imegoma.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu hoja ya *NBC* ya 60 bilioni nilizungumza wakati nachangia hotuba ya Wizara ya

Fedha na nimerudia tena jana. Napenda kusesitiza kuwa majibu ya Waziri siku ya vifungu hayakutoa nilichouliza.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza Bunge liletewe majina ya wadaiwa wote na liweze kufanya azimio kwani watu hawa wapo mjini na wengi wao ni matajiri. Hatuwezi kuwa na Serikali nyonge. Naomba majibu kwani tofauti na majibu nitaleta hoja binafsi.

Mheshimiwa Spika, tatu, hoja ya taarifa ya Mashirika yaliyobinafsishwa; tangu mwaka 2011 tumekubaliana hapa Bungeni na Spika akaelekeza Serikali ilete majibu/ilete taarifa ya mashirika yaliyouzwa. Mpaka leo 2013 bado Serikali/Wizara ya Fedha imegoma kuleta taarifa hii. Nataka majibu kwani mgomo huu unadhaliisha Bunge zima na kiti cha Spika.

Mheshimiwa Spika, nne, hoja ya *Telecoms* na Madini kusajiliwa kwenye soko la mitaji. Tangu 2010 Bunge limepitisha sheria kwa makampuni haya yawe *listed* kwenye *stock Market*. Mpaka leo 2013, bado Serikali imegoma kutengeneza kanuni ili kutekeleza sheria hizi. Kwa nini kama sio ufisadi?

Mheshimiwa Spika, tano, hoja ya mashirika ambayo Serikali ina hisa kuwa *listed* kwenye *DSE*. Narudia tena na nasisitiza tena, Serikali ihakikishe angalau nusu ya hisa zake ziwe *listed* kwenye *DSE* ili Serikali ipate mapato stahiki.

Mheshimiwa Spika, sita, Makampuni ya Utafutaji Mafuta na Gesi; hapa naomba kuzidi kushauri haya yote yawe *listed* japo 10% ya hisa zake *DSE* kwa lengo la kuhakikisha uwazi na hivyo kodi kupatikana, lakini pia mapato kwa *DSE* na kuifanya *DSE* isiendelee kuwa tegemezi kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, saba, hoja ya *Bank* kuwa *listed DSE*; naomba kusesitiza tena kama nilivyosisitiza nilipochangia Wizara ya Fedha. Hii ni nchi yenye *Bank* nyingi katika *SADC*, *Stock market* itasaidia, jifunzeni Sri-Lanka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya ubatili wa Bodi ya

*PSPF*; Bodi ya *PSPF* iko kinyume cha Sheria. Waziri wa Fedha (ambaye ndiye mamlaka ya uteuzi wa wajumbe wa Bodi) aliwateua wajumbe kinyume na matakwa ya sheria.

Mheshimiwa Spika, *PSPF Act (No 2 ya 1999) Section 52* ndiyo ilikuwa inaongelea *composition ya Board. Act No 5 ya 2012, section 136* ndiyo iliyobadili *section 52 ya PSPF* kuhusu *composition ya Bodi*. Ninao ushahidi hata barua kutoka kwa AG inaonesha kuwa Bodi ya sasa ya *PSPF* ni batili kwa mujibu wa sheria na ndio maana nashangaa kuona Ofisi ya CAG ambayo ilitoa barua kuonesha ubatili wa Bodi, bado na yeye anashiriki na bodi hiyo. Hapa nakusudia kuleta hoja binafsi, Bunge lichunguze kwa nini na litoe azimio kwa uvunjifu huu wa sheria.

**SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu na niongezee pale pongezi zangu za dhati na shukrani kwa kuongoza mabadiliko ya mchakato wa bajeti ambao naamini kabisa yataleta manufaa kwa Taifa letu. Vile vile napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Naibu Mawaziri na watendaji wote kwa kuitikia mabadiliko haya na kuonyesha utayari wao katika kwenda na mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, nasimama hapa kutoa mchango na vile vile kutoa ufafanuzi kwa hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge hususan zile zinazohusu uwekezaji, uwezeshaji na maendeleo ya sekta binafsi. Lakini kabla sijafika kwenye ufafanuzi wa hoja hizo naomba niseme mambo machache ya kiujumla ya kisera.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni kwamba, kutoka miaka ya 1990 tulivyoachana na uchumi hodhi, sera za Serikali zimejielekeza katika kuimarisha sekta binafsi ili isaidiane na Serikali katika kuleta maendeleo ya haraka ya uchumi. Jambo la msingi ni uwekezaji ili kuinua na kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa uwekezaji katika kuinua uchumi wetu na ukuaji wa uchumi hauna mjadala na ni muhimu sana kuona kwamba, uwekezaji wa ndani ndio unachukua hatma ya uchumi wa nchi hii kwa sababu ni endelevu. Lakini tunajua kabisa kwamba, utamaduni na desturi za Watanzania za kuweka akiba zikiunganishwa na umaskini wetu ni mdogo sana na kwa hivyo haiepukiki kuhamasisha uwekezaji kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, najua sio nchi maskini tu ambazo zinahamasisha uwekezaji kutoka nje hata zile tajiri kama China, Uingereza na hata Marekani ambayo ni tajiri kuliko nchi zote zinahamasisha uwekezaji kutoka nje. Kwa hivyo, Serikali ya Tanzania na Taifa kwa ujumla lazima zijitahidi sana katika kuhamasisha uwekezaji kutoka ndani na kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, naungana na Wabunge wenzangu na Watanzania wengine kulaani yaliyotokea Arusha na napenda kuwapa pole wale waliofiwa na wale waliojeruhiwa kutokana na tukio la bomu kule kwetu Arusha. Mazingira kama yale yatawafukuza wawekezaji sio tu wa nje hata wa ndani na hasa ukizingatia kwamba Arusha ni eneo la utalii.

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi na sisi tulivyoshuhudia Bunge hili lilivyokuwa na amani wale marafiki zetu wasipokuwa humu ndani; bila ya kuweza kurefusha ninayotaka kueleza. Fujo za humu ndani zimehamia nje, kwa hivyo Watanzania lazima wajue kwamba, fujo hazileti tija na fujo hazitajenga nchi yetu. Naomba sana mazingira ya amani na utulivu pamoja na mshikamano tuyaimarishe ili wawekezaji wachukue jukumu la kuwekeza na kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo nataka niliseme ni kwamba, haitoshi kuwa na maliasili, haitoshi kuwa na rasilimali, lazima tuwe na uwekezaji. Ili tuweze kutumia maliasili ambayo ametupa Mwenyezi Mungu inabidi tuwe na mitaji ya kutosha kuweza kubadili maliasili na rasilimali kwa ujumla kuwa bidhaa, kuwa huduma na kuweza kuleta manufaa na maisha bora kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaombeni sana, tuelewe pamoja na kwamba Mungu ameijalia nchi yetu ya Tanzania maliasili nyingi, lakini ukosefu wa mitaji na sisi kutokujipanga hatunufaiki na utajiri wa nchi yetu. Haitoshi kuwa na rasilimali na haitoshi kuwa na mitaji, inabidi tujipange kama nchi ili tuweze kuwekeza kwenye maeneo ambayo yataleta manufaa na maisha bora kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ndio maana nimeona sasa na naelewa kukerwa kwa Mama Anne Kilango Malecela alipotoa taarifa hapa Bungeni kwamba, kuna mwekezaji ambaye amepewa shamba la mkonge ambalo hajaliendeleza. Nina hakika kwa hili mtaniruhusu nisome kwa sababu ni taarifa ambayo ni rasmi nataka kumpa.

Mwekezaji yule aliyepewa shamba kutokana na taarifa nilizopata kutoka Kituo chetu cha Uwekezaji, taarifa za awali zinaonesha kuwa shamba hilo lenye ukubwa wa hekta 1,485 linamilikiwa na Kampuni ya Uwekezaji wa ndani iitwayo *L. M. Investment Limited*.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mama Anne Malecela hakusema jina la Kampuni hiyo, naamini ndio hilo. Kampuni hiyo ilinunua shamba hilo kutoka kwa Mamlaka ya Mkonge tarehe 15 Januari, 1998 na mradi ulisajiliwa kwa upanuzi na ukarabati wa shamba hilo katika Kituo cha Uwekezaji tarehe 26 Mei, 2005 na kupewa Hati ya Uwekezaji namba 010168.

Mheshimiwa Spika, taarifa zaidi zinaeleza kuwa kwa bahati mbaya mwenye Kampuni hiyo alifariki na wengine wote ni ndugu zake. Naamini kwamba labda wanajipanga vizuri, lakini nitafuatilia kwa karibu sana kuona kwamba shamba hilo linaendelezwa na kwa sababu Wizara hii vile vile ni Wizara ya Uwezeshaji tuone ni namna gani mwekezaji huyu wa ndani anaweza kujizatiti na kama sivyo basi, tulichukue na tulipeleke kwa mwingine ambaye atakuwa na uwezo nalo.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingine zilizotolewa za



unafuu za kodi zinazotolewa na *TIC* kwa wawekezaji. Hili ni gumu hasa kwa wale wawekezaji wanaotoka nje kupewa misamaha ya kodi. Naomba tuelewe kwamba, hatutoi msamaha wa kodi kwa mwekezaji, bali tunatoa msamaha wa kodi kwa mtaji ambao unapaswa kuwekezwa, ukiupunguza maana yake uwekezaji unapungua. Lakini ni kweli vile vile kwamba hawa wanaopewa msamaha, wakati Serikali na Taifa linataka kutoa msamaha ili uwekezaji uwe mkubwa na manufaa ya uwekezaji yapatikane, kuna watu ambao wamepita katikati na kutumia misamaha hiyo vibaya.

Mheshimiwa Spika, sasa hii inataka uduhulizi wa Serikali kufuatilia kama vile ambavyo tulikuwa tumepanga ndicho kinachofanyika. Hata hivyo, katika bajeti ya mwaka huu Mheshimiwa Waziri wa Fedha amepunguza ile misamaha kwa kiasi cha asilimia 15. Kwenye bajeti ya mwaka jana walipewa msamaha kwa kiasi cha asilimia 90 na sasa hivi wamepewa msamaha kwa kiasi cha asilimia 75.

Mheshimiwa Spika, narudia tena, msamaha unatolewa ili mtaji usipunguzwe na kodi ili uwekezwe: uweze kutoa ajira, uweze kutoa huduma, uweze kutoa bidhaa na ni kazi ya Serikali kufuatilia kwamba hao wanaopewa misamaha hiyo wanaitumia vizuri. Pale ambapo haitumiki vizuri, tutachukua hatua zinazotakiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kurudia kwamba, suala la kutoa misamaha ya kodi kwa kweli sio jambo la kuendekeza, kwa sababu tusipolipa kodi maana yake hatutakuwa na maendeleo, tutakuwa wategemezi zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda vile vile kusemea urasimu wa *TIC*. *TIC* inapaswa kuwa *one stop centre*, kituo ambacho mtu akienda anataka kuwekeza, anatoka siku hiyo hiyo anaanza kuwekeza. Kwa bahati mbaya kama tulivyosema bado mambo yetu yanasuasua na tutajitahidi sana hasa pale ambapo kuna miradi ya *PPP*.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri wa Fedha na wenzake kutenganisha miradi ya *PPP* na ununuzi

wa Serikali kwa sababu inapowekeza sekta binafsi si Serikali na *PPRA* inahusisha manunuzi ndani ya Serikali. Naamini kutenganishwa huku kwa manunuzi ya Serikali na miradi ya *PPP* itatufanya sisi tuwapate wawekezaji, kwa sababu kwa maoni yangu binafsi, naona ni dhambi mahali ambapo sekta binafsi inawekeza, Serikali iende ikawekeze na kuwakosesha watu dawa na elimu. Kwa hivyo, pale ambapo sekta binafsi itapata faida, tutahakikisha kwamba, wanawekeza ili fedha za Serikali ziende kule ambako sekta binafsi haiwezi kwenda.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno haya, nakushukuru tena kwa nafasi hii uliyonipa. Naomba tena nilaani matukio ya kuondoa amani na utulivu kwa sababu tunafukuza wawekezaji wa nje na tunawakatisha tamaa wa ndani. Pia Watanzania watakuwa na wasiwasi wa kwenda mashambani, viwandani na kwenda kwenye shughuli zao za kiuchumi na huku ni kudidimiza uchumi wa Taifa letu na kukosesha Watanzania maisha bora.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na nampongeza.  
(*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA – WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza napenda nianze kwa kuunga mkono hoja na pili nichukue fursa hii kuwapongeza watani zetu *CUF* kwa kuchukua Ubunge kule Kisiwani, Pemba.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile nitumie fursa hii kukipongeza Chama changu cha Mapinduzi kwa kushinda viti 16 vya Udiwani ikiwemo Kata ya Mnima kule Mtwara Vijijini ambako watani wetu wa jadi tumewagalagaza na kuwanyang'anya Kata yao ambayo tuliwaonjesha kwa kipindi cha miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda pia nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwanza kwa jinsi unavyoliendesha Bunge letu Tukufu kwa ujasiri na kwa umahiri mkubwa pamoja na changamoto za hapa na pale. Pia kwa kuanzisha utaratibu huu mpya ambao tunaanza kwanza mapema mwezi wa Aprili na tunamaliza mwezi Juni tukimalizia na bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba mwanzo tulikuwa na wasiwasi, kwa kweli huu utaratibu ni mzuri sana kwa sababu Waheshimiwa Wabunge walishachangia sana katika bajeti nyingine, kwa hiyo tunapofika katika hii bajeti ya mwisho hata vile vigongo kwa kiasi kikubwa vinapungua sana.

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze Serikali kwa kupeleka fedha nyingi sana na za kutosha katika Halmashauri zetu kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Niwaombe Wakurugenzi na Watendaji wa Halmashauri kuhakikisha kwamba, fedha zinazopelekwa katika maeneo yao wanazitumia kwa miradi ambayo imekusudiwa.

Mheshimiwa Spika, nawaomba wafuate sheria, kanuni na taratibu ambazo tumejiwekea. Pia niwaombe Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Madiwani tumechaguliwa na wananchi kuwawakilisha katika Halmashauri zetu kwa ajili ya kusimamia fedha zilizopo katika Halmashauri kwa niaba yao, tufanye hiyo kazi ya kuhakikisha kwamba fedha zilizopelekwa katika Halmashauri zinatumiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana ofisi yangu tulifanya kikao na Wakurugenzi na kuwaelezea upungufu wao na *agenda* kubwa ambayo tuliizungumzia katika kikao chetu cha mwaka jana ilikuwa ni kwa kiasi gani tunaweza tukaondokana na hati chafu ambazo zilikuwepo katika Halmashauri pamoja na hati zisizoridhisha.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba, katika taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali mwaka

huu, hati chafu hatuna hata moja ukiacha Mbarali ambapo Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali ameshindwa kutoa maoni yake ni hati ya aina gani ambayo anawapa. Mwaka huu tulikuwa na kikao Morogoro na Wakurugenzi wote, tulimwalika Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na Wizara za Kisekta zote ambazo kwa pamoja tunafanya kazi na Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI).

Mheshimiwa Spika, malengo makuu ilikuwa ni kwa kiasi gani kwa pamoja tunaweza tukajipanga kwa kushirikiana na Wizara hizo za Kisekta kuhakikisha kwamba, si suala la kupata hati safi tu, sasa tunachotaka katika bajeti ya mwaka huu inayokuja, ni kuhakikisha kwamba, thamani ya fedha inapatikana katika miradi inayokaguliwa. Hati ifanane na miradi iliyotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, napenda nikuhakikishie tumejizatiti Ofisi ya Waziri Mkuu na tutahakikisha watendaji wote ambao watumia fedha za Serikali kinyume na sheria, kanuni na taratibu tunawachukulia hatua zinazostahili. Pia mwaka huu tumefanya kikao na Halmashauri ambazo zimepindukia mwaka wakiwa na fedha za bakaa za mwaka 2011/2012 wamefika nazo 2012/2013 na bado inavyoelekea wangeweza kufika nazo mwaka 2013/2014 na wenyewe pia tumewapa maelekezo nini cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii tena kuwakumbusha, tumekubaliana kwa kuwa fedha zinazotoka katika Mfuko wa Barabara, kila mwaka zinafika kwa asilimia mia moja. Tumewaagiza inapofika tarehe 1 Julai, 2013, watangaze tenda zote kwa barabara ambazo bajeti yake imepitishwa na Bunge lako Tukufu ili fedha tu inapofika katika Halmashauri ule mradi uanze kutekelezwa na sio kusubiri fedha zifike, ndipo waanze kutangaza tenda. Zipo Halmashauri fedha walizopata Oktoba, 2012, tenda imekuja kutangazwa mwaka huu mwezi Machi, kwa kweli hatutaweza kuwavumilia na tumewaambia nini kitafuata iwapo wataendelea kubaki na fedha za bakaa.

Mheshimiwa Spika, napenda niungane na wenzangu

waliosema kwamba amani na utulivu ndio rasilimali pekee ambayo itatusaidia Tanzania kusonga mbele. Miradi yote iliyopitishwa, bajeti yote tuliyoipitisha pasipokuwa na amani, sidhani kama miradi hiyo itaweza kutekelezwa. Nakumbuka kuwasikia baadhi ya viongozi wa Chama cha CHADEMA wakisema kwamba watahakikisha kwamba nchi haitawaliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wanasema vile nilikuwa sijui wanamaanisha nini, lakini sasa tunaona kwamba, vitendo vyao, mikakati yao, ya kuhakikisha kuwa nchi haitawaliki tunayaona yanayotokea, tumeona Arusha, Mbeya, Mwanza, Mtwara na Iringa. Ninachojiuliza wale waliosimama wakasema watahakikisha haitawaliki, kwa nini hayo wanayoyafanya kwenye Mikoa ya wenzao, hawafanyi katika Mkoa wao.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa Mtwara Ijumaa na Jumamosi; Jumatatu nilikuwa Moshi na Jumanne nilikuwa Arusha lakini niliyoyaona Mtwara barabara zimechomwa moto, niliyoyaona Arusha, sikuyaona Moshi, nimekaa Moshi Mji msafi, hakuna barabara iliyochochomwa, hakuna fujo, lakini Mheshimiwa Ndesamburo na Bwana Mbowe ambao wamesema nchi haitawaliki wao kazi yao ni kwenda Mbeya, Arusha, Mtwara na Mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, sasa niwaombe wananchi akili za kuambiwa hebu wajaribu kuchanganya na za kwao. Pia wajulize na wajitambue hao Wabunge wenye uchungu na Mikoa ya wenzao ambao hawana uchungu na Mikoa yao ni Wabunge wa aina gani?

Mheshimiwa Spika, ninachokiona hii sasa siyo siasa ni biashara, wanachotaka ni wawekezaji wasiende katika Mikoa mingine bali waende katika Mikoa yao, Watalii wasiende Arusha bali waende Moshi, ndicho nilichokiona; wawekezaji wasiende Mtwara, wasiende Mbeya na nia ni kuhakikisha kuwa Mikoa yote inayochipua basi wawekezaji wasiende warudi huko ambako wanakuona wao ndiko kunakotawalika.

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kuwaomba wananchi, tuienzi amani yetu na pale wanaposhawishiwa hebu na wao wawaombe hao ambao wanasema nchi haitawaliki waende na huko kwao, wakatie fujo kwa sababu kama ni upinzani, Mkoa wa Kilimanjaro, ndio unaoongoza kwa kuwa na wapinzani.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimwambe Kaka yangu Bwana Barwany ile Mikutano ya uchochezi aliyofanya Mtwara akafanye na Mkoani kwake Lindi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Profesa Mwandosya, atamalizia Naibu Waziri, Mheshimiwa Masele.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuwa mmoja wa wale ambao mwanzo kabisa kabla hataujaendelea nasema naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza na kuwashukuru sana Watanzania kwa kukiamini Chama cha Mapinduzi na imani hiyo wameionyesha Jumapili iliyopita kwa kutupa kura nyingi za kutosha na kutupa viti 16 vya Udiwani katika aya ya 22, hii ni ishara ya yale yanayokuja mwaka kesho na mwaka keshokutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisisahau kukupongeza wewe umelisimamia Bunge na hasa Mkutano huu, Mkutano ambao wengi tulikuwa na wasiwasi kama ungefanikiwa kutokana na mabadiliko ya mfumo na mzunguko wa bajeti, lakini ulitulia ukasema inawezekana na imewezekana tunakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa namwambia Mheshimiwa Mgimwa kuwa, kazi ya Uwaziri wa Fedha katika nchi masikini ni sawasawa na kazi ya kuwa Waziri unayeshughulikia na Navy katika nchi ambayo haina bahari. Ni kazi ngumu sana

lakini ni kazi ambayo wameifanya kwa ufanisi, wametuletea bajeti nzuri hapa, kwa kweli nawapongeza sana yeye na Manaibu Waziri hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sitazungumzia masuala ya kiuchumi wala ya kifedha, nitarudi kwa masuala ambayo tunajuliza Mtanzania ni nani? Maana ndiyo Mtanzania huyo atakayeliendeleza hili Taifa na kuendeleza Uchumi sifa ambazo zinatutambulisha sisi kama Watanzania kokote duniani, tukienda ni zifuatazo kumi:-

Wanasema Mtanzania ni mtulivu, wanasema Mtanzania ni mtu makini, wanasema Mtanzania ni muaminifu, ukiwa katika kundi la watu wanasema Mtanzania siyo mgomvi, wanasema Mtanzania ni mpatanishi, wanasema Mtanzania ni kiongozi asilia yaani *is the National leader*, wanasema Mtanzania ni mpenda amani, Mtanzania ni mpole, Mtanzania ni mcha Mungu, lakini kwa yote Mtanzania ni mstaarabu *(Makofi)*.

Mheshimiwa Spika, sasa tuanze kujipima haya yanayotokea siku hizi yanaendana na haya ambayo wenzetu wanatuona kama Watanzania kwa sifa zote hizi? Basi nadhani tujirudi, tuseme nini kimetokea? Nilisema hapo awali kuwa katika maisha ya Taifa shetani huwa anapita, basi tuamini kuwa shetani anapita, atashindwa na kipindi hiki ni cha mpito tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunelekea katika kuhitimisha Dira ya Taifa ya 2020/2025 na vile vile tunaelekea katika kuhitimisha Malengo ya Milenia, lakini tutahitimishaje Malengo haya ya Millenia mwaka 2015 na vile vile yale tuliyoyalenga kuyafikia katika Dira ya Taifa 2025, naongeza sifa nyingine ambazo ni lazima tuwe nazo kama Watanzania, ni lazima tuwe na nidhamu na nidhamu hiyo siyo Watanzania tu lakini sisi viongozi ni lazima tuonyeshe mfano ni kitu muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, lazima tuenzi na tupende kazi yoyote ile tunayoifanya hiyo ni moja ya sifa ambayo

itatuwezesha kufikia hapo ambapo tunataka kwenda mwaka 2015 na mwaka 2025. Vilevile tuendeleo kukataa na kupiga vita kwa nguvu zetu zote rushwa na ufisadi, tutafika tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuwe Wazalendo, tuipende nchi yetu, tunapozungumza ni kama vile hatutoki Tanzania, ni kama vile ni wageni wa nchi hii na matendo yetu hayafanani na kuipenda nchi yetu, tutakwenda wapi Tanzania ikivurugika? Mheshimiwa Waziri Mkuu ametukumbusha asubuhi kuwa sisi ndiyo tegemeo la Mataifa yote yakiharibika huko wanakuja huku, sasa sisi tutakwenda wapi? Tutakwenda Malawi, Zambia au Kenya? Haiwezekani!

Kwa hiyo, tuipende nchi yetu Uzalendo ni jambo muhimu sana. Wamarekani hata ufanye nini watasema Vyama vingi, watasema sijui demokrasia, watasema haki za binadamu kitu kikubwa zaidi, wanasema wao ni Wamarekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote hayo mwisho wa siku, mwanzo wa siku sisi ni Watanzania na hii ndiyo nchi yetu, hatuna nchi nyingine, hatuna mahali pengine pa kwenda, tuipende nchi yetu kama tunavyoimba kwenye Tanzania, Tanzania na Vyama vya siasa na huo wimbo wa Tanzania, Tanzania, nakupenda kwa moyo wote, ungekuwa ndiyo wimbo wa kwanza kuimba, nadhani hata vurugu hazitakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sifa nyingine katika hizo sifa tano ambazo tunaweza kuwa nazo na tukiwa nazo tunaweza kufikia malengo yetu ya Dira na Malengo yetu ya Mileniani kujiamini, Taifa lisilojiamini au watu wasiojiamini hawawezi kufanikisha malengo yao hata siku moja. Tunazungumza kama vile Taifa hili watu hatujafanya kazi, Chama cha Mapinduzi hakijafanya kazi, Serikali hajafanya kazi mambo ya ajabu sana. Wengine wanasema miaka 50 ya Uhuru na wao wana miaka 30, wanasema miaka 50 ya Uhuru hawajui hata tulikotoka wanasema hakuna kitu kilichofanyika maajabu kabisa.



Mheshimiwa Spika, sasa wenzetu wanatuona vizuri sana na Mheshimiwa Wasira ametukumbusha katika Hotuba yake anasema:

“Benki ya Dunia kwa vigezo vyote vile inasema Tanzania ni moja ya nchi zinazokuwa kwa haraka sana duniani.” sisi tunasema hamna kilichofanyika, sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Wasira ametukumbusha vile vile kuwa Kamisheni ya Uchumi ya Afrika inasema Tanzania ndiyo nchi itakayokuwa kwa haraka sana katika nchi kumi Afrika, sisi tunasema hakuna kilichofanyika. Shirika la Kimataifa la Fedha (*IMF*) linasema kuwa, Tanzania ni moja kati ya nchi kumi duniani zitakazokuwa kwa haraka sana ifikapo 2015, sisi tunasema hapana hakuna kilichofanyika. Tusipojamini sisi wenyewe nani atatuamini? Sisi tungesema kama mnatuamini hivyo, basi sisi tufanye makubwa zaidi ndipo tunapoweza kuendelea kwa kasi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2014, kuna chaguzi za Serikali za Mitaa, naamini Watanzania watachagua mambo matano mwaka 2014 na mwaka 2015; watachagua amani dhidi ya shari; watachagua upendo dhidi ya uhasama; watachagua mshikamano dhidi ya mfarakano; watachagua utulivu dhidi ya fujo na watachagua nuru dhidi ya giza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kukipongeza Chama cha Wananchi (*CUF*) kwa kushinda kiti cha Ubunge na ndiyo demokrasia na ndivyo nchi inavyokwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Naunga mkono hoja asante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. STEPHEN J. MASELE):** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Fedha na Naibu Mawaziri kwa kazi nzuri

waliyoifanya na nikupongeze wewe mwenyewe binafsi kwa kuleta mfumo huu mzuri wa bajeti ambao utaongeza tija katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba nijibu hoja zilizochangiwa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia bajeti ya Serikali. Kwa haraka nitaanza na hoja ambayo ilichangiwa na Mheshimiwa Vita Kawawa, aliuliza mradi wa Mkuju utaanza lini na hatua gani Serikali imefikia katika kukamilisha mkataba wa mradi wa *Uranium* wa Mkuju.

Mheshimiwa Spika, kwa takribani miaka mitano iliyopita nadhani mradi huu ndiyo utakuwa mkataba wa kwanza kwa mgodi mkubwa hapa nchini tutakapokamilisha kusaini mkataba wa mradi wa Mkuju. Serikali inajitahidi kufanya kazi hii kwa umakini na kuangalia kasoro zilizokuwa zikijitokeza katika mikataba mingine ya nyuma ili tuweze kuwa na mkataba mzuri na kuweza kutibu tatizo ambalo Watanzania wamekuwa wakilalamika kuhusu mikataba ya madini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yako maeneo ambayo yamefanya mradi huu uchelewe, si kwa lengo la kukataza uwekezaji bali kwa lengo la kuboresha kuhakikisha mkataba na mradi huu unakuwa na faida kwa nchi kwa vizazi vya sasa na vizazi vya baadaye. Maeneo ambayo tumekuwa tukibishana na wawekezaji ni kwenye misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa hapa wamekuwa wakizungumza sana kuhusu misamaha ya kodi na timu yetu ya Serikali ya majadiliano imefanya kazi nzuri kuhakikisha kuwa misamaha isiyo ya lazima isikubaliwe. Kwa hiyo, kuna eneo la misamaha, kwa mfano, *withholding tax* katika *interest* na *service* ambayo wawekezaji walikuwa wanasisitiza ni lazima wapate misamaha ile na Serikali imesema misamaha kama hiyo haitatolewa.

Mheshimiwa Spika, lakini liko eneo lingine katika *definition* za Kisheria, kwa mfano, katika Sheria zetu za Kodi,

tunapo-define *capital goods* kuna vitu vimeainishwa pale *capital goods* ni vitu gani hivyo, lakini kuna eneo pia wenyewe wanasisitiza watumie *critical goods*. Sasa orodha ya *critical goods* hazijawa *defined* na Sheria zetu. Kwa hiyo, ili kuhakikisha kuwa mkataba huu unakuwa mzuri Serikali imeendelea kushikilia msimamo kuwa wafuate Sheria yetu inavyo-define *capital goods* na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hivi sasa Serikali imekwishaweka msimamo, imeshaweka *position* yetu kuwa, kodi hizo walizomba tuwasamehe hatutasamehe na *definition* ya *capital goods* waifuate badala ya *critical goods*. Pia tumeomba watupe *definition* ya *fair market value* katika mkataba ule ili tuweze kujua kabisa kuwa mkataba huu utakapokamilika uwe na manufaa zaidi kwa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeshakamilisha upande wetu na sasa tumeshawaandikia na tumewapa upande wao, sasa wanapaswa kuamua, kuchukua ofa hiyo au kutafakari nini cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Kafumu amezungumzia kuhusu *TMAA*. *TMAA* ilianzishwa mwaka 2009 na hii ilianzishwa kuchukua nafasi ya kampuni ile ya *Alex Stuart* ambayo ilikuwa ikifanya ukaguzi kwenye migodi kote iliyoanzishwa hapa nchini, pesa nyingi zilikuwa zikilipwa kwenye kampuni ile na ilikuwa inapata malipo kwa *percent* ya kazi ile waliyokuwa wakifanya.

Waheshimiwa Wabunge mlipinga na Serikali kwa makusudi kabisa ili kuongeza jicho katika shughuli za uzalishaji wa migodi ikaunda *Agency* hii ya *TMAA* ambayo kazi yake kubwa ni kuhakikisha uzalishaji wa migodi kuanzia kule chini wanakochimba *process* yote na mpaka kwenye mauzo, kuangalia bei wanayouza ni sawasawa na bei waliyoandika katika ripoti zetu kule kwenye soko la mwisho na baada ya pale kuangalia kiasi gani Serikali inapaswa ikusanye kama kodi na kiasi gani Serikali inapaswa ikusanye kama mrabaha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, *TMAA* ni *Specialized Agency* ambayo inafanya kazi kubwa ya kusimamia migodi hii na ilianzishwa kwa makusudi kabisa na Serikali na watu walikaa wakatafakari na ndiyo maana wakaanzisha chombo hiki. Kwa hiyo, bado naamini na Serikali bado inaamini kuwa *TMAA* inafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kinachotakiwa ni kuboresha shughuli zao na kuwaongezea nguvu ili waweze kusaidiana na *TRA* katika kuhakikisha kuwa mapato yanayotokana na madini ili Serikali iweze kupata mapato yote stahiki.

Mheshimiwa Spika, chombo hiki tangu kimeundwa kimeweza kusababisha Serikali ikusanye mapato mengi ambayo mwanzoni yalikuwa hayaonekani. Tumeweza kukusanya *service levy* hizi katika Halmashauri zetu ambazo mwanzoni hazikuonekana. *TMAA* wameweza kuokoa madini yaliyokuwa yakitoroshwa maeneo ya *airport* na maeneo mengine ambayo Serikali imeokoa zaidi ya bilioni 13 kwa kipindi cha miezi kumi tangu wameweka mageti katika viwanja vya ndege. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia fedha nyingi tu kwa takwimu ambazo zimekusanywa na imeweza kutusaidia kujua hali halisi ya soko la madini katika soko la dunia na kile kinachozalishwa na migodi. Kwa hiyo, Serikali imeendelea kusisitiza kuwa *TMAA* ni chombo ambacho kinatusaidia na tunatakiwa tukiboreshwe zaidi kwa kuzingatia *size* ya uwekezaji wa migodi ambayo inaendelea kuja nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni matarajio yetu kuwa sekta hii itaendelea kupanuka na tunatakiwa tujiandae vizuri kuwa na chombo ambacho kitaweza kusimamia maslahi ya nchi katika migodi. Kwa taarifa tu nchi zingine kama Sudan, Kenya watakuja kujifunza hapa namna sisi tunavyosimamia na kukagua migodi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mkosamali alizungumzia michanga inayobebwa kutoka kwenye migodi kwenda nje. Ni kweli kuna michanga ambayo maarufu kwa

jina la *concentrate* ambayo inasafirishwa kwenda nje na hii inatokana na kwamba tulikuwa na *refinery* zamani hapa ilikuwa inaitwa Mwananchi *refinery* kule Vingunguti.

Mheshimiwa Spika, *Refinery* hiyo ilianzishwa na Benki Kuu lakini kwa sababu mbalimbali ilishindwa kufanya kazi vizuri na kusababisha kuwa *concentrate* hizi zipelekwe nje kwa ajili ya kufanyiwa *refinery* na kupelekwa sokoni. Kinachofanyika kwa sasa siyo utorohaji, tuna maabara zetu ikiwepo maabara ya *TMAA* inachukua *sample* katika kila *concentrate* na kujua *percent* ya dhahabu iliyomo mle, kujua *percent* ya shaba na *silver* zilizomo mle na zote wanazipigia hesabu na zinalipiwa kodi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, siyo kwamba michanga ile inaondoka tu bila kusimamiwa. Lakini mchango wa madini katika Taifa; miaka miwili iliyopita mchango wa sekta ya madini ilikuwa ni kutoka 2.8% katika *GDP* sasa hivi tuko katika 3.5% ya *GDP*. Kwa hiyo, unaweza kuona sekta inakua na tunatakiwa kuongeza usimamizi zaidi kuhakikisha kuwa sekta hii inatoa mchango mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini fedha hizi zote zinakwenda kwenye Mfuko wa Hazina na ndiyo zinagawanywa na humu Wabunge ndiyo tunagawana wote ikiwemo na wanafunzi katika Bodi ya Mikopo, fedha hizi ndizo wanazozitumia kwa sababu ndiyo zinachanganywa mle mle, kwa sababu kuna hoja ilitolewa kwamba, sekta ya madini haichangii na fedha hazionekani. Fedha zinakwenda Hazina na ndiyo tunagawana wote kwenye miradi ya maji, barabara na Bodi ya Mikopo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Martha Mlata amezungumzia maeneo tengefu ya wachimbaji wadogo Singida na maeneo mengine. Tunaendelea kugawa maeneo haya likiwemo lile eneo la Singida ambalo mwanzoni lilikuwa lina leseni kubwa, tumelitenga kwa ajili ya leseni ya wachimbaji wadogo, eneo la Ibagaa.

Mheshimiwa Spika, sasa kama eneo hilo limepewa

tena leseni kubwa kama alivyoripoti kwenye mchango wake, tutachukua hatua kuhakikisha kuwa aliyepewa leseni hiyo tutaifuta na eneo hilo lillotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo libakie kuwa la wachimbaji wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa John Cheyo amezungumzia gesi ya Mtwara, kwanza nimshukuru sana amefafanua ameonesha uzee ni dawa amefafanua vizuri faida ya gesi ya Mtwara na wananchi wa Mtwara kwa namna ambayo watanufaika. Namshukuru sana na hili la Mtwara limeeleweka na limetolewa maelezo mengi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu matumizi ya *TANESCO* kipaumbele chetu kama Serikali na kama Wizara, ni kuhakikisha Watanzania wanapata mwanga, tunapata mwanga kwa gharama kubwa, kwa sababu tunazalisha umeme kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, tunachopigania sasa hivi ni kuhakikisha tunazalisha umeme kwa gharama nafuu ili pesa zote hizi ambazo zimepitishwa na Bunge lako Tukufu zinazokwenda ku-*support TANESCO* kuzalisha umeme zielekezwe kwenye shughuli zingine za maendeleo na siyo kuzalisha umeme kwa mafuta kama tunavyolipa gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni kipindi cha miezi 18 bomba litakapokamilika ndipo tutaacha kutumia umeme wa mafuta na tutajielekeza kwenye umeme wa gesi. Kwa hiyo, mitambo hii ambayo tunaitumia kwa 78% sasa tutaweza kupunguza matumizi hayo na hela hizi tutazipeleka katika shughuli zingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ntukamazina amezungumzia mgodi wa Kabanga. Mgodi huu sasa hivi tumeshaanza kujadiliana mkataba wake, lakini changamoto kama alizozisema ni reli kwa sababu *Nickel*/ni nzito, inatakiwa kusafirishwa na reli, lakini pia kuna *project* ya umeme, lakini *project* ya reli pia ni *Tripertite* ambayo inahusisha nchi tatu

nchi ya Burundi, Rwanda na Tanzania. Kwa hiyo, pamoja na kusimamia na kuangalia mkataba na leseni yao, lakini pia tunashughulikia tatizo la umeme pamoja na reli kwa ajili ya kusafirisha *Nickel*.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge sasa napenda niwapeleke katika kifungu cha 106(1) cha Kanuni za Bunge ambacho kinasema "Mjadala kuhusu hotuba ya bajeti ya Serikali utaendelea kwa siku zisizozidi saba ambazo dakika zitakazotumika ni kumi kama tulivyokuwa tukitumia.

Halafu pia napenda niwapeleke kwenye Kanuni ya 107(1) na (2) kwamba mjadala kuhusu hotuba ya bajeti ya Serikali utakapomalizika, Spika atalihoji Bunge litoe uamuzi wake kwa kupitisha au kutopitisha bajeti ya Serikali ili kukidhi matakwa ya Ibara ya 90(2)(b) ya Katiba.

Kanuni hiyo hiyo ya pili inasema: "Uamuzi wa Bunge wa kupitisha au kutopitisha bajeti ya Serikali utafanywa kwa kupiga kura ya wazi kwa kuita jina la Mbunge mmoja mmoja". Sasa Ibara ya Katiba ya 90(2)(b) inasema: "Ni wakati gani kuwa Rais hawezi kuvunja Bunge isipokuwa kwa masharti mengine yametajwa, mojawapo ni kama Bunge limekataa kupitisha bajeti iliyopendekezwa na Serikali". Hilo ni sharti mojawapo.

Kwa hiyo, hii ni kwa faida yetu sisi wote. Sasa Waheshimiwa Wabunge tumesema mjadala huu umekubalika kujadiliwa siyo zaidi ya siku saba, leo ni siku ya nne na wachangiaji wote walioomba na waliokuwepo wamemalizika.

Waheshimiwa Wabunge, kwa maana hiyo nafunga mjadala wa kujadili na nimeshafunga, ila kwa sababu ya kifungu cha 109 (1) na (2) kwanza kabisa ningependa Waziri

wa Fedha afanye kazi ya kujumuisha mambo yote mliyozungumza hapa kwa ufasaha. Hiyo ni moja ya nafasi inayotolewa.

Pili, kwa mabadiliko ya mfumo tuliofanya, *Finance Bill* zamani wakati Waziri amesoma mwanzoni, anakuwa na miezi miwili yote anacheza nayo tu na Kamati, lakini kwa safari hii *Finance Bill* imesomwa mara ya kwanza juzi. Hivi sasa Kamati yangu ya Bajeti inapitia kule, lakini hawajakaa na Serikali, maana Serikali tulikuwa tunawabana hapa. Kwa hiyo, kuanzia leo tumemaliza mjadala, kesho tutakuwa na kipindi cha maswali basi, halafu Waziri na timu yake na Wataalam wake watakaa na Kamati ya bajeti kupitia ile Sheria.

Waheshimiwa Wabunge, sisi kwa upande wetu tutakuwa na Mkutano wa *TAPAC* ambao utaanza baada ya kumaliza kipindi cha maswali kule katika Ukumbi wa Msekwa, utakuwa kesho na keshokutwa, walikuwa wafanye keshokutwa na Jumapili lakini kwa sababu hii basi wataanza kesho, watamaliza Mkutano keshokutwa na Wabunge wote ni wanachama wa huo Mkutano. Kwa hiyo, wote mnakaribishwa kesho baada ya kipindi cha maswali.

Wakati huo huo naona wengine mmepata kadi na wote mnatakiwa kupata kadi nilishaeleza asubuhi kuwa tutafanya hafla ya kumpongeza Mheshimiwa Sitta kwa uongozi wake wa Bunge la Tisa, kwa hiyo, nawaombeni Waheshimiwa Wabunge pamoja na shughuli zenu mlizonazo, jioni kesho muwepo na kadi zinagawiwa, wote mfike, tukae pamoja tuweze kufanya shughuli hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa michango yenu mizuri sana katika mjadala huu na kama tulivyosema mabadiliko haya ni mapya na kitu chochote kipya hakiwezi kukosa changamoto, sasa haya tuliyojifunza, mengine tutayafanyia uimarishaji baadaye kidogo. Nadhani tutakapoanza kipindi kingine tutakuwa na hali nzuri zaidi, kwanza tumeanzia katikati wakati utaratibu huu ulitakiwa tuanze mwezi wa Oktoba.



20 JUNI, 2013

Kwa hiyo, naamini pia Serikali wameshaona na sisi tumeshaona palipo pabovu ni mahali gani tunaweza kupaimarisha. Kwa hiyo, nashukuru kwa michango yenu mizuri sana ambayo imekuwa ya staha hasa wiki hii, tumekaa kama Bunge tulilokuwa tunalifahamu sisi miaka yote. *(Makofi)*

Baada ya kusema hivyo, naomba niaahirishe shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa, tarehe 21 Juni, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*